**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Thelathini na Nne – Tarehe 27 Julai, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Sylvester Massele Mabumba) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha, 2011/2012.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI**:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha, 2011/2012.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Kilimo na Uvuvi kwa Mwaka 2010/2011 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

## MASWALI NA WAJIBU

Na. 312

**Kuimarisha Barabara ya Mpopera – Mkarongo – Kipatimu**

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU** aliuliza:-

Kata ya Kandawale ni kisiwa ambapo mvua zinanyesha na hakuna daraja kwenye Mto Matandu la kuunganisha Njinjo na Kandawale.

Je, Serikali i na mpango gani wa kuimarisha barabara ya Wilaya ya Mpopera – Mkarongo – Kipatimu ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa iliomba fedha za ziada kwa ajili ya hiyo miaka sita iliyopita.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa barabara za Halmashauri zikiwemo barabara za Kata ya Kandawale. Kwa kutambua umuhimu wa barabara hiyo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, Serikali kuanzia mwaka 2007/2008 hadi mwaka 2010/2011 iliidhinisha kiasi cha shilingi bilioni 1.327 kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 832 ili ziweze kupitika wakati wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012 Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa imeidhinishiwa shilingi milioni 436 kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 284. Hali hii inaonesha kuwa fedha za matengenezo ya barabara katika Halmashauri ya wilaya ya Lindi zimekuwa zikiongezeka mwaka hadi mwaka sawa na ongezeko la asilimia hamsini na tano (55%) ya Bajeti.

Aidha, kwa mwaka 2011/2012 Halmashauri imetenga shilingi milioni 27 kwa ajili ya kuifanyia matengenezo barabara ya Mkarongo – Kipatimu yenye urefu wa kilomita 12 kupitia *TASAF.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri inashauriwa kuweka kipaumbele na kutenga fedha kupitia Mfuko wa Barabara ili kutengeneza barabara hii ili iweze kupitika wakati wote. *(Makofi)*

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Majibu ya Mheshimiwa Waziri kwa imani yangu hayawiani na swali ambalo nimeuliza. Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa iliomba fedha maalum kupitia Mfuko wa Barabara, ili barabara hii iweze kutengenezwa. Wilaya ya Kilwa na Mheshimiwa Waziri mwenyewe anajua ukubwa wake ni *almost* karibu mkoa mzima wa Kilimanjaro. Shilingi bilioni 1.3 kwa kipindi cha miaka mitano (5) kwa ajili ya kutengeneza barabara zote za Wilaya ya Kilwa ni jambo ambalo halipo.

(i) Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba Mheshimiwa Waziri anikubalie na aliambie Bunge hili na wananchi wa wilaya ya Kilwa, kama yuko tayari kwenda kutembelea eneo husika ili majibu yake au utekelezaji wa Serikali uwiane na matakwa halisi, siyo takwimu ambazo zinaletwa hapa na Wataalam ambazo siyo sahihi na si za kweli. Hilo la kwanza.

(ii)Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa wananchi wanasumbuka sana kuzunguka umbali mrefu mno, lakini bado tuna tatizo la daraja katika barabara hiyo, kipande cha kati ya Njinjo na Kandawale, mto Matandu.

Je, Waziri yupo tayari kufuatana na mimi tukaangalie eneo hilo ili aone uhalisia na atutengee fedha ili daraja lijengwe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mbunge wa Kilwa Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi wala sipati taabu kuelewa kitu anachozungumzia Mheshimiwa Murtaza Mangungu. Hii shida wanayopata pale hajaeleza zaidi, hapo kwenye hilo daraja analolisema amewahi kufa mtu. Kwa hiyo, siyo jambo ambalo mimi ninalichukua kwa utani hapa au silichukulii uzito unaostahili. Serikali inatambua tatizo hilo. Mheshimiwa Mbunge anafahamu kabisa kwamba, lile eneo analolizungumzia wameweka *drift.* Kwa hiyo, mvua zikinyesha pale watu hawawezi kupita kwenda hospitali, kwenda Makao Makuu ya Wilaya, sokoni na wala sihitaji hata kufika Kilwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua kwamba kuna tatizo kubwa sana na ndiyo maana nimemwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hii tukae. Nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge kilichotokea; wana daraja lingine ambalo halitaji hapa, linaitwa Mikungo Chapita ambalo ndilo lililochukua fedha nyingi sana na waliliona kama ni kipaumbele, sitaki kutumia takwimu hizi kutetea jambo hili, wakazipeleka fedha kule. Nimewauliza kwamba ni kwanini mlipeleka fedha kule? Wakasema hili daraja ni muhimu sana, sana kwa sababu lile hata kama ni wakati wa kiangazi hawawezi pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimthibitishie Mheshimiwa Murtaza Mangungu kwamba tunatambua daraja hili lina matatizo, kama ni kwenda Kilwa amwambie Mzee Mtopa, mimi nitakuja twende wote tukaone hilo eneo ili tupate tawkimu sahihi. Lakini nataka niseme kwamba anachosema Mheshimiwa Mbunge ni kweli kuna tatizo pale, kwa hiyo tutakwenda kumsaidia.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo makubwa ya barabara ambayo watu wa Kilwa Kaskazini wana- *face* ni matatizo makubwa kwenye barabara zote za halmashauri, manispaa na majiji. Nilikuwa namwuliza Mheshimiwa Waziri, hivi si umefika wakati sasa Serikali ifanye maamuzi ili barabara zote nchini zihudumiwe na mtu mmoja ili iwe rahisi kujua upungufu wa fedha tunazozihitaji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Peter Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kama nitakuwa nimempata vizuri sana, lakini naona anachotaka kusema ni kwamba barabara zote zirudishwe Wizara ya Ujenzi au TAMISEMI. Ninachokifahamu katika jambo hili ambalo analizungumzia Mheshimiwa Mbunge, na labda baadaye nitamfuata ili tujue vizuri anachokisema.

Hapo nyuma tuliwambia watu kwamba tunakwenda kwenye kitu kinachoitwa *D by D* (*Decentralisation by Delovution*) maana yake unapeleka madaraka kwa wananchi, lakini wakati huohuo unawapelekea nyenzo za kufanyiakazi.

Sasa kama utarudi nyuma ukasema tupeleke barabara zote Wizara ya Ujenzi, dhana nzima ya kupeleka madaraka kwa wananchi inakuwa imekufa, inakuwa haipo. Tunachotaka hapa ni kwamba wananchi wenyewe ndiyo wanaojua matatizo waliyonayo kule katika maeneo yao, kwa hiyo wao ndiyo wanaoibua miradi na kusema mradi huu tunadhani sisi kwetu ni kipaumbele.

Ukiwaondolea wananchi nafasi hiyo maana yake umewaondolea hata umiliki wa mchakato mzima unaohusikana na maendeleo yao tutakuwa tunarudi kule kule. Makao Makuu Dodoma na Dar es Salaam, ndiyo watakuwa wanafanya maamuzi kwa niaba ya wananchi, kitu ambacho kwa maoni yangu kitakuwa tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Mheshimiwa Peter Serukamba anazungumzia habari ya kuwa na chombo maalum kitakachosimama kwa ajili ya barabara, lakini ambacho kitabeba mawazo ya wananchi kule waliko, mimi sina tatizo nacho. Hilo ni suala la kisera, tutapokea hayo tutapeleka katika mamlaka tuzungumze vizuri. Nakiri kwamba sikumpata vizuri, lakini hayo ndiyo mawazo ambayo mimi naona yanaweza yakatusaidia.

Na. 313

**Fedha zilizotengwa kwa ajili ya Uendeshaji wa Shule**

**MHE. TUNDU A. LISSU** aliuliza: -

Serikali katika mwaka wa fedha 2009/2010 ilitenga jumla ya shilingi 55,553,525,822.75/= kwa ajili ya uendeshaji shule. Kati ya fedha hizo, shilingi 35,656,504,688.15/= ndizo zilizotumika kwa kusudio hilo hadi kufikia mwezi Machi, 2010 na shilingi 21,396,303,806.40/= zilibaki.

Lakini licha ya kutengwa fedha hizo, wananchi katika maeneo mbalimbali nchini wamekuwa wakilazimishwa kuchangia ujenzi wa shule za Sekondari za Kata kwa kujenga madarasa, nyumba za Walimu, kununua madawati, karatasi, kulipia taaluma, mitihani na walinzi wa shule hizo:-

(a) Je, kwa nini fedha zinazotolewa hazitumiki zote badala yake Wananchi wanachangishwa kwa nguvu kwa kisingizio kuwa Serikali haina fedha za kutosha kujenga na kuendesha shule?

(b) Je, kiasi cha shilingi 21,396,303,806.40/= zilizobaki hadi kufikia Machi, 2010 zimepelekwa wapi?

(c) Je, Serikali iko tayari kupiga marufuku michango hiyo ya nguvu na kueleza sababu za kubaki kwa fedha hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tundu Antiphas Lissu, Mbunge wa Singida Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na ( c ) kwa pamoja kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (MMEM), fedha zote zinazotengwa katika Bajeti hupelekwa katika Halmashauri kwa awamu kila robo ya mwaka na baadaye Halmashauri husika huzipeleka shuleni.

Aidha, utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya elimu hufanywa kwa ubia kati ya Serikali na Wananchi kwa kuzingatia dhana ya Ugatuaji wa Madaraka kwa Wananchi wenyewe. Hivyo, hakuna mwananchi anayelazimishwa kuchangia kwa nguvu shughuli za ujenzi kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge alisema, bali michango hiyo huamuliwa na wananchi wenyewe kupitia vikao vyao halali vya Serikali ya Kijiji, pia hata Kata.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha shilingi bilioni 21.4 zilizosemwa na Mheshimiwa Mbunge zilizotumwa mwaka katika mwaka wa fedha 2009/2010 na kwamba zilirudishwa, zilikuwa katika akaunti ya shule za msingi kwa matumizi ya vitabu asilimia arobaini (40%), vifaa vya kufundishia asilimia ishirini (20%), ukarabati wa majengo asilimia ishirini (20%), mitihani ya ndani ya asilimia kumi (10%) na utawala kumsaidia Mwalimu Mkuu pale na shule yake ni asilimia kumi (10%).

Mchakato wa matumizi katika shule hutegemea sana mahitaji na baada ya kuidhinishwa na Kamati za Shule yenyewe. Kwa upande wa vitabu na vifaa vingine vya kufundishia malipo yake hufanywa baada ya wauzaji kuwasilisha vitabu na vifaa shuleni. Hivyo, fedha hizo zilikuwa katika mihadi ya shule.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali Serikali haitumii nguvu kuwachangisha wananchi bali wanashirikishwa katika kuibua, kupanga na kuendesha miradi yao wenyewe na hii inasababisha kuona kuwa miradi hiyo ni ya kwao wenyewe. Utaratibu huu unasaidia wananchi kufanya ufuatiliaji na tathmini kuhusu matumizi ya fedha za Serikali ikiwemo michango waliyotoa kwa ajili ya maendeleo ya Shule. Aidha, natumia fursa hii kuwaagiza Wakuu wa Shule kuzingatia matumizi mazuri ya fedha za uendeshaji na utoaji taarifa kwa Wananchi kwa mujibu wa Sheria na Taratibu zilizopo.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza niseme kwamba mimi namheshimu sana Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa kweli huwa nakuwa mzito sana kusema Waziri

amesema uongo. Lakini katika majibu haya naomba nitoe tamko kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri ameliambia Bunge hili uongo, na naomba nipewe nafasi ya kuthibitisha uongo huo leoleo, tena kwa ushahidi wa maandishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niulize swali dogo la nyongeza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa samahani naomba Mheshimiwa umekiri katika maelezo yako kwamba Waziri ameshindwa kukuridhisha, maelezo yake hayalingani na swali lako.

Kwa vile hutakuwa na nafasi ya swali la nyongeza nimtake Mheshimiwa Waziri, *No!* Nikutake wewe unipe ukweli kuhusu suala hili. Tafadhali naomba uliambie Bunge hili ukweli wa suala hili na bahati nzuri umesema hapo ulipo uko tayari kutoa maelezo haya. Tafadhali nafasi ni yako!

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijasema Waziri ameshindwa kuniridhisha, nimesema Mheshimiwa Naibu Waziri amesema uongo. Ndiyo maneno niliyoyatumia.

Mheshimiwa Naibu Waziri amesema uongo, na uthibitisho ni kwamba mimi mwenyewe hapa hapa Bungeni, nina barua ya tarehe 2 Mei, 2005 iliyoandikwa na aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Singida wakati huo, anaitwa Mheshimiwa Capt. James C. Yamungu, ambayo kichwa chake cha habari kinasema: 'Amri Na.1 ya Mkuu wa Wilaya ya Singida'. Barua hiyo inalazimisha wananchi kulipa michango.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu!

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu!

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 68, huu ni wakati wa kipindi cha Maswali na Majibu.

**MWENYEKITI:** Sitini na Nane (68) ngapi?

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu!

**WABUNGE FULANI**: Endelea.

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema huu ni wakati wa kipindi cha Maswali na Majibu na kwa sababu Mbunge aliyeuliza swali alisema anaweza kuthibitisha, mimi nilikuwa nafikiri wewe ungeweza kumtaka athibitishe kwa wakati wake baadaye, lakini sasa hivi kipindi cha maswali na majibu kiendelee. (*Makofi*).

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge kwa vile baadaye tuna hoja ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ninaomba Mheshimiwa Tundu Lissu uwasilishe maelezo hayo ambayo unasema una barua ambayo ulikuwa unaoisoma sasa hivi, mezani halafu utaratibu mwingine utafuatia. Tafadhali!

Kwa hiyo, sasa itakuwa ni swali katika Wizara ya ....

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Mwenyekiti! Mheshimiwa Mwenyekiti!

**MWENYEKITI:** No! No! No! Hapana!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Mwenyekiti!

**MWENYEKITI:** Samahani! Samahani! Samahani! ... naomba ukae Mheshimiwa Waziri, naomba ukae, naomba ukae! Hutakuwa na kitu cha kujibu pale. Naomba nimwite muulizaji wa swali la nyongeza kama lipo.Mheshimiwa Regia Mtema!

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi nina tatizo na *modality* ambavyo Halmashauri zetu za Wilaya zinavyokusanya michango. Wanatumia mgambo, wanawalazimisha wananchi wachange, kama hawana wale mgambo wanawapiga na wakati mwingine wanawapekeka selo. Hiki ni kinyume cha Haki za Binadamu.

Mheshimiwa Naibu Waziri, hivi hakuna njia nyingine ya kistaarabu ya kukusanya michango hii? Naomba majibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri naomba ujibu swali la Mheshimiwa Regia Mtema.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa michango yote ya maendeleo kwenye maeneo yetu ya vijiji ni utaratibu unaoamuliwa na wananchi wenyewe kulingana na mahitaji yao kwa maendeleo yao wenyewe.

Uongozi wa Serikali ya Kijiji unakaa unakubaliana mradi wanaoutaka wanapanga utaratibu na Halmashauri kupitia wawakilishi ambao Wabunge wenyewe ndio sehemu ya wawakilishi wenu mnafika kwenye Halmashauri mnaipa kipaumbele mnatuma fedha na wananchi wanachangia nguvu zao kwa kiwango kile ambacho wao wanaweza kutolea michango pale.

Hakuna utaratibu wa nguvu unaotumika labda kama wao wenyewe wamejiamulia kuweka utaratibu huo, lakini Serikali haina mpango wala haina utaratibu wa kumlazimisha mwananchi kuchangia mchango wowote kwa nguvu, huo ndio utaratibu unaotumika maeneo yote. Kama kwenye Halmashauri yenu Halmashauri ile ya Kijiji imeamua kutumia nguvu huo sio mpango wa Serikali ni wananchi wenyewe kwenye maeneo yao.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu aliyoyatoa. Huu utaratibu wa wananchi kuchangia maendeleo yao kwanza ni jambo la kimsingi kwamba maendeleo ya watu yanaletwa na watu wenyewe na kwamba wananchi hawa katika suala la kuwapelekea madaraka unawapa madaraka ya kuamua na unawapa madaraka ya kusimamia utekelezaji wa maamuzi yao.

Kwa hiyo katika ngazi ya Kijiji wananchi wanapofikia maamuzi kwamba tutajenga zahanati na gharama ya kazi yetu sisi ni kuleta viashiria wananchi wale wataleta viashiria kutokana na maagizo wanayoyafanya wao wenyewe na watasimamia kazi hiyo. Ndiyo maana ya kuwa na Serikali katika ngazi ya Kijiji, hivi kuna Serikali gani ambayo inaamua halafu haisimamii utekelezaji.

Sasa ikiwa linatokana kosa hapa na pale haliwezi kuhukumu *concept* nzima ya watu kujitegemea na tuna miradi mingi. Kwa mfano miradi ya maji inayogharamiwa na Benki ya Dunia ina *concept* ya watu kuchangia. Miradi ya TASAF yote lazima wananchi wenyewe wanaibua na wanachangia. Kwa hiyo, kusema kweli tukianza kukataa mfumo mzima wa kuchangia tutakuwa tunawarudisha nyuma wananchi na tutarudisha nyuma maendeleo yao. Kama kuna dosari mahali tuna-*deal* na dosari pale pale ilipo tunasahihisha hapo hapo ilipo. (*Makofi)*

Na. 314

**Milipuko ya Mabomu Kwenye Kambi za Jeshi**

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR** aliuliza:-

Tulipopata tatizo la milipuko ya mabomu kwenye Kambi ya Jeshi Mbagala na kupoteza ndugu zetu na madhara mengine mbalimbali, wananchi walishauri kwamba Kambi za Jeshi zenye silaha kali kama mabomu ziwekwe mbali na makazi ya wananchi lakini tarehe 16 Februari, 2011 milipuko mikubwa ya mabomu ilitokea tena kwenye Kambi ya Jeshi Gongo la Mboto na kusababisha vifo na maafa makubwa:-

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kukabiliana na tatizo hili la milipuko ya mabomu Tanzania Bara na Tanzania Visiwani?

(b) Je, Serikali inapochelewa kuwahamisha wananchi walio karibu na Kambi hizo haioni kuwa madhara hayo yanaweza kurudia na kusababisha hasara kubwa zaidi kwa Serikali na wananchi pia?

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA NA UTAMADUNI (K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu swali la Mhe. Fakharia Khamis Shomar, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia ajali za milipuko zilizotokea Serikali imejipanga kuchukua hatua za muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Hatua za muda mfupi ni kufanya ukaguzi wa maghala yote, kujenga matuta makubwa ya udongo kati ya ghala moja na ghala nyingine na kuendeleza utaratibu uliyopo wa kuteketeza milipuko iliyokwisha muda wake. Hatua za muda wa kati ni ujenzi wa maghala yanayokidhi viwango kwa lengo la kuweka usalama wa watu na mali zao, na Wanajeshi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za muda mrefu ni pamoja na kupitia upya mipaka ya Kambi zote nchini kwa madhumuni ya kutekeleza mapendekezo ya kuwa na angalau kilomita moja baina ya maeneo ya Jeshi na makazi ya watu. Zoezi hili litahitaji tathmini ya kina ifanywe ili kuona uwezekano wa kuwahamisha wananchi walio karibu sana na Makambi yenye kuhifadhi milipuko.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa Zanzibar baadhi ya Kambi za Jeshi ziko jirani na makazi ya wananchi. Namwuliza Mheshimiwa Waziri je, Wizara yake imechukua tahadhari gani au mafunzo gani au elimu gani kuwaelimisha wananchi wanaokaa jirani na Kambi hizo kwa bahati mbaya kama itatokea milipuko ya aina hiyo?

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kama nilivyosema awali kuhusu tahadhari za msingi tutakazozichukua katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Naomba tu kwa namna ya pekee niupokee ushauri mzito kabisa wa Mheshimiwa Fakharia wa kuona umuhimu wa kutoa mafunzo kwa wananchi wa Zanzibar na wananchi wa maeneo mengine ili waweze kuchukua tahadhari wenyewe mambo ya namna hiyo yanapotokea. Serikali imechukua kwa uzito unaostahili.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina suala moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa maghala ya silaha katika nchi nyingi zilizoendelea na zinazoendelea ni kitu muhimu sana kwa sababu yanahodhi silaha ambazo gharama yake ni kubwa. Na kwa kuwa maghala mara nyingi huwa yanachimbwa chini ya ardhi na silaha hizo kuwekwa sehemu hiyo ili yanapotokea madhara yasiweze kuenea katika maeneo yanayoishi binadamu.

Je, Serikali yetu hasa ukizingatia na bajeti hii ambayo tumeipitisha hivi karibuni ina mikakati gani hasa ya dhati ukizingatia ukweli wa mambo kwamba mwaka huu hazikutengwa fedha za kutosha za kuyafanyia matengenezo sisemi kwa namna ambayo tunataka kujenga maghala mapya ambayo yatahimili misukosuko kama hiyo inayotokezea nchini Tanzania?

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA NA UTAMADUNI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alieleza kwa kina mipango ya Serikali ya kujenga maghala ya kudumu na imara wakati wa bajeti na Bunge hili likaridhia. Nataka nikuhakikishie kwamba Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama imepokea mipango ya Serikali ya kina ambayo haiwezi kusemwa ndani ya Bunge na imeiridhia. Kwa hiyo nawatoa hofu Waheshimiwa Wabunge kuhusu jambo hilo.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka kujua ni sababu gani licha ya mchango wangu wa maandishi kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwamba kuna mabomu yaliyoachwa kwenye eneo la Kijiji cha Bunere eneo lililochukuliwa na Jeshi bila ya ridhaa ya wananchi? Tatizo ni nini na juzi tena ilitokea milipuko na wananchi wanahofu kama tatizo ni usafiri niko tayari kutoa usafiri?

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepokea tatizo alilolitoa Mheshimiwa Lugola na kweli dhamira yake ya kutoa mchango wa gari ili kufanikisha zoezi inaonyesha alivyo na nia njema kabisa na watu wa eneo lake. Nimhakikishie kwamba uzito aliouweka mbele ya Bunge hili Serikali inauchukua kwa uzito huo huo na itafanyiwa kazi.

Na. 315

**Askari Walioshiriki Vita Kuu ya Pili ya Dunia**

**MHE. IDDI MOHAMED AZZAN (K.n.y. MHE. MUSSA AZZAN ZUNGU**) aliuliza:-

Tanzania ilitoa askari wake kushiriki Vita Kuu ya Pili ya Dunia, na Serikali ya Uingereza kwa kuthamini na kuuenzi mchango wa askari hao iliamua kuwanunulia jengo ambalo askari hao wanalitumia kama sehemu ya kukutania na kitega uchumi chao.

Lakini jengo hilo limevunjwa kwa maelekezo kuwa jengo limepata mwekezaji lakini utaratibu wa kumpata mwekezaji huyo hawakushirikishwa hivyo kuwapa hofu ya kunyang'anywa jengo lao:-

Je, Serikali inalifahamu jambo hilo, na kama inalifahamu, inatoa tamko gani lenye kuonyesha hatma ya jengo hilo?

**WAZIRI WA HABARI, VIJANA NA UTAMADUNI (K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA) TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu swali la Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwa askari waliopigana vita kuu ya pili ya Dunia wanalo jengo wanalolimiliki kupitia umoja wao unaoitwa *Tanzania Legions and Company*, (TLC), kwenye *Plot* Na. 1082 Upanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo mwaka 2007, uongozi wa TLC uliingia mkataba na mwekezaji wa kujenga jengo jipya kama kitega uchumi. Pia Wizara inatambua kuwa jengo hilo kwa sasa limevunjwa. Maamuzi ya uongozi wa *TLC* kuingia mkataba na mwekezaji umezua mgawanyiko baina ya uongozi na wanachama wa TLC, baadhi ya wanachama wameenda Mahakamani kupinga mkataba huo. Hivyo kwa sasa Serikali haiwezi kuliongelea zaidi suala hilo.

**MHE. IDDI MOHAMED AZZAN:** Liko Mahakamani Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tuliwache tu.

Na. 316

**Athari za Tatizo la Umeme Kwa Ajira za Vijana**

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE** aliuliza:-

Kwa miaka mitano iliyopita, kumekuwa na tatizo lisilokwisha la Nishati ya Umeme.

Je, Serikali imefanya utafiti kujua ni kwa namna gani na kwa kiasi gani mgao wa umeme umeathiri shughuli ndogondogo za kujiajiri za vijana kama vile vinyozi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ukosefu wa Nishati ya Umeme ni kweli linaathiri maendeleo na ukuaji wa uchumi wa sekta mbalimbali pamoja na sekta ambazo vijana wanajiajiri kwa shughuli zao za kimaisha. Ni dhahiri mgao wa umeme umeathiri shughuli ndogo ndogo za kujiajiri za vijana kama vile shughuli za vinyozi, biashara za vinywaji baridi, biashara za kuchomea vyuma na mageti, mafundi wa magari, fani za ushonaji, mafundi seremala, mashine za kusagisha na kukoboa na kadhalika, shughuli ambazo zinahusisha Watanzania wengi mjini na hata vijijini.

Upana wa shughuli hizo unaonyesha ukubwa wa tatizo hili kama alivyokusudia kuonyesha Mheshimiwa Magige, kwani shughuli hizo hulazimika kusimama mara umeme unapokatika au wamiliki hulazimika kutumia jenereta jambo ambalo huwaongezea gharama za uendeshaji wa biashara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Mipango na Idara mbalimbali kwa kuwa ni suala mtambuka, inafanya utafiti kubaini athari za mgao wa umeme kwa kila sekta. Utafiti huo utakapokamilika Serikali itatoa taarifa ni kwa kiasi gani mgao wa umeme umeathiri sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii zikiwemo biashara ndogo ndogo za vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, pamoja na tathmini hiyo ambayo ni muhimu, kwa sasa Serikali inajielekeza kwenye kulipatia ufumbuzi wa tatizo hili kwa haraka katika kipindi kifupi kijacho kadri itakavyowekeana, ili sekta zote za uchumi wa Tanzania ziendelee bila kuathiriwa na tatizo la ukosefu wa umeme. Nia ni kufanya umeme uwe ni mchangiaji wa maendeleo ya Watanzania na haswa vijana na shughuli zao na siyo kikwazo.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize swali moja dogo la nyongeza.
Kwa kuwa tatizo hili la umeme limeathiri maisha ya vijana wengi walio vyuoni na wafanyabiashara ndogo ndogo. Je, Serikali inaweza kutamka ni lini vijana watarajie tatizo hili kumalizika ili wafanye shughuli zao kwa ufanisi zaidi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la kupatikana umeme Tanzania kama tulivyolisema sasa hivi lina sura ya uzalishaji na sura ya usambazaji. Bunge hili wiki mbili zilizopita ilipopokea Makadirio ya Wizara yetu ilitoa ushauri kwamba Serikali irejee na mpango wa dharura na ndio tunaufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa mahitaji yanayotakiwa yanazidi kupanda kutoka hata zile megawati 260 zilizokuwepo awali kwenda mpaka kwenye megawati 300 au 400. Tulizungumzia suala la kuleta mitambo kwa dharura na Bunge hili lilishauri kwamba mitambo hiyo isiwe mitambo ya kukodi kwa sababu gharama zake ni kubwa iwe ni mitambo ya kununua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba niseme tu kwamba tutakaporejea katika kuhitimisha Makadirio ya Wizara tunatarajia tuje na mpango huo wa dharura ambao utakidhi mahitaji na kuondoa labda tatizo hili la mgao wa umeme kadri tutakavyokubaliana ndani ya Bunge kwa muda wa kama miezi 9 mpaka 12 ijayo.

Lakini zoezi hilo linatarajiwa liwe la awamu kwa maana tutaingiza megawati 50 halafu 50, mpaka tatizo lenyewe lifikie kuondokana na hizo megawati 300 au 400 zinazosababisha tatizo hili kwa sasa.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. swali moja tu dogo la nyongeza.

Wakati msukosuko wa kiuchumi duniani ulipotokea Serikali ilikuja Bungeni ikaomba idadi ya fedha ya shilingi Trilioni 1.7 ili kuyasaidia Makampuni kuyafufua kiuchumi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia watu walioathirika kiuchumi kutokana na tatizo hili la kukatika kwa umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwenye jibu langu kwa swali la msingi nilisema kwamba kwanza kabisa lazima tufanye zoezi la kutathmini ni kiwango gani athari hii ya mgao imeenea katika maeneo mbalimbali ya kiuchumi ya Kitanzania.

Lakini kusema ule ukweli kabisa ni lazima tukubaliane athari hii ni kubwa na inaathiri maeneo mbalimbali. Kwamba itaathiri sekta isiyo rasmi *"The Informal Sector"* lakini pia hata sekta yenyewe viwanda vikubwa na vidogo vyote vimeathirika, wengine wanashindwa kufanya kazi, wanapunguzwa wafanyakazi na kadhalika.

Kwa hiyo athari ni kubwa ndio maana nasema kuifanyia tathmini sasa hivi na kuiambia Serikali iweze kufidia nadhani litakuwa suala ambalo sio *realistic.* Lakini tunachoweza kufanya na ndiyo ahadi ya Serikali ni kwamba ni lazima tuondokane na hili tatizo *as soon as possible.* Kwa sababu tatizo hili halipungui na tukiliacha litazidi kukua.

Na. 317

**Kuzalisha Umeme kwa Makaa ya Mawe ya Mchuchuma**

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE** aliuliza:-

Umeme unachangia kwa asilimia 47 ya maendeleo ya nchi yoyote Duniani na kwa nchi yetu inatakiwa iwe na umeme wa kutosha lakini hivi sasa nchi inakabiliwa na tatizo sugu la umeme.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutumia Makaa ya Mawe ya Mchuchuma ambayo yana uwezo wa kuzalisha zaidi ya megawati 600 za umeme utakaoweza kutumiwa na wana-Ludewa na Watanzania wote?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deo Haule Filikunjombe, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Filikunjombe kuhusu umuhimu wa mchango wa nishati ya umeme kwa ukuaji wa uchumi wa nchi kama alivyouliza kwenye swali la msingi.

Hata hivyo, upatikanaji wa nishati ya umeme una changamoto tofauti mbalimbali kwa kila nchi na jamii zake. Serikali yetu kwa kutambua changamoto tulizonazo sisi, tumebuni mipango

ya kuendeleza rasilimali zetu kama hizi za Mchuchuma na zinginezo kwa ajili ya kukabiliana na ukuaji wa mahitaji ya umeme ya kila mwaka kulingana na ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)* imeingia ubia na Kampuni ya *Sichuan Hongda* ya China kwa ajili ya kuendeleza mradi wa umeme wa Mchuchuma kwa kiwango cha MW 600.

Mradi huu utatekelezwa katika awamu mbili, awamu ya kwanza zitazalishwa MW 300 zitakazotumika kuyeyushia chuma cha Liganga na awamu ya pili zitalishwa MW 300 ambazo zitaingizwa kwenye gridi ya taifa. Mradi unatarajiwa kukamilika mwaka 2014/2015 na miradi hiyo miwili inaendelezwa kwa pamoja *(integrated project)* kwa kutambua faida zake kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa utekelezaji wa miradi ya namna hii inachukua muda mrefu na ina gharama kubwa ninaomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kushirikiana kwa karibu na Wizara yangu na wahusika wengine, ili mosi awe na taarifa za wakati, za maendeleo ya miradi hii yote miwili na pili ili pamoja tuhakikishe kuwa maendeleo ya utekelezaji wa miradi unajumuisha maslahi ya wananchi wa Ludewa ikiwa ni pamoja na kupata ajira na huduma zingine muhimu kadri itakavyowezekana.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mradi wa Liganga na Mchuchuma ni miradi ambayo imekwishatajwa sana na mara kwa mara unasema itakamilika kwa kiasi fulani lakini utekelezaji huwa hauonekani. Sasa Mheshimiwa Waziri anasema itakamilika mwaka 2014/2015, naomba aliimbie Bunge lako Tukufu na alithibitishie miradi hii inaanza lini kwa miundombinu ipi na kwa mikakati ipi. Swali la kwanza.

Swali la pili, Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la umeme ni tatizo la kutengenezwa, viashiria vyote vinaonyesha kabisa kwamba kuna watu wachache wananufaika hukuhuku Serikalini na hili tatizo. Kwa mfano Kamati yangu ya Hesabu za Mashirika ya Umma inaushahidi kwamba Wizara ya Nishati na Madini inapinga na haitaki kuendeleza miradi hii ya Liganga na Mchuchuma.

Kwenye Kamati yangu ya Bunge tulishamwita Katibu Mkuu aliyepita Ndg. David Jairo barua yake tunayo tunataka Mheshimiwa Waziri alithibitishie Bunge na Watanzania tumechoka na Megawatt, Watanzania tunataka umeme. Alithibitishie Bunge hili kwamba Wizara yake inashirikiana na iko tayari kuendeleza miradhi hiyo ya Liganga na Mchuchuma.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali lake la kwanza naomba uniruhusu kwa ridhaa yako nimpe maelezo ya ratiba ya utekelezaji kwa kifupi. Tumesema ipo miradi miwili kwa pamoja. Mradi wa kwanza wa makaa ya mawe ambayo yanalenga kwenda kwenye mradi wa Liganga ambapo yeye anajua kwa sababu ni Mbunge wa kule na mimi nimefika kule kwa sababu ya kukagua ile miradi. Liganga ni kama kilomita 30 kutoka pale Mchuchuma. Lakini mradi huu wa kwanza utalenga ku-feed makaa ya mawe kwa ajili ya Liganga. Kukamilisha mikataba ya uwekezaji tunatarajia Agosti 2011 kwa yote miwili.

Lakini kunakukamilisha tafiti za kuhakiki mashapo, ni Machi, 2012. Kukamilisha ujenzi wa Mgodi wa Makaa ya Mawe Juni, 2013 na kukamilisha ujenzi wa kituo cha umeme ni Novemba 2014. Huo ndiyo mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma. Kwa upande wa Liganga ni kukamilisha utafiti Oktoba 2012, kukamilisha mgodi wa chuma Aprili 2014 na kukamilisha ujenzi wa mitambo ya chuma Oktoba 2015. Hiyo ndiyo ratiba ambayo imekuja kutoka kwa mwekezaji pamoja na *NDC.*

Kwa hiyo nasema nilikuwa naomba na yeye tushirikiane katika kulifuatilia hili na kuhakikisha kwamba linapata utekelezaji lakini kwa sasa ndiyo ratiba hiyo. Hili la pili yeye anasema Kamati ina ushahidi wa kwamba hili ni tatizo la kutengeneza na kwamba Wizara ya Nishati na Madini ina-*conspire* kwa ajili ya kutokutekeleza miradi hii.

Mimi nadhani kauli hiyo si ya kweli lakini naomba tuvumiliane kwamba tutakapofika kuhitimisha hoja ya Waziri wa Nishati na Madini tumekubaliana kwamba tutakuja kwanza na Mpango wa Dharura kwa sababu tatizo hili ni tatizo la leo. Kwa hiyo kwanza tutakuja na Mpango wa Dharura wa namna ya kuondokana na tatizo hili katika kipindi kifupi kijacho halafu hiyo mipango mingine itafuata utekelezaji kwa kadri ambavyo Serikali itashirikiana na wawekezaji na sekta binafsi. *(Makofi)*

Na. 318

**Mpango wa Kuongeza Idadi ya Walimu**

**MHE. PHILIPA G. MTURANO** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikifanya jitihada katika kuandaa walimu wa kutosha na hata kuanzisha mkakati wa kuongeza udahili wa fani ya ualimu katika vyuo vikuu sambamba na kuwalipia ada kwa upendeleo.

(a) Je, ni walimu wangapi waliokuwa kwenye mpango huo ambao baada ya kuhitimu vyuo vikuu na kupangiwa vituo vya kazi hawakuripoti kabisa na badala yake kujiunga na fani nyingine?

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani kwa walimu hao?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Philipa Geofrey Mturano, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana katika Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (MMEM) na Mpango wa Elimu ya Sekondari (MMES) yamesababisha changamoto za ongezeko la mahitaji ya walimu wenye sifa stahiki katika shule za msingi na sekondari. Kwa hali hiyo, Wizara yangu imefanya jitihada za kubuni mikakati ya kukabiliana na changamoto za ongezeko la mahitaji ya walimu ikiwa ni pamoja na kuongeza udahili wa fani ya walimu na kutoa/kuwapa mikopo ya kugharamia elimu yao vyuoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/201 jumla ya wahitimu 5,015 wa Shahada ya Kwanza ya Ualimu walipangiwa kuripoti katika Halmashauri zote nchini. Kati ya hao ni walimu 3,783 waliripoti sehemu walizopangiwa kazi sawa na asilimia 75 ya wahitimu wote na wahitimu 1,232 hawakuripoti katika vituo walivyopangiwa kazi katika Halmashauri mbalimbali.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuwachukulia hatua walimu ambao hawakuripoti katika vituo vya kazi, kama nilivyojibu kwenye swali na 219 lililojibiwa tarehe 12 Julai, 2011 katika Bunge lako Tukufu, zoezi hili lina changamoto kubwa kutokana na kuwapo kwa soko huria la ajira pamoja na kutokuwepo utaratibu wa kisheria wa kuwataka wahitimu kuitumikia Serikali kwa kipindi maalum. Hali hii inasababisha wahitimu kwenda kufanya kazi sehemu yoyote bila kubanwa na Sheria au mwongozo wowote unaowataka kuripoti sehemu za kazi walizopangiwa na Serikali.

**MHE. PHILIPA G. MTURANO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Wameajiriwa watu ambao ni wahitimu wa Vyuo Vikuu ambao hawana taaluma ya ualimu. Tunashukuru pengine ni katika kukabiliana na tatizo la walimu. Lakini ni kwanini walimu wastaafu waliopo ambao wana nguvu wasiajiriwe kwa mkataba ili kupunguza hili wimbi la ukosefu wa walimu?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na ni suala ambalo tunaweza tukaliangalia ili kuweza kupunguza lau kwa kiasi fulani tatizo la walimu ambalo tuko nalo hivi sasa na pengine tutakuwa nalo kwa miaka michache tu inayokuja isiyozidi mitatu tatizo hili hatutegemei tena kuwa nalo hapa nchini.

Na. 319

**Uhamisho wa Askari Polisi Bila Malipo**

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH** aliuliza:-

Imeonekana kwamba, malalamiko mengi kutoka Jeshi la Polisi yanahusu uhamisho wa Askari Polisi bila kupatiwa malipo kwa wakati:-

(a) Je, ni askari wangapi waliohamishwa na ambao hawajalipwa hadi sasa?

(b) Je, huko wanakohamishiwa wanapewa nyumba za kuishi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2010 askari waliohamishwa na ambao walikuwa hawajalipwa fedha zao ni 22,603. Hata hivyo tarehe 30 Juni, 2011 Serikali imetoa shilingi 19.6 bilioni kwa ajili ya kulipa madeni ya askari pamoja na wazabuni. Zoezi la kuwalipa askari hao linaendelea.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, askari anapohamishwa anastahiki kupewa nyumba ya kuishi. Hata hivyo, kutokana na uhaba wa nyumba askari waishio nje ya kambi hupewa posho ya pango ambayo ni asilimia kumi na tano ya mshahara wake ili akapange nyumba uraiani.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuwa vijana wetu hawa *in ethics* wanashindwa kudai haki zao kwa maandamano au kwa mgomo. Kwanini wanacheleweshewa malipo yao na hawalipwi kwa wakati?

Swali la pili. Je, Wizara ina mpango gani wa kuwalipa wanaohamishwa hawa baada ya kupata fedha za uhamisho?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, sahihi kwamba tunao Askari wetu ambao ni wazalendo na kama ulivyosema na nimekuwa nikisema hapahapa nyumba hii Tukufu kwamba sisi wenyewe kama Wizara jambo hili linatusononesha kwa sababu hizi ni haki zao na tunadhani wana haki wa kuzipata wakati mwafaka na si vinginevyo.

Lakini kwa kuwa Wizara yenyewe kama ya Mambo ya Ndani ya Nchi hatuna fedha na unajua hali ya kifedha tuliyonayo katika Serikli. Kwa hiyo jinsi tunavyopata zile fedha ndivyo jinsi tunalipa madeni yakiwemo madeni ya Askari. Lakini jitihada zimekuwa zinafanyika kuhakikisha kwamba kipaumbele inakuwa ni Askari walipwe madeni yao halafu kuna madeni ya wazabuni pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili wale wanaohamishwa sasa hivi Wizara inasema kwamba Askari wasihamishwe mpaka pale ambapo pesa zipo ndipo ahamishwe ili kuondokana na matatizo ya malimbikizano ya madeni.

Na. 320

**Mradi wa Umwagiliaji Jimbo la Solwa**

**MHE. AHMED ALLY SALUM** aliuliza:-

Halmashauri ya Shinyanga Vijijini iliahidi shilingi milioni 900 kwa ajili ya Mradi wa Umwagiliaji katika Jimbo la Solwa Kata ya Samuye, lakini hadi leo hii kipindi cha miaka miwili ahadi hiyo haijatekelezwa :-

(a) Je, Serikali inafahamu kuwa ni heri aliyetumainishwa kwa maana hatachukia?

(b) Je, ni lini fedha hizo zitapatikana na kuwezesha mradi huo kuanza?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Solwa, lenye sehemu (a) na (b) yote kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kuomba fedha za miradi ya umwagiliaji unaanzia katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs)* baada ya kuibuliwa na wananchi wenyewe. Miradi inayopitishwa na Halmashauri ya Wilaya na kutengewa fedha za *DADPs/DADG* hujadiliwa na kuombewa fedha za nyongeza kutoka katika Mfuko wa kuendeleza umwagiliaji, Ngazi ya Wilaya *(DIDF)* kama gharama za mradi hazizidi shilingi milioni 800.

Bwawa la Masengwa lilifanyiwa usanifu wa awali mwaka 2007 makadirio ya ujenzi yalikuwa shilingi milini 900 lakini baada ya kufanyiwa usanifu wa kina na gharama ziliongezeka kufikia shilingi bilioni 1.3 ambapo Halmashauri ya Wilaya ilitenga shilingi milioni 46 sawa na asilimia 3.5 ya gharama za ujenzi. Kutokana na gharama za mradi kuwa kubwa ilikubalika kwamba mradi utafutiwe fedha za kutosha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na maneno ya Mheshimiwa Mbunge kwamba naomba kunukuu: '*Heri aliyetumainishwa maana hatachukia'*. Nafurahi sasa kumwarifu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Solwa kwamba kwa sababu gharama ya ujenzi wa bwawa la Masengwa imezidi kiwango kinachoruhusiwa kwenye ngazi ya Wilaya, katika mwaka 2011/2012 Serikali itajenga bwawa hilo kwa kutumia Mfuko wa kuendeleza umwagiliaji, Ngazi ya Taifa *(NIDF).*

**MHE. AHMED ALLY SALUM**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana yenye matumaini mazuri sana kwa wananchi wa Kata ya Masengwa napenda kuuliza maswali madogo mawili. *(Makofi)*

Kwa kuwa moja katika zoezi ambalo linaweza kutuondoa kwenye adha ya tatizo la njaa kila mwaka kwenye Jimbo la Solwa na maeneo mengine Mkoa wa Shinyanga ni suala zima la umwagiliaji.

Mheshimiwa Waziri unasemaje kuendelea kutusaidia kwa maana ya kuwa na mabwa wa katika skimu za umwagiliaji tano zilizopo katika Jimbo la Solwa ikiwemo Msalala, Mwamala na zingine ili inapotokea ukame tuweze kutumia maji hayo kulima na kuweza kupata mazao na kutokuisumbua Serikali kupata chakula?

Swali la pili, hivi karibuni mwezi uliopita walikuja wahandisi kutoka skimu ya umwagiliaji kutoka Mwaza walipita Kata ya Mwakitolyo pamoja na Lyabukande kutizama ni maeneo gani wanaweza kuibua mradi huu. Naomba kujua Mheshimiwa Waziri anasemaje na imefikia wapi ili sasa wananchi wa Kata ya Mwakitolyo na Lyabukande waweze kupata matumaini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakumbuka mwaka 2008 mimi mwenyewe nikiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji nilitembelea maeneo yale anayoyasema ya Mwakitolyo, Lyabukande na nikayaona kama ni mabonde mazuri yanayofaa na ndipo nilitoa maagizo kwenye ofisi ya kanda kuyakagua na kuyafanyia upembuzi.

Nadhani baada ya ziara yangu ndiyo ilizaa matunda haya na ndiyo maana wataalam wamekwenda na kuyakagua na wameyaona kama yanafaa.

Ninachoweza kusema sasa kinachochelewesha miradi hii pamoja na hiyo anayosema ni wataalam walioko kule Wilayani kuhakikisha kwamba wanawasaidia wananchi kuibua miradi hii kwa sababu wataalam ndiyo wanajua vigezo gani vinatakiwa kuingizwa katika maandiko ya miradi.

Lakini uzoefu unaonyesha kwamba mara nyingi wanawaachia wakulima ndiyo waibue, hapana. Hapa mimi nasema wataalam wafanye kitu kinachoitwa *guided* uibuaji. Wawasaidie wakulima kuibua miradi ili iweze kufikia kiwango. Kwa hiyo watakapowasaidia wale wananchi kwa haya maeneo ninahakika miradi aliyoitaja nayo itaingizwa kwenye mipango ya maendeleo. *(Maakofi)*

Na. 321

**Matumizi ya Mbolea za Chumvi Chumvi**

**MHE. SAID AMOUR ARFI** aliuliza:-

Matumizi ya muda mrefu ya mbolea ya chumvi Chumvi hupelekea ardhi kupoteza rutuba yake ya asili na kuwa sumu kwa mimea:-

Je, Serikali ina mpango gani mbadala wa kuwaondosha wakulima wetu kuwa tegemezi kwa mbolea za chumvichumvi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda wa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haina mpango wa kuondoa mbolea za Chumvi Chumvi kwa sababu bado zina umuhimu katika kufikisha kilimo chetu katika Mapinduzi ya Kijani. Pamoja na kwamba matumizi ya mbolea za chumvi chumvi yanaonesha kuongezeka kila mwaka bado matumizi ya mbolea hapa Tanzania ni kiwango cha chini sana ikilinganishwa na nchi nyingine Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Kwa mfano, wakati Wakulima wa Tanzania wanatumia kilo nane ya viini lishe vya mbolea kwa hekta, Malawi wanatumia wastani wa kilo 16 kwa hekta na Afrika Kusini, kilo 51 kwa hekta. Tunahitaji kuongeza matumizi ya mbolea kufikia angalau kilo 50 kwa hekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba matumizi ya mbolea ya chumvichumvi lazima yazingatie aina ya udongo ili baadaye yasilete madhara makubwa kwa udongo wetu.

Katika juhudi za kupunguza matumizi ya makubwa ya mbolea ya chumvi chumvi, Serikali inahimiza wakulima kuongeza matumizi ya samadi na mboji katika maeneo ambayo mbolea hizo zinapatikana kwa wingi hususan maeneo ya wafugaji.

Aidha, Wizara yangu inaendelea kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mbolea za chumvi chumvi sambamba na kuhamasisha matumizi ya mazao ya jamii ya mikunde ili kuongeza rutuba ya udongo. Mfano mmoja ni kilimo cha kuchanganya zao la mbaazi na Mahindi kama inavyofanyika katika Mikoa ya Manyara, Arusha, Kilimanjaro na Dodoma.

Mfano mwingine ni ubadilishaji wa mazao kwa mazunguko kati ya nafaka na mikunde, (kama soya na Mahindi), mfumo ambao umeanza kupewa msukumo katika Mkoa wa Ruvuma. Nawapongeza wakulima wa Mikoa hiyo kwa kukipa msukumo kilimo cha aina hii ambacho kinalenga kuhifadhi udongo pamoja na kutunza mazingira na afya zetu.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Pamoja na mfano mzuri ambao Mheshimiwa Waziri ameeleza ya wakulima kuanza kuchanganya kilimo hiki kilikuwa kikifanyika miaka mingi iliyopita kabla ya matumizi ya mbolea za chumvi chumvi kwa maana hiyo sasa Serikali au Wizara inasema nini juu ya kilimo mseto ambacho kinaonesha kurutubisha ardhi?

La pili, kwa kuwa wakulima wetu wamekuwa sasa ni tegemezi wa mbolea za chumvi chumvi…

**MWENYEKITI:** Naomba uulize swali, usizunguke maelezo!

**MHE. SAID A. ARFI:** Kwa kuwa wakulima wetu wamekuwa tegemezi kwa mbolea za chumvi chumvi; mbolea hizi hazifiki kwa wakati, hakuna kiwanda cha mbolea; kuna mpango gani wa kuhakikisha sasa kwa msimu huu unaoanza, mbolea itawafikia wakulima kwa wakati?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawiili ya nyongeza ya Mheshimiwa Arfi kwa ufupi tu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema, kilimo hiki kilikuwepo tangu zamani. Lakini bado tunaendelea kusisitiza na kuendelea kutoa elimu, unajua elimu haina mwisho. Hata sasa hivi siyo kwamba wale wakulima wa zamani walivyokuwa wanafanya, tukiwatazama kwamba ndivyo ilikuwa sahihi tu. Sasa hivi kuna utafiti unaendelea. Tunaendelea kuangalia jinsi gani waboreshe kilimo chao ndiyo maana nimetaja katika majibu ya msingi kwamba tunatakiwa tuangalie jinsi ya kuchanganya mazao mbalimbali yanayoweza ku-*fix nitrogen* na kurutubisha ardhi ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, kwa kifupi tu niseme kwamba tumejipanga vizuri sisi kama Serikali kuhakikisha kwamba mbolea inawafikia wakulima kwa wakati. Tumeangalia upungufu uliokuwepo katika mfumo uliotumika msimu uliopita na hayo ndiyo tunayafanyia kazi. Mheshimiwa Waziri alieleza kwa kirefu sana, nakumbuka katika hotuba hii. Lakini pia niseme kwamba pamoja na hayo, upo mpango mkubwa wa kujenga kiwanda chetu wenyewe hapa. Tuna utaratibu, tayari tumeshakubaliana na kampuni ya *Wentworth Resources Limited* ambayo itajenga Kiwanda cha mbolea Mtwara kitakachotumia gesi asilia ambayo inapatikana pale. Kiwanda kile kitatusaidia kwa sehemu kubwa kupunguza kuchelewa kwa mbolea kuagizwa kutoka nje. *(Makofi)*

Na. 322.

**Mkakati wa Kudhibiti Wizi wa Kazi za Wasanii Nchini**

**MHE. ESTER A. BULAYA** aliuliza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kuhusiana na wizi wa kazi za wasanii hapa nchini:-

Je, Serikali ina mkakati gani mpya katika kipindi cha miaka mitano ijayo katika kupambana na wizi wa kazi za wasanii nchini hasa baada ya ya mikakati ya awali kushindwa kutoa suluhisho?

Je, Serikali imefanya tathmini ili kubaini kiasi gani cha mapato kinapotea kwa mwaka kutokana na kazi za wasanii kuuzwa kinyemela?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (K.N.Y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto zilizojitokeza katika mpango wa awali wa kupambana na wizi wa kazi za wasanii, Serikali katika kipindi cha miaka mitano ijayo, imepanga kutekelza utaratibu wa wasambazaji wote wa kazi za wasanii kubandika *sticker* ya usalama *(security device)* ijulikanayo kama *Hakigram* kwenye kila nakala ya kazi itakayosambazwa ili kuhakikisha kuwa kazi za wasanii haziibiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utaratibu huu kila msambazaji ataingia mkataba na msanii kusambaza idadi fulani ya nakala na kupewa *sticker* za *Hakigram* ambazo zitabandikwa kwa kila nakala. Kwa maana hiyo, nakala za kazi ambazo hazina *sticker* zitatambuliwa kama nakala bandia na kuondolewa katika soko. *Hakigram* zitatolewa na Chama cha Hakimiliki cha Tanzania *(COSOTA)* na tayari muundo wa *Hakigram* hizo umeishatayarishwa. Aidha, naomba ijulikane kwamba wizi wa kazi za wasanii ni kosa la jinai na yeyote anayejihusisha na wizi huu atachukuliwa hatua za kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilifanya tathmini na kubaini kwamba ukubwa wa soko la kazi za wasanii kupitia soko la kanda za sauti na *CD* ulifikia nakala milioni 20 kwa mwaka. Hiyo inatokana na ukweli kwamba kanda zinazozalishwa nchini Tanzania zilikuwa zinauzwa katika nchi za jirani za Burundi, Kongo, Malawi, Rwanda na Zambia. Kwa maana hiyo, mauzo hayo hayakuwanufaisha wasanii wa Tanzania wenye hatimiliki na Serikali kwa ujumla kwa maana ya mapato. Utafiti huo pia ulibaini kwamba nakala nyingi kati ya hizo zilikuwa zinauzwa kinyemela na ni bandia. Kwa wakati huo bei ya kanda ya sauti ilikuwa ni shilingi 1000/=, kanda ya *video* shilingi 1500/= na *CD* shilingi 3000/= kwa kanda. Biashara hiyo ingeweza kuingiza shilingi bilioni 20 kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukomesha vitendo vya wizi wa kazi za wasanii, Serikali itashirikiana na nchi za *EAC* na *SADC* kupambana na wizi wa hatimiliki za kazi za wasanii wetu. *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu yale yale ambayo wasanii wameshachoka kuyasikia, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza:-

Kwanza kabisa kwa kuwa suala zima la usambazaji limeachiwa kwa watu binafsi maarufu kama Wadosi na wamekuwa wakiiba kwa kiasi kikubwa kazi za wasanii; sasa kwa nini Serikali isianzishe chombo kitakacho-*deal* na usambazaji wa kazi za wasanii kama wanavyofanya jirani zetu Uganda ili kudhibiti wizi wa kazi za wasanii na chombo hicho kishuke mpaka ngazi za Halmashauri zetu?

Pili, kwa sababu Serikali kwa muda mrefu imekosa *strategy* za ku-*penetrate* katika soko la Kimataifa kwa upande wa *music industry*, filamu, *comedy* na wasanii wengine na ukizingatia wasanii wetu hawana tofauti na wasanii ambao wameshapiga hatua kama akina Willy Smith, akina Dibanj, akina…

**MWENYEKITI:** Uliza swali, uliza swali! Naomba uulize swali Mheshimiwa!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Akina Genevieve na akina Ramsey. Kwa nini Serikali isianzishe vitengo maalum kwenye Balozi zetu nje ya nchi ili iweze ku-*promote* wasanii wetu na kusimamia mauzo ya kazi zao Kimataifa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (K.N.Y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Ester Bulaya hakusikia majibu yangu katika swali la msingi. Nilikuwa nimesema hivi, umeuliza ni mikakati gani mipya kutokana na ile ya zamani uliyokuwa unaijua.

Sasa mikakati ya zamani ilikuwa ni kujaribu ku-*patrol* kidogo na nini na kudhibiti. Lakini sasa tunasema kwa sababu ya uchache wa watendaji hili jambo limeonekana haliwezekani. Sasa kila msanii atakuwa na *stickers* zake na yule *distributing agency*, wewe msanii unakubaliana naye, unampa nakala zako labda 200/300 au 1000, unampa na *stickers* zako anabandika pale. *Another thing* ni kwamba katika jambo hili, sisi tunapokea kanda za *DVD* zinaletwa kutoka China na wapi

na wapi na wote tunanunua mitaani. Sasa *issue* ya *copyrights* ni *issue* ambayo ni kubwa kwa sababu *technology* yenyewe ya kuzalisha mikanda ni kitu chepesi. Unachukua tu picha ya Ester pale, unaiweka, una-*scan*, unanunua *CD* zako 500/600, unazi-*reproduce* nyumbani kwako, unatoka unaziuza. Kwa hiyo, *it's a difficult problem* na ni tatizo ambalo kusema kweli ni *worldwide*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi tunasema tutatumia *stickers* zile za *Hakigram* ambazo mwaka jana zimetengewa kama milioni 470 hivi kwa ajili ya mkakati wa kuanza lakini ni mkakati wa muda mrefu na katika utekelezaji huu tunatarajia wadau wote watahusika ili jambo lipate utekelezaji. Lakini mwisho wa yote ni sisi wenyewe wananchi, tunapokutana na *fake products* (bidhaa bandia) tujue kwamba ukizinunua, unamuumiza msanii ambaye ameifanyia kazi kwa bidii. *(Makofi)*

Mheshimwia Mwenyekiti, hili lingine la Serikali imekosa soko la ku-*penetrate*, mimi sidhani kama ni kweli. Wasanii wetu ukiwaangalia wapo kwenye *VH1,* wapo kwenye *DSTV* na kwa upande wetu sisi Afrika maana miziki yetu huwezi kutegemea utaipeleka China watu wakaruka mdundo, ni miziki yetu ya Kiswahili. Kwa hiyo, kwa sasa hivi Tanzania kuanzia sinema zetu mpaka miziki yetu iko *very popular* kwa Kanda ya *EAC* na *SADC* na ndiyo maana tumesema tutazungumza na nchi hizi ili kuhakikisha kwamba na wao wanatambua kwamba kuna kazi maalum ya kufanya ya ku-*protect copyright* za wasanii wetu hata katika nchi zao kwa sababu nao watu ambao...

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la Balozi nadhani kazi za *music promotion* ni ya wasanii wenyewe na *promoters* wao ambavyo ndivyo inavyofanywa *worldwide*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nimemaliza kujibu. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nakushukuru. Muda wa maswali umekwisha. Kabla ya matangazo, naomba niseme yafuatayo:-

Kwa mujibu wa Kanuni ya 63(3),(4) na (5), Mheshimiwa Tundu Lissu, wakati Mheshimiwa Waziri akijibu swali lako namba 313, umemtuhumu Waziri kwamba amesema uongo. Ninaomba utoe uthibitisho wa ukweli kuhusu suala hili na uthibitishe ukweli huo kwa kupeleka uthibitisho kwa Katibu wa Bunge kabla ya saa 5.00 asubuhi hii ya leo na kama utahisi ni vema, nitakuomba pia kama huna uthibitisho, ufute kauli yako. Baada ya agizo hilo, naomba nitoe matangazo yafuatayo:-

Tuna wageni wafuatao katika ukumbi wetu, tunao wageni wa Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ambao ni Ndugu Pamela David Mathayo, mke wa Mheshimiwa Waziri. Karibu sana.

Tunaye Ndugu Cleopatra Reena, ni mtoto wa Mheshimiwa Waziri, karibu. Tunaye Ndugu Jaji Upendo Msuya ambaye ni Jaji wa Mahakama Kuu, ni mjomba wake na Mheshimiwa Waziri, karibu Mheshimiwa. *(Makofi)*

Pia tuna Mheshimiwa Lawrence Kego Masha, Waziri wa zamani wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Karibu Mheshimiwa! *(Makofi)*

Tunaye ndugu Jemina Lukuvi, ni mke wa Mheshimiwa Waziri Lukuvi. Karibu mama! Ahsante, karibu sana. Tunaye ndugu Brown Lukuvi, ni mtoto wa Mheshimiwa Waziri Lukuvi na ndugu Aneticia Lukuvi, ni mtoto wake pia Mheshimiwa Waziri, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna watendaji wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi wakiongozwa na Dkt. Charles Nyamlunda, Katibu Mkuu, tunaomba wasimame popote walipo wote. Karibuni sana, karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunao wageni 18 wa Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ambao ni wafugaji kutoka Pwani, Morogoro, Kiteto na Bagamoyo.

Popote walipo wasimame, karibuni sana. Tunaye pia Bibi Naomi ambaye ni mke wa Mheshimwia Naibu Waziri. Karibu mama popote ulipo. Karibu sana. *(Makofi)*

Pia tuna wageni saba wa Mheshimiwa Sylvester Kasulumbayi, Waziri Kivuli wa Mandeleo ya Mifugo na Uvuvi, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tuna wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo, wanafunzi 40 na walimu wao wanne kutoka shule ya *Celestian Seminary* Dodoma. Karibuni popote mlipo! Karibuni sana. Pia tuna wanafunzi 16 na walimu watano kutoka shule ya msingi na chekechea ya *Lincolin Academy*. Karibuni wanafunzi na walimu pia na tuna wanafunzi 79 pamoja na walimu sita kutoka Shule ya Msingi Montesori Kiloleni, Ilemela Mwanza. Karibuni na poleni kwa safari popote mlipo. Karibuni sana. Tunao pia wanafunzi kumi wa Chuo cha Ustawi wa Jamii wakiongozwa na Ndugu Chrisant Mutatina. Karibuni. Haya, karibuni sana. *(Makofi)*

Tangazo la kazi, tangazo la kikao cha Kamati ya Bunge ya Miundombinu. Tafadhali naomba uwatangazie wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuwa kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo leo tarehe 27 saa 7.00 mchana katika ukumbi namba 231 jengo la utawala ghorofa ya pili. Tangazo limetolewa na Mwenyekiti, Mheshimiwa Peter Serukamba. Naomba mzingatie saa 7.00 mchana chumba namba 231, mfike bila kukosa. Asanteni sana.

Baada ya matangazo haya, naomba tuendelee. *(Makofi)*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mwongozo wa Spika!

**MWENYEKITI:** Mwongozo!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) ambayo naomba ninukuu; "Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge, na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadaye kadri atakavyoona inafaa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee.

**MWENYEKITI:** Endelea!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Kuna hoja hapa imeibuka mapema ndani ya Bunge letu wakati Mheshimiwa Tundu Lissu anauliza maswali ya nyongeza na kutoa ufafanuzi kuhusina na michango ambayo wananchi wetu wamekuwa wanachangishwa kwa ajili ya ujenzi wa shule mbalimbali hapa nchini. Sasa na ametakiwa kama ambavyo umeelekeza kwamba ikifika saa 5.00 asubuhi awasilishe maelezo yake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, naomba ukae, samahani, tafadhali naomba ukae.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Nitaomba lakini nimalize pia Mheshimiwa Mwenyekiti!

**MWENYEKITI:** Naomba ukae!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Nakaa, nitaomba nimalize!

**MWENYEKITI:** Tusibishane Mheshimiwa, wewe mwenyewe umeshakiri, nimeshatoa Mwongozo. Na kwa mujibu wa Kanuni, ukishatoa Mwongozo, hakuna tena suala lingine la Mwongozo juu ya Mwongozo. Kanuni ya 68(10), naomba noisome; "Uamuzi wa Spika, kuhusu suala lolote la utaratibu utakuwa ni wa mwisho."

Sasa kama Kanuni hizi tunazipinga, umetumia Kanuni na kuna Kanuni ambayo inamwagiza Spika akishatoa Mwongozo, wote tufuate Mwongozo huo. Nimemwagiza Mheshimiwa Tundu Lissu, saa 5.00 asubuhi ya leo, athibitishe *allegation* zake na kama hana uthibitisho, pia kuna *room*, afute kauli. Ni jambo la kiungwana. Naomba tuendelee. *(Makofi)*

**TAARIFA**

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa! Ni taarifa, siyo Mwongozo! Naomba kutoa Taarifa!

**MWENYEKITI:** Toa taarifa!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MWENYEKITI:** Toa taarifa!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Kanuni ya 68(8) naomba ninukuu; "Vile vile Mbunge yeyote anaweza kusimama mahala pake na kusema "Taarifa"'na kwa ruhusa ya Spika atatoa taarifa au ufafanuzi kwa Mbunge anayesema…

**MWENYEKITI:** Toa taarifa yako!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** ...Mbunge anayesema, ambapo Spika atatamka Mbunge...
**MWENYEKITI:** Toa taarifa yako!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Tundu Lissu, Mbunge wa Singida…

*(Hapa Wabunge fulani walisikika wakizungumza bila ridhaa ya kiti)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Ni taarifa yangu hii msinipangie kwamba nitoe taarifa kwa utaratibu gani!

**MWENYEKITI:** Toa taarifa Mheshimiwa Machali!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Wakae kimya kwanza pia Mheshimiwa Mwenyekiti!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, acha kujibizana na Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Sizungumzi na wao, naomba wakae kimya kwanza pia, nidhamu ni kwa wote. Naomba niendelee. Nidhamu ni kwa wote. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali, samahani naomba ukae kidogo. Mheshimiwa Moses Machali, umetaka kutoa taarifa, nimekuruhusu. Unajibishana na Wabunge…
*(Hapa Wabunge fulani walisikika wakizungumza bila ridhaa ya kiti)*

**MWENYEKITI:** Sikiliza, sikiliza, sikiliza! Nafikiri kwamba hasira hazitusaidii. Hasira hazitusaidii. Mheshimiwa Tundu Lissu kaa chini. Mheshimiwa Tundu Lissu kaa chini, sijakuruhusu, hapa siyo kilabu ya pombe, ni sehemu takatifu sana. Naomba mheshimu sana. Naomba tuheshimu sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Machali, kama ulikuwa na taarifa itoe taarifa yako, usisikilize maneno ya wengine. Toa taarifa, mimi nitakwambia taarifa yako inakwenda kwa nani, nitaifikisha. *(Makofi)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mbunge wa Singida Mheshimiwa Tundu Lissu ni Mbunge na shughuli za Bunge zinaendelea ndani ya Bunge letu, kwa hiyo, kitendo cha kumtaka Mheshimiwa Tundu Lissu awasilishe taarifa yake saa tano kwa maandishi, nadhani tutakuwa hatujamtendea haki. Kwa nini suala hili lisiweze kuahirishwa na

Mheshimiwa Tundu Lissu akawasilisha ushahidi wake itakapofika saa saba mchana. Kuna udharura gani wa Mheshimiwa Tundu Lissu kuweza kufanya hivyo kama siyo uonevu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mnisikilize.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(7) jambo hili lisilete jazba, siyo jambo kubwa, ni jambo dogo sana na halina sababu ya Waheshimiwa Wabunge hapa kupoteza muda na kutunishiana misuli. Kwanza Mheshimiwa Tundu Lissu mwenyewe ukichukua *Hansard* alitaka mwenyewe kuwasilisha sasa hivi. Nataka niwahakikishie Wabunge wakachukue *Hansard* kwa maneno aliyosema Tundu Lissu kwamba yupo tayari kuwasilisha ile barua sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama alivyosema ndugu yangu hapa Mheshimiwa Mbunge, kama Mheshimiwa Tundu Lissu na yupo hapa, hili siyo jambo la kufa na kupona, kama akiona saa tano haijamtosha atamuandikia Mheshimiwa Mwenyekiti, muda ambao unafaa atawasilisha ni jambo la heri tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nilikuwa nataka Mwongozo wako, jambo hili linajulikana, kama Mheshimiwa Mbunge pengine makabati yake amesahau funguo na karatasi ile haioni, atakuandikia wewe, utampa muda mwingine, haina sababu ya kupigizana kelele. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri naomba nikushukuru sana, kwa sababu Mheshimiwa Moses Machali unapomsaidia mtu pia uangalie, usipende tu kujiweka kifua mbele. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Tundu Lissu amesema mwenyewe kwamba anaweza kuthibitisha sasa hivi, hata tukifuata *Hansard.* Mimi nilichofanya hapa ni kwamba yeye amesema sasa hivi, kwa upendeleo nimempa karibu saa moja na nusu ili aweze kuandika vizuri taarifa yake, ailete hapa. Yeye ametaka kuthibitisha papo kwa papo, mimi nimempendelea kwa kumpa saa moja na nusu. Naomba usiwe unaweka kifua mbele mambo mengine. Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge tuendelee.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kuahirisha Bunge kujadili jambo la dharura…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge kaa chini. Kanuni inayoagiza tuahirishe Bunge kwa ajili ya hoja ya dharura ni pale nchi yetu ipo vitani, lakini hatupo vitani.

*(Hapa Wabunge fulani walisikika wakizungumza bila ridhaa ya kiti)*

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti ni jambo la dharura.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge usije ukanisababisha nikamwita *Serjeant-at-Arm* akutoe nje, naomba ukae chini.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala la dharura kwa maslahi ya Taifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge kaa chini.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja ya dharura kulingana na Kanuni za Bunge.

**MWENYEKITI:** *Serjeant-at-Arm please* naomba umtoe nje Mheshimiwa Wenje.

**WABUNGE FULANI:** Taarifa Mheshimiwa Mwenyekiti, msitutishee…

**WABUNGE FULANI:** Msitutishe.

*(Hapa Mheshimiwa Ezekia Wenje alitolewa ndani ya Ukumbi wa Bunge na Serjeant-at-Arm)*

**WABUNGE FULANI:** Tokeni, atoke…

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuendelee, Katibu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2011/2012
### Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji inayohusu Wizara, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Matumizi ya fedha ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2011/2012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine kuliongoza Taifa letu kwa kipindi cha pili cha Serikali ya Awamu ya Nne. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kuchaguliwa kwao ni kielelezo cha imani tuliyonayo Watanzania kwa uongozi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Jimbo la Katavi, kwa kuteuliwa tena na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na baadaye kuthibitishwa kwa kura nyingi na Bunge lako Tukufu kushika wadhifa huo mkubwa. Kuteuliwa kwake tena kunaonyesha imani kubwa aliyonayo Mheshimiwa Rais juu ya uwezo na utendaji wake wa kazi katika kusimamia majukumu ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie pia nafasi hii kumpongeza Spika, Mheshimiwa Anne Semamba Makinda, Mbunge wa Jimbo la Njombe Kusini, pamoja na Naibu Spika, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Jimbo la Kongwa, kwa kuchaguliwa kwenu kwa kura nyingi kuliongoza Bunge hili Tukufu. Ushindi wao ni kielelezo cha imani kubwa waliyonayo Waheshimiwa Wabunge katika kusimamia shughuli za Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri samahani, Waheshimiwa Wabunge naomba *order in the house,* tumsikilize Waziri ili tuweze kuwa wazuri katika kuchangia hotuba yake. Tafadhali naomba ukimya.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawapongeza Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Peramiho; Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Jimbo la Kibakwe na Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba, Mbunge wa Jimbo la Dole kwa kuchaguliwa kwao kuwa Wenyeviti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kuteuliwa kwao na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara mbalimbali. Pia nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa na walioteuliwa kuingia katika Bunge hili Tukufu. Napenda kuwashukuru wapiga kura na wananchi wa Jimbo la Same Magharibi kwa kunichagua kuwa Mbunge wao kwa kura nyingi sana na hivyo kuendelea kunipa heshima kubwa ya kuliwakilisha Jimbo letu na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Ninawaahidi kupitia Bunge lako Tukufu kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa juhudi kubwa na kushirikiana nao katika kuleta maendeleo katika Jimbo letu na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Profesa David Homeli Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi, kwa ushirikiano wao mkubwa waliotupatia katika maandalizi ya Bajeti hii, ambapo ushauri na maoni yao yamezingatiwa. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu itazingatia ushauri, mapendekezo na maoni yaliyotolewa na Kamati na yale yatakayotolewa na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kwa hotuba yake nzuri yenye kutoa malengo ya Serikali na mwelekeo wa utendaji wa sekta mbalimbali pamoja na kazi za Serikali kwa mwaka 2011/2012. *(Makofi)*

Aidha, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, kwa hotuba yake kuhusu hali ya uchumi wa nchi yetu na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2011/2012. Pia nawapongeza Mawaziri wote walionitangulia kwa hotuba zao ambazo zimeainisha maeneo mbalimbali tunayoshirikiana katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi nchini. Vilevile nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao kuhusu masuala ya maendeleo ya sekta za mifugo na uvuvi kupitia hotuba zilizotangulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali halisi ya sekta za mifugo na uvuvi nchini, sekta za mifugo na uvuvi zina umuhimu mkubwa katika kuwapatia wananchi lishe bora, ajira na kipato hivyo huchangia katika kumuondolea mwananchi umaskini. Kulingana na takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu mwaka 2011, idadi ya mifugo nchini inafikia ng'ombe milioni 21.3, mbuzi milioni 15.2 na kondoo milioni 6.4. Pia wapo kuku wa asili milioni 35 na wa kisasa milioni 23 na nguruwe milioni 1.9. *(Makofi)*

Aidha, viwango vya ulaji wa mazao ya mifugo kwa sasa ni wastani wa kilo 12 za nyama, lita 44 za maziwa na mayai 75 kwa mtu kwa mwaka. Ulaji huu bado ni mdogo ikilinganishwa na viwango vya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(FAO)* vya kilo 50 za nyama, lita 200 za maziwa na mayai 300 kwa mtu kwa mwaka. Katika mwaka 2010, sekta ya mifugo ilikua kwa asilimia 3.4 ikilinganishwa na asilimia 2.3 mwaka 2009 na kuchangia asilimia 3.8 katika Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 4.0 mwaka 2009. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inayo maeneo mengi ya uvuvi, ikiwa ni pamoja na kilometa za mraba 64,000 za ukanda wa bahari, kilometa za mraba 223,000 za Bahari Kuu, maziwa makuu ya Victoria (kilometa za mraba 35,088), Tanganyika (kilometa za mraba 13,489) na Nyasa (kilometa za mraba 5,700). Pia yapo maziwa ya kati na madogo 29 na mabwawa 19,039. Kutokana na utafiti uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi nchini *(TAFIRI)* mwaka 2009, kiasi cha samaki kilichopo katika maziwa makubwa ni takriban tani 2,914,296 (Ziwa Victoria tani 2,451,296, Ziwa Tanganyika tani 295,000 na Ziwa Nyasa tani 168,000). Katika mwaka 2010, sekta ya uvuvi ilikua kwa asilimia 1.5 ikilinganishwa na asilimia 2.7 mwaka 2009 na kuchangia asilimia 1.4 katika Pato la Taifa kama ilivyokuwa mwaka 2009. Aidha, ulaji wa mazao ya uvuvi kwa mtu kwa mwaka ni kilo 8.0 ikilinganishwa na kilo 10.7 zinazopendekezwa na *FAO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta za mifugo na uvuvi kwa kipindi cha mwaka 2010/2011 zimeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuainisha, kupima, kumilikisha na kuendeleza maeneo ya ufugaji endelevu ili kudhibiti kuhamahama, kupunguza migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, kupunguza uharibifu wa mazingira na kuzuia kuenea kwa magonjwa ya mifugo, kuwa na wataalam wa kutosha kukidhi mahitaji ya sekta za mifugo na uvuvi, kuongeza uwekezaji katika sekta za mifugo na uvuvi ili kuongeza uzalishaji, tija na thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi, kudhibiti magonjwa mbalimbali ya mifugo, hususan ya milipuko, kupatikana kwa mikopo yenye masharti nafuu kwa ufugaji na uvuvi na kupatikana kwa pembejeo na zana za gharama nafuu kwa ajili ya ufugaji na uvuvi.

Pia kupatikana kwa soko la uhakika la mazao ya mifugo na uvuvi, kudhibiti uvuvi na biashara haramu ya samaki na mazao ya uvuvi, kuwa na rasilimali fedha ya kutosha kukidhi mahitaji ya sekta za mifugo na uvuvi na upatikanaji wa elimu na teknolojia pamoja na matumizi ya teknolojia za kisasa kwa wafugaji na wavuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu ya sekta za mifugo na uvuvi, Wizara imezingatia maelekezo yaliyomo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010. Ilani inatambua mchango mkubwa unaoweza kutolewa na sekta hizi katika kuwapunguzia wananchi umaskini na kuongeza Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili sekta ya mifugo iweze kutoa mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa, Serikali imeelekezwa kutekeleza yafuatayo:-

Kwanza mapinduzi ya ufugaji, Serikali iandae programu kabambe ya kuendeleza sekta ya mifugo na ufugaji. Programu hiyo ijumuishe pamoja na mambo mengine masuala ya uendelezaji wa maeneo ya malisho, kuchimba na kujenga malambo, mabwawa, majosho na huduma za ugani ili hatimaye wafugaji waondokane na ufugaji wa kuhamahama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya mifugo imekamilisha rasimu ya programu ya kuendeleza sekta ya mifugo ambayo itatekelezwa kwa kipindi cha mwaka 2011/2012 hadi 2015/2016. Programu hii imeainisha pamoja na mambo mengine masuala ya uendelezaji wa maeneo ya malisho, kuchimba na kujenga malambo, mabwawa, majosho na huduma za ugani ili hatimaye wafugaji waondokane na ufugaji wa kuhamahama. Aidha, programu imeainisha maeneo ya kipaumbele yatakayotekelezwa kwa kila mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Kilimo itakayoanzishwa iwe pia Benki ya Mifugo ili iweze kutoa mikopo kwa wasomi wenye nia ya kufuga na kuwawezesha kuingia kwa wingi katika ufugaji wa kisasa. Wizara inaendelea kuhamasisha wafugaji hususan wasomi kutumia uwepo wa dirisha dogo katika Benki ya Taifa ya Rasilimali kukopa fedha kwa ajili ya kuendeleza ufugaji wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuelimisha wafugaji kuhusu umuhimu wa uwiano kati ya idadi ya mifugo na eneo; Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri imeendelea kuelimisha wafugaji kuhusu kutekeleza Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo Na. 13 ya mwaka 2010 ambayo pamoja na mambo mengine, inawataka wafugaji kufuga mifugo kulingana na uwezo wa ardhi, kutunza malambo na vyanzo vya maji, kuendeleza na kuhifadhi malisho na kutenga maeneo ya akiba kwa ajili ya kiangazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali isimamie kwa ufanisi mkubwa mradi wa kopa ng'ombe/mbuzi, lipa ng'ombe/mbuzi kama hatua ya kueneza ufugaji wa kisasa wenye tija kubwa; Wizara imewezesha upatikanaji wa mitamba bora ya maziwa 10,470 kupitia Mashamba ya Kuzalisha Mitamba ya Kitulo, Mabuki, Nangaramo, Ngerengere na *Sao Hill* pamoja na ranchi za *NARCO* na mipango ya kopa ng'ombe lipa ng'ombe. Vilevile, mbuzi wa maziwa 3,216 wamesambazwa kupitia mpango wa kopa mbuzi lipa mbuzi. *(Makofi)*

Pili, kuendeleza elimu kwa wafugaji ili wajue kuwa mifugo waliyonayo ni mali inayoweza kuvunwa katika umri na uzito muafaka unaokidhi mahitaji ya soko ili kuwaondolea umaskini wao badala ya kuridhika na wingi wa mifugo iliyo duni na maisha ya kuhamahama; Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri na Asasi mbalimbali kama vile *Land O' Lakes, Heifer Project Tanzania (HPT), World Vision* na *Care Tanzania* imetoa mafunzo kwa wafugaji 8,796 kuhusu mbinu za ufugaji bora wa mifugo. Aidha, jitihada za makusudi za kuchochea uvunaji na uuzaji wa mifugo na mazao yake katika maeneo ya wafugaji zimefanyika kwa kuwekeza katika ujenzi wa machinjio ya kisasa Simanjiro na Monduli. Pia kiwanda cha kusindika maziwa kimejengwa Simanjiro kwa lengo hilo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa mitamba upanuliwe kwa kiwango kikubwa kwa Serikali kuvutia na kuwezesha sekta binafsi katika uzalishaji na ufugaji wa kisasa, Wizara imeendelea kuboresha mashamba ya kuzalisha mifugo ili kuongeza upatikanaji wa mitamba

ambapo ng'ombe wazazi 77 wamenunuliwa kwa ajili ya mashamba hayo. Aidha, mitamba 712 ilizalishwa na kusambazwa kwa wafugaji. Vilevile Serikali imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa mitamba kwa kuwapatia mafunzo ya mbinu za ufugaji bora na ziara za mafunzo ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufufua na kujenga majosho na malambo mapya kwa ajili ya mifugo na kuhimiza uogeshaji endelevu, Serikali kupitia *DADPs* na *DASIP* imekarabati majosho 30 na malambo 20 na kujenga majosho 37 na malambo 62. Aidha, ili kuhimiza uogeshaji endelevu, Serikali ilinunua lita 109,389 za dawa za kuogesha mifugo kwa kutoa ruzuku ya shilingi bilioni 1.82 na kuzisambaza katika Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha utafiti wa mifugo kwa kuboresha na kuhifadhi kosaafu za mifugo ya asili ili kuongeza uzalishaji endelevu, katika utekelezaji Wizara imeimarisha utafiti wa mifugo wenye lengo la kuboresha na kuhifadhi kosaafu za mifugo ya asili kwa kukusanya na kuchambua takwimu mbalimbali za maendeleo ya ukuaji na uzalishaji kwa mbari za mifugo ya asili kwa mifugo ifuatayo:-

(i) Ng'ombe 44 wa aina ya Ufipa, 3O aina ya *Ankole* na 20 aina ya *Singida White*;

(ii) Mbuzi 60 aina ya *Pare White,* 30 *Sonjo Red,* 93 *Gogo White* na 125 Newala na Kondoo 100 aina ya *Red Maasai*; na

(iii) Kosaafu za mbari za kuku 50 wa Kawaida, 35 Sasamala, 45 Kishingo, 41 Kisunzu, 39 Bukini, 39 Kuchi, 25 Mtewa, 26 Kuza, 49 Sukuma, 41 Msumbiji na 26 Njachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha huduma za ugani na mafunzo ya watalaam na wafugaji, Wizara imeendelea kuimarisha huduma za ugani na mafunzo ya watalaam na wafugaji kwa kutekeleza yafuatayo:-

Kwanza kukarabati na kuvipatia vitendea kazi vyuo sita vya mafunzo ya mifugo ambapo, kompyuta 12, basi moja, trekta tatu na zana zake, madawati 55, vitanda na magodoro 68 vimenunuliwa na kukarabati madarasa mawili, mabweni matano na bwalo moja la chakula;

Pili, kutoa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ambapo wakufunzi 24 walipata mafunzo ya mbinu za ufundishaji na watano wanaendelea na mafunzo ya shahada ya uzamili;

Tatu, kutoa mafunzo kwa wagani wa mifugo watarajali 1,498 ambapo, 613 wamehitimu mafunzo mwaka 2010/2011;

Nne, kutoa mafunzo kwa wataalam 32 kutoka Halmashauri za Kanda ya Kati mikoa ya Dodoma na Singida kuhusu upangaji wa mipango shirikishi ya ugani na mbinu ya shamba darasa; na

Tano, kuhuisha mitaala miwili ya mafunzo ya mifugo kuwa mtaala mmoja kwa ajili ya stashahada mpya ya uzalishaji na afya ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza na kuimarisha vituo vya uzalishaji mbegu bora za mifugo na kuhimiza matumizi ya mbegu hizo, Wizara imeendelea kuimarisha vituo vya uzalishaji mbegu bora za mifugo na huduma za uhimilishaji kwa kuimarisha Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji *(NAIC Usa River)* na vituo vitano vya Kanda. Aidha, vituo vipya vya Kanda za Kusini (Lindi) na Nyanda za Juu Kusini (Mbeya) vimejengwa. Kutokana na juhudi hizo, uhimilishaji umeongezeka kutoka ng'ombe 73,900 mwaka 2009/2010 hadi 76,800 mwaka 2010/2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha huduma za afya ya mifugo kwa kudhibiti magonjwa ya mifugo hasa ya milipuko na uanzishwaji wa maeneo huru kwa magonjwa ya mifugo, utekelezaji wa Wizara imeendelea kuimarisha huduma za afya ya mifugo na udhibiti wa magonjwa ya milipuko kwa kuchanja ng'ombe milioni 7.2 dhidi ya ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe

*(CBPP);* kuendelea kutekeleza mkakati wa kudhibiti ugonjwa wa miguu na midomo; kushirikiana na Halmashauri za Mikoa ya Mbeya, Iringa na Dar es Salaam katika kudhibiti Homa ya Nguruwe ambapo dawa za kupulizia lita 400 na mabomba sita vimenunuliwa na kupelekwa kwenye Halmashauri zilizoathirika na mkakati wa kudhibiti mafua makali ya ndege umeendelea kutekelezwa ambapo mpango wa tahadhari na udhibiti umeandaliwa. Hata hivyo, ugonjwa haujaingia nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhimiza wafugaji kutekeleza kanuni za ufugaji bora na kuingia katika ufugaji endelevu wa kisasa na kibiashara unaozingatia hifadhi ya mazingira, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri na wadau wengine imeendelea kuhamasisha wafugaji kufuga kisasa kwa kutekeleza yafuatayo:-

Kwanza kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu kanuni za ufugaji bora, kutekeleza Sheria na Kanuni mbalimbali zinazosimamia sekta ya mifugo, kutekeleza mpango wa kuendeleza malisho ambapo sekta binafsi imewekeza katika uzalishaji wa malisho bora na kuzalisha marobota 509,980 ya hei, kuboresha kosaafu za mifugo kwa njia ya uhimilishaji na matumizi ya mbegu bora, kujenga na kukarabati miundombinu kwa ajili ya mifugo kupitia miradi ya *DADPs* na *DASIP,* kudhibiti magonjwa ya mifugo kwa kutoa chanjo na kuogesha mifugo na kuhamasisha unenepeshaji wa ng'ombe na ujenzi wa machinjio za kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuhamasisha uimarishaji wa vikundi vya wafugaji ambapo jumla ya vikundi 1,728 vya wafugaji vimeundwa. Lengo ni kuwa na vikundi ambavyo vinaweza kusajiliwa na hivyo kuwa na uwezo wa kupata mikopo, kuwa na nguvu kwenye soko kuhusu bei ya mazao yao na kupata elimu ya ufugaji bora na wa kibiashara kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI imehamasisha Halmashauri 105 na vyama vya kitaaluma vya *Tanzania Veterinary Association (TVA), Tanzania Veterinary Para-proffesional Association (TAVEPA)* na *Tanzania Society of Animal Production (TSAP)* juu ya ushirikishaji wa sekta binafsi katika kutoa huduma mbalimbali za mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sekta ya uvuvi, Ilani imeelekeza sekta hii kuwa ya kisasa zaidi na iweze kuchangia mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa. Hivyo Serikali imeelekezwa kutekeleza yafuatayo:-

Wizara ianzishe na kuendesha vyuo vyake vya uvuvi ili iweze kuandaa wataalam wengi wa sekta ya uvuvi kukidhi mahitaji yote yanayotakiwa kwa ajili ya kuboresha uvuvi nchini. Wizara imeendelea kuimarisha Vyuo vyake viwili vya Uvuvi vya Nyegezi na Mbegani kwa kukarabati, kujenga miundombinu, kuongeza vifaa vya mafunzo na wakufunzi ambapo uwezo wa vyuo hivyo wa kuchukua wanafunzi umeongezeka kutoka wanafunzi 240 mwaka 2007/2008 hadi 500 mwaka 2010/2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuweka ulinzi madhubuti wa bahari zetu dhidi ya wavuvi haramu ikiwa ni pamoja na kukamata vyombo vyao vya uvuvi na kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria. Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi katika bahari na maeneo mengine ya uvuvi kwa kufanya yafuatayo:-

Kwanza, kufanya doria ya siku-kazi 4,962 kwenye maji, angani na nchi kavu, pili, kufanya mikutano ya wadau wa sekta ya uvuvi kuhusu udhibiti wa uvuvi na biashara haramu, tatu, kutoa elimu kwa wadau 193 kwa njia ya mikutano kuhusu elimu ya athari za uvuvi wa mabomu na kuhamasisha ushirikiano baina ya wadau wa sekta ya uvuvi katika kudhibiti uvuvi na biashara haramu ya uvuvi, nne, kununua boti za doria 16 na kuzigawa katika Halmashauri za Mkinga, Bagamoyo, Mkuranga, Pangani na Lindi, Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu, vituo vya doria vya Tanga, Dar es Salaam, Mafia na Mtwara; Idara ya Misitu na tano, kuandaa na kurusha hewani vipindi vya redio 26 na vya luninga sita kuhusu usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuandaa na kutekeleza programu yenye malengo yanayopimika mwaka hadi mwaka kuhusu haja ya kuleta mapinduzi ya uvuvi yanayotumia zana na maarifa ya kisasa. Wizara kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya uvuvi imekamilisha rasimu ya programu ya kuendeleza sekta ya uvuvi ambayo itatekelezwa kwa kipindi cha mwaka 2011/2012 hadi 2015/2016.

Programu hii, imeainisha pamoja na mambo mengine masuala ya uendelezaji wa uvuvi na ukuzaji wa viumbe kwenye maji, uhifadhi wa rasilimali, matumizi endelevu ya rasilimali pamoja na uhifadhi wa mazingira. Aidha, programu itahusisha uimarishaji wa huduma za ugani, utafiti, mafunzo na upatikanaji wa takwimu sahihi za rasilimali ya uvuvi. Pia programu imeainisha maeneo ya kipaumbele yatakayotekelezwa kwa kila mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuimarisha ushirikishwaji wa jamii na wadau katika ulinzi, usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri imeendelea kuwashirikisha wadau katika ulinzi, usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali ya uvuvi kwa kuanzisha vikundi vipya 23 vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi *(BMUs)* katika Halmashauri za Kinondoni, Temeke na Mkuranga. Aidha, vikundi 680 katika maeneo mbalimbali nchini vimeimarishwa kwa kuvipatia mafunzo, vitendea kazi na kuviwezesha kuanzisha miradi midogo ya uzalishaji ili viwe endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuimarisha miundombinu ya uvuvi kwa kujenga mialo, masoko ya kisasa, vituo vya kutotolea vifaranga vya samaki na maabara, Wizara imeendelea kuimarisha miundombinu ya uvuvi kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kukarabati mialo 25 ya kushushia na kupokelea samaki katika ukanda wa Ziwa Victoria na kujenga mialo mitatu katika ukanda wa Pwani na kuainisha maeneo ya kujenga mialo minne katika ukanda wa Ziwa Tanganyika;

(ii) Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri, imeendelea kuratibu miundombinu ya masoko makubwa ya samaki ya Feri (Dar es Salaam) na Kirumba (Mwanza) pamoja na masoko mengine ya samaki; na

(iii) Kuimarisha kituo cha kutotoleshea vifaranga cha Mbegani kwa kujenga matanki matatu na mabwawa manne ya kuzalisha na kufugia samaki wa maji bahari. Vilevile kwa upande wa maji baridi, Kituo cha Ufugaji wa Samaki cha Mtama kimeimarishwa kwa kujenga matanki matano ya kuhifadhia vifaranga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuboresha mazao ya uvuvi kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi, Wizara kupitia Maabara ya Taifa ya Uthibiti wa Ubora wa Samaki Nyegezi - Mwanza imeendelea kuhakiki usalama na ubora wa mazao ya uvuvi kwa ajili ya soko la ndani na nje kwa kufanya uchunguzi kwa jumla ya sampuli 1,727 ili kuhakiki ubora na usalama wake. Aidha, kaguzi 2,486 zilifanyika ili kuhakiki ubora na usalama wa mazao ya uvuvi kabla ya kusafirishwa nje ya nchi. Vilevile Wizara ilifanya kaguzi 620 ili kuhakiki ubora wa viwanda 28 vya kuchakata mazao ya uvuvi na maghala 39 ya kuhifadhi mazao ya uvuvi katika kanda za Ziwa Victoria na Pwani. Mazao ya uvuvi, viwanda na maghala yaliyokaguliwa yalionekana kukidhi viwango vya ubora na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kujenga mazingira ya kuvutia uwekezaji katika sekta ya uvuvi hususan ujenzi wa viwanda vya samaki, Serikali imeendelea kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji katika sekta ya uvuvi na viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuendelea kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye zana za uvuvi ikiwa ni pamoja na injini za kupachika na vifungashio. Katika mwaka 2011/2012, kodi hiyo pia imeondolewa kwenye nyuzi za kutengenezea nyavu *(nylon fishing twines)* na kufuta Kodi ya Zuio kwa usafirishaji wa samaki nje ya nchi kwa kutumia ndege za nje;

(ii) Kuendelea kutoza ushuru wa samaki wanaoingizwa kutoka nchi za nje kwa dola za Kimarekani 0.25 kwa kilo;

(iii) Kuondoa mrabaha kwenye mazao yanayokuzwa kwenye maji, ambayo ni mwani na kambamiti;

(iv) Kuendelea kuboresha udhibiti wa ubora na usalama wa mazao ya uvuvi pamoja na miundombinu;

(v) Kupitia upya Sera na Mikakati ya Uvuvi ya mwaka 1997 kwa lengo la kuihuisha ili iweze kukidhi mahitaji ya sasa na ya wakati ujao;

(vi) Kuainisha fursa za uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi kulingana na mazingira ya sasa; na

(vii) Kutoa mafunzo kwa wadau 1,935 kutoka Halmashauri 16 za mwambao wa pwani kuhusu mwenendo na mahitaji ya soko la Kimataifa la mazao ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuhamasisha wawekezaji wa ndani na wa nje kuwekeza katika uvuvi kwenye Bahari Kuu, Wizara imeendelea kuhamasisha wawekezaji wa ndani na wa nje kuwekeza katika uvuvi kwenye Bahari Kuu kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuwezesha Mamlaka ya Usimamizi wa Uvuvi katika Bahari Kuu kufanya kazi zake kwa lengo la kusimamia uvuvi katika Bahari Kuu;

(ii) Kuweka vifaa vya kuvutia samaki *(Fish Aggregating Devices – FADs)* kwenye Ukanda wa Uchumi wa Bahari;

(iii) Kujenga kituo cha hali ya bahari *(Satellite Receiving Station)* katika ofisi za TAFIRI - Kunduchi cha kubaini maeneo yenye samaki wengi katika tabaka la juu la maji kwenye Bahari ya Kitaifa *(Territorial Sea)* na Ukanda wa Uchumi wa Bahari;

(iv) Kufunga kifaa cha kufuatilia mienendo ya meli za uvuvi *(Vessel Monitoring System)* katika bahari kwa ajili ya usalama wa meli na kudhibiti uvuvi haramu; na

(v) Kufanya mikutano mbalimbali na wawekezaji wa ndani na nje kuhusu kuwekeza katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuimarisha na kuendeleza uanzishwaji wa maeneo tengefu kwenye maziwa makuu hususan Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa sekta, inaendelea na taratibu za kurekebisha Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu *(Marine Parks and Reserves Act)* Na. 29 ya mwaka 1994 ili kuingiza kipengele cha kuanzisha maeneo tengefu kwenye maji baridi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuhamasisha uimarishaji na uanzishaji wa vikundi vya ushirika wa wavuvi na wafugaji wa samaki, Wizara imeendelea kuhamasisha wananchi kuanzisha vikundi vya ushirika wa wavuvi na wafugaji wa samaki kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuwezesha vikundi 20 vyenye wanachama 267 (wanaume 151 na wanawake 116) wa jamii za pwani kubuni na kutekeleza miradi 20 ya kiuchumi yenye thamani ya shilingi milioni 336.9;

(ii) Kuwezesha uanzishwaji wa vikundi 71 vya ufugaji wa samaki, unenepeshaji wa kaa, ukuzaji wa chaza wa lulu na ukulima wa mwani katika mwambao wa pwani; na

(iii) Kuhamasisha wananchi wa mwambao wa pwani kuanzisha Benki za Wananchi Vijijini katika Wilaya za Kilwa, Mafia na Rufiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuimarisha usimamizi wa mazingira katika maeneo ya uvuvi, ukuzaji wa viumbe kwenye maji na maeneo tengefu, Wizara imeendelea kuimarisha

usimamizi wa mazingira katika maeneo ya uvuvi, ukuzaji wa viumbe kwenye maji na maeneo tengefu kama ifuatavyo:-

(i) Kuandaa Mpango wa Jumla wa Usimamizi *(General Management Plan)* kwa ajili ya Hifadhi ya Bahari ya Silikanti - Tanga;

(ii) Kupitia mpango wa jumla wa usimamizi wa Hifadhi za Bahari za Mafia na Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma; na

(iii) Kushirikiana na wadau kufanya doria za siku-kazi 3,894 kudhibiti uvuvi haramu na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuhimiza shughuli mbadala za kiuchumi kwa jamii za wavuvi ili kupunguza nguvu ya uvuvi kwenye maji ya asili na maeneo tengefu, Wizara imezijengea uwezo jamii zilizopo katika maeneo ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu kwa kuanzisha miradi sita kuhusu kilimo cha mwani, ukuzaji wa lulu, ufugaji wa kaa, ufugaji wa kuku, utengenezaji wa batiki na shughuli za uongozaji watalii. Aidha, kupitia Mradi wa *MACEMP*, miradi 20 ya kiuchumi yenye thamani ya shilingi milioni 336.9 imeanzishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkutano wa wadau wa sekta ya mifugo nchini ulifanyika mjini Dodoma tarehe 24 na 25 Januari, 2011 na ulishirikisha wadau 300. Mkutano huo ulitoa maoni na michango mbalimbali iliyotumika kuboresha rasimu ya mwisho ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Mifugo Nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkutano wa wadau wa sekta ya uvuvi nchini ulifanyika mjini Dodoma tarehe 26 hadi 28 Januari, 2011. Mkutano huu uliwashirikisha wadau 270 na uliweka mikakati ya kuimarisha usimamizi, uhifadhi, ulinzi na uendelezaji wa rasilimali za uvuvi na uboreshaji wa ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali. Aidha, mkutano huo ulitoa maoni na michango iliyowezesha kuboresha rasimu ya mwisho ya programu ya kuendeleza sekta ya uvuvi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ukame mkali uliojitokeza mwaka 2008/2009 katika mikoa wa Kaskazini mwa nchi yetu, Serikali ilifanya tathmini kubaini athari zilizotokana na ukame huo. Tathmini hiyo ilionyesha kuwa baadhi ya wafugaji walipoteza mifugo yao yote katika mkoa wa Arusha na hasa katika Wilaya za Longido, Monduli na Ngorongoro. Serikali kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu akihitimisha hotuba yake hapa Bungeni tarehe 1 Julai, 2011, iliahidi kutoa kifuta machozi kwa kaya 4,336 zilizopoteza mifugo yote katika Wilaya hizo ambapo kila kaya itapatiwa ng'ombe watano ikiwa ni mitamba minne na dume moja wenye umri wa miaka miwili na dume mmoja wa miaka mitatu. Jumla ya ng'ombe 21,680 kama mbegu wanatarajiwa kununuliwa na zoezi hili litagharimu shilingi bilioni 8.7 ambazo zimetengwa chini ya Kitengo cha Maafa, Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la kuwakusanya na kuwasambaza ng'ombe watakaonunuliwa litafanywa na wananchi wenyewe watakaochaguliwa kutoka maeneo hayo. Inashauriwa ng'ombe hao wapatikane kutoka wilaya husika na wilaya jirani zenye mazingira yanayowiana na hali iliyopo katika maeneo yaliyoathirika. Aidha, Wizara yangu itashirikiana na Halmashauri husika na wadau wengine kuhakikisha kuwa zoezi hili linatekelezwa kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Wizara ilitarajia kukusanya kiasi cha shilingi 13,633,400,000.00. Kati ya hizo shilingi 3,528,502,000.00 (26%) ni kutoka sekta ya mifugo na shilingi 10,104,898,000.00 (74%) ni kutoka sekta ya uvuvi. Hadi mwezi Juni, 2011 jumla ya shilingi 13,721,094,895.36 zimekusanywa ikiwa ni asilimia 100.6 ya lengo la makusanyo. Katika mwaka 2011/2012, Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 19,635,527,000.00. Kati ya hizo shilingi 8,248,525,000.00 zitatoka kwenye Sekta ya Mifugo na shilingi 11,387,002,000.00 zitatoka kwenye Sekta ya Uvuvi. *(Makofi)*

Wizara ilitengewa jumla ya shilingi 62,233,483,080; kati ya hizo shilingi 15,074,016,887 kwa ajili ya mishahara ya watumishi *(PE);* shilingi 20,912,414,193 kwa ajili ya matumizi mengine *(OC);* na shilingi

25,347,052,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya hizo, shilingi 8,717,387,000 zilikuwa fedha za ndani na shilingi 16,629,665,000 ni fedha za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Juni, 2011, jumla ya shilingi 31,576,111,004.44 zimetolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, sawa na asilimia 85.6. Kati ya hizo, shilingi 15,974,016,887.00 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 15,602,094,117.44 ni kwa ajili ya matumizi mengine *(OC).* Kati ya fedha hizo, jumla ya shilingi 31,561,010,270 (99.9%) zimetumika. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya shilingi 14,220,033,650 (56.1%) zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya hizo fedha za ndani ni shilingi 1,689,897,497 na shilingi 12,530,136,153 ni za nje. Kati ya fedha hizo, jumla ya shilingi 14,201,545,970 (99.87%) zimetumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sera ya Taifa ya Mifugo (2006), Wizara imeendelea kusambaza na kutoa elimu kwa wadau kuhusu Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006. Jumla ya nakala 7,500 za sera hii zimesambazwa kwa wadau na elimu kuhusu sera hiyo imeendelea kutolewa kupitia matukio mbalimbali ya Kitaifa yakiwemo Sikukuu ya Wakulima Nanenane, Wiki ya Uhamasishaji Unywaji wa Maziwa, Wiki ya Utumishi wa Umma pamoja na mikutano mbalimbali ya kitaaluma na ya wadau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo nchini umepitishwa na Serikali mwezi Machi, 2011. Taratibu za kutafsiri na kuchapisha mkakati huo katika lugha ya Kiswahili zinaendelea ambapo nakala 5,000 zitasambazwa kwa wadau katika mwaka wa fedha 2011/2012 kwa ajili ya utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Taifa ya Uvuvi ya mwaka 1997 katika mwaka 2010/2011, Wizara imefanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Uvuvi na mkakati wake wa mwaka 1997 ambapo rasimu ya Sera ya Taifa ya Uvuvi imekamilika. Vilevile rasimu ya mkakati wa kutekeleza sera hiyo inaandaliwa ambao utakamilishwa katika mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa sekta, imeendelea kuandaa na kutoa mapendekezo ya marekebisho ya sheria za sekta za mifugo na uvuvi. Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama *(Grazingland and Animal Feed Resources Act)* Na. 13 ya mwaka 2010 imepitishwa na kuanza kutumika tarehe 1 Oktoba, 2010. Vilevile Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo *(Livestock Identification, Registration and Traceability Act)* Na. 12 ya mwaka 2010 imepitishwa na kuanza kutumika tarehe 1 Desemba, 2010 isipokuwa kwenye vipengele vyenye kipindi cha mpito cha miaka mitatu. Aidha, Wizara ipo katika hatua mbalimbali za kuandaa mapendekezo ya kutunga na kurekebisha Sheria zifuatazo:-

(i) Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu *(Marine Parks and Reserves Act)* Na. 29 ya mwaka 1994;

(ii) Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi *(Tanzania Fisheries Research Institute Act)* Na. 6 ya mwaka 1980;

(iii) Sheria ya kuanzisha Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Mifugo *(Tanzania Livestock Research Institute Act);* na

(iv) Sheria ya Uzalishaji wa Mbari Bora ya Wanyama *(Animal Breeding Act).*

Aidha, katika mwaka 2010/2011, Wizara imeandaa kanuni mbalimbali za kutekeleza sheria za mifugo na uvuvi kama ifuatavyo:-

(i) Kanuni sita za Sheria ya Biashara ya Ngozi Na. 18 ya mwaka 2008 zenye *GN* Na. 149, 150, 151, 152, 153 na 154;

(ii) Kanuni nne za Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na. 19 ya mwaka 2008 zenye *GN* Na. 183, 184, 185 na 186;

(iii) Kanuni za Sheria ya Magonjwa ya Mifugo Na. 17 ya mwaka 2003 kuhusu Utotoaji wa Vifaranga *(Hatcheries Regulations)* zenye *GN* Na. 155;

(iv) Kanuni sita za Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006;

(v) Kanuni za Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo Na. 12 ya mwaka 2010; na

(vi) Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009 GN Na. 308 zinatafsiriwa katika lugha ya Kiswahili.

Katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na wadau itakamilisha Sheria na Kanuni zilizoainishwa hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi na Bodi Zilizo Chini ya Wizara, Kampuni ya Ranchi za Taifa *(National Ranching Company - NARCO)* jukumu la Kampuni ya Ranchi za Taifa *(NARCO)* ni kuzalisha, kunenepesha na kuuza mifugo kwa ajili ya nyama. Kampuni imetoa huduma za ushauri kwa wafugaji wanaozunguka ranchi 10 za Kikulula, Kagoma na Missenyi (Kagera), Kongwa (Dodoma), Mzeri (Tanga), Ruvu (Pwani), Mkata (Morogoro), Kalambo (Rukwa) na *West Kilimanjaro* (Kilimanjaro). Ranchi hizo kwa pamoja zina jumla ya hekta 230,384 zenye uwezo wa kuweka ng'ombe kati ya 80,000 na 90,000. Kwa sasa Kampuni ina jumla ya ng'ombe 26,050, kondoo 1,771, mbuzi 902, farasi 50 na punda 53.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, *NARCO* imetekeleza yafuatayo:-

(i) Kuzalisha na kukuza ndama 5,869 kutokana na ng'ombe wazazi 10,616 sawa na asilimia 59.3 ya malengo ya uzalishaji;

(ii) Kuuza ng'ombe 8,722 wenye thamani ya shilingi bilioni 2.6 wakiwemo walionunuliwa chini ya Programu ya Unenepeshaji 447, walionunuliwa na *NARCO* na kunenepeshwa 649 na waliozaliwa na kukuzwa katika ranchi za *NARCO* 7,626;

(iii) Kukamilisha Mpango wa Biashara wa Unenepeshaji ambao umewezesha *NARCO* kukopa kutoka Benki ya Rasilimali *(TIB)* kiasi cha shilingi bilioni 2.86 na kiasi cha shilingi milioni 420 kutoka Benki ya *CRDB*;

(iv) Kununua ng'ombe 3,453 kutoka kwa wafugaji wanaozunguka maeneo ya ranchi kwa ajili ya programu ya unenepeshaji;

(v) Kuendelea na ujenzi wa machinjio ya kisasa katika Ranchi ya Ruvu ambao umefikia asilimia 50;

(vi) Kutoa hati miliki ndogo *(sub-lease)* 56;

(vii) Kusimamia na kutoa ushauri wa ufugaji bora katika ranchi ndogo zilizomilikishwa kwa wawekezaji wazalendo, ambapo ranchi hizo zimewekeza ng'ombe 50,227, mbuzi 4,266 na kondoo 1,212; na

(viii) Kutafuta wawekezaji kwa ajili ya ranchi ambapo kwa sasa, mazungumzo na wawekezaji watatu (3) kwa ajili ya Ranchi za Ruvu, *West Kilimanjaro* na sehemu ya Kongwa yanaendelea kukamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, *NARCO* itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuzalisha na kukuza ndama 7,173 kutokana na ng'ombe wazazi 9,347 walioko kwenye ranchi za *NARCO*;

(ii) Kuendelea na ujenzi wa machinjio katika ranchi ya Ruvu;

(iii) Kuuza ng'ombe 15,056 watakaokuwa na thamani ya takribani shilingi bilioni 7.5 wakiwemo 6,600 watakaonunuliwa chini ya programu ya unenepeshaji, 2,550 watakaonunuliwa na fedha ya *NARCO* kutoka kwa wafugaji wanaozunguka maeneo ya ranchi na 5,906 waliozaliwa na kukuzwa katika Ranchi za *NARCO*;

(iv) Kusimamia na kushauri ufugaji bora katika ranchi ndogo zilizomilikishwa kwa wawekezaji watanzania; na

(v) Kuendelea kutafuta wawekezaji ili waingie ubia na *NARCO* katika masuala ya mifugo katika ranchi nyingine saba zilizobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Nyama Tanzania jukumu la Bodi ya Nyama Tanzania ni kusimamia maendeleo ya sekta ndogo ya nyama kwa mujibu wa Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006. Katika mwaka 2010/2011, Bodi imehamasisha uundwaji wa vyama vya wafugaji katika ngazi za Wilaya ikiwa ni hatua ya awali ya uundwaji wa chama cha wafugaji Kitaifa. Vyama vinne vya wafugaji katika Halmashauri za Kibaha, Kahama, Kiteto na Babati vimeundwa. Aidha, vyama vitatu vya Jumuia ya Wafugaji Ruvu na vijiji vinavyoizunguka Ranchi ya Manyara (Mralipa, Mswalipa na Olipa) vimeundwa na kupata usajili kwa mujibu wa sheria. Kazi nyingine zilizotekelezwa na Bodi ya Nyama ni pamoja na:-

(i) Kukamilisha nyaraka muhimu zilizowezesha kuteuliwa kwa Msajili wa Bodi. Aidha, taratibu za kuajiri watumishi wengine wa Sekretarieti ya Bodi zinaendelea;

(ii) Kuelimisha na kuhamasisha kuhusu Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006 ambapo wataalam 51 kutoka Halmashauri 37 walihusika;

(iii) Kuhamasisha uundwaji wa vyama kumi vya wafugaji katika Halmashauri za Bagamoyo, Kahama, Kiteto, Babati Vijijini na katika Vijiji nane vinavyoizunguka Ranchi ya Manyara katika Halmashauri ya wilaya ya Monduli ambavyo vimeunda vyama vya msingi vitano vya wafugaji ambavyo vimejiunga na kuunda chama kikubwa cha ushirika kinachoitwa *Manyara Ranch Livestock Production Assocciation (MRALIPA);*

(iv) Kujenga uwezo wa Chama cha Wasindikaji wa Nyama *(TAMEPA)* na Chama cha Wafugaji Kanda ya Mashariki (UWAKAMA) ambapo viongozi sita walipatiwa mafunzo kuhusu uendeshaji wa vyama; na

(v) Kuwatambua wadau wakuu katika sekta ya nyama katika mikoa ya Tanga, Shinyanga na Manyara. Wadau hao ni pamoja na wafugaji 4,996 wenye idadi ya ng'ombe zaidi ya 20 kila mmoja, ranchi binafsi saba, wafanyabiashara wa mifugo na nyama 42 na vyama vya wadau 32 katika ngazi ya kata. Wadau hao wamehamasishwa kuanzisha mtandao wa ushirikiano wa uzalishaji ili kuhakikisha uendelevu wa sekta ya nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012 Bodi ya Nyama itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kuajiri watumishi wanne wa Sekretariati ya Bodi;

(ii) Kuendelea kuhamasisha wadau kuhusu sheria na kanuni za nyama na kujiunga na vyama vya wadau wa nyama kitaifa;

(iii) Kupitia na kuelimisha wadau juu ya viwango vya ubora wa nyama vilivyopo na kuweka utaratibu wa kudhibiti ubora wa nyama kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania *(TBS);*

(iv) Kuendelea kutambua wadau wakuu katika tasnia ya nyama na kuanzisha mtandao wa ushirikiano kwa kushirikiana na Halmashauri;

(v) Kuhamasisha wadau wa tasnia ya nyama kushiriki katika maonesho ya Sabasaba na Nanenane Kitaifa;

(vi) Kuandaa rejista kwa ajili ya kusajili wadau wa nyama; na

(vii) Kuandaa Mpango Mkakati wa Kuendeleza Tasnia ya Nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Maziwa Tanzania iliyoundwa kwa Sheria ya Maziwa Na. 8 ya mwaka 2004 imeendelea kuratibu tasnia ya maziwa. Katika mwaka 2010/2011, Bodi imeendelea kusimamia programu ya unywaji wa maziwa shuleni ambayo imefanyika kwenye shule 91 na kunufaisha jumla ya wanafunzi 62,900 ikilinganishwa na wanafunzi 57,350 katika shule 81 mwaka 2009/2010 (Jedwali Namba 1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingine zilizotekelezwa na Bodi ya Maziwa ni pamoja na:-

(i) Kutoa mafunzo kwa wakaguzi wa maziwa 44 kutoka Mikoa ya majaribio ya Arusha na Mwanza ili kudhibiti ubora wa maziwa;

(ii) Kusajili wadau wa maziwa 200 wakiwemo wazalishaji, wachuuzi na wakusanyaji wa maziwa katika mikoa ya Mwanza, Arusha, Tanga, Kilimanjaro, Manyara, Morogoro na Dar es Salaam;

(iii) Kuelimisha wadau wa maziwa 250 wa mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam, Manyara, Arusha na Kilimanjaro kuhusu Sheria ya Maziwa Na. 8 ya Mwaka 2004;

(iv) Kufanya mikutano ya Bodi na mkutano wa mwaka wa Baraza la Wadau wa Maziwa;

(v) Kuratibu maadhimisho ya Wiki ya Uhamasishaji Unywaji wa Maziwa yaliyofanyika Kitaifa Mkoani Dar es Salaam;

(vi) Kuratibu Kongamano na Maonesho ya Saba ya Maziwa ya Afrika yaliyoandaliwa na *Eastern and Southern Africa Dairy Association – ESADA* na kufanyika Dar es Salaam tarehe 25 – 27 Mei, 2011; na

(vii) Kushiriki kwenye maonesho mbalimbali ya Kitaifa ikiwemo Nane Nane na Saba Saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Bodi ya Maziwa itaendelea kufanya kazi zake ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kusajili wadau wa maziwa 300 katika mikoa ya Iringa, Mbeya, Mara, Ruvuma na Kagera kwa lengo la kuratibu shughuli zao;

(ii) Kurasimisha wachuuzi wa maziwa 300 na kuendesha mafunzo kwa wadau 250 juu ya utekelezaji wa Sheria ya Maziwa Na. 8 ya mwaka 2004;

(iii) Kuandaa maadhimisho ya Wiki ya Uhamasishaji Unywaji Maziwa nchini yatakayofanyika katika Manispaa ya Moshi, mwezi Mei/Juni 2012 na maadhimisho ya Siku ya Unywaji wa Maziwa Shuleni Duniani mwezi Septemba 2011;

(iv) Kuajiri watumishi wanne kwa ajili ya kuimarisha Sekretariati ya Bodi;

(v) Kuhamasisha na kuelimisha wadau sheria ya maziwa katika mikoa mitano ya Morogoro, Iringa, Mbeya, Ruvuma na Rukwa;

(vi) Kuitisha vikao vya Bodi na Baraza la Wadau wa Maziwa kwa mujibu wa Sheria;

(vii) Kushiriki kwenye mikutano ya Baraza la Wasimamizi wa Sekta ya Maziwa wa Nchi za Jumuia ya Afrika Mashariki *(East Africa Dairy Regulatory Authorities Council – EADRAC);* na

(viii) Kuendelea na uratibu wa Programu ya Unywaji wa Maziwa Shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu *(Marine Parks and Reserves Unit - MPRU),* katika mwaka 2010/2011 Wizara kupitia Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu imeendelea kusimamia, kulinda na kuhifadhi rasilimali za bahari katika maeneo yote ya hifadhi kwa kuandaa Mpango wa Jumla wa Usimamizi *(General Management Plan)* kwa ajili ya Hifadhi ya Bahari ya Silikanti - Tanga. Mpango huo umeandaliwa ili kuwawezesha wadau mbalimbali kuelewa na kushiriki kikamilifu katika uhifadhi wa rasilimali za Bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingine zilizotekelezwa na Kitengo ni pamoja na:-

(i) Kushirikiana na wadau kufanya doria za siku-kazi 394 zilizowezesha kukamatwa kwa makokoro 104, baruti 105, mikuki 67 na mitumbwi 52;

(ii) Kupitia mradi wa *MACEMP* Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu kimewezeshwa kujenga jengo la ofisi za Hifadhi za Bahari ya Silikanti ya Tanga, Hifadhi ya Bahari ya Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma Mtwara, nyumba ya watumishi katika Hifadhi ya Bahari ya Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma Mtwara na jengo la maabara na malazi kwenye Hifadhi ya Bahari Mafia. Aidha, Kitengo kimepatiwa gari moja na boti za doria tano;

(iii) Kuhamasisha wananchi 100 katika vijiji vitano kuunda vikundi vya kushiriki shughuli za uhifadhi katika Maeneo Tengefu ya Nyororo, Shungimbili na Mbarakuni katika Wilaya ya Mafia. Aidha, wananchi 342 katika vijiji tisa na mitaa kumi katika Hifadhi ya Bahari ya Silikanti Tanga wamehamasishwa kuunda kamati za ulinzi wa rasilimali za Bahari;

(iv) Kujenga uwezo wa kitengo kwa kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi tisa na ya muda mfupi kwa watumishi 15;

(v) Kuendelea kutangaza vivutio vya utalii vilivyomo katika maeneo yote ya hifadhi na taratibu za uwekezaji zinazozingatia mazingira rafiki kupitia tovuti, redio na magazeti na kushiriki katika maonesho mbalimbali yakiwemo ya Sabasaba, Nanenane na *Karibu Travel and Tourism Fair*;

(vi) Kuzijengea uwezo jamii zilizopo katika maeneo ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu kwa kuendeleza na kuanzisha miradi ya shughuli mbadala, ambapo miradi sita kuhusu kilimo cha mwani, ukuzaji wa lulu, ufugaji wa kaa, ufugaji wa kuku wa asili, utengenezaji wa batiki na shughuli za uongozaji watalii imeanzishwa;

(vii) Kutoa mafunzo ya shughuli za utalii kwa wanavijiji 44 ndani ya Hifadhi ya Bahari ya Mafia, Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma na Maeneo Tengefu ya Dar es Salaam;

(viii) Kuendeleza ukuzaji wa samaki katika mabwawa saba na ufugaji nyuki (mizinga 45) kwenye Hifadhi ya Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma; na

(ix) Kuendeleza kilimo cha mwani na ukuzaji wa chaza wa lulu kwa vikundi kumi kwenye Hifadhi ya Bahari ya Ghuba ya Mnazi na Maingilio ya Mto Ruvuma na Kisiwa cha Mafia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu kitatekeleza yafuatayo:-

(i) Kuendelea kulinda na kuhifadhi rasilimali za bahari katika maeneo yote ya hifadhi kwa kuimarisha doria na kuwashirikisha wadau ili kudhibiti uvuvi haramu kwa kufanya siku kazi za doria 400;

(ii) Kuendelea kujenga uwezo wa Kitengo kwa kuajiri watumishi wapya 17 ili kuimarisha ulinzi wa rasilimali katika Hifadhi ya Bahari ya Silikanti Tanga;

(iii) Kuendelea kutangaza vivutio vya utalii vilivyomo katika maeneo yote ya hifadhi na taratibu za uwekezaji zinazozingatia mazingira rafiki. Pia, Kitengo kitashiriki katika maonesho mbalimbali yakiwemo ya Sabasaba, Nanenane na *Karibu Travel and Tourism Fair*;

(iv) Kutangaza taarifa za vivutio vya utalii vilivyomo katika maeneo mapya ya Hifadhi na Maeneo Tengefu katika Mikoa ya Tanga, Dar es Salaam na Mtwara kupitia kwenye tovuti, redio, televisheni na magazeti; na

(v) Kuimarisha na kuboresha mazingira ya kazi ya watumishi kwa kuwapa vitendea kazi na mafunzo ya muda mfupi na mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania *(Tanzania Fisheries Research Institute - TAFIRI),* katika mwaka 2010/2011, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania, imeendelea na tafiti mbalimbali ili kubaini wingi, mtawanyiko na aina za rasilimali zinazopatikana katika maji ya asili. Kazi ya kutathmini wingi wa kambamiti kwenye maji ya Bahari ya Hindi baada ya kufunga uvuvi wa kambamiti kwa meli kubwa imefanyika na kuna dalili za kuongezeka kwa ukubwa na wingi wa kambamiti kwenye maji ya Tanzania. Taasisi imetafiti hali ya uvuvi na samaki katika Ziwa Rukwa na kubaini uchafuzi mkubwa wa maji unaosadikiwa kuletwa na kazi za kilimo na uchimbaji holela wa madini kwenye bonde la ziwa hilo hususan katika Wilaya ya Chunya.

Kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kuandaa tungo tano kuhusu ufugaji wa samaki na uhifadhi wa samaki kwa kutumia jua ili kupunguza uharibifu wa samaki baada ya mavuno *(post harvest losses).* Tungo hizo zimekubaliwa kufadhiliwa na fedha kutoka Tume ya Sayansi na Teknolojia *(COSTECH);*

(ii) Kuwezesha watafiti nane kupata mafunzo ya Shahada za Uzamivu watano na Uzamili watatu;

(iii) Kupitia Mradi wa Kufuatilia Mazingira Afrika kwa Maendeleo Endelevu *(African Monitoring of Environment for Sustainable Development-AMESD),* Taasisi imejenga kituo cha hali ya bahari *(Satellite Receiving Station)* ambacho kitatumika kubaini maeneo yenye samaki wengi katika tabaka la juu la maji kwenye Bahari ya Kitaifa *(Territorial Sea)* na Ukanda wa Uchumi wa Bahari. Kituo hiki kimejengwa *TAFIRI* Makao Makuu, Kunduchi, Dar es Salaam; na

(iv) Kukamilisha kuandaa *agenda* ya Kitaifa ya Utafiti wa Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Taasisi kwa kushirikiana na wadau wengine itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kujenga ofisi na maabara ya Kituo cha Utafiti cha Dar es Salaam;

(ii) Kubaini teknolojia sahihi *(appropriate technology)* ya kuzalisha vifaranga bora vya samaki;

(iii) Kuwapatia wakulima elimu ya ufugaji wa samaki kwa njia ya mabwawa ya mfano yatakayojengwa katika vituo vya Mwanza, Sota, Kigoma, Kyela na Dar es Salaam;

(iv) Kufanya utafiti wa samaki na mazingira katika mito iliyo ndani ya hifadhi ya mbuga za wanyama ya Ruvuma na Mara pamoja na maziwa madogo yaliyo karibu na Ziwa Victoria na Ziwa Rukwa;

(v) Kufanya tathmini ya uvuvi wa mishipi katika Ziwa Tanganyika na ukanda wa pwani ya Bahari ya Hindi;

(vi) Kufanya utafiti wa masoko ya uvuvi na maendeleo ya jamii katika Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika; na

(vii) Kuboresha miundombinu ya Taasisi, ukarabati wa majengo ya vituo vya Kyela na Sota, ununuzi wa vitendea kazi kwa vituo vya Kyela, Mwanza, Sota na Makao Makuu na ukarabati wa meli za utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi Bahari Kuu *(Deep Sea Fishing Authority – DSFA),* Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi Bahari Kuu ilianza kazi rasmi Machi, 2010 kwa mujibu wa Sheria Na. 1 ya mwaka 1998 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 4 ya mwaka 2007 na Kanuni zake za mwaka 2009. Majukumu makuu ya mamlaka ni kusimamia na kuendeleza uvuvi katika Bahari Kuu. Katika mwaka 2010/2011 Mamlaka ilitekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya Mamlaka zinazojengwa eneo la Fumba Zanzibar;

(ii) Kutoa leseni za uvuvi katika Bahari Kuu ambapo leseni 72 zilitolewa kwa Meli kutoka nchi mbalimbali na jumla ya Dola za Kimarekani 2,111,400 sawa na shilingi 3,399,354,000 zilipatikana;

(iii) Kushirikiana na Jeshi la Wanamaji, Polisi na Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) doria za saa 1,490 za maji na anga zilifanyika ili kudhibiti uvuvi haramu Baharini;

(iv)Kununua na kufunga chombo cha kuwezesha Mamlaka kufuatilia mwenendo wa meli zilizopewa leseni;

(v) Kufanya ukaguzi wa meli ambapo meli saba zenye usajili wa Tanzania zimekaguliwa kwenye bandari mbalimbali;

(vi) Kuweka vifaa vya kuvutia samaki *(Fish Agregating Devices - FADs)* katika Ukanda wa Uchumi takriban maili 25 za bahari kutoka Pwani ya Dar es Salaam na 35 kutoka kusini mwa Zanzibar (Kizimkazi) kwa lengo la kutathmini uwezekano wa kuwa na uvuvi wa kibiashara utakaofanywa na raia wa Tanzania;

(vii) Kuandaa miongozo ya kuhifadhi bioanuai ya Bahari Kuu itakayotekelezwa na meli zinazovua kwenye Ukanda wa Uchumi ili kuwezesha Uvuvi endelevu; na

(viii) Kuandaa vigezo vitakavyowezesha Taifa kupata stahili yake ya kiwango cha samaki kinachoruhusiwa kuvuliwa kwa msimu *(Quota system)* wa Ukanda wa Uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, mamlaka itaendelea kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kukamilisha ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya Mamlaka;

(ii) Kutoa leseni za uvuvi katika Bahari Kuu;

(iii) Kufanya doria za kwenye maji na anga kwa kushirikiana na Jeshi la Wanamaji, Polisi na KMKM kudhibiti uvuvi haramu baharini;

(iv) Kufuatilia utendaji wa meli zenye usajili wa Tanzania na zilizopewa leseni za uvuvi ukanda wa uchumi;

(v) Kuongeza idadi ya vifaa vya kuvutia samaki *(FADs)* kutoka nne hadi 42;

(vi) Kwa kushirikiana na sekta binafsi, tathmini itaendelezwa ya uwezekano wa raia wa Tanzania kuvua kibiashara katika ukanda wa uchumi kwa kutumia *FADs;* na

(vii) Kushirikiana na Mashirika ya Kikanda, *Indian Ocean Tuna Commission – IOTC* na *South West Indian Fisheries Commission – SWIOFC* yote yakiwa chini ya *FAO,* katika kutathmini hali ya samaki kwenye ukanda wa uchumi na kutathmini kiwango stahili kwa taifa letu cha samaki wa ukanda wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Mifugo - Mpwapwa na Vituo vya Utafiti wa Mifugo katika mwaka 2010/2011 Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Mifugo - Mpwapwa pamoja

na vituo sita vya utafiti vya Kongwa, Mabuki, Naliendele, Tanga, Uyole na *West Kilimanjaro* imeendelea na utafiti wa mifugo na malisho kwa lengo la kupata teknolojia sahihi za kuongeza tija na uzalishaji wa mifugo nchini. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kutathmini na Kusambaza Mifugo Bora Vijijini, Wizara kupitia Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Mifugo Mpwapwa na vituo vyake imeendelea kukusanya takwimu mbalimbali za maendeleo ya ukuaji na uzalishaji wa mbari za mifugo bora na ya asili. Jumla ya ndama 199 aina ya Mpwapwa walizaliwa katika kituo cha Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Mifugo-Mpwapwa wakiwa na wastani wa uzito wa kuzaliwa wa kilo 22. Aidha, ng'ombe 135 aina ya Mpwapwa na chotara wa Mpwapwa na Boran walisambazwa kwa wafugaji.

Katika mwaka 2010/2011, tathmini ya uzalishaji na ukuaji kwa mbuzi aina ya Malya pamoja na chotara wake iliendelea. Jumla ya mbuzi 58 wa chotara walizaliwa wakiwa na wastani wa uzito wa kilo 3.0 ikilinganishwa na kilo 1.5 kwa mbuzi wa asili. Aidha, mbuzi bora aina ya Malya 947 walisambazwa kwa wafugaji katika maeneo mbalimbali nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, jumla ya kuku wa asili 612 kutoka mbari 11 walifanyiwa tathmini ili kubaini uwezo wa ukuaji na utagaji. Matokeo ya awali ya tathmini yanaonesha kuwa uzito wa mayai ni kati ya gramu 30 na 45 na uzito wa kuku katika umri wa miezi 2 ni kati ya gramu 800 na 1,200. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wa malisho ya mifugo katika mwaka 2010/2011, utafiti wa malisho na utunzaji wa benki ya vinasaba uliendelea ambapo jumla ya vinasaba 152 vilifanyiwa tathmini katika vituo vya utafiti vya Mpwapwa 80 na Uyole 72. Jumla ya kilo 930 za mbegu za malisho aina ya *Chloris gayana* na kilo 1,045.5 za *Cenchrus ciliaris* zilivunwa na kusambazwa kwa wadau. Aidha, jumla ya miche 10,670 ya miti ya malisho ilizalishwa katika Kituo cha Utafiti wa Mifugo Uyole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012 taasisi itaendelea na utafiti na kusambaza teknolojia sahihi katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kuboresha ng'ombe wa asili wa nyama ambapo madume 100 aina ya Mpwapwa yatasambazwa katika vijiji mbalimbali. Jumla ya ng'ombe 20 aina ya *Iringa Red* na 20 aina ya *Maasai* watanunuliwa kwa ajili ya utafiti. Aidha, tathimini itafanyika katika Wilaya za Manyoni, Mpwapwa na Iramba ili kubaini maendeleo ya ng'ombe aina ya Mpwapwa waliosambazwa kwa wafugaji.

(ii) Uzalishaji wa mbuzi na kondoo wa asili aina ya *Gogo White*, *Newala*, *Pare White*, *Sonjo Red* na kondoo aina ya *Red Maasai* na *Blackhead Persian.* Madume 100 ya mbuzi bora aina ya Malya yatasambazwa vijijini. Pia, jumla ya mbuzi 20 aina ya *Ujiji* na 20 aina ya *Maasai* watanunuliwa kwa ajili ya utafiti.

(iii) Uzalishaji wa nguruwe ambapo nguruwe 150 wa mbegu bora watasambazwa vijijini. Pia, utafiti utafanyika kwenye kuku wa asili kuongeza utagaji na ukuaji.

(iv) Uzalishaji wa malisho bora ambapo kilo 3,500 za mbegu za nyasi na kilo 700 za mbegu za mikunde ya malisho zitazalishwa na kusambazwa kwa wadau. Aidha, aina nyingine 50 za malisho kutoka nje na ndani ya nchi zinatarajiwa kukusanywa, kustawishwa, kutathminiwa na kuhifadhiwa.

(v) Kuboresha vituo saba vya utafiti vya Mpwapwa, *West Kilimanjaro,* Kongwa, Tanga, Naliendele, Uyole na Mabuki kwa kuvipatia vitendea kazi, kuimarisha miundombinu na kujenga uwezo wa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuimarisha vituo vya utafiti katika mwaka 2010/2011, Taasisi ilinunua matrekta matano na zana zake kwa ajili vituo vya utafiti vya Tanga, Kongwa, *West Kilimanjaro,* Naliendele na Mpwapwa. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kuimarisha vituo vya utafiti kwa kuvipatia vitendea kazi muhimu, kujenga na kukarabati miundombinu.

Mashine za kufunga marobota ya hei *(balers)* tatu na reki za hei tatu vitanunuliwa kwa ajili ya vituo vya utafiti vya Tanga, *West Kilimanjaro* na Naliendele.

Aidha, ofisi moja kwa ajili ya Kituo cha Utafiti wa Mifugo Tanga itajengwa na kukamilisha ujenzi wa ofisi ya Naliendele na *rest house* ya taasisi ya Mpwapwa. Pia mizani nne za kupimia ng'ombe na mbuzi zitanunuliwa na kukarabati miundombinu ya maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maabara Kuu ya Mifugo – Temeke, majukumu ya Maabara Kuu ya Mifugo - Temeke ni pamoja na kufanya uchunguzi, utambuzi na utafiti wa magonjwa mbalimbali ya mifugo; kufanya majaribio ya dawa mpya na chanjo za mifugo; kutafiti na kutengeneza chanjo za kuzuia magonjwa ya mifugo; na kuchunguza ubora wa bidhaa zitokanazo na mifugo, nguvu za dawa za majosho na ubora wa vyakula vya mifugo. Pia, hutoa mafunzo ya Stashahada ya Ufundi Sanifu Maabara *(Veterinary Laboratory Technology).*

Katika mwaka 2010/2011, Maabara Kuu ilitekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Uzalishaji na usambazaji wa dozi milioni 41.5 za chanjo ya kuzuia ugonjwa wa Mdondo, dozi 336,400 za kuzuia Chambavu na dozi 232,000 za chanjo ya kuzuia kimeta, dozi 45,350 za kuzuia ugonjwa wa Kutupa Mimba na dozi 2,350 za chanjo ya mchanganyiko wa magonjwa ya kimeta na chambavu katika Halmashauri zote nchini. Aidha, majaribio ya utengenezaji wa chanjo ya Homa ya Bonde la Ufa *(RVF)* na Homa ya Mapafu ya Ng'ombe *(CBPP)* yanaendelea.

(ii) Uchunguzi na utambuzi wa magonjwa mbalimbali ya mifugo ambapo sampuli 11,380 zilipokelewa na kufanyiwa uchunguzi. Baadhi ya magonjwa yaliyothibitishwa ni Sotoka ya Mbuzi na Kondoo *(Peste des Petit Ruminantia - PPR),* Kichaa cha Mbwa, Ugonjwa wa Kiwele *(Mastitis),* Homa ya Nguruwe, Ndigana Kali, Mkojo Mwekundu *(Babesiosis),* Ndigana baridi, Nagana *(Trypanosomosis),* Ugonjwa wa Miguu na Midomo, Mdondo *(Newcastle disease), Marek's disease* na *Colibacillosis;*

(iii) Uendelezaji wa teknolojia ya kudhibiti mbung'o na nagana kwa kufuga ndorobo kwenye maabara ambapo jumla ya mbung'o 41,060 na mabuu *(pupae)* milioni 1.4 yalizalishwa na kuhasiwa kwa mionzi *(Sterile Insect Technique)* katika Kituo cha Utafiti Tanga;

(iv) Tathmini ya mtawanyiko wa mbung'o katika wilaya za Kahama, Bukombe, Chunya na Mpanda yakiwa ni maandalizi ya udhibiti wa mbung'o katika maeneo hayo;

(v) Uchunguzi wa sampuli 347 za vyakula vya kuku na 90 za malighafi ya kutengenezea vyakula vya mifugo ulifanyika. Aidha, sampuli 213 za malisho kutoka mashamba ya ng'ombe zilichunguzwa ubora wake na ushauri ulitolewa kulingana na matokeo ya utafiti;

(vi) Uchunguzi wa sampuli 684 za mazao ya wanyama yakiwemo maziwa, nyama na mayai kubaini mabaki ya dawa na uwepo wa bakteria katika mazao hayo ambapo matokeo yameonesha kuwa vyakula hivyo ni salama kwa matumizi ya binadamu;

(vii) Kuendelea na ujenzi wa kituo kipya cha utafiti na uzalishaji wa chanjo Kibaha ambapo nyumba mbili za watumishi zimekamilika na jengo la maabara limefikia asilimia 80 ya ujenzi; na

(viii) Kuimarisha Maabara Kuu ya Mifugo na vituo vyake kwa kuvipatia vitendea kazi na kuboresha miundombinu. Aidha, Maabara ya Uchunguzi wa Magonjwa ya Kuambukiza Mifugo *(Centre for Infectious Diseases and Biotechnology - CIDB)* imefanyiwa tathmini ya kubadilishwa kuwa Maabara ya Rufaa *(Bio Security Level 3 - BSL 3)* katika nchi za *SADC* kwa ajili ya magonjwa ya Homa ya Mapafu ya Ng'ombe *(CBPP)* na Miguu na Midomo *(FMD)* na ukarabati umeanza kulingana na tathmini iliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Maabara Kuu ya Mifugo itaendelea na lengo lake la kuzalisha chanjo za kuzuia magonjwa mbalimbali ikiwa ni pamoja na dozi milioni 100 za Mdondo, 500,000 za Kimeta, 400,000 za Chambavu 250,000 za Ugonjwa wa Kutupa Mimba,

200,000 za Homa ya Bonde la Ufa na 100,000 za Homa ya Mapafu na kuzisambaza katika Halmashauri. Pia, Maabara itafanya kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea kufanya uchunguzi wa ubora wa vyakula vya mifugo, kuhakiki na kutathmini njia za kuchunguza kemikali za sumu *(toxicological analytical assays)* kwenye mifugo na mazao yake na kufanya uchunguzi wa dawa za kuogeshea mifugo;

(ii) Kufanya uchunguzi na utafiti wa magonjwa mbalimbali ya mifugo na kufanya majaribio ya chanjo za kudhibiti magonjwa ya mlipuko;

(iii) Kuandaa na kuweka katika matumizi teknolojia za kudhibiti mbung'o na kupe na magonjwa wayaenezayo; na

(iv) Kukarabati na kuipatia vifaa Maabara Kuu ya Mifugo – Temeke na vituo vya Luguruni, Kibaha, Tanga na Kigoma na kuandaa Maabara ili ipate ithibati ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maabara ya Taifa ya Udhibiti wa Ubora wa Samaki – Nyegezi, Mwanza imeendelea na majukumu yake ya kukusanya sampuli na kufanya uchunguzi wa sampuli za samaki, maji na tope ili kubaini vimelea haribifu na masalia ya kemikali yatokanayo na mbolea za mazao, uchafu wa viwandani na majitaka ya majumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Maabara imeimarishwa kwa kupatiwa vifaa vya uchunguzi wa vimelea na kemikali, kufanyiwa ukarabati wa majengo, kuongezewa watumishi na kupatiwa mafunzo ambapo watumishi watatu wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na wanne muda mfupi. Jumla ya sampuli 1,374 zilichunguzwa ili kuhakiki ubora na usalama wa mazao ya uvuvi ambapo kati ya hizo, 1,144 ni kwa ajili ya vimelea haribifu na 230 ni kwa ajili ya mabaki ya sumu, dawa na madini tembo. Uchunguzi huo ulifanyika katika Maabara ya Taifa ya Uthibiti wa Ubora wa Samaki Nyegezi (Mwanza), Shirika la Viwango Tanzania (Dar es Salaam), *Chemiphar* (Uganda) na Shirika la Viwango la Afrika Kusini *(SABS).* Sampuli zote zilizochunguzwa zilionekana kukidhi viwango vya usalama. Maabara inaendelea kukamilisha taratibu za kupata ithibati kwa ajili ya uchunguzi wa viuatilifu na mabaki ya sumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kuimarisha na kuwezesha utendaji kazi wa Maabara ya Samaki – Nyegezi, Mwanza kwa kuipatia vitendea kazi na kutoa mafunzo kwa watumishi. Aidha, itaendeleza taratibu za kupata ithibati kwa ajili ya uchunguzi wa viuatilifu na mabaki ya sumu. Pia Maabara itafanya uchunguzi wa sampuli 800 za minofu ya samaki, maji na udongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maabara ya Uchunguzi wa Sumu ya Mwani unaoelea kwenye Maji *(Harmful Algal Blooms-HABs)* – Temeke, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki *(International Atomic Energy Agency)* imeendelea kuiimarisha Maabara ya uchunguzi wa sumu kwenye mwani unaoelea chini ya Mradi wa *Coastal Zone Management* unaotekelezwa na nchi sita za Angola, Afrika Kusini, Kenya, Namibia, Tanzania na Tunisia kwa kutumia teknolojia ya nguvu za Atomiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kuu la mradi huu ni kuziwezesha nchi shiriki kutumia teknolojia ya Atomiki kufanya tafiti za mwani unaoelea ambao hutoa sumu inayoathiri usalama wa mazao ya uvuvi na viumbe vinavyoishi kwenye maji. Maabara hiyo imepatiwa vifaa vya uchunguzi, pikipiki na Kompyuta. Aidha, mtaalam mmoja ameshiriki kwenye mafunzo kuhusu uendeshaji wa Maabara za aina hii yaliyofanyika Mombasa, Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kuimarisha Maabara ya *HABs* na kuiwezesha kuanza kazi za uchunguzi wa sumu kwenye maji kwa kuipatia vitendea kazi na kutoa mafunzo kwa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Baraza la Veterinari iliendelea kuboresha huduma zinazotolewa na wataalam wa huduma za afya ya mifugo kwa kuboresha ukaguzi wa viwango vya taaluma katika vyuo vya Morogoro na Mpwapwa, usajili wa madaktari wa mifugo 18 na

kuhamasisha wataalam kujiendeleza kitaaluma. Vilevile wataalam walihamasishwa juu ya utekelezaji wa sera ya ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kutoa huduma za mifugo.

Kazi nyingine zilizotekelezwa na Baraza la Veterinari ni pamoja na:-

(i) Kutathmini na kuboresha miongozo mitatu ya watoa huduma za afya ya mifugo juu ya vituo vya kutolea huduma za mifugo, dawa na vifaa vya tiba ambapo wadau walishirikishwa;

(ii) Kuhamasisha wadau juu ya matumizi ya huduma bora kwa njia ya maonesho ya Kitaifa yakiwemo Nanenane, Wiki ya Utumishi wa Umma, Siku ya Kichaa cha Mbwa Duniani, Siku ya Wanawake Duniani na Siku ya Veterinari Duniani;

(iii) Kushiriki katika mikutano ya kitaaluma, kimataifa (Shirika la Afya ya Wanyama Duniani, *OIE)* na Kikanda ikiwemo ya *SADC* na Jumuiya ya Afrika Mashariki kujadili viwango vya mitaala katika elimu za taaluma;

(iv) Kutoa mafunzo kwa wakaguzi 51 kutoka Halmashauri 47 wa Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza na Kanda tatu za Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo za Mashariki, Kati na Kusini kuhusu kanuni na taratibu za ukaguzi. Pia, mafunzo hayo yametolewa kwa wahitimu 613 wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo wa Astashahada na Stashahada;

(v) Kukagua vituo 89 vya huduma ya afya ya mifugo kwa kushirikiana na wakaguzi wa Halmashauri, mikoa na kanda ambapo wamiliki wa vituo sita wamepatiwa ushauri wa kuviboresha ili visajiliwe;

(vi) Kusajili vituo 16 vya huduma za afya ya mifugo na kuorodhesha na kuandikisha wataalam wasaidizi wa afya ya mifugo 331;

(vii) Kuwezesha Baraza kufanya mikutano na kikao cha Kamati za Mitihani na Nidhamu kwa mujibu wa Sheria;

(viii) Kukusanya takwimu za kada za wataalam wa uzalishaji mifugo wanaostahili kupata mafunzo yatakayowawezesha kutoa huduma ya afya ya mifugo katika mikoa yote ya Tanzania Bara;

(ix) Kuhamasisha Halmashauri 105 na vyama vya kitaaluma vya *Tanzania Veterinary Association (TVA), Tanzania Veterinary Para-proffesional Association (TAVEPA)* na *Tanzania Society of Animal Production (TSAP)* juu ya ushirikishaji wa sekta binafsi; na

(x) Kuwezesha watumishi watatu kupata mafunzo ya kompyuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Baraza kwa kushirikiana na Halmashauri nchini litasimamia ubora wa huduma kwa kuimarisha ukaguzi na usajili wa madaktari wa mifugo 35 na vituo 20 vya kutolea huduma, kuandikisha na kuorodhesha wataalam wenye Astashahada na Stashahada 180.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ubora wa wataalam utafuatiliwa kwa kutoa kozi fupi juu ya sheria na kanuni zinazohusu huduma za afya ya mifugo kwa wahitimu wa vyuo wakiwemo wa vyuo vya sekta binafsi. Aidha, wahitimu wa vyuo vya nje watahakikiwa. Kazi nyingine zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kuandaa viwango vya vituo vya huduma ya mifugo;

(ii) Kukagua ubora wa mitaala ya taaluma ya veterinari katika vyuo vya mafunzo ya mifugo vya umma na sekta binafsi;

(iii) Kutoa mafunzo kwa wataalam 150 wa maabara, uhimilishaji na wakaguzi kuhusu maadili na ukaguzi wa taaluma ya veterinari;

(iv) Kuandaa nakala 3,000 za miongozo ya taaluma ya veterinari na kuzisambaza kwa wadau kwa ajili ya uhamasishaji;

(v) Kufanya ukaguzi wa vituo 150 pamoja na maadili ya watoa huduma katika sekta za umma na binafsi;

(vi) Kuhuisha miongozo ya kufundishia taaluma ya veterinari hapa nchini na nchi nyingine ili kuvitambua; na

(vii) Kuijengea uwezo Sekretariati na wajumbe tisa wa Baraza kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Veterinari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu utafiti wa sekta za mifugo na uvuvi nchini. Katika mwaka 2010/2011 Wizara ilikamilisha kuandaa rasimu ya *agenda* ya Utafiti wa Mifugo itakayokuwa dira kwa watafiti wanaotaka kufanya utafiti wa mifugo katika nchi yetu. Aidha, Wizara imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa utafiti wa mifugo wakiwemo Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia; Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika; *ASARECA; SUA; COSTECH; Climate Change, Agriculture and Food Security - CCAFS; Consultative Group for International Agricultural Research - CGIAR*; *International Atomic Energy Agency - IAEA;* na *EAC* katika kuandaa na kupima mipango mbalimbali ya utafiti. *(Makofi)*

Vilevile Wizara imeshirikiana na wadau hao kutayarisha, pamoja na mambo mengine, mikakati ya utafiti katika maeneo muhimu kama vile ufugaji, mabadiliko ya tabia nchi, uhakika wa chakula, mbinu za kuzuia na kukabiliana na athari za ukame. Kupitia mradi wa *East Africa Agricultural Productivity Project (EAAPP),* vituo vitatu vya kuzalisha mbegu za malisho na kimoja cha uhimilishaji *(AI)* na Maabara Kuu ya Taifa ya Mifugo *(CVL)* viliimarishwa kwa kununuliwa vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa utafiti katika maendeleo ya ufugaji, Wizara kupitia *ASDP* imeendelea kujenga uwezo wa utafiti kwa kuimarisha Mifuko ya Utafiti na Maendeleo ya Kanda saba za utafiti wa mifugo *(Zonal Agricultural Research, Developmet and Extension Fund – ZARDEF* na *Zonal Information and Extension Liaison Units - ZIELU)* kwa kuzipatia jumla ya shilingi milioni 362.2 na vitendea kazi kwa ajili ya kugharamia na kusimamia miradi ya utafiti kulingana na vipaumbele vya kanda husika na kutayarisha matokeo ya utafiti huo katika mfumo rahisi na kuwapelekea wafugaji. Pia miradi 43 ya utafiti wa mifugo imeendelea kufadhiliwa na mfuko huo ambapo miradi 30 iliyoanza 2008/2009 imekamilika. Wataalam 18 wa mifugo kutoka Kanda ya Mashariki wamepatiwa mafunzo ya kufanya utafiti shirikishi wa kilimo na mifugo kulingana na mahitaji ya wadau *(Client Oriented Research and Development Management Approach – CORDEMA).* Pia kupitia programu ya *ASDP, COSTECH* na wafadhili wengine, watafiti 73 wa mifugo na uvuvi wanaendelea na masomo, kati yao 23 Shahada ya Uzamivu na 50 Shahada ya Uzamili. (Jedwali Na. 2).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kuratibu, kufuatilia na kutathmini utafiti na utoaji huduma za utafiti na maendeleo ya mifugo na uvuvi kulingana na programu zilizotayarishwa;

(ii) Kuimarisha mfumo wa utunzaji kumbukumbu za utafiti wa mifugo na uvuvi nchini na kushirikiana na taasisi za kitaifa na kimataifa kuratibu utafiti shirikishi wa mifugo;

(iii) Kuwawezesha watafiti 12 kuendelea na masomo ya Uzamivu na Uzamili;

(iv) Kuwezesha Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Mifugo Mpwapwa, Maabara Kuu ya Taifa ya Mifugo - Temeke na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi kuendeleza utafiti wa mifugo na uvuvi nchini;

(v) Kuwezesha mifuko ya *ZARDEF* ili iendelee kugharamia utafiti kulingana na vipaumbele vya kanda na mahitaji ya wadau chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo – *ASDP;*

(vi) Kuwezesha na kuratibu utoaji mafunzo ya utafiti shirikishi (CORDEMA) katika awamu ya pili;

(vii) Kuendelea kutoa ushauri wa kitaalam juu ya uandishi wa tungo za tafiti kwa watafiti wa vituoni; na

(viii) Kukusanya na kutunza matokeo mbalimbali ya tafiti zilizofanyika nchini ikiwa ni pamoja na kuimarisha mfumo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, jumla ya wanachuo 1,498 (Stashahada 892 na Astashahada 606) wameendelea na mafunzo katika vyuo sita vya mifugo vya Buhuri, Madaba, Morogoro, Mpwapwa, Temeke na Tengeru (Jedwali Na. 3). Kati ya hao, 613 wamemaliza mafunzo yao mwezi Juni, 2011 wakiwemo 357 wa Stashahada na 256 wa Astashahada.

Vilevile vyuo hivyo vimeendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wafugaji kwa ushirikiano kati ya Wizara na Wafadhili mbalimbali wakiwemo *HPT, World Vision*, Taasisi za Dini, MVIWATA na Halmashauri. Jumla ya wafugaji 8,796 walipatiwa mafunzo katika nyanja za ufugaji wa ng'ombe na mbuzi wa maziwa, nyuki, kuku, uendelezaji wa malisho na zao la ngozi, usindikaji wa maziwa na afya ya mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kujenga uwezo wa vyuo vya mafunzo ya mifugo kwa kukarabati miundombinu na kununua vifaa vya kufundishia ambapo jumla ya madarasa manne, hosteli tano na bwalo moja vimekarabatiwa pamoja na kuendelea kuimarisha majengo ya mifugo katika vyuo hivyo.

Aidha, vyuo hivyo vimepatiwa vitendea kazi vikiwemo kompyuta 12, basi moja, trekta tatu na zana zake, madawati na viti 55, vitanda na magodoro 68. Pia wakufunzi saba wanafadhiliwa masomo ambapo shahada ya uzamili ni watano, uzamivu wawili na 12 wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kuimarisha uwezo wa vyuo vya mifugo ili kuweza kuchukua wanafunzi 2,000 kwa mwaka wakiwemo 1,000 wa Astashahada na 1,000 wa Stashahada. Mwaka huu vyuo vitakuwa na jumla ya wanafunzi 1,500;

(ii) Kukamilisha taratibu za kuanzisha wakala wa mafunzo ya mifugo;

(iii) Kuwaendeleza wakufunzi 20 kwa kuwapatia mafunzo katika ngazi mbalimbali; na

(iv) Kuendelea na taratibu za kukamilisha ithibati kwa vyuo vyote vya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara kupitia mradi wa *MACEMP* na wafadhili wengine imeendelea kugharamia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ya taaluma za uvuvi kwa watumishi 44, wakiwemo watano wa Shahada ya Uzamivu; 17 wa Shahada ya Uzamili; watano wa Shahada ya Kwanza na 17 wa mafunzo ya muda mfupi.

Aidha, Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya uvuvi kwa wanafunzi 481 katika Vyuo vya Uvuvi vya Mbegani na Nyegezi (Jedwali Na. 3) katika ngazi za Stashahada (236) na Astashahada (245). Pia vyuo hivyo vimetoa mafunzo ya ufundi mchundo kwa wanafunzi 40. Watakaohitimu mwaka huu ni 176 ambapo 102 ni wa Astashahada na 74 ni wa Stashahada.

Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kukarabati na kununua vifaa vya kufundishia kwa Vyuo vya Uvuvi vya Nyegezi na Mbegani ili viweze kutoa mafunzo ya uvuvi katika ngazi ya Astashahada na Stashahada kwa wanachuo 500 na kuchangia gharama za mafunzo hayo. Aidha, Wizara itagharamia mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 27 na muda mfupi watumishi 12. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uendelezaji wa mifugo na mazao yake, zao la maziwa katika mwaka 2010/2011, tasnia ya maziwa imeendelea kukua kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji, ukusanyaji na usindikaji wa maziwa. Uzalishaji wa maziwa uliongezeka kutoka lita bilioni 1.65 mwaka 2009/2010 hadi lita bilioni 1.74 mwaka 2010/2011, sawa na ongezeko la asilimia 5.2 (Jedwali Na. 4). Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa ukusanyaji wa maziwa kutoka kwenye kundi la ng'ombe wa asili. Kutokana na ongezeko hilo, unywaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita 43 kwa mtu kwa mwaka 2009/2010 hadi lita 44 kwa mtu kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, jumla ya mitamba 712 ilizalishwa na kusambazwa kwa wafugaji, sawa na ongezeko la asilimia 12 ukilinganisha na mitamba 624 iliyozalishwa mwaka 2009/2010. Wizara imeendelea kuboresha mashamba ya kuzalisha mifugo ili kuongeza upatikanaji wa mitamba kwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kununua ng'ombe wazazi 75 kwa ajili ya mashamba ya Ngerengere (40) na Nangaramo (35), madume bora mawili ya ng'ombe wa mbegu kwa ajili ya *Sao Hill* na madume ya mbuzi aina ya Boer 10 kwa ajili ya Ngerengere;

(ii) Kukarabati miundombinu mbalimbali ya shamba ikiwa ni pamoja na kuboresha mifumo ya maji, barabara na njia za kuzuia moto; na

(iii) Kukarabati nyumba tisa za watumishi.

Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kuimarisha mashamba yake ikiwa ni pamoja na kuendelea kukamilisha kazi ya kuyapima ili yapate hatimiliki, kununua mifugo wazazi pamoja na vitendea kazi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika ukusanyaji na usindikaji maziwa. Katika mwaka 2010/2011, usindikaji wa maziwa umeongezeka na kufikia lita 112,400 kwa siku sawa na asilimia 6.2 ikilinganishwa na lita 105,380 mwaka 2009/2010. Kiwanda cha *New Northern Creameries* cha Arusha, kilichofungwa tangu mwaka 2009 kimeanza kufanya kazi ya kusindika maziwa. Juhudi nyingine zilizofanywa na Wizara kuhamasisha ukusanyaji na usindikaji wa maziwa nchini ni pamoja na:-

(i) Kuandaa andiko la Mpango wa Kitaifa la unywaji wa maziwa shuleni;

(ii) Kuwezesha vikundi viwili vya Nronga na Enaboishu kupata vifaa vya kupoza na kusindika maziwa;

(iii) Kuhamasisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kusimamia na kudhibiti ubora wa maziwa katika maeneo ya wafugaji. Vikundi 12 vya uzalishaji wa maziwa vya ushirika wa NJOLIFA vinavyouza maziwa katika kiwanda cha *CEFA* Njombe vimewezeshwa kupima maziwa ili kukidhi viwango vya ubora na masharti ya mkataba; na

(iv) Kuwezesha wanachama 18 wa vikundi vya kuzalisha, kukusanya na kusindika maziwa na wataalam wanne kufanya ziara ya mafunzo Nakuru Kenya kuhusu ufugaji, ukusanyaji na usindikaji wa maziwa.

Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kuhamasisha wadau kuwekeza na kuongeza usindikaji wa maziwa ili kusindika lita 130,000 kwa siku. Aidha, Wizara itaendelea kubaini maeneo yenye maziwa mengi katika Kanda za Kaskazini na Magharibi ili kuendelea kuhamasisha wadau wa maziwa kuwekeza katika biashara na usindikaji wa maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya uhimilishaji kama njia yenye tija ya kuzalisha mifugo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji – *NAIC Usa River* na Vituo vya Kanda vya Mwanza, Dodoma, Kibaha, Lindi na Mbeya vimeimarishwa. Aidha, jumla ya dozi 150,000 za mbegu bora zimezalishwa ikilinganishwa na dozi 110,000 zilizozalishwa mwaka 2009/2010 ikiwa ni ongezeko la asilimia 36. Pia, jumla ya ng'ombe 76,800 walihimilishwa ikilinganishwa na ng'ombe 73,900 waliohimilishwa mwaka 2009/2010. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kuzalisha lita 38,400 za kimiminika cha naitrojeni *(Liquid Nitrogen)* katika kituo cha *NAIC* na kwenye vituo vitatu vya uhimilishaji vya kanda vya Dodoma, Kibaha na Mwanza;

(ii) Kufundisha wataalam 320 wa uhimilishaji kutoka kwenye maeneo mbalimbali nchini;

(iii) Kufanya tathmini ya awali kwa ajili ya ujenzi wa kituo kipya cha uhimilishaji mifugo cha Sao Hill – Iringa;

(iv) Kufanya tathmini ya awali kwa ajili ya kujenga vituo viwili vya uhimilishaji vya Tanga na Tabora; na

(v) Kuwapatia mafunzo ya uhimilishaji watumishi 10 kutoka kwenye mashamba ya kuzalisha mifugo na vituo vya kanda za Kusini (Lindi) na Nyanda za Juu Kusini (Mbeya).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara itafanya yafuatayo:-

(i) Kuendelea kuboresha vituo vyake vya uhimilishaji kwa kuimarisha miundombinu na kuviongezea vitendea kazi;

(ii) Kuzalisha dozi 180,000 za mbegu bora za uhimilishaji;

(iii) Kufanya tathmini ya matumizi ya uhimilishaji nchini; na

(iv) Kufundisha wataalam 350 wa uhimilishaji kutoka kwenye maeneo mbalimbali nchini; na

(v) Kuanza maandalizi ya ujenzi wa kituo kipya cha uhimilishaji mifugo cha *Sao Hill,* Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, uzalishaji wa nyama umeongezeka kwa asilimia 10.7 kutoka tani 449,673 mwaka 2009/2010 hadi tani 503,496 mwaka 2010/2011. Kati ya hizo, nyama ya ng'ombe ni tani 262,606, mbuzi na kondoo tani 103,709, nguruwe tani 43,647 na kuku tani 93,534. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa mahitaji ya nyama na mazao yake kwa sababu ya kupanuka kwa wigo wa masoko, ambapo masoko maalum kama vile maduka makubwa, migodi na hoteli yameongeza ununuzi wa nyama inayozalishwa hapa nchini na kupunguza uagizaji kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa imeendelea kuhamasisha wafugaji na wafanyabiashara wa mifugo kunenepesha mifugo ili kuzalisha nyama bora. Katika mwaka 2010/2011, ng'ombe walionenepeshwa wameongezeka kwa asilimia 32.7 kutoka ng'ombe 74,400 mwaka 2009/2010 na kufikia ng'ombe 98,700. Ongezeko hili limetokana na baadhi ya wafugaji na wafanyabiashara wa mifugo wa mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Kagera, Tabora, Singida, Arusha, Manyara, Rukwa, Iringa, Morogoro na Pwani kupokea na kutekeleza mfumo wa unenepeshaji (Jedwali Na. 5). *(Makofi)*

Katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa nyama, itaendelea kuhamasisha wafugaji na wafanyabiashara ya mifugo kuwekeza kwenye ufugaji wa kisasa ukiwemo wa ranchi pamoja na kunenepesha ng'ombe zaidi ya 120,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na ongezeko la uzalishaji wa kuku na mayai nchini. Katika mwaka 2010/2011, jumla ya vifaranga milioni 38.4 vya kuku wa nyama na mayai vilizalishwa

nchini ikilinganishwa na vifaranga milioni 35.6 mwaka 2009/2010. Pia, vifaranga 330,000 vya kuku wazazi na mayai milioni 7.1 ya kutotolesha vifaranga yaliingizwa nchini ikilinganishwa na vifaranga 251,503 na mayai milioni 6.03 kwa mwaka 2009/2010. Vilevile, uzalishaji wa mayai uliongezeka kutoka bilioni 2.9 mwaka 2009/2010 hadi mayai bilioni 3.34 mwaka 2010/2011.

Katika juhudi za kuhamasisha ufugaji wa kuku wa asili, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo (*FAO*) na Halmashauri zimeendelea kuhamasisha teknolojia rahisi ya kukuza vifaranga kwa kasha maalum linaloweza kutumika kwenye maeneo ya vijijini ambako nishati ya umeme haipatikani kirahisi. Vilevile, wawakilishi 40 wa wadau wa tasnia ya kuku wamehamasishwa kuunda Chama cha Wazalishaji wa Kuku Nchini.

Katika mwaka wa 2011/2012, Wizara itaendelea kuhamasisha uzalishaji wa mayai na matumizi ya teknolojia sahihi za ufugaji wa kuku ikiwemo ya utumiaji wa kasha la kutunzia vifaranga katika Mikoa kumi ya Singida, Dodoma, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Pwani, Morogoro, Kagera, Arusha na Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji wa nguruwe nchini umeendelea kukua kutokana na kuongezeka kwa mahitaji. Katika mwaka 2010/2011, uzalishaji wa nyama ya nguruwe umeongezeka kwa asilimia 12.5 kutoka tani 38,180 mwaka 2009/2010 hadi tani 43,643. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kuimarisha uzalishaji wa nguruwe nchini kwa kuendeleza shamba la Ngerengere kwa kulipatia nguruwe wazazi madume watano kwa ajili ya kuzalisha na kusambaza kwa wafugaji. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika ufugaji wa nguruwe wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa ufugaji wa asili unahitaji kutenga maeneo ya malisho, kuyaendeleza na kuyasimamia ambapo ni pamoja na kutathmini uwezo wake na kuyawekea miundombinu muhimu. Katika mwaka 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na TAMISEMI zimetenga maeneo ya malisho hekta 858,995.45 na kufanya eneo lililotengwa kwa ajili hiyo kufikia hekta milioni 2.3 katika vijiji 440 vya Halmashauri za Wilaya 49.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuendeleza malisho ya mifugo nchini, ni muhimu kuhakikisha kwamba mbegu bora za malisho zinapatikana karibu na wafugaji. Katika mwaka 2010/2011, Wizara imeendelea kuimarisha mashamba yake ya mbegu za malisho ya Vikuge (Pwani), Langwira (Mbeya), Kizota (Dodoma), *PRC* Kongwa (Dodoma), Mabuki (Mwanza), *Sao Hill* (Iringa) na *LRC* (Tanga) kwa kuyapatia vitendea kazi muhimu.

Jumla ya tani 48 za mbegu bora za malisho na marobota 770,100 ya hei yamezalishwa na kusambazwa kwa wafugaji. Kati ya hayo, marobota 350,000 yamezalishwa kutoka katika mashamba ya Serikali na 420,100 kutoka sekta binafsi. Mbegu za malisho zilizozalishwa zimesambazwa kwa wafugaji na taasisi katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Morogoro, Mtwara na Pwani, pamoja na nchi ya Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha vikundi 1,265 vya wafugaji wa asili na kuwezesha uundaji wa uongozi wa juu wa Umoja wa Wafugaji Kanda ya Mashariki *(UWAKAMA)* kutoka Mikoa ya Pwani na Morogoro. Vilevile, kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali *Care International Tanzania*, jumla ya vyama vya kiraia 40 vilipatiwa mafunzo mbalimbali kuhusu Sheria za Ardhi na taratibu za kumilikishwa ardhi kwa wafugaji wa asili chini ya mfuko wa kuendeleza ufugaji wa asili *(Pastoral Basket Fund).* Mfuko huu unafadhiliwa na *Irish Aid* na *IFAD/ILC;*

(ii) Kushiriki katika usuluhishi wa migogoro ya matumizi ya ardhi kati ya mwekezaji na jamii ya wafugaji wa vijiji 22 vya Wilaya ya Ngorongoro;

(iii) Kuhamasisha na kuratibu mipango ya matumizi ya ardhi katika Wilaya nne za Kondoa, Kiteto, Bahi na Chamwino chini ya Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Nyanda za Malisho unaofadhiliwa na *IFAD* na *ILC*;

(iv) Kuwajengea uwezo wataalam kutoka Wilaya 45 kuhusu uzalishaji, uhifadhi na matumizi ya malisho na ukaguzi wa vyakula vya mifugo;

(v) Kutoa mafunzo kwa wataalam 40 katika Halmashauri 40 kuhusu matumizi ya *Geographical Information System (GIS);*

(vi) Kutoa mafunzo kuhusu ukusanyaji wa takwimu katika mfumo wa tahadhari ya majanga kwa wataalam 65 kutoka Mikoa ya Arusha (9), Dodoma (7), Kilimanjaro (9), Manyara (7), Mara (6), Mwanza (8), Shinyanga (10) na Singida (9); na

(vii) Kuandaa kanuni nne (4) za kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali ya Vyakula vya Wanyama Na. 13 ya Mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kukarabati na kuyawezesha mashamba nane ya kuzalisha mbegu bora za malisho ili kuzalisha tani 50 za mbegu na marobota 360,000 ya hei;

(ii) Kuratibu na kuwezesha Wiki ya Ufugaji wa Asili kwa kushirikiana na wadau mbalimbali;

(iii) Kuandaa kanuni chini ya Sheria Na. 13 ya Nyanda za Malisho na Vyakula vya Wanyama ya mwaka 2010;

(iv) Kuhamasisha matumizi endelevu ya raslimali ardhi ili kupunguza migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa rasilimali ardhi;

(v) Kuwezesha maandalizi ya mipango ya usimamizi wa maeneo yaliyopimwa na kutengwa kwa ajili ya malisho katika Halmashauri 50;

(vi) Kuwezesha ukusanyaji wa takwimu na kuandaa Mpango Mkakati wa kukabiliana na majanga ya mifugo, pamoja na kuandaa mafunzo ya *GIS* katika Halmashauri 10 kwa ajili ya kukusanya takwimu za hali ya malisho na maji kwa mifugo; na

(vii) Kuendelea kuimarisha mfumo wa tahadhari ya majanga ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usindikaji wa Vyakula vya Mifugo Wizara imeendelea kuratibu usindikaji na kusimamia ubora wa vyakula vya mifugo vinavyozalishwa na sekta binafsi ambayo imezalisha jumla ya tani 852,000 za vyakula vya mifugo kutoka katika viwanda 65. Katika mwaka 2010/2011, Wizara ilitoa mafunzo kwa Wakaguzi wa vyakula vya mifugo 63 kutoka Halmashauri 58 katika Mikoa 15 ya Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mbeya, Manyara, Pwani, Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Mara, Iringa, Morogoro na Tanga ili kuwajengea uwezo wa kudhibiti ubora wa vyakula vya mifugo. Katika mwaka 2011/2012. Wizara itazijengea uwezo Halmashauri 20 kuhusu udhibiti na ukaguzi wa vyakula vya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs)* iliwezesha kujenga malambo 62 na visima virefu 22 na kukarabati malambo 20. Kazi nyingine zilizotekelezwa na Wizara ni pamoja na:-

(i) Kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu uendelezaji na ukarabati wa miundombinu ya maji kwa mifugo katika Halmashauri za Ngorongoro, Nachingwea, Chunya, Kilindi na Serengeti; na

(ii) Kuandaa mfumo wa digitali wa kuorodhesha vyanzo vyote vya maji kwa ajili ya mifugo vilivyoendelezwa nchini.

Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau wengine kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu uendelezaji wa vyanzo vya maji kwa mifugo; na

(ii) Kuendelea kuorodhesha vyanzo vya maji vilivyoendelezwa kwa ajili ya mifugo kupitia mfumo wa digitali na kuanzisha benki ya takwimu katika Wilaya 15 za Mikoa ya Shinyanga, Arusha, Manyara, Kilimanjaro na Tanga. Mfumo huu utasaidia kujua mtandao wa vyanzo vya maji na mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kudhibiti magonjwa ya mifugo na hasa ya mlipuko. Jumla ya dozi milioni 2.8 za chanjo dhidi ya ugonjwa wa homa ya mMapafu ya ng'ombe zilinunuliwa kupitia mradi wa *Vaccines for Control of Neglected Animal Diseases in Africa (VACNADA)* unaofadhiliwa na Jumuia ya Ulaya, na kutumika kuchanja ng'ombe milioni 2.7 dhidi ya ugonjwa huo katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara. Aidha, dozi milioni tano zilinunuliwa kupitia mpango wa *Roll Back Vaccination* mwishoni mwa mwaka 2009/2010 ambapo ng'ombe milioni 4.5 walichanjwa katika Mikoa ya Shinyanga na Kagera. Pia, kupitia mpango huo, dozi milioni tatu za chanjo zilinunuliwa mwaka 2010/2011 kwa ajili ya kuendelea kuchanja mifugo dhidi ugonjwa huo katika Mikoa ya Kagera na Shinyanga. Vilevile, tathmini ya awali ya ugonjwa wa homa ya mapafu ya ng'ombe imefanyika katika Mikoa ya Singida, Kigoma na Tabora na imeonyesha kuwa ugonjwa huo umepungua.

Katika mwaka 2011/2012, Wizara itawezesha na kuendelea kuratibu uchanjaji wa ng'ombe milioni tano katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa na Kaskazini chini ya mpango wa *Roll Back Vaccination*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mradi wa *VACNADA* mbuzi na kondoo milioni 1.25 wamechanjwa dhidi ya ugonjwa wa Sotoka ya mbuzi na kondoo *(PPR)* katika Mikoa ya Arusha na Mara. Kazi nyingine zilizotekelezwa kupitia mradi huu ni:-

(i) Kujengea uwezo wataalam 33 wa maabara kutoka vituo vyote saba vya uchunguzi wa magonjwa ya mifugo *(VICs)* na Maabara Kuu ya Mifugo *(CVL)* Temeke;

(ii) Kuwezesha mafunzo kwa watumishi 20 kutoka Halmashauri zote za Mkoa wa Arusha na Halmashauri za Tarime, Rorya na Serengeti mkoa wa Mara;

(iii) Kununua vifaa vya maabara na dawa kwa ajili ya uchunguzi wa magonjwa ya homa ya mapafu ya ng'ombe na Sotoka ya mbuzi na kondoo kwa Maabara za *CVL, VIC* Mwanza na Arusha; na

(iv) Kugharimia huduma za chanjo na kutengeneza vipeperushi 11,000 kwa ajili ya kuhamasisha udhibiti wa magonjwa ya mlipuko.

Katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na *FAO* itawezesha na kuendelea kuratibu uchanjaji wa mbuzi na kondoo milioni tatu katika Mikoa ya Kanda ya Kusini na Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkakati wa Kudhibiti Ugonjwa wa Miguu na Midomo *(FMD)* umeendelea kutekelezwa na Wizara kupitia Mradi wa Kuimarisha Uwezo wa Kudhibiti Magonjwa ya Mlipuko ya Mifugo *(SADC-TADs).* Sampuli 30 za nyati zilichukuliwa kutoka Hifadhi ya Taifa ya Katavi na ng'ombe 60 katika maeneo yanayozunguka hifadhi hiyo ili kubaini aina ya virusi vya ugonjwa. Aidha, sampuli nyingine 71 zilichukuliwa katika Halmashauri 20 za Mkuranga, Missenyi, Karagwe, Ulanga, Kilombero, Bagamoyo, Kibaha, Rufiji, Ngorongoro, Newala, Nachingwea, Mtwara, Sengerema, Muleba, Sumbawanga (Mjini), Sumbawanga (Vijijini), Iringa Manispaa, Misungwi, Serengeti na Tarime. Sampuli hizi zinafanyiwa uchunguzi katika Maabara za Botswana, Afrika ya Kusini, Uingereza na hapa nchini. Matokeo ya uchunguzi huu yatawezesha

kutengenezwa kwa chanjo stahili ambayo itakinga ugonjwa uliopo. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kutekeleza mkakati wa kudhibiti Ugonjwa wa Miguu na Midomo *(FMD).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkakati wa Tahadhari dhidi ya ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege umeendelea kutekelezwa ambapo hadi sasa, hakuna taarifa za kuwepo kwa ugonjwa huu hapa nchini. Hata hivyo, Tanzania bado ipo katika hatari ya kupatwa na ugonjwa huu kutokana na urahisi wa kusafirisha mazao ya mifugo ulivyo sasa, ikizingatiwa kuwa ugonjwa umeendelea kuwepo Misri na Vietnam, hivyo tahadhari ya ugonjwa inabidi kuendelezwa. Taarifa kutoka Shirika la Afya ya Wanyama Duniani *(OIE)* na *FAO* zinaonyesha kuwa hadi kufikia mwezi Juni, 2011, nchi 62 duniani zilikuwa zimeambukizwa ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege. Kati ya hizo, nchi 11 ni za Bara la Afrika ambazo ni Nigeria, Misri, Niger, Cameroon, Burkina Faso, Sudan, *Cote d'Ivore,* Djibouti, Ghana, Benin na Togo. Hadi sasa, nchi 50 kati ya hizo, zimeweza kudhibiti ugonjwa huo na nchi 12 zilizobakia zinaendelea kuudhibiti kwa lengo la kuutokomeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara ilitekeleza kazi zifuatazo ili kudhibiti tishio la Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege:-

(i) Kuijengea uwezo Maabara Kuu ya Mifugo - Temeke kuchunguza na kutambua virusi vya ugonjwa;
(ii) Kufuatilia ugonjwa huo, kwenye njia kuu za mapitio ya ndege pori na katika makundi ya kuku na bata wafugwao ambapo jumla ya sampuli 2,200 za ndege pori, kuku na bata zilichunguzwa na kuthibitishwa kutokuwepo kwa ugonjwa nchini;

(iii) Kuzuia uingizaji wa ndege, kuku na mazao yake kutoka nchi zilizoathirika na ugonjwa huo;

(iv) Kutoa elimu kwa watotoleshaji na wadau 40 kuhusu kanuni za utotoleshaji wa vifaranga;

(v) Kuandaa Mwongozo wa Ufugaji Bora ambao utachapishwa na kusambazwa kwa wadau;

(vi) Kufanya marejeo ya Mpango wa Tahadhari na Udhibiti wa Mafua Makali ya Ndege na Binadamu;

(vii) Kununua magari manne kuwezesha utekelezaji wa mkakati wa kudhibiti Mafua Makali ya Ndege;

(viii) Kujenga uwezo wa wadau 44 kutoka Halmashauri katika mikoa ya Kanda ya Ziwa Victoria kupitia mradi wa Kudhibiti Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege unaotekelezwa na nchi za Mashariki ya Afrika zikiwemo Kenya, Tanzania, Uganda, Sudan na Ethiopia; na

(ix) Kufanya tathmini ya Mnyororo wa Thamani *(Poultry Value Chain Analysis)* katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Dodoma na Singida kwa lengo la kuboresha ufugaji wa kuku wa asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012 Wizara itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kukamilisha na kusambaza Mpango Mkakati wa Tahadhari dhidi ya Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege *(National Influenza Emergency Preparedness and Response Plan);* na

(ii) Kurejea na kuboresha Mpango Mkakati wa Mawasiliano katika Tahadhari na udhibiti wa Mafua Makali ya Ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea na mkakati wa kudhibiti Ugonjwa wa Mdondo nchini kwa kusambaza chanjo katika Halmashauri kupitia vituo vya kanda vya uchunguzi wa magonjwa ya mifugo. Tathmini ya matumizi ya chanjo hii inaonyesha kupungua kwa vifo vya kuku kutoka asilimia 90 hadi nne katika maeneo ambayo chanjo ilitumika. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itakamilisha Mpango Mkakati wa Udhibiti wa Mdondo na kuanzisha kampeni ya Kitaifa ya chanjo dhidi ya ugonjwa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, matukio ya ugonjwa wa Homa ya Nguruwe *(African Swine Fever – ASF)* yaliripotiwa katika Mikoa ya Mbeya, Iringa na Dar es Salaam ambapo jumla ya nguruwe 11,445 wamekufa katika Halmashauri za Kyela 966; Rungwe 1,933; Ileje 14; Mbarali 2,919; Mbeya Vijijini 322; Jiji la Mbeya 1,476; Mbozi 505; Chunya 2,058; Ludewa 572; Makete 80; Kinondoni 423; Temeke 129 na Ilala 48. Aidha, katika kudhibiti ugonjwa huo Mikoa ya Mbeya, Iringa na Dar es Salaam iliwekwa chini ya karantini na masharti kulegezwa pale ugonjwa ulipoonyesha kupungua. Pia, Wizara imenunua pampu za injini nne, dawa aina za *V-Rid* lita 200 na *Formalin* lita 200 na kuzisambaza kwa ajili ya kupulizia mabanda 4,135 na magari 1,970 na vizuizi 11 vya ukaguzi vimeanzishwa katika maeneo hayo. Vilevile, wafugaji walihamasishwa kujenga mabanda bora ya nguruwe, ambapo mabanda 3,815 yamejengwa na kupuliziwa dawa. Pia, Wizara imechapisha mabango 1,000 na vipeperushi 5,000 kuhusu tahadhari na udhibiti wa ugonjwa huo na kuvisambaza. Pia, Wizara ilitoa elimu kupitia vyombo vya habari.

Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri kutoa elimu kwa wafugaji na kudhibiti usafirishaji holela wa nguruwe na mazao yake ili kuudhibiti ugonjwa huu ambao bado hauna tiba wala kinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Udhibiti wa Kupe na Magonjwa Wanayoeneza, magonjwa yaenezwayo na kupe yanachangia zaidi ya asilimia 70 ya vifo vya ng'ombe vinavyotokea kila mwaka na kuleta athari kubwa kwa afya na uzalishaji mifugo.

Katika mwaka 2010/2011, Serikali kupitia *DADPs* na *DASIP* ilikarabati majosho 30 na kujenga majosho mapya 37 na hivyo kufikisha idadi ya majosho yanayofanya kazi 1,756. Aidha, kupitia mpango wa ruzuku ya dawa za kuogesha mifugo, Serikali ilinunua lita 109,389 za dawa ya kuogesha mifugo kwa gharama ya shilingi bilioni 1.82 na kuzisambaza katika Mikoa 21. Ruzuku inayotolewa na Serikali ni asilimia 40 na wafugaji wananunua dawa hizo kwa asilimia 60 ya bei ya soko. Pia, kwa kushirikiana na sekta binafsi, ng'ombe 133,944 walichanjwa dhidi ya ugonjwa hatari wa ndigana kali katika Mikoa 15 ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Pwani, Singida, Tabora na Tanga.

Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri katika kuhamasisha ukarabati wa majosho na kujenga mapya na ununuzi wa lita 80,000 za dawa ya ruzuku ya kuogesha mifugo. Pia, itanunua dozi 105,000 za chanjo ya ndigana kali kwa ajili ya kutekeleza mkakati wa kudhibiti magonjwa yaenezwayo na kupe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ugonjwa wa Nagana unaoenezwa na Mbung'o, mbali na kusababisha vifo pia hudumaza mifugo. Katika mwaka 2010/2011, kazi zilizofanyika ili kukabiliana na ugonjwa huu ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuhamasisha na kutoa elimu kwa wafugaji 196 katika Wilaya ya Nachingwea Mkoa wa Lindi na 178 katika Wilaya za Kisarawe 53, Rufiji 29 na Bagamoyo 96 Mkoa wa Pwani kuhusu udhibiti shirikishi wa mbung'o na ndorobo;

(ii) Kununua mitego ya mbung'o 155, vitambaa vya kutengenezea vyambo mita 4,000, viuatilifu aina ya *Glossinex* lita 35, mabomba ya kunyunyizia viuatilifu 150, *'masks'* za mdomo na pua 2,000 na glovu 1,000. Vifaa hivyo vilisambazwa katika Halmashauri za Mikoa ya Rukwa (Mpanda, Nkasi na Hifadhi ya Taifa ya Katavi); Lindi (Lindi Vijijini, Kilwa, Nachingwea); Pwani (Kisarawe, Bagamoyo, Rufiji); Kigoma (Kibondo); Tabora (Urambo); Tanga (Handeni na Pangani); Arusha (Monduli); Kagera (Karagwe, Missenyi); na Taasisi ya Utafiti wa Ndorobo – Tanga;

(iii) Kufanya uchunguzi na tathmini ya mtawanyiko wa mbung'o katika Mikoa ya Rukwa, Dodoma na Singida ili kuchora ramani mpya. Aidha, tathmini ya awali ya mtawanyiko wa mbung'o inaonesha kupungua kwa eneo lenye mbung'o hapa nchini kutoka asilimia 60 mwaka 1967 hadi asilimia 43 mwaka 2010 kutokana na udhibiti wa mbung'o, shughuli za kilimo na makazi. Maeneo yenye kukaliwa zaidi na mbung'o ni Mbuga na Hifadhi za Wanyamapori; na

(iv) Kuendelea kutekeleza Mpango wa Kutokomeza Mbung'o na Ndorobo Barani Afrika *(Pan African Tsetse and Trypanosomosis Eradication Campaign - PATTEC)* kwa kufuatilia taarifa za ugonjwa wa nagana katika Mikoa ya Rukwa, Pwani na Manyara na kununua vifaa vya uchoraji ramani na kompyuta.

(v) Aidha, mafunzo kuhusu matumizi ya mtandao wa kutathmini mtawanyiko wa malale yametolewa kwa wataalam 15 wa Wizara za Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na Afya na Ustawi wa Jamii, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu *(NIMR)* na Taasisi ya Utafiti wa Raslimali ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *(IRA).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea na utekelezaji wa mkakati wa kudhibiti mbung'o na ndorobo kwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuhamasisha Halmashauri za Mikoa ya Arusha, Singida na Tanga kuhusu matumizi ya mbinu shirikishi na endelevu za kudhibiti mbung'o na ndorobo;

(ii) Kununua vifaa vya kudhibiti mbung'o na ndorobo kama viuatilifu, mitego na vyambo vya kuua mbung'o na kuvisambaza katika Halmashauri za Mikoa ya Lindi, Pwani, Tabora, Morogoro na Dodoma; na

(iii) Kuchunguza na kutathmini mtawanyiko wa mbung'o na kuchora ramani mpya katika Mikoa ya Mbeya, Pwani na Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kudhibiti magonjwa ya mifugo yanayoambukiza binadamu yakiwemo Kichaa cha Mbwa, Homa ya Bonde la Ufa, Kimeta, Kutupa Mimba na Kifua Kikuu cha Ng'ombe kwa kutekeleza yafuatayo:-

Katika mwaka 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia Mradi unaofadhiliwa na Taasisi ya *Bill and Melinda Gates* imeendelea kutekeleza mkakati wa kudhibiti Kichaa cha Mbwa katika Halmashauri 24 za Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Mtwara, Lindi, Morogoro kwa Tanzania Bara na Kisiwa cha Pemba kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Jumla ya mbwa 61,895 na paka 6,098 wamechanjwa na zoezi la kuchanja bado linaendelea. Pia, pikipiki 17 zilinunuliwa na kusambazwa katika Halmashauri zinazotekeleza mradi.

Aidha, Wizara ilinunua na kusambaza dozi 100,000 za chanjo katika Halmashauri 97 zilizopo nje ya eneo la Mradi huo ambapo jumla ya mbwa 93,280 walichanjwa. Vilevile, Halmashauri 17 na sekta binafsi walinunua na kusambaza dozi 49,736 ambapo mbwa 35,153 na paka 6,589 walichanjwa.

Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kudhibiti Kichaa cha Mbwa kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuendelea kutekeleza Mradi wa kudhibiti Kichaa cha Mbwa kwa kununua na kusambaza dozi 100,000 za chanjo katika Halmashauri 24 zilizopo kwenye mradi;

(ii) Kuhamasisha na kuratibu kampeni za uchanjaji kwa lengo la kuchanja mbwa na paka 200,000 kwenye maeneo ya nje ya mradi; na

(iii) Kuandaa maadhimisho ya Siku ya Kichaa cha Mbwa Duniani yanayofanyika tarehe 28 Septemba ya kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinga dhidi ya ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa iliendelea kutolewa kwa ng'ombe, mbuzi na kondoo katika Halmashauri zilizokuwa katika hatari ya kupata ugonjwa huo kufuatia mlipuko wa ugonjwa huo uliotokea mwezi Januari, 2007. Katika mwaka 2010/2011, Wizara ilinunua jumla ya dozi 500,000 za chanjo na kuzisambaza katika Halmashauri sita za Simanjiro, Mpwapwa, Babati, Ngorongoro, Chamwino, na Monduli. Jumla ya ng'ombe 149,409, mbuzi 154,835 na kondoo 160,414 walichanjwa. Aidha, elimu kuhusu ugonjwa huo na hatua za kuchukua ili kuudhibiti ilitolewa kwa wananchi katika maeneo hayo.

Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kudhibiti Ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa kwa kununua dozi milioni moja na kuzisambaza katika Halmashauri 15 zilizo kwenye maeneo hatari ya kupata ugonjwa huo. Pia, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu ugonjwa huo na kuwashauri hatua za kuchukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa ugonjwa wa Kimeta uliendelea nchini katika maeneo ya Halmashauri yaliyotolewa taarifa kuwa na ugonjwa huo. Maeneo hayo yanajumuisha Pori la Akiba la Maswa na eneo linalozunguka Mto Rufiji. Ili kukinga mifugo iliyoko katika maeneo hayo, jumla ya ng'ombe 58,000 walipatiwa chanjo ya kuzuia Kimeta.

Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kuratibu udhibiti wa ugonjwa wa kimeta katika Halmashauri zitakazokuwa katika hatari ya kupata ugonjwa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kudhibiti ugonjwa wa Kutupa Mimba kwa kupima viwango vya maambukizi ya ugonjwa huo. Katika mwaka 2010/2011, jumla ya ng'ombe 1,844, mbuzi tisa, kondoo wawili na ngamia wawili walipimwa ugonjwa wa Kutupa Mimba ambapo ng'ombe 252 walithibitika kuwa na ugonjwa huo.

Katika mwaka 2011/2012, Wizara itafanya uchunguzi wa ng'ombe 5,000, mbuzi 2,500 na kondoo 2,500 dhidi ya ugonjwa huo katika mashamba ya kuzalisha mitamba, ranchi za Taifa pamoja na mashamba ya Taasisi za umma na ya sekta binafsi nchini. Aidha, Wizara itanunua chanjo dozi 100,000 kwa ajili ya udhibiti wa ugonjwa huo kwenye mashamba ya mifugo ya Serikali na ya sekta binafsi. Pia, Wizara itaandaa Mkakati na Kanuni za kusimamia udhibiti wa Ugonjwa wa Kutupa Mimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuimarisha Vituo vya Ukaguzi wa Mifugo na Mazao yake ili kuviwezesha kufuatilia usafirishaji wa mifugo na mazao yake kutoka ndani na nje ya nchi. Kwa sasa vipo vituo vya ukaguzi 36 vilivyoko mipakani, viwanja vya ndege, bandari, reli na nchi kavu; vituo 19 vya kupumzikia mifugo na vituo 381 vilivyo chini ya Halmashauri. Katika mwaka 2010/2011 Wizara ilitekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Vituo 11 vya ukaguzi vimeimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi zikiwemo pikipiki 11 na kompyuta;

(ii) Kituo cha karantini cha Kwala (Kibaha) kimeimarishwa kwa kujenga zizi la mbuzi na kuweka vibao vya kuonyesha mipaka ya Kituo; na

(iii) Kusimamia uingizaji wa vifaranga vya kuku wa mayai 719,963 na mayai ya kutotolesha vifaranga 8,231,207 na kukagua ng'ombe 1,041 na mazao ya mifugo kabla ya kusafirisha nje ya nchi.

Katika mwaka 2011/2012 Wizara itaendelea kuimarisha vituo 18 kwa kuvipatia vitendea kazi pamoja na mafunzo kwa wataalam kuhusu utambuzi na ufuatiliaji wa magonjwa ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara imeendelea kusimamia usalama na ubora wa vyakula vitokanavyo na mifugo. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Viwango la Taifa ilitoa mafunzo kwa wataalam 40 juu ya uandaaji wa viwango vya vyakula na 25 kuhusu udhibiti wa usalama na ubora wa vyakula. Aidha, jumla ya vipeperushi 1,000 vya kuelimisha jamii kuhusu usalama na ubora wa maziwa na nyama viliandaliwa na kutolewa kwa wadau katika maonyesho ya Nane Nane. Vilevile, vipindi vya redio kuhusu usalama na ubora wa chakula viliandaliwa na kurushwa hewani.

Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kusimamia usalama na ubora wa vyakula vitokanavyo na mifugo kwa kuandaa vijarida 2,000 na vipindi viwili vya redio vya kuhamasisha jamii. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na *FAO* itaendelea kuwajengea uwezo wa kudhibiti usalama wa vyakula wataalam 25. Pia, Wizara kwa kushirikiana na nchi za *SADC* itaandaa mpango wa kuboresha usalama na ubora wa vyakula vitokanavyo na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Chakula na Dawa *(TFDA)* iliendelea kusimamia ubora wa dawa, chanjo na vifaa tiba vinavyoingizwa nchini kwa ajili ya magonjwa ya mifugo. Aidha, jamii imeendelea kuhamasishwa kutumia pembejeo za mifugo ambazo zimesajiliwa. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu nchini *(TPRI)* ilisimamia uingizaji wa viuatilifu vinavyoingia nchini.

Jumla ya maduka 50 ya pembejeo za mifugo, katika Kanda za Ziwa 10 na Nyanda za Juu Kusini 40 na viwanda vitatu vya kusindika vyakula vya mifugo vilikaguliwa na ushauri juu ya hifadhi ya malighafi na vyakula vilivyosindikwa ili kudhibiti ubora na usalama ulitolewa.

Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kusimamia ubora na usalama wa pembejeo za mifugo ili kuwahakikishia wafugaji upatikanaji wake. Aidha, wakaguzi 30 watapatiwa mafunzo juu ya udhibiti wa pembejeo za mifugo na ukaguzi wa maduka ya pembejeo za mifugo utafanyika katika Mikoa ya kanda za Kati na Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara ilifanya ukaguzi wa machinjio 83 katika Halmashauri za Wilaya na Manispaa za Mikoa ya Mwanza, Kagera, Shinyanga, Mbeya, Iringa, Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Tanga na Mara kwa lengo la kudhibiti usafi na ubora wa nyama na ngozi zinazozalishwa kwenye machinjio hayo. Kati ya hizo, machinjio 44 zilifikia vigezo vilivyowekwa na hivyo kuingizwa kwenye mchakato wa kusajiliwa. Aidha, wamiliki wa machinjio 39 zilizokosa sifa za usajili walipewa ushauri ili waweze kufikia vigezo vya kuwawezesha kusajiliwa. Pia, katika ukaguzi wa nyama, jumla ya ng'ombe 1,059,513, mbuzi 455,697, kondoo 181,398, kuku 3,054,453 na nguruwe 115,956 walichinjwa na kukaguliwa.

Katika mwaka 2011/2012, Wizara itatoa mafunzo rejea kwa wakaguzi 113 wa nyama na ngozi katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na Kati pamoja na kuendelea na zoezi la ukaguzi wa machinjio na uhakiki wa ubora wa ukaguzi wa nyama na ngozi katika Kanda hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Biashara ya Mifugo na Mazao Yake, Wizara imeendelea kuratibu biashara ya mifugo kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara. Idadi ya mifugo iliyouzwa minadani imeongezeka kutoka ng'ombe 857,208, mbuzi 682,992 na kondoo 122,035 wenye thamani ya shilingi bilioni 382.4 mwaka 2009/2010 hadi kufikia ng'ombe 925,097, mbuzi 704,987 na kondoo 168,313 wenye thamani ya shilingi bilioni 423.9 mwaka 2010/2011. Ongezeko hilo la idadi ya mifugo iliyouzwa linatokana na kuimarishwa kwa huduma za minada, kuongezeka kwa mahitaji ya nyama katika miji na masoko maalum kama maduka ya kisasa, hoteli na migodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, mifugo iliyouzwa nchi za nje (Comoro, Rwanda na Kenya) ni ng'ombe 1,041 na mbuzi 657 wenye thamani ya shilingi milioni 965.4. Aidha, tani 20.3 za nyama ya ng'ombe, tani 286 za nyama ya mbuzi na tani 97 za nyama ya kondoo zenye thamani ya shilingi bilioni 1.6 ziliuzwa katika nchi za Oman na Kuwait.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukusanyaji wa ngozi umeendelea kuongezeka na hivyo kuongeza kasi ya usindikaji na mauzo ya ngozi. Jumla ya vipande milioni 2.5 vya ngozi za ng'ombe, milioni 2.4 vya mbuzi na 200,000 vya kondoo vyenye thamani ya shilingi bilioni 16.1 vilikusanywa ikiwa ni ongezeko la asilimia 89.4 ya thamani ya ngozi zilizokusanywa ikilinganishwa na shilingi bilioni 8.5 mwaka 2009/2010.

Kati ya vipande vya ngozi vilivyokusanywa, vipande vya ngozi za ng'ombe 1,719,506; mbuzi 2,111,176 na kondoo 83,600 viliuzwa nje ya nchi kwa thamani ya shilingi bilioni 17.4 ikilinganishwa na vipande vya ngozi za ng'ombe 739,315, mbuzi 1,900,000 na kondoo 176,400 vilivyouzwa nje ya nchi kwa thamani ya shilingi bilioni 8.2 mwaka 2009/2010 sawa na ongezeko la asilimia 112.2. Ongezeko hili, pamoja na masuala mengine, limechangiwa na kuimarika kwa soko la ngozi duniani na kufanya mahitaji na bei ya ngozi hapa nchini kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuhamasisha usindikaji wa ngozi ambapo vipande vya ngozi zilizosindikwa vimeongezeka kutoka vipande vya ngozi za ng'ombe 275,000 na vya mbuzi 1,440,000 vyenye thamani ya shilingi bilioni 6.2 mwaka 2009/2010 hadi kufikia vipande

vya ngozi za ng'ombe 782,447; vya mbuzi 1,535,562 na vya kondoo 61,200 vyenye thamani ya shilingi bilioni 10.6 mwaka 2010/2011. Kuongezeka kwa idadi ya ngozi zilizosindikwa kumetokana na kuimarika kwa soko; kuongezeka kwa ubora wa ngozi; kuimarisha udhibiti wa ulipaji wa ushuru kwa ngozi ghafi zinazosafirishwa nje ya nchi na kuhamasisha wafanyabiashara, wanaouza ngozi ghafi nje ya nchi na wawekezaji, kusindika ngozi hapa nchini. Hatua hizi zimechangia kuongezeka kwa kiwanda kipya cha *Petro City* na kupanuliwa kwa viwanda vya Moshi *Leather Industries* na *Himo Tannery* na kufanya viwanda vya kusindika ngozi kufikia nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kusimamia na kutekeleza mkakati wa kufufua na kuendeleza sekta na viwanda vya ngozi nchini kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Halmashauri 65 na Chama cha Wadau wa Ngozi. Katika mwaka 2010/2011, Wizara kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo *(Livestock Development Fund)* imeimarisha huduma za ugani kwa kununua pikipiki 10 na kuzisambaza katika Halmashauri za Bagamoyo, Chato, Karagwe, Kibaha, Kilosa, Misenyi, Morogoro, Mpanda, Mvomero na Sumbawanga. Aidha, jumla ya visu 6,500 vya kuchunia, 3,200 vya kuwekea mikato ya awali, vinoleo 3,200 na vifaa 130 vya kunyanyulia mnyama anayechunwa vimesambazwa katika Halmashauri zote zinazotekeleza mkakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudi za kutoa elimu ya uboreshaji wa zao la ngozi, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, Halmashauri na Chama cha Wadau wa Ngozi *(LAT)* imetoa mafunzo kwa wadau 14,855 wakiwemo wafugaji 6,433, wachinjaji/wachunaji 2,225, wawambaji na wachambuzi wa madaraja 1,229, wasindikaji 313, wafanyabiashara 1,067, maafisa ugani 1,772 na wadau wengine 1,816. Vilevile, Wizara imezindua Kamati ya Ushauri wa Ngozi ambayo imeainishwa kwenye Sheria ya Ngozi Na. 18 ya Mwaka 2008. Kamati hiyo ina jukumu la kushauri juu ya maendeleo ya tasnia ya ngozi nchini. Aidha, Sheria hiyo imetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili, kuchapishwa na kusambazwa katika Halmashauri zote nchini. Pia, Mwongozo wa Uzalishaji Bora wa Ngozi umeandaliwa na kusambazwa katika Halmashauri zote.

Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kutekeleza mkakati huo kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuendelea kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali ili kuboresha zao la ngozi;

(ii) Kuwezesha uendeshaji wa Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa ngozi ili iweze kutekeleza majukumu yake;

(iii) Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Ngozi na kanuni zake; na

(iv) Kusimamia ulipaji wa ushuru wa ngozi ghafi zinazouzwa nje ya nchi kwa lengo la kuwezesha ngozi zote ghafi kusindikwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu imara ya masoko ya mifugo ni muhimu katika kuboresha biashara ya mifugo na mazao yake. Katika mwaka 2010/2011, Wizara imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kukarabati minada ya upili ya Pugu na Kizota;

(ii) Kununua mizani ya kupima uzito wa mifugo kwa ajili ya minada ya Pugu, Mhunze, Weruweru na Themi;

(iii) Kukusanya, kuchambua, kuhifadhi na kusambaza taarifa za masoko ya mifugo kutoka minada 53; na

(iv) Kuhamasisha ukusanyaji wa maduhuli ya minadani ambapo jumla ya shilingi bilioni 4.1 zilikusanywa ikiwa ni ongezeko la asilimia 51.8 ikilinganishwa na shilingi bilioni 2.7 mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kukusanya na kutoa taarifa za masoko kutoka minada 53 iliyounganishwa na Mtandao wa mawasiliano (*LINKS)*. Pia, Wizara itaweka mizani kwenye minada ya Igunga, Ipuli, Korogwe na Meserani. Vilevile, Wizara itatoa mafunzo kuhusu ukusanyaji wa takwimu kwa wataalam 120 wanaosimamia minada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji Mifugo na Mazao Yake, Wizara imeendelea kuimarisha Mfumo wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji Mifugo na Mazao yake. Katika mwaka 2010/2011, madaftari ya usajili 2,211 na chapa 4,057 zimesambazwa katika Halmashauri 17 katika Mikoa ya Arusha (chapa 606 na madaftari ya usajili 846), Dodoma (chapa 306, madaftari 153), Shinyanga (chapa 896, madaftari 448), Mwanza (chapa 1,236, madaftari 618), na Kagera (chapa 773, madaftari 386). Kazi nyingine zilizofanyika ni:-

(i) Kutoa mafunzo kwa wataalam 110 kutoka Halmashauri za Kanda ya Ziwa juu ya Mfumo wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo; Kutoa mafunzo kwa Wakaguzi wa Ustawi wa Wanyama 95 kutoka Halmashauri za Nyanda na Juu Kusini 30 na Kanda ya Ziwa 65 juu ya usimamizi wa Sheria ya Ustawi wa Wanyama;

(ii) Kuandaa nakala 5,000 za vipeperushi vya kitaaluma na kuvisambaza wakati wa maonesho ya Nane Nane ya mwaka 2010, wiki ya Utumishi wa Umma, wiki ya Uhamasishaji wa Unywaji wa Maziwa na matukio mengine ya Kitaifa;

(iii) Kusajili wafugaji 8,185 na kuwatambua kwa chapa ya kitaifa *(branding)* ng'ombe 93,793 katika Mikoa ya Kagera, Mara, Shinyanga, na Mwanza; na

(iv) Kuunda na kuzindua Baraza la Ushauri wa Ustawi wa Wanyama kwa mujibu wa Sheria ya Ustawi wa Wanyama, Sura ya 154 *(The Animal Welfare Act, Cap 154)* na kuliwezesha kufanya vikao viwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kutoa mafunzo kwa wataalam 100 wa mifugo katika Halmashauri kuhusu usimamizi na uendeshaji wa mfumo wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji mifugo na mazao yake;
(ii) Kutengeneza benki ya takwimu ya kitaifa ya kumbukumbu za utambuzi, usajili na ufuatiliaji mifugo *(Livestock Identification and Traceability Database);*

(iii) Kuratibu utekelezaji wa mfumo wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji mifugo katika ufugaji wa asili na ufugaji wa kibiashara kwa kusajili wafugaji 300,000 na kutambua ng'ombe 600,000;

(iv) Kuwajengea uwezo Wakaguzi 200 wa Halmashauri kuhusu usimamizi wa Sheria ya Ustawi wa Wanyama;

(v) Kutoa elimu kuhusu Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji mifugo kwa wafugaji na wadau wengine;

(vi) Kuratibu na kusimamia uzingatiaji wa ustawi wa wanyama nchini; na

(vii) Kuliwezesha Baraza la Ushauri la Ustawi wa Wanyama kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliendelea kutoa huduma za ushauri kwa wafugaji ili kuwawezesha kuongeza ubora wa mifugo na mazao yatokanayo na mifugo na hivyo kuongeza tija. Katika mwaka 2010/2011, Wizara ilisambaza kwa wadau nakala za vipeperushi 52,000, mabango 30,000 na vijitabu 13,000 kuhusu ufugaji bora kwa Halmashauri zote nchini.

Aidha, vipindi 52 vya redio na 12 vya televisheni viliandaliwa na kurushwa hewani. Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri katika Mikoa ya Arusha, Dodoma, Kagera, Kilimanjaro, Manyara, Mwanza, Tabora na Tanga ilitoa mafunzo kwa wafugaji 8,796 kuhusu ufugaji wa kibiashara kupitia vyuo sita vya mafunzo ya mifugo *(LITIs)* na vyuo vya mafunzo ya wafugaji *(FTCs)* vya Mabuki na

Kikulula. Pia, Wizara ilitoa mafunzo kuhusu upangaji wa mipango shirikishi ya ugani kwa wataalam 26 wa Kanda ya Ziwa na mbinu za Shamba Darasa kwa wataalam 32 wa Kanda za Kati na Kusini. Vilevile, Wizara kupitia mradi wa *EAAPP* ilitoa mafunzo kwa wafugaji 84 kutoka Kanda za Nyanda za Juu Kusini na Mashariki kuhusu usindikaji wa maziwa na bidhaa zake.

Aidha, wafugaji 18 kutoka Kanda za Nyanda za Juu Kusini na Mashariki walishiriki kwenye ziara ya mafunzo nchini Kenya kuhusu usindikaji, masoko ya maziwa na ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara itatekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kuchapisha na kusambaza kwa wadau nakala 50,000 za vipeperushi, 15,000 za mabango na 7,000 za vijitabu kuhusu ufugaji bora wa mifugo;

(ii) Kuandaa na kurusha hewani vipindi vya redio 26 na vya televisheni sita kuhusu ufugaji bora wa mifugo;

(iii) Kutoa mafunzo kwa wataalam wakufunzi 50 wa ugani kutoka Halmashauri za Mikoa ya Kanda za Kusini na Mashariki kuhusu mbinu shirikishi ya Shamba Darasa;

(iv) Kutoa mafunzo kwa wataalam 60 wa ugani kuhusu Upangaji wa Mipango Shirikishi ya Ugani na Shamba Darasa kutoka Wilaya 23 za Kanda za Nyanda za Juu Kusini na Mashariki;

(v) Kuimarisha Kitengo cha Ugani kwa kukipatia vitendea kazi;

(vi) Kushirikiana na Halmashauri kutoa mafunzo kwa wafugaji 5,000 kuhusu ufugaji bora na wa kibiashara;

(vii) Kukarabati na kuimarisha vituo viwili vya mafunzo kwa wafugaji vya Mabuki (Mwanza) na Kikulula (Kagera) na kuanzisha kituo kipya katika Wilaya ya Rorya (Mara) ili viweze kutoa mafunzo kwa wafugaji wengi zaidi;

(viii) Kushirikiana na wadau wengine kuandaa na kushiriki katika maadhimisho mbalimbali ya Kitaifa ikiwa ni pamoja na Nane Nane na Siku ya Chakula Duniani; na

(ix) Kushirikiana na Nchi za Afrika Mashariki na Kati kutekeleza mradi wa *EAAPP* unaolenga kuongeza tija katika Sekta ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa wadau kuhusu athari za uvuvi haramu, matumizi bora ya raslimali za uvuvi, utunzaji wa mazingira, mbinu shirikishi za usimamizi wa raslimali za uvuvi na ukuzaji wa viumbe kwenye maji nchini. Elimu hiyo ilitolewa kwa wavuvi 1,015 kutoka Halmashauri 14 za Mafia, Rufiji, Mkinga, Muheza, Mwanga, Moshi Vijijini, Singida vijijini, Babati, Iramba, Mpwapwa, Manispaa ya Singida, Jiji la Tanga na Manispaa za Dar es Salaam. Pia, elimu ya ufugaji wa samaki ilitolewa kwa wakulima 147 katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Singida, Dodoma na Manyara. Aidha, vipindi 52 vya radio na 15 vya luninga viliandaliwa na kurushwa hewani. Vilevile, mabango 10, vitabu 2,118 na vipeperushi 6,425 kuhusu mbinu bora za ufugaji wa samaki na hifadhi ya mazao ya uvuvi zimechapishwa na kusambazwa kwa wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara itatekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kuandaa na kurusha hewani vipindi 26 vya redio na sita vya televisheni kuhusu uvuvi endelevu;

(ii) Kutoa mafunzo rejea ya ukuzaji bora wa viumbe kwenye maji kwa Maafisa Ugani 50 na wafugaji wa samaki 300 katika Halmashauri 15;

(iii) Kuandaa na kusambaza mabango sita, vijitabu 1,500 na vipeperushi 2,500 kuhusu uvuvi endelevu na ukuzaji bora wa viumbe kwenye maji; na

(iv) Kutoa mafunzo ya kuhimiza shughuli mbadala za kiuchumi kama vile ufugaji wa samaki, ng'ombe na mbuzi wa maziwa, kuku na ukulima wa bustani za mboga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika; na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI ilifanya uchambuzi wa taarifa ya matokeo ya Sensa ya Mifugo iliyofanyika kwa Njia ya Sampuli mwaka 2007/2008. Aidha, Wizara chini ya Mradi wa Benki ya Dunia wa Kuboresha Takwimu za Mifugo *(Livestock Data Innovation in Africa)* imeshiriki katika mafunzo ya kujenga uwezo kwa Maafisa Takwimu za Mifugo katika kuchambua na kuainisha kwa ufasaha nafasi na mchango halisi wa Sekta ya Mifugo katika pato la Taifa yaliyofanyika nchini Zambia mwezi Aprili, 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, ili kuimarisha upatikanaji wa takwimu sahihi za mifugo, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu kukamilisha uchambuzi wa takwimu kutokana na matokeo ya Sensa ya Sampuli kwa ngazi ya mikoa na Wilaya;
(ii) Kuendelea kushiriki katika Mradi wa Kuboresha Ukusanyaji na Uchambuzi wa Takwimu za Mifugo wa Afrika chini ya Benki ya Dunia ambapo mafunzo ya muda mfupi yatatolewa kwa wataalam wa mifugo;

(iii) Kushirikiana na Sekretariat ya *SADC* na Ofisi ya Taifa ya Takwimu kukusanya na kuchambua takwimu za uzalishaji, biashara na masoko ya mifugo na mazao yake;

(iv) Kuboresha Benki ya Takwimu ya Mifugo kuzingatia mapendekezo ya Mradi wa Kuboresha Ukusanyaji na Uchambuzi wa Takwimu za Mifugo wa Afrika; na

(v) Kuendelea kutafuta fedha za kuwezesha kufanyika kwa Sensa kamili ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa sekta ya uvuvi katika kupunguza umaskini, uhakika wa chakula na kuchangia katika pato la Taifa, Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia uvunaji endelevu wa rasilimali za uvuvi nchini. Katika mwaka 2010/2011, tani 347,156.9 za samaki zenye thamani ya shilingi bilioni 774.5 zilivunwa ikilinganishwa na tani 335,674.3 zenye thamani ya shilingi bilioni 401.42 zilizovunwa mwaka 2009/2010. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 3.3.

Aidha, nguvu ya uvuvi imeongezeka kwa asilimia 3.7 kutoka wavuvi 170,038 waliotumia vyombo vya uvuvi 52,327 mwaka 2009/2010 hadi kufikia wavuvi 176,632 waliotumia vyombo vya uvuvi 54,997 katika mwaka 2010/2011. Pia, tani 39,771.9 za mazao ya samaki na samaki hai wa mapambo 40,552 waliuzwa nje ya nchi kwa thamani ya shilingi bilioni 263.1. Mauzo hayo yaliliingizia Taifa jumla ya shilingi bilioni 5.9 kama mrabaha wa kusafirisha mazao ya uvuvi nje ya nchi *(export royality).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara ilitoa mafunzo ya kulinda, kuvuna na kusimamia utumiaji endelevu wa raslimali za uvuvi pamoja na kuhifadhi mazingira kwa wadau 1,215 katika vijiji 21 vya Halmashauri za Iringa (5), Chamwino (3), Mpwapwa (3), Nkasi (6) na Sumbawanga (4). Aidha, Wizara imeandaa andiko la fursa za uwekezaji katika sekta ya uvuvi ili kuwawezesha wawekezaji wa ndani na nje kufahamu na kuzitumia fursa hizo. Pia, Wizara imeandaa rasimu ya Programu ya Uendelezaji wa Sekta ya Uvuvi ambayo inaainisha maeneo ya kipaumbele ya kuwekeza ili kuendeleza sekta.

Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia uvunaji endelevu wa raslimali za uvuvi pamoja na kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya uvuvi. Pia, kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa kazi za maendeleo ya uvuvi katika vituo, miradi na taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudi za Serikali za kudhibiti uvuvi haramu na utoroshaji wa samaki na mazao ya ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi, uvuvi mipakani, Wizara imekamilisha kutafsiri Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009 katika lugha ya Kiswahili ili kuwawezesha wavuvi na wadau wengine kuzielewa kwa urahisi na kuzitekeleza.

Katika mwaka 2010/2011, Wizara imeendelea kuimarisha vituo 19 vya doria vya Dar es Salaam, Mwanza, Musoma, Bukoba, Tanga, Mtwara, Mafia, Kilwa, Horohoro, Kipili, Kasanga, Sota, Sirari, Kasumulu, Rusumo, Kanyigo, Kabanga, Kigoma na Tunduma kwa kuvifanyia ukarabati, kuvipatia vitendea kazi yakiwemo magari matatu, pikipiki mbili, boti nne za doria, na kompyuta nne.

Kazi nyingine zilizofanyika ni:-

(i) Kuanzisha kituo cha doria cha Mbamba Bay;

(ii) Kukamilisha ukarabati wa majengo ya iliyokuwa Kampuni ya Uvuvi Tanzania *(TAFICO)* eneo la Ras-Mkwavi (Kigamboni) kwa ajili ya kutumiwa na kituo cha doria cha Kanda ya Dar es Salaam na Pwani pamoja na Kituo cha Doria cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Kanda ya Dar es Salaam;

(iii) Kukamilisha ukarabati wa jengo la Oofisi ya Kituo cha Doria cha Kigoma, nyumba tatu za kuishi watumishi wa Kituo cha Doria cha Kipili (Nkasi); na

(iv) Kuendelea na ujenzi wa ofisi mpya za vituo vya doria vya Kasanga (Sumbawanga) na Kipili (Nkasi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara, kwa kushirikiana na wadau, imeendelea kusimamia matumizi endelevu ya raslimali za uvuvi kwa kufanya jumla ya siku-kazi 8,135 za doria kwenye maji, angani na nchi kavu. Doria hizo ziliwezesha kukamatwa makokoro 1,358, kamba za kokoro mita 403,968, nyavu ndogo za makila 7,659, nyavu za utali *(monofilament)* 3,158, nyavu za dagaa 209, kokoro za vyandarua vya mbu 194, bunduki za kwenye maji 56, nyavu za kimia 356, mikuki 56, mitungi ya gesi ya oksijeni 76, mabomu 51, vifaa vya kulipua mabomu (*detonators*) vipande 602, mbolea ya kutengeneza mabomu kilo 400, mafuta ya petroli lita 120, viatu vya kuzamia ili kukusanya samaki wa mabomu jozi 26, miwani ya kuzamia 38, mitumbwi 807, kasia 256, injini za boti 48, magari 186, baiskeli 41 na pikipiki 9. Pia, sangara wachanga kilo 85,480, sato wachanga kilo 15,132, samaki waliovuliwa kwa kokoro kilo 49,463, dagaa kilo 56,765, furu kilo 3,980, majongoo bahari kilo 234, samaki wa mabomu kilo 1,235, sato waliovuliwa kwa sumu kilo 220 na samaki wakubwa kilo 4,143.

Aidha, watuhumiwa 1,198 walikamatwa, kesi 53 zilifunguliwa mahakamani na shilingi milioni 60.3 za faini zililipwa.

Kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kufanya mikutano mitano ya kutoa elimu ya athari za uvuvi wa mabomu na kuhamasisha ushiriki wao katika kudhibiti uvuvi huo kwa wadau 193 katika Mikoa ya Tanga (80), Pwani (8), Dar es Salaam (27), Lindi (32) na Mtwara (46);

(ii) Kufanya warsha ya wadau 46 wa kambamiti *(prawns)* iliyojadili mbinu na mikakati ya kuondoa migongano inayoweza kutokea kati ya wavuvi wakubwa na wadogo katika maeneo ya uvuvi wa kambamiti;

(iii) Kutoa mafunzo kwa watumishi nane kuhusu uangalizi wa bahari na watumishi saba kuhusu matumizi ya *Vessel Monitoring System;* na

(iv) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 12 na mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 27 katika shahada za Uzamivu (5), Uzamili (17) na ya kwanza (5).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri imeendelea kuimarisha vikundi 680 vya Usimamizi Shirikishi wa Raslimali za Uvuvi *(BMUs),* ambapo vikundi 433 vipo katika ukanda wa Ziwa Victoria, 19 ukanda wa Ziwa Tanganyika, 29 Bwawa la Mtera, 20 Bwawa la Nyumba ya Mungu, 11 Mto Ruhuhu, 24 Wilaya ya Kyela na 144 Ukanda wa Pwani. Aidha, jamii za wavuvi na viongozi wa Serikali za Mitaa 2,088 (wanaume 1,556 na wanawake 532) wamepatiwa mafunzo ya uanzishaji wa vikundi vya Usimamizi wa Raslimali za Uvuvi katika Halmashauri za Kinondoni (536), Temeke (701) na Mkuranga (851). Kutokana na mafunzo hayo, vikundi vipya 23 vimeanzishwa Kinondoni (4), Temeke (8) na Mkuranga (11) na kufanya jumla ya vikundi vilivyopo nchini kufikia 703.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mipango ya Usimamizi wa Raslimali za Uvuvi kwa vikundi sita vilivyopo katika Halmashauri za Pangani (3) na Mtwara (3) imeandaliwa.

Kazi nyingine zilizofanyika ni pamoja na:

(i) Kutoa mafunzo ya utengenezaji wa Mipango ya Usimamizi wa Raslimali za Uvuvi kwa vikundi 35 vilivyopo katika Halmashauri za Rufiji (23), Mafia (10) na Kilwa (2);

(ii) Kukamilisha kuandaa rasimu ya Mwongozo wa kuanzisha Maeneo ya Usimamizi wa Pamoja wa Raslimali za Uvuvi *(Guidelines for Establishment of Collaborative Fisheries Management Areas)* kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali la *World Wide Fund For Nature (WWF);*

(iii) Kuanzisha maeneo matatu ya Usimamizi wa Pamoja wa Raslimali za Uvuvi katika Wilaya za Rufiji na Kilwa; na

(iv) Kukamilisha rasimu ya Mwongozo wa Utendaji Kazi wa Pamoja wa Mtandao wa Vikundi vya Ulinzi wa Raslimali za Uvuvi *(Beach Management Units Network).*

Katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa sekta itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kufanya mapitio ya Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 kulingana na Sera ya Uvuvi;

(ii) Kufanya siku-kazi 6,000 za doria ili kuimarisha usimamizi wa raslimali za uvuvi kwa kuzingatia sheria;

(iii) Kushirikiana na Halmashauri kuhamasisha uanzishwaji wa vikundi 10 vya Usimamizi Shirikishi wa Raslimali za Uvuvi *(BMUs)* pamoja na kuimarisha utendaji kazi wa vikundi vilivyopo;

(iv) Kuendelea kuhamasisha wadau kuwekeza kwenye uvuvi wa bahari kuu na viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi kwenye ukanda wa Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa;

(v) Kuhamasisha wananchi kutengeneza na kutumia boti za *fibreglass* ili kupunguza ukataji mkubwa wa miti kwa ajili ya ujenzi wa boti za mbao;

(vi) Kuendelea kuhamasisha jamii kuanzisha Vyama vya Ushirika wa Wavuvi, Wachakataji, Akiba na Mikopo *(SACCOs);* na

(vii) Kutoa michango kwenye Miradi na Programu shirikishi kama vile *Lake Victoria Fisheries Organization, Indian Ocean* Tuna *Commission* na *International Whalling Commission.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Udhibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi, Wizara imeendelea kuhakiki usalama na ubora wa mazao ya uvuvi kwa ajili ya soko la ndani na nje ambapo kaguzi 2,486 zilifanyika. Aidha, Wizara ilifanya kaguzi 620 za kuhakiki ubora wa viwanda 28 vya kuchakata mazao ya uvuvi na maghala 39 ya kuhifadhi mazao ya uvuvi katika kanda za Ziwa Victoria na Pwani. Viwanda na maghala yaliyokaguliwa yalionekana kukidhi viwango vya ubora na hivyo kuruhusiwa kuendelea na uzalishaji. Pia, jumla ya sampuli 1,727 zilichunguzwa ili kuhakiki ubora na usalama wa mazao ya uvuvi ambapo kati ya hizo, 1,368 ni kwa ajili ya vimelea na 359 ni kwa ajili ya mabaki ya sumu, madawa na madini-tembo *(heavy metals).* Uchunguzi huo ulifanyika

katika Maabara ya Taifa ya Uthibiti wa Ubora wa Samaki Nyegezi-Mwanza, Shirika la Viwango *Tanzania-TBS, Chemiphar* (Uganda) na *SABS* (Afrika Kusini) ambapo sampuli zote zilionekana kuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilitoa mafunzo kwa wachakataji wa samaki 440 kutoka Wilaya za Nkasi (60), Sumbawanga Vijijini (134), Iringa Vijijini (91), Mpwapwa (60), Kijiji cha Tamsisiri-Mtera (50) na Halmashauri za Kigoma na Kigoma-Ujiji (45) kuhusu teknolojia ya kukausha samaki kwa kutumia moshi kwa jiko sanifu linalotumia kuni chache linalijulikana kwa jina la *Chokor (Ghana oven).* Aidha, wakaguzi 10 wa samaki, wachakataji wa samaki 45 na mafundi sanifu wa maabara wawili (2) walipewa mafunzo ya usimamizi wa ubora na usalama wa samaki na mazao yake *(Fish Inspection and Quality Control-FIQA).* Vilevile, Wadau 619 wamepata mafunzo kuhusu uzalishaji wa mazao yenye viwango vya ubora na usalama wa mazao ya uvuvi vinavyokubalika kimataifa katika ukanda wa Ziwa Victoria na Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imetoa mafunzo kwa wadau 1,935 kutoka Halmashauri 16 za mwambao wa Pwani kuhusu mwenendo na mahitaji ya soko la samaki la Jumuiya ya Ulaya. Vile vile, vituo nane vya ukaguzi wa ubora na usalama wa mazao ya uvuvi vya Bukoba, Dar es salaam na Pwani, Kigoma, Kilwa, Mafia, Musoma, Mwanza na Tanga vimeimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi na wataalam. Aidha, mialo 25 ya kupokelea na kuhudumia samaki imekarabatiwa katika ukanda wa Ziwa Victoria, kuainisha maeneo ya ujenzi wa mialo minne katika ukanda wa Ziwa Tanganyika chini ya Programu ya Uwiano wa Bonde la Ziwa Tanganyika na mialo mitatu inajengwa katika ukanda wa Pwani chini ya Mradi wa *MACEMP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012 Wizara itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuimarisha na kuwezesha Maabara ya Uvuvi Nyegezi na Maabara ya Kuchunguza Sumu zinazotolewa na mwani kwa kutumia nguvu za atomiki;

(ii) Kufanya chunguzi za kimaabara kwa sampuli 800 za minofu ya samaki, maji, maji taka na tope kutoka kwenye maeneo ya uvuvi; na

(iii) Kufanya kaguzi 3,500 za ubora wa samaki na mazao yake wakati wa kusafirisha nje ya nchi na kaguzi 100 katika viwanda vinavyochakata na kuhifadhi mazao ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ilitoa mafunzo ya ukusanyaji wa takwimu kwa vikundi 38 vya Usimamizi Shirikishi wa Raslimali za Uvuvi *(BMUs)* katika Halmashauri 13 za Pangani, Muheza, Mkinga, Jiji la Tanga, Bagamoyo, Mkuranga, Kilwa, Mafia, Rufiji, Manispaa ya Lindi, Lindi Vijijini, Manispaa ya Mtwara-Mikindani na Mtwara Vijijini. Aidha, Wizara imefanya sensa ya uvuvi katika Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika na Bwawa la Mtera na kubaini yafuatayo:-

(i) Kupungua kwa wavuvi katika Ziwa Victoria kutoka wavuvi 105,016 waliotumia vyombo vya uvuvi 30,208 mwaka 2008/2009 hadi wavuvi 95,303 wanaotumia vyombo vya uvuvi 26,988 mwaka 2010/2011;

(ii) Kupungua kwa wavuvi katika Ziwa Nyasa, kutoka wavuvi 6,557 waliotumia vyombo vya uvuvi 2,013 mwaka 2008/2009 hadi wavuvi 5,550 wanaotumia vyombo vya uvuvi 2,632 mwaka 2010/2011; na

(iii) Kuongezeka kwa wavuvi katika Ziwa Tanganyika kutoka wavuvi 12,574 waliotumia vyombo vya uvuvi 7,129 mwaka 2008/2009 hadi wavuvi 26,612 wanaotumia vyombo vya uvuvi 11,506 mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea kusimamia na kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa takwimu, ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa sahihi za uvuvi. Aidha, sensa ya nguvu za uvuvi itafanyika kwenye Ziwa Rukwa na maziwa madogo na mabwawa yaliyopo katika Mkoa wa Singida na Tabora. Pia, kutoa mafunzo ya ukusanyaji wa takwimu kwa Vikundi vya Usimamizi wa Raslimali za Uvuvi 13 katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuendeleza ukuzaji wa viumbe kwenye maji kwa kuimarisha vituo vinane vya kuzalisha vifaranga vya samaki vya Kingolwira, Luhira, Mtama, Karanga, Musoma, Mwanza, Bukoba na Tabora. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kujenga matenki matano ya kuhifadhia vifaranga kwenye Kituo cha Mtama (Lindi); kuvipatia pikipiki mbili vituo vya Luhira-Songea, moja na Mtama-Lindi, moja; kujenga matenki matatu na mabwawa manne ya kuzalisha na kufugia samaki katika Chuo cha Maendeleo ya Uvuvi Mbegani. Aidha, Chuo hiki kimepatiwa kifaa cha kupima ubora wa maji *(Water Analysis Kit)* kitakachowezesha kujua ubora wa maji kwa ajili ya kufugia samaki na vifaranga wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, jumla ya vifaranga 3,828,359 vya samaki aina ya perege na kambale vimezalishwa na kusambazwa kwa wafugaji wa samaki na kwenye malambo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Pwani, Tanga, Dodoma, Iringa, Ruvuma, Mara, Kagera, Lindi, Morogoro na Kaskazini Unguja. Aidha, vifaranga 1,598,359 vimezalishwa katika vituo vya Kingolwira (perege 788,859 na kambale 809,000), Luhira (kambale 80,000) na Mbegani (kambale 729,500) na sekta binafsi wamezalisha jumla ya vifaranga 2,230,000 vya sato na kambale ambapo *Mwanza Fishing Industries Ltd* imezalisha sato 660,000 na kambale 300,000, *Luhanga J & B Fishing Co* (sato 260,000 na kambale 100,000), Peramiho (sato 550,000) na *Mogabiri Agricultural Centre* (sato 360,000). Pia, jumla ya samaki wazazi 5,000 aina ya sato kutoka Ziwa Victoria wamepandikizwa katika mabwawa ya Vituo vya Kingolwira - Morogoro (2,600) na Luhira – Songea (2,400) kwa ajili ya kuzalisha vifaranga bora vya sato.

Vilevile, samaki wazazi 600 aina ya Kambale kutoka Mto Wami wamepandikizwa kwenye mabwawa ya Kingolwira kwa ajili ya kuzalisha vifaranga. Pia, samaki wazazi 200 aina ya Mwatiko wanafugwa kwa ajili ya majaribio ya kuzalisha vifaranga kwenye kituo cha Mbegani. Aidha, samaki wazazi 220 wa maji baridi aina ya Perege wanafanyiwa majaribio ya kufugwa katika maji ya bahari kwenye kituo cha Mbegani (60) na kijiji cha Machui Manispaa ya Tanga (160).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingine zilizotekelezwa na Wizara ni pamoja na:-

(i) Kutambua na kufanya tathmini ya maeneo mawili ya Mwanzugi (Igunga) na Nyamirembe (Chato) ambapo yalionekana kuwa yanafaa kuanzisha vituo vya kuzalisha vifaranga vya samaki. Wizara imeendelea kuwasiliana na mamlaka husika ili kuweza kupata umiliki wa maeneo hayo;

(ii) Kuainisha maeneo yanayofaa kwa uwekezaji wa ufugaji samaki kibiashara katika Wilaya za Morogoro Vijijini, Mvomero na Kilombero ambapo maeneo 86 yamepimwa na kazi ya kuandaa ramani inaendelea;

(iii) Kuandaa Mpango wa kutekeleza Mkakati wa Maendeleo ya Ukuzaji wa Viumbe kwenye Maji; na

(iv) Kufikia makubaliano ya ushirikiano wa uendeshaji wa Kituo cha Ufugaji wa Samaki cha Luhira baina ya Wizara, Kikundi cha Ufugaji Samaki Songea *(Songea Fish Farmers Association – SOFFA)* na Mkoa wa Ruvuma kwa kuzingatia Sera ya Ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia mradi wa *MACEMP* imewezesha kufanyika kwa majaribio ya ukuzaji chaza wa lulu 1,262 katika Wilaya za Mafia (328), Mtwara Vijijini (475), Bagamoyo (200) na Mkinga (259). Kati ya hizo, lulu 607 zenye thamani ya shilingi milioni 15.2 zimevunwa Mtwara. Aidha, vikundi viwili vya *Kipusa Group* na *Wakapa Group* katika Wilaya ya Pangani vimenenepesha na kuuza nje ya nchi kaa 5,040 wenye thamani ya shilingi milioni 25.2. Pia, vizimba 930 vimetengenezwa kwa ajili ya kufugia kaa katika Manispaa ya Mtwara-Mikindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, jumla ya tani 651 za mwani wenye thamani ya shilingi milioni 260.6 zimezalishwa na kusafirishwa nje ya nchi, ikilinganishwa na tani 527 mwaka 2009/2010. Aidha, majaribio ya kilimo cha mwani yanafanywa na vikundi vya Mkombozi kilichopo Kijiji cha Pande (Bagamoyo) na Mgoji kilichopo Mtwara Vijijini kwa kutumia chelezo 15

zenye wastani wa eneo la mita za mraba 16 kila moja katika maji yenye kina kirefu. Matokeo ya awali yanaonyesha kuwa, kwa kutumia teknolojia hii, mbegu za mwani zinaweza kupatikana kwa mwaka mzima. Vilevile, uzalishaji wa kambamiti katika mabwawa ya *Alphakrust* (Mafia) umeongezeka kutoka tani 60 mwaka 2009/2010 hadi tani 231.5 mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara imetoa mafunzo kwa wadau 545 kuhusu ukuzaji na usimamizi wa chaza wa lulu, Mwatiko, unenepeshaji wa kaa na kilimo cha mwani katika Halmashauri sita za Mtwara Vijijini, Lindi Vijijini, Bagamoyo, Mafia, Jiji la Tanga na Mkinga. Aidha, Wizara imewezesha maafisa watatu kushiriki mafunzo ya muda mfupi kuhusu uzalishaji na usimamizi wa ukuzaji viumbe kwenye maji nchini, Misri mmoja na Israel wawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuimarisha vituo saba vya ufugaji wa samaki katika Mikoa ya Kilimanjaro, Mara, Kagera, Morogoro, Ruvuma, Tabora na Lindi ili kuzalisha vifaranga milioni 2.5 vya perege na 500,000 vya kambale kwa ajili ya kusambazwa kwa wafugaji;

(ii) Kuimarisha Kituo cha Mbegani (Pwani) na kuanzisha vituo vya Machui (Tanga) na Chihiko (Mtwara) vya kuzalisha mbegu za viumbe wanaofugwa kwenye maji ya bahari;

(iii) Kuhamasisha ufugaji bora wa viumbe kwenye maji kwa kutumia teknolojia sahihi za ufugaji samaki, ukuzaji wa lulu na ukulima wa mwani;

(iv) Kupandikiza samaki kwenye mabwawa ya kuchimba na malambo ya asili; na

(v) Kuwezesha mafunzo ya Shahada ya Uzamili kwa watumishi wawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatekeleza Mradi wa Kuimarisha Uwezo wa Kudhibiti Magonjwa ya Milipuko ya Mifugo *(SADC–TADs Project)* unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)* katika nchi tano za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(SADC)* zikiwemo Angola, Malawi, Msumbiji, Tanzania na Zambia. Mradi unalenga katika kudhibiti magonjwa ya Homa ya Mapafu ya Ng'ombe na Ugonjwa wa Miguu na Midomo na magonjwa mengine ya mlipuko yanayojitokeza. Katika mwaka 2010/2011, Wizara imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kununua vitendea kazi kwa ajili ya uchunguzi wa Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe *(CBPP),* Ugonjwa wa Miguu na Midomo *(FMD),* ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo na magonjwa mengine kwa ajili ya Maabara Kuu ya Mifugo - Temeke na Vituo vya Kanda vya Uchunguzi wa magonjwa ya mifugo;

(ii) Kumpata mtalaam mwelekezi wa kutathmini Maabara Kuu ya Mifugo – Temeke kwa ajili ya kupata ithibati;

(iii) Kuwezesha kufanya uchunguzi wa Ugonjwa wa Miguu na Midomo kwenye nyati katika Hifadhi ya Taifa ya Katavi na ng'ombe katika maeneo yanayozunguka Hifadhi hiyo na maeneo mengine nchini;

(iv) Kuwezesha kufanya uchunguzi wa sampuli 6,000 kwa ajili ya Ugonjwa wa Sotoka ya mbuzi na kondoo katika Wilaya za Sumbawanga Vijijini, Mbozi, Ileje, Mtwara Vijijini, Newala, Tandahimba, Masasi, Tunduru, Nanyumbu, Longido, Ngorongoro, Arusha, Arumeru, Karatu, Monduli, Tarime, Rorya na Serengeti; na

(v) Kununua pikipiki 18 kwa ajili ya vituo vya mpakani na Vituo vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo *(VICs)* nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012 mradi utaendelea kuwezesha mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa wataalam na watafiti 120 ndani na nje ya nchi. Pia, kuendelea kufanya uchunguzi wa magonjwa ya mlipuko (Homa ya Mapafu ya Ng'ombe, Ugonjwa wa Miguu na Midomo na Sotoka ya Mbuzi na Kondoo) na ununuzi wa vifaa vya

maabara kwa ajili ya Maabara Kuu ya Mifugo na Vituo vya Kanda vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo *(VICs).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *MACEMP* unatekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya uratibu wa Wizara zenye dhamana ya uvuvi. Gharama ya mradi ni jumla ya Dola za Kimarekani milioni 61 na unatekelezwa kwa kipindi cha miaka sita, kuanzia Agosti, 2005 hadi Agosti 2011, chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia *(IDA)* kwa mkopo nafuu (Dola milioni 51 za Kimarekani) na msaada wa Mfuko wa Kimataifa wa Mazingira *(the Global Environment Facility - GEF)* Dola milioni 10. Mgawanyo wa fedha za mkopo, ni Dola za Kimarekani milioni 30.6 (asilimia 60) kwa Tanzania Bara na Dola za Kimarekani milioni 20.4 (asilimia 40) kwa Tanzania Zanzibar. Aidha, mgawanyo wa fedha za msaada ni Dola za Kimarekani milioni tano kwa kila upande wa Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa *MACEMP* una lengo la kuhakikisha usimamizi na matumizi endelevu ya raslimali za pwani na baharini. Kwa upande wa Tanzania Bara, Wizara inatekeleza mradi huu kwa kushirikina na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Halmashauri zote 16 za mwambao wa pwani ya Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, kwa upande wa Tanzania Bara, kupitia mradi huu yafuatayo yametekelezwa:-

(i) Ujenzi wa Vituo vitatu vya Jamii *(Community Centres)* katika Wilaya za Kilwa, Mafia na Rufiji;

(ii) Ujenzi wa mialo ya kupokelea samaki na mazao ya uvuvi ya Masoko Pwani (Kilwa), Kilindoni (Mafia) na Nyamisati (Rufiji) na ujenzi umefikia asilimia 70;

(iii) Ununuzi na usambazaji wa boti 16 za doria kwa Halmashauri za Wilaya za Bagamoyo (1), Lindi Vijijini (1), Pangani (1), Mkinga (1), na Mkuranga (1), Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu za Mnazi Bay Mtwara (1), Mafia (1), Dar es Salaam (2) na Silikanti-Tanga (1); Wizara ya Maliasili na Utalii - Idara ya Misitu na Nyuki (2) na vituo vya doria vya Wizara vya Dar es Salaam (1), Mafia (1) Tanga (1) na Mtwara (1);

(iv) Utekelezaji wa miradi shirikishi 20 ya kiuchumi inayohusu ufugaji wa kuku, nyuki, samaki na uvuvi katika Halmashauri za Temeke (15) na Mtwara Vijijini (5) iliyohusisha wananchi 267 (wanaume 151 na wanawake 116);

(v) Kutoa mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi kwa watumishi 27 wa Wizara pamoja na Halmashauri zinazotekeleza mradi;

(vi) Ujenzi wa Jengo la Mvuvi *(Mvuvi House)* katika Ofisi za Wizara Temeke Vetenari ambao umefikia asilimia 90;

(vii) Kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kujenga Ofisi ya Makao Makuu ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi katika Ukanda wa Bahari Kuu katika eneo la Fumba, Zanzibar, ambao umefikia asilimia 80;

(viii) Kuainisha vyanzo vya mapato ili kuwezesha kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Uvuvi *(Marine Legacy Fund).* Mfuko huu unaanzishwa kwa lengo la kuendeleza kazi nzuri iliyoanzishwa na mradi wa *MACEMP* ya kusimamia matumizi endelevu ya raslimali za bahari na pwani;

(ix) Kushirikiana na Umoja wa Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo *(Savings and Credit Cooperative Union League of Tanzania- SCCULT)* kuhamasisha wananchi katika Wilaya za Kilwa, Mafia na Rufiji kuanzisha *SACCOs* na Benki ya Wananchi ambapo Wilaya ya Mafia imekusanya shilingi milioni 29 kati ya shilingi milioni 250 zinazohitajika kuanzisha benki ya aina hiyo;

(x) Kushirikiana na Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi kutengeneza ramani kwa ajili ya kuhakiki raslimali na kupanga mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji vya Mkenda, Kivinja 'A', Kivinja 'B', Msindaji na Mchungu (Rufiji) na Mitaa 15 katika kata za Msinjahili, Jamhuri na Ras Bura (Lindi); na

(xi) Kushirikiana na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* kuandaa na kuidhinisha Mipango ya Matumizi ya Uwiano wa Raslimali za Bahari na Ukanda wa Pwani katika Halmashauri 15 za Ukanda wa Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, kupitia mradi wa *MACEMP* kazi zifuatazo zitatekelezwa:-

(i) Kuandaa na kutekeleza Mipango ya Usimamizi Shirikishi wa Raslimali za Uvuvi *(BMUs)* katika vijiji 60 vilivyopo katika Halmashauri 16 za ukanda wa pwani wa bahari na kusaidia utekelezaji wake;

(ii) Kukamilisha Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi katika vijiji 46 katika ukanda wa Pwani;

(iii) Kufuatilia na kutathmini miradi midogo 459 ya uzalishaji ya jamii za wavuvi katika eneo la Mradi;

(iv) Kukamilisha ujenzi wa ofisi za Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi Bahari Kuu na mialo ya kupokelea samaki ya Kilwa, Mafia na Rufiji;

(v) Kuimarisha na kuwezesha uanzishwaji wa hifadhi mpya za bahari na maeneo tengefu;

(vi) Kukamilisha uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Uvuvi *(Marine Legacy Fund)* ili kuendeleza shughuli za mradi utakapomalizika;

(vii) Kufanya tafiti za samaki wanaoishi kwenye matumbawe; na

(viii) Kukarabati majengo ya kihistoria na kukamilisha ujenzi wa ofisi ya Hifadhi ya Bahari ya Silikanti ya Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu ya Usimamizi wa Bonde la Ziwa Tanganyika yenye vipengele vya mazingira, uvuvi na mfumo wa majisafi na majitaka chini ya uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kutekelezwa katika nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya *Congo (DRC),* Tanzania na Zambia. Kwa upande wa Tanzania, programu hii inatekelezwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa za Kigoma, Kigoma - Ujiji, Mpanda, Nkasi na Sumbawanga. Katika mwaka 2010/2011, kazi zifuatazo zimetekelezwa kwa upande wa Sekta ya Uvuvi:-

(i) Kuainisha vijiji 20 kwa ajili ya kuanzisha Kamati za Usimamizi wa Raslimali za Uvuvi *(Fisheries Management Committees);*

(ii) Kuainisha mialo 47 ya kupokelea samaki katika Mamlaka za Serikali za Mitaa za Kigoma (10), Kigoma-Ujiji (4), Mpanda (3), Nkasi (27) na Sumbawanga (3) ambapo taratibu za ujenzi wa miundombinu kwenye mialo minne, katika Mikoa ya Kigoma miwili (2) na Rukwa miwili (2) zinaendelea;

(iii) Kutoa mafunzo kwa watalaam 65 kutoka TAFIRI (Kigoma), vituo vya doria (Kasanga na Kipili) na Mamlaka za Serikali za Mitaa husika kuhusu uanzishaji na ufuatiliaji wa miradi midogo ya jamii za wavuvi;

(iv) Kufanya sensa ya uvuvi katika Ziwa Tanganyika;

(v) Kuanzisha *BMUs* 19 na kutoa mafunzo kwa viongozi wake katika Mamlaka za Serikali za Mitaa za Kigoma-Ujiji (2), Kigoma Vijijini (5), Nkasi (4), Mpanda (4) na Sumbawanga (4); na

(vi) Kuwezesha ujenzi unaoendelea wa Ofisi za Vituo vya Doria vya Kipili na Kasanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Programu ya Usimamizi wa Bonde la Ziwa Tanganyika kwa kushirikiana na wadau itaendelea kusimamia matumizi endelevu ya raslimali za uvuvi na kuboresha miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Utekelezaji wa Mpango wa Usimamizi wa Uvuvi katika Ziwa Victoria *(Implementation of a Fisheries Management Plan Project for Lake Victoria - IFMP),* Mradi wa Utekelezaji wa Mpango wa Usimamizi wa Uvuvi katika Ziwa Victoria *(IFMP)* umemaliza muda wake katika kipindi cha mwaka 2010/2011. Katika kipindi hicho, Mradi umewezesha kutoa mafunzo kuhusu madhara ya uvuvi haramu kwa wadau 9,552 kutoka Halmashauri 14 katika Mikoa ya Mwanza, Mara na Kagera.

Pia, ujenzi wa mialo sita ya Marehe (Missenyi), Kikumbaitare (Chato), Bwai (Musoma), Sota (Rorya), Kigangama (Magu) na Kahunda (Sengerema) umekamilika na kukabidhiwa kwa Halmashauri husika. Vilevile, mradi umewezesha kufanyika kwa siku-kazi za doria 535 katika ukanda wa Ziwa Victoria ambapo makokoro 1,799, nyavu za makila 19,106, nyavu za dagaa 34, nyavu za Utali *(monofillaments)* 2,474, katuli 152, kamba za kokoro mita 125,210, magari 12 na mitumbwi 479 vilikamatwa. Aidha, sangara wachanga kilo 87,823, sato wachanga kilo 24,292 na watuhumiwa 388 walikamatwa. Pia, Sh. 14,706,537/= zilikusanywa kutokana na faini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *(Ecosystem Approach to Fisheries - EAF Nansen Project),* Mradi wa Usimamizi wa Uvuvi Unaojumuisha Ikolojia na Mazingira unatekelezwa katika ukanda wa Pwani kwa kipindi cha miezi 18 kuanzia mwezi Septemba, 2010 na unafadhiliwa na *FAO*. Katika mwaka 2010/2011, mradi umetekeleza yafuatayo:-

(i) Kuwajengea uwezo watalaam 14 wa Sekta ya Uvuvi ili watoe mafunzo ya kuhamasisha usimamizi wa uvuvi kwa kutumia mbinu za kiikolojia kwa watekelezaji wa mradi; na

(ii) Kutoa mafunzo kuhusu usimamizi wa uvuvi kwa kutumia mbinu za kiikolojia kwa wadau 98 wakiwemo watalaam (42) kutoka Idara ya Maendeleo ya Uvuvi, Maafisa Uvuvi nane kutoka Halmashauri za Pangani, Muheza, Mkinga na Jiji la Tanga na Wavuvi (48) kutoka Jiji la Tanga; kuandaa na kusambaza vipeperushi 422 na mabango 300 kwa wadau.

Katika mwaka 2011/2012 mradi utatekeleza yafuatayo:-

(i) Kuandaa na kukamilisha Mpango wa Usimamizi wa Samaki Wanaopatikana katika Tabaka la Juu la Maji;

(ii) Kutoa mafunzo ya uhamasishaji wa usimamizi wa uvuvi unaojumuisha ikolojia na mazingira kwa taasisi nyingine na wavuvi wa Mikoa ya Lindi, Mtwara na Pwani; na

(iii) Kuwezesha ziara ya mafunzo katika Jamhuri ya Shelisheli ili kujifunza namna nchi hiyo inavyosimamia samaki wanaopatikana katika matabaka mengine ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara imewapandisha vyeo watumishi 380 na kuwathibitisha kazini 80. Pia, watumishi 200 wa kada mbalimbali wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu (50) na ya muda mfupi (150).

Kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kuandaa na kurusha hewani vipindi vya redio kuhusu Huduma ya Mkataba kwa Mteja;

(ii) Kutoa mafunzo kwa watumishi kuhusu uandaaji wa Benki ya takwimu *(Data Bank)* za watumishi kwa ajili ya kutunza kumbukumbu;

(iii) Kushirikiana na vyama vya wafanyakazi na Baraza la Wafanyakazi kufanya vikao viwili vya Baraza la Wafanyakazi na wafanyakazi wote kwa lengo la kujenga uhusiano mzuri kati ya wafanyakazi na mwajiri;

(iv) Kuhamasisha wafanyakazi kushiriki katika michezo ili kuboresha afya zao na kuimarisha uelewano miongoni mwao;

(v) Kuanzisha huduma za usafi na ulinzi katika vituo vya Dar es Salaam (Kurasini na Kigamboni), Mwanza (*VIC* na Kituo cha Doria), Kibaha na *LITI* Morogoro; na

(vi) Kutekeleza mfumo wa wazi wa kupima utendaji kazi *(OPRAS)* kwa wafanyakazi wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara itaajiri jumla ya wataalam 142 wakiwemo wa sekta za mifugo 80, uvuvi 40 na fani nyingine 22. Aidha, watumishi 256 watapandishwa vyeo. Pia, watumishi 150 wa kada mbalimbali watapatiwa mafunzo ya muda mrefu (50) na muda mfupi (100).

Kazi nyingine zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kuhamasisha watumishi wa Wizara kuzingatia miongozo ya kazi na maadili;

(ii) Kutoa mafunzo kwa watumishi 10 watakaofundisha wenzao *(TOT)* juu ya utawala bora;

(iii) Kuimarisha idara kwa kuipatia vitendea kazi;

(iv) Kuratibu shughuli za Baraza la Wafanyakazi na Vyama vya Wafanyakazi *(TUGHE, RAAWU na CHODAWU);*

(v) Kuhamasisha wafanyakazi kushiriki katika michezo ili kuboresha afya zao na kuimarisha uelewano miongoni mwao;

(vi) Kuwawezesha watumishi 80 kushiriki katika mashindano ya michezo mbalimbali;

(vii) Kuwezesha sekta binafsi kutoa huduma za usafi na ulinzi;

(viii) Kuimarisha ofisi ya utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka za Serikali; na

(ix) Kuendelea kuimarisha mfumo wa wazi wa kupima utendaji kazi *(OPRAS)* ndani ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutayarisha na kusambaza taarifa za matukio mbalimbali kuhusu maendeleo ya sekta za mifugo na uvuvi. Baadhi ya matukio hayo ni maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma, Nane Nane, Wiki ya Maziwa na Siku ya Chakula Duniani. Katika mwaka 2010/2011, Wizara imetayarisha na kusambaza nakala 1,000 za majarida na nakala 1,000 za mabango kuhusu mafanikio ya Sekta za Mifugo na Uvuvi katika Miaka 50 ya Uhuru. Pia, nakala 4,000 za kalenda na nakala 1,200 za vipeperushi zinazoelezea kazi na majukumu mbalimbali ya Wizara zilichapishwa na kusambazwa. Aidha, Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano kimeimarishwa kwa kupewa vitendea kazi vikiwemo gari moja, kompyuta moja na seti moja ya televisheni. Vilevile, watumishi watatu wa Kitengo hiki wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kutayarisha na kusambaza taarifa za matukio mbalimbali kuhusu maendeleo ya Sekta za Mifugo na Uvuvi kupitia vyombo vya habari, ikiwemo mafanikio ya miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara. Vilevile, nakala za majarida 1,000, kalenda 4,000, vipeperushi 1,200 na mabango 1,000 kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara zitatayarishwa na kusambazwa. Aidha, watumishi wawili wa Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano watapatiwa mafunzo ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara imeendelea kutekeleza Utawala bora kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya Serikali ikiwemo masuala ya ajira, utekelezaji wa Mkakati wa Kuzuia na Kuziba Mianya ya Rushwa, Mkataba wa Huduma kwa Mteja na kuzingatia Sheria ya Matumizi ya Fedha za Umma na Sheria ya Ununuzi. Aidha, masuala ya jinsia yameendelea kuzingatiwa katika mipango ya maendeleo ya Wizara, ajira na upandishwaji vyeo. Pia, Wizara imewezesha Kamati ya Jinsia kupata mafunzo juu ya jinsi ya kujumuisha masuala ya kijinsia katika mipango na utekelezaji wa majukumu yake. Vilevile, Wizara imeendelea kuhamasisha watumishi kupima afya zao ili kujikinga na maambukizi mapya ikiwa ni moja ya mikakati ya kuzuia maambukizi mapya ya UKIMWI ambapo watumishi 13 waliothibitika kuathirika wanapata msaada wa chakula. Kufuatia kukamilika kwa tathmini ya hali ya UKIMWI katika Wizara, Mpango Mkakati wa Wizara wa Kuzuia maambukizi mapya ya UKIMWI umeandaliwa.

Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kuzuia na Kuziba Mianya ya Rushwa; kufanya tathmini ya jinsia ili kujumuisha masuala ya jinsia katika mipango ya Wizara kwa lengo la kuleta usawa wa jinsia; kuhamasisha watumishi kupima afya zao kwa hiari; kuwahudumia walioathirika na kutoa elimu kwa waelimishaji rika na washauri nasaha wa masuala ya UKIMWI ili kuzuia maambukizi mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi katika Sekta za Mifugo na Uvuvi, Wizara kwa kushirikiana na wakala wa hali ya hewa nchini, iliendelea kutoa taarifa za tahadhari kwa wadau wa sekta hizo kuhusu mwenendo wa hali ya hewa. Katika sekta ya mifugo, mwenendo wa tahadhari za kupungua kwa upatikanaji wa maji na malisho ziliendelea kutolewa na mikakati ya kupata takwimu za mwenendo wa hali ya mifugo zimeainishwa katika Mikoa. Aidha, Wilaya za Ngorongoro, Monduli, Longido na Meatu zilikuwa na upungufu wa maji na malisho mwanzoni mwa mwaka 2011. Mikoa zaidi ya 14 ilikuwa na mvua za masika chini ya wastani, hivyo kuwa na maeneo yatakayokuwa na upungufu wa malisho na maji wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuelimisha na kuhamasisha wafugaji kuhifadhi mazingira na kuwa na matumizi endelevu ya raslimali katika ardhi. Aidha, kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Uholanzi *(SNV)* inaendelea kuelimisha wafugaji kuhifadhi mazingira kwa kupunguza ukataji miti na kuhamasisha matumizi ya *biogas* kama nishati mbadala ambapo jumla ya wataalam 15 wamepatiwa mafunzo ya matumizi ya mitambo ya gesi inayotokana na samadi ya ng'ombe. Vilevile, mitambo mitano ya mfano inajengwa katika Wilaya za Mwanga (1), Same (2) na Longido (2). Katika mwaka 2011/2012, Wizara itakamilisha na kusambaza Mwongozo wa Matumizi ya *Biogas* kwa Wafugaji wa Asili na kuhamasisha Halmashauri 20 kuhusu ujenzi, utumiaji na matengenezo ya mitambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa Sekta za Mifugo na Uvuvi ilishiriki katika maadhimisho ya sikukuu ya wakulima nchini – Nane Nane. Maadhimisho hayo yalifanyika kitaifa Mkoani Dodoma na kauli mbiu ya maonesho hayo ilikuwa ni "Kilimo Kwanza – Mapinduzi ya Kijani, Uhakika wa Chakula na Kipato". Katika maonyesho hayo, Wizara na wadau walionyesha matumizi ya teknolojia mbalimbali za kuongeza uzalishaji wenye tija. Aidha, umma ulielimishwa kuhusu Sera, Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali ya Sekta za Mifugo na Uvuvi.

Katika mwaka 2011/2012, Wizara itashiriki katika kuandaa maadhimisho hayo ambayo kitaifa yatajumuisha maadhimisho ya miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara. Maadhimisho hayo, pamoja na mambo mengine, yatashindanisha mifugo bora ya wadau kutoka kanda zote saba za Kilimo. Kaulimbiu ya maonyesho hayo itakuwa "Kilimo Kwanza - Tumethubutu, Tumeweza - Tunazidi Kusonga Mbele".

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara iliandaa na kuratibu Wiki ya Uhamasishaji Unywaji wa Maziwa iliyoadhimishwa kitaifa Mkoani Dar es Salaam kuanzia tarehe 29 Mei mpaka 1 Juni, 2011. Kaulimbiu ya maadhimisho haya ilikuwa, "Kunywa Maziwa kwa Afya Yako; Jenga Uchumi wa Nchi Yako". Kilele cha maadhimisho hayo, ni tarehe 1 Juni kila mwaka na huadhimishwa na nchi mbalimbali duniani chini ya uratibu wa *FAO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ilikuwa mwenyeji wa Kongamano na Maonesho ya Saba ya Kimataifa ya Maziwa yaliyofanyika Dar es Salaam kuanzia tarehe 25 hadi 27 Mei, 2011. Kongamano na maonesho hayo yaliandaliwa na Chama cha Wadau wa Maziwa Mashariki na Kusini mwa Afrika *(Eastern and Southern African Dairy Association - ESADA)* ikishirikiana na Wizara. Kongamano hilo liliwakutanisha wadau 354 wa ndani na nje wakiwemo wataalam wa maziwa, watafiti, wafanyabiashara wa tasnia ya maziwa na wawekezaji mbalimbali. Maudhui ya kongamano na maonesho hayo yalikuwa *"African Dairy: the next dairy frontier,"* yaani Tasnia ya Maziwa Afrika: Eneo Jipya la Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, pamoja na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(FAO)*, iliandaa na kuadhimisha Siku ya Chakula Duniani iliyofanyika Kitaifa Tarafa ya Kigamboni, Kata ya Kimbiji, Dar es Salaam. Maadhimisho hayo hufanyika duniani kote tarehe 16 Oktoba kila mwaka kwa lengo la kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kuzalisha chakula cha kutosha na kuwa na lishe bora. Kaulimbiu ilikuwa, "Tuungane Dhidi ya Njaa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kongamano la Kisayansi la Vyama vya Wataalam wa Uzalishaji Mifugo na Madaktari wa Mifugo, Wizara hushiriki katika makongamano ya kila mwaka ya Wataalam wa Uzalishaji Mifugo na Madaktari wa Mifugo nchini. Katika mwaka 2010/2011, kongamano la pamoja kati ya wataalam hao lilifanyika mjini Arusha tarehe 18 – 20 Januari, 2011, na maudhui yake yalikuwa ni "Ufugaji kwa Maendeleo: Fursa na Changamoto."

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika wiki ya mwisho ya mwezi Aprili kila mwaka, wadau wa afya ya mifugo duniani huadhimisha siku ya taaluma ya Veterinari. Maadhimisho haya ambayo husimamiwa na Chama cha Madaktari wa Mifugo Duniani *(World Veterinary Association -WVA)* na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani *(OIE)*, huambatana na kaulimbiu maalum ambapo kwa mwaka 2010/2011 ilikuwa "Hamasisha, Zuia na Dhibiti Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa." Aidha, maadhimisho ya mwaka huu yalikuwa ya kipekee kutokana na tamko rasmi la *OIE* kuwa Taaluma ya Veterinari inatimiza miaka 250 tangu kuanzishwa kwake. Wananchi walihamasishwa kwa njia ya matangazo kupitia vyombo vya habari na mabango kuhusu ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa na utoaji chanjo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, maadhimisho yote niliyoyaeleza hapo juu yametoa changamoto, msukumo na mchango mkubwa katika kuboresha maendeleo ya Sekta za Mifugo na uvuvi. Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine inaendelea kuyafanyia kazi maazimio yaliyotokana na matukio hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wafugaji na wavuvi kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi hapa nchini. Wizara inaomba waendeleze juhudi hizo na itaendelea kushirikiana nao kuleta mapinduzi katika Sekta za Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuzitambua na kuzishukuru Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)*, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)*, Umoja wa Nchi za Ulaya *(EU)*, Serikali za Australia, Austria, Denmark, Japan, Jamhuri ya Afrika ya Kusini, Jamhuri ya Watu wa China, Ireland, Marekani, Misri, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Uswisi na Italia pamoja na mashirika ya Umoja wa Mataifa ya *FAO, IAEA, UNICEF, UNDP* na *WHO* na mifuko ya kimataifa ya *GEF* na *IFAD* kwa kuchangia katika maendeleo ya sekta za mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, napenda kutambua na kuzishukuru taasisi za kimataifa ambazo ni pamoja na Benki ya Dunia *(WB)*, Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)*; Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Japani *(JICA)*, Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Jamhuri ya Korea *(KOICA)*, Shirika la Misaada la Ireland *(Irish Aid)*, Shirika la Misaada la Marekani *(USAID)*, Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza *(DfID)*, Taasisi ya Raslimali za Wanyama ya Umoja wa Afrika *(AU/IBAR)*, Shirika la Afya ya Wanyama Duniani *(OIE)*, Shirika la Maendeleo la Uswisi *(SDC)*, Shirika la Ushirikiano la Ujerumani *(GTZ)*, Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Denmark *(DANIDA)*, Shirika la

Kimataifa la Maendeleo la Sweden *(SIDA)* na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Norway *(NORAD)* kwa michango yao katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi.

Aidha, napenda kuyashukuru Mashirika na Taasisi za hiari za *Bill and Melinda Gates Foundation*, *Association for Agricultural Research in East and Central Africa (ASARECA), International Livestock Research Institute (ILRI)*, *World Wide Fund for Nature (WWF), Heifer Project Tanzania (HPT)*, *Overseas Fisheries Co-operation Foundation of Japan (OFCF), Vetaid, Care International*, *OXFAM, Welcome Trust*, *Austro-Project, World Vision, FARM Africa, Land O' Lakes, Bangladesh Rural Advancement Committee (BRAC), World Society for Protection of Animals (WSPA), Global Alliance for Livestock and Veterinary Medicine (GALVmed), Institute of Security Studies (ISS), International Land Coalition (ILC),* Mashirika na Taasisi mbalimbali za humu nchini zinazojihusisha na uendelezaji wa Sekta za Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimalizie kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Benedict Ole Nangoro - Mbunge wa Jimbo la Kiteto na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Katibu Mkuu - Dkt. Charles Nyamrunda, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Yohana Budeba, Wakuu wa Idara na Taasisi za Wizara, Wafanyakazi na Wadau wote kwa mshikamano wao katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Wizara inaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ya jumla ya Sh. 57,165,193,000/= kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sh. 12,758,085,000/= ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi (PE); Sh. 23,553,425,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengine *(OC);* na Sh. 20,853,683,000/= ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya hizo, Sh. 4,358,694,000/= ni fedha za ndani na Sh. 16,494,989,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena nitoe shukurani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza na hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani: *www.mifugo.go.tz*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba hii, nimeambatanisha Randama ya Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. SAID J. NKUMBA – K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kabla sijaanza napenda kwanza kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Profesa David Homeli Mwakyusa, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo, Maji na Mifugo kwa kuniamini na kunipa jukumu la kuiwasilisha taarifa hii kwa niaba yao. Aidha, nawashukuru vile vile kwa namna ya pekee wananchi wa Jimbo la Sikonge na chama changu, Chama cha Mapinduzi kwa kuniamini na kunichagua mara ya tatu mfululizo, nawaahidi utumishi ulio tukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti kabla sijaanza kuwasilisha taarifa hii, lipo jambo muhimu kwa afya za Watanzania. Zipo taarifa zilizoripotiwa kupitia vyombo vya habari juu ya kuingizwa nchini samaki toka Japan wanaosadikiwa kwamba wana mionzi ya nyuklia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka hapa ninaposimama leo pamoja na uzito wa jambo hili na usalama wa afya za Watanzania, Serikali haijatoa tamko lolote juu ya ukweli wa suala hili. Kwa hiyo, kwa niaba ya Kamati, lakini vile vile kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wote na kwa niaba ya Watanzania nimepewa leo majukumu makubwa. Naagiza na kuielekeza Serikali leo hii itoe tamko ikiwaeleza Watanzania ukweli wa suala hili na hatua zinazochukuliwa na Serikali.

Ushahidi upo, lipo gazeti la *Citizen* hili hapa la tarehe 26 limetoa maelezo. Magazeti ya Nipashe na magezeti kadhaa yametoa maelezo. Sasa naomba niendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, kwa niaba ya Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ilikutana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi katika Ofisi Ndogo ya Bunge ya Dar es Salaam tarehe 30 na 31 Mei, 2011. Katika kikao hicho Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi alitoa maelezo kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2010/2011, changamoto za utekelezaji kwa kipindi cha mwaka 2010/2011, malengo na maeneo ya kipaumbele pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2010/2011, wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2010/2011, Kamati ilitoa maoni na ushauri wa kuzingatiwa. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa Wizara imeyafanyia kazi maoni na ushauri wa Kamati. Baadhi ya maeneo yaliyofanyiwa kazi ni pamoja na yafuatayo:-

(a) Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga shilingi bilioni 30 kupitia Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia - *COSTECH* kwa ajili ya kuendeleza utafiti nchini. Wizara iliutumia mgao wake kwa kuwapeleka wataalam wake kusomea shahada za uzamili na uzamivu ili kujenga msingi wa kuhakikisha azma ya Serikali ya Kilimo Kwanza inafanikiwa. Aidha, Wizara imeandaa programu za kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi ili zichangie kikamilifu katika pato la Taifa.

(b) Ili kukabiliana na uhaba wa wataalam katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi, Wizara imeendelea kuongeza udahili wa wanafunzi katika vyuo vyake vinane (Tengeru, Mpwapwa, Madaba, Morogoro, Buhuri na Temeke vya mifugo na Nyegezi na Mbegani vya uvuvi);

(c) Wizara imeendelea kutoa ushauri katika kusimamia na kuratibu utekelezaji wa miradi mbali mbali ya Kitaifa. Aidha, Wizara imeteua waratibu wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi,

(d) Ili kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Maziwa, Serikali imeondoa ushuru wa vifungashio vya maziwa vinavyotengenezwa katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(e) Sheria ya Ngozi Na.18 ya mwaka 2008, pamoja na kanuni zake sita zimetafsiriwa katika lugha ya Kiswahili na kusambazwa katika halmashauri zote nchini na tayari zinatumika;

(f) Ili kuongeza thamani ya ngozi hapa nchini, kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara na Chama cha Wadau wa Ngozi, Wizara imeendelea kuhamasisha uwekezaji katika usindikaji wa ngozi ndani ya nchi badala ya kuuza nje zikiwa ghafi; na

(g) Chini ya mradi wa *MACEMP*, jamii za Ukanda wa Pwani zimewezeshwa kutekeleza miradi midogo midogo ya uzalishaji wa mali kama vile ufugaji wa nyuki, uchongaji wa mizinga ya nyuki, utengenezaji wa boti na utengenezaji wa majiko sanifu ya kukaushia samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Wizara pia imekumbana na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2010/2011. Changamoto hizo ni pamoja na:-

(a) Kuchelewa kutolewa kwa fedha za miradi ya maendeleo;

(b) Kutopatikana kwa mikopo yenye masharti nafuu kwa wafugaji na wavuvi;

(c) Kutopatikana kwa pembejeo na zana za gharama nafuu kwa ajili ya ufugaji na uvuvi;

(d) Uhaba wa soko la uhakika la mazao ya mifugo na uvuvi;

(e) Elimu na teknolojia za kisasa kutokuwafikia wafugaji na wavuvi;

(f) Uwekezaji mdogo katika Sekta za Mifugo na Uvuvi, na
(g) Kudhibiti uvuvi na biashara haramu ya samaki na mazao ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha na malengo ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi chini ya Fungu 99, inaomba jumla ya Sh. 57,165,193,000/=. Kati ya fedha hizo, Sh. 36,311,510,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. 20,853,683,000/= ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida, Sh. 12,758,085,000/= ni kwa ajili ya mishahara na Sh. 23,553,425,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC).* Aidha, kati ya fedha za maendeleo, Sh.4,358,694,000/= ni fedha za ndani na Sh. 16,494,989,000/= ni fedha kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi hayo ya fedha yatawezesha Wizara kutekeleza kazi mbalimbali ilizojipangia. Baadhi ya kazi hizo ni kama ifuatavyo:-

(a) Sekta ya Mifugo:-

(i) Kukamilisha ujenzi wa machinjio ya Ruvu na kuanzisha mfumo wa kuwawezesha wafugaji kunenepesha mifugo kwa ajili ya machinjio hiyo;

(ii) Kukamilisha ujenzi wa kituo cha kuzalisha chanjo za mifugo kilichopo Kibaha chini ya Maabara Kuu ya Mifugo - Temeke na kukarabati vituo vya ndorobo Tanga na Kigoma;

(iii) Kuimarisha huduma za ugani na utafiti wa mifugo; na

(iv) Kuanzisha maandalizi ya kufanya sensa kamili ya mifugo na kuanzisha mfumo wa kutambua na kusajili mifugo kwa mfumo wa ufuatiliaji.

(b) Sekta ya Uvuvi:-

(i) Kuimarisha udhibiti wa raslimali za uvuvi na biashara ya mazao ya uvuvi kwenye bahari, maziwa na mabwawa;
(ii) Kutekeleza ahadi ya Serikali ya kuchangia dola za kimarekeni 600,000 kwa ajili ya doria maalum ya kanda katika Ziwa Victoria;

(iii) Kujenga Kituo cha Utafiti wa Uvuvi cha Dar es Salaam, kukarabati meli mbili za utafiti na kununua vitendea kazi kwa ajili ya utafiti;

(iv) Kujenga Maabara ya Uvuvi ya Kurasini. Pia kuiwezesha Maabara ya Taifa ya Uvuvi Nyegezi kupata ithibati, na

(v) Kujenga na kukarabati miundombinu ya ufugaji wa viumbe kwenye maji na kujenga vituo vipya vitatu vya Igunga, Mtama (Lindi) na Nyamirembe (Chato).

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati kwa Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, baada ya kueleza kazi zilizopangwa kutekelezwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Wizara bado ni ndogo na tegemezi kwa asilimia kubwa kwa wahisani kutoka nje. Mwaka 2010/2011 Wizara ilitengewa Shilingi bilioni 58.8 wakati mwaka 2011/2012 Wizara imetengewa shilingi bilioni 57.2 tu ikiwa ni pungufu ya Shilingi bilioni 1.6. Wizara hii

ina majukumu mengi sana kuendana na dhamira ya Serikali ya kuifanya sekta hii ichangie kikamilifu katika pato la Taifa. Kamati inaishauri Serikali kuiangalia Wizara hii kwa umuhimu wake kwani majukumu yake yatafanikiwa iwapo itatengewa fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaamini kwamba dhana ya Kilimo Kwanza imekuja kwa nia ya kuleta mapinduzi ya kijani na kukifanya kilimo chetu kuwa cha kisasa na cha kibiashara. Hata hivyo, wakati wa kupitia bajeti ya Wizara, Kamati imebaini kwamba dhana hii bado haijafahamika kwa wananchi na hivyo kuishauri Serikali kuchukua hatua za makusudi za kuielimisha jamii juu ya dhana ya Kilimo Kwanza. Aidha, Serikali iendelee kuhamasisha sekta binafsi katika utekelezaji wa Kilimo Kwanza kwa kuhakikisha inawawekea vivutio muafaka kwa kuzingatia kwamba sekta binafsi inachangia kwa asilimia kubwa katika kukua kwa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa wataalam ni tatizo kubwa katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi na hivyo kuathiri mchango wa sekta hii katika pato la Taifa.

Kamati inaamini uwepo wa wataalam wa kutosha na wenye kuwezeshwa kwa kupatiwa vitendea kazi na kuboreshewa maslahi yao ni mojawapo ya njia itakayoziwezesha sekta hizi muhimu kukua kwa kasi inayotakiwa kwani watafikisha huduma inayostahili kwa wafugaji na wavuvi. Kamati inaishauri Serikali iongeze wataalam hao kwa kuongeza idadi ya wahitimu wa fani ya ugani katika vyuo vilivyopo ili waweze kukidhi mahitaji halisi katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi za Utafiti ni muhimu sana katika kuongeza tija katika uzalishaji na utoaji huduma ndani ya jamii. Pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali katika kuongeza bajeti ya taasisi hizi, bado hazijafikia kiwango kinachotakiwa. Kamati inaishauri Serikali iendelee kuongeza bajeti inayotengwa kwa taasisi hizi. Aidha, Wizara ihakikishe matokeo ya utafiti yanawafikia walengwa ambao ni wavuvi na wafugaji ili kuendelea kuboresha sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingi ya ufugaji na uvuvi ipo kwenye Halmashauri ambazo ndizo mamlaka za utekelezaji, Kamati inashauri Serikali kuimarisha mahusiano ya kikazi yaliyopo kati ya Wizara na TAMISEMI (Halmashauri) ili kuleta ufanisi zaidi wa kazi katika kutekeleza miradi hiyo. Aidha, Idara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na wataalam wake walioko katika Halmashauri zitenganishwe badala ya utaratibu wa sasa wa kuunganishwa na Idara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unywaji wa maziwa katika nchi yetu bado upo chini ambapo takwimu zinaonesha kuwa Mtanzania anakunywa wastani wa lita 44 kwa mwaka ambapo Shirika la Chakula na Kilimo *FAO* linashauri unywaji wa lita 200 za maziwa kwa mwaka. Unywaji huu hafifu unatokana na sababu mbali mbali zikiwemo bei kubwa ya maziwa, uhaba wa viwanda vya kusindika maziwa, gharama kubwa ya vifungashio pamoja na miundombinu mibovu ya kufikisha maziwa katika soko. Kutokana na matatizo yanayoonekana kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kufanya zao hili kutotumiwa ipasavyo. Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

§ Serikali iendelee kuwahamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa kunywa maziwa. Aidha, programu ya unywaji maziwa katika shule iendelezwe katika maeneo yote nchini.

§ Dhana ya uhamasishaji wa wananchi kunywa maziwa ni nzuri sana lakini maziwa hayatoshelezi mahitaji. Kamati inashauri wasindikaji wa maziwa wapatiwe mikopo yenye riba nafuu ili kuwavutia na kuleta maziwa sokoni kwa wingi.

§ Serikali iangalie uwezekano wa kuingiza vifungashio vya maziwa toka nchi zilizopo nje ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kama vile China kwa nia ya kupata vifungashio vyenye ubora, lakini kwa bei nafuu zaidi. Aidha, Serikali iweke mikakati ya kutengeneza vifungashio hivyo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngozi ni zao ambalo likitumiwa vizuri linaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika pato la Taifa. Ngozi za mifugo bado hazichangii ipasavyo katika Pato la Taifa ikilinganishwa na idadi ya mifugo tuliyonayo na hii inatokana na ngozi zetu kutokuwa na ubora unaotakiwa katika soko. Kamati inasisitiza yafuatayo:-

§ Elimu zaidi iendelee kutolewa kwa wafugaji kuhusu umuhimu wa kutunza mifugo yao.

§ Ili kukuza soko la ngozi nchini, Serikali iweke utaratibu wa viwanda vya Tanzania kutengeneza bidhaa za ngozi zinazozalishwa nchini ikiwa ni pamoja na viatu na mikoba ili kuviuza kwa bei nafuu kwa nia ya kuitangaza ngozi ya Tanzania ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imebarikiwa kuwa na mifugo mingi wakiwemo ng'ombe takribani milioni 19.1 na mbuzi milioni 13.6. Inasikitisha kuona hatuna machinjio za kisasa na ya kutosha na viwanda kwa ajili ya kusindika nyama. Kamati inasisitiza yafuatayo:-

§ Serikali ijenge machinjio ya kutosha katika maeneo mbalimbali nchini na kuyakodisha kwa makampuni binafsi ili kuongeza ubora wa nyama na kuongeza pato la Serikali.
§ Serikali iendelee kujenga machinjio ya kisasa kama ile inayojengwa Ruvu ili kuendelea kuimarisha sekta hii na kuinua uchumi wa nchi.

§ Serikali ifungue minada ya upili ya kutosha kwa ajili ya wafugaji kuuza mifugo yao.

§ Viwanda vyote vya nyama ambavyo walipewa wawekezaji na kushindwa kuviendeleza virudishwe Serikalini ili watafutwe wawekezaji watakaoweza kuviendeleza.

§ Serikali itenge maeneo yasiyo na maradhi *(Disease Free Zone)* kwa ajili ya unenepeshaji wa mifugo itakayokidhi kiwango cha soko la kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu kwa muda mrefu sasa imekuwa na migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Hii inatokana na kutokuwepo kwa mpango madhubuti wa matumizi ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, Sekta ya Mifugo imekuwa haipewi umuhimu stahiki katika jamii. Kutokana na hali hii, Kamati inashauri yafuatayo:-

§ Ipo haja kwa Wizara husika kukaa na kutazama ni namna gani itapata ufumbuzi wa kudumu kuhusu maeneo ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi ili kupunguza maafa yanayotokea mara kwa mara kati ya makundi haya.

§ Ranchi ambazo walipewa wawekezaji, lakini wakashindwa kuziendeleza zigawiwe kwa wafugaji watakaoweza kuendeleza maeneo hayo kiufugaji.

§ Serikali iendelee kutoa elimu juu ya ufugaji wa kisasa wa kuwa na mifugo michache na kuinenepesha ili kuongeza thamani ya mifugo yao kabla ya kwenda sokoni na hivyo kujiongezea kipato chao wenyewe na pato la Taifa kwa ujumla.

§ Elimu kuhusu umuhimu wa uvunaji wa mifugo itolewe ili kuongeza pato la mfugaji na pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuziboresha maabara za mifugo pamoja na kujenga maabara mpya katika maeneo mbalimbali nchini. Majukumu ya Maabara hizi ni makubwa sana na hivyo kuhitaji kujitegemea badala ya kuwa moja ya Idara katika Wizara. Kamati inashauri vituo vya utafiti wa mifugo *(VIC)* katika Kanda mbalimbali ziwe ni sehemu ya Maabara kuu *(Central Veterinary Laboratory)*. Aidha, Serikali ione umuhimu wa kuyapa hadhi Maabara ya Mifugo na kuyafanya Wakala wa Serikali na kuiongezea fedha ili kupanua uwezo wake katika utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo iliyopo nchini ni mingi sana ikilinganishwa na uwezo wa miundombinu ya kuihudumia kama malambo na majosho. Kamati inaishauri Serikali kuanzisha mpango maalum wa kujenga malambo na mabwawa kwa ajili ya kuipatia mifugo maji na majosho ya kuogesha mifugo ili kudhibiti kuenea kwa magonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi ni sekta muhimu katika nchi hii kutokana na mchango wake mkubwa katika kuwapatia wananchi ajira, lishe, kipato na kuingizia nchini fedha za kigeni. Pamoja na umuhimu wake bado Sekta hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo Kamati inashauri lazima kuwepo na mikakati maalum ya kukabiliana nazo. Changamoto hizo ni pamoja na:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa juhudi inazochukua ili kupambana na uvuvi haramu katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Pamoja na juhudi hizo uvuvi haramu bado unaendelea katika baadhi ya maeneo. Kamati inashauri:-

§ Mamlaka husika kuendelea kusimamia sheria zilizopo na ikibidi katika maeneo ya vijijini zitungwe sheria ndogo ili kudhibiti uvuvi huo;

§ Wauzaji wa zana za uvuvi wafuatiliwe kwa karibu kwa vile nao wanahusika katika kusambaza zana haramu; na

§ Serikali iendelee kutoa elimu kwa wavuvi juu ya umuhimu wa kutumia zana bora za uvuvi na hii iende sambamba na kuwapatia wavuvi mikopo yenye masharti nafuu ili waweze kununua zana bora za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza jitihada zinazofanywa na Mradi wa Usimamizi wa Mazingira katika Ukanda wa Pwani *(MACEMP)* ili kuboresha maisha ya wananchi waishio maeneo hayo. Pamoja na pongezi hizo, Kamati inaishauri Wizara kufanya tathmini ya awamu ya kwanza ya mradi huu wa *MACEMP* ili kubaini mafanikio na changamoto ili kuweza kukabiliana na changamoto hizo kwa awamu ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua kuwa ili Sekta ya Uvuvi ikue kwa kiwango cha kuridhisha na kuchangia kukua kwa uchumi ni lazima kuwepo na uwekezaji wa kutosha. Uwekezaji katika sekta hii bado hauridhishi ingawa sekta hii ina raslimali za kutosha kuinua kipato cha wananchi na Taifa kwa ujumla. Kamati inaishauri Serikali iboreshe mazingira yatakayowavutia wawekezaji wakubwa watakaofanya uvuvi wa kibiashara *(Large Scale Fishing)* na kujenga viwanda vya kusindika samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatoa pongezi kwa uanzishwaji wa ufugaji wa vifaranga vya samaki. Kamati inaishauri Serikali kuongeza uzalishaji wa vifaranga hivyo, wakati huo huo wananchi wapewe elimu kuhusu ufugaji huo ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha kuchimba mabwawa ya kufugia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa nafasi hii ili kuwasilisha Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Prof. David H. Mwakyusa - Mwenyekiti, Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Asaa Othman Hamad, Mheshimiwa Abdusalaam S. Ameir, Mheshimiwa Salim H. Khamis, Mheshimiwa Namelok E. M. Sokoine, Mheshimiwa Dr. Christine G. Ishengoma, Mheshimiwa Seleman Said Jafo, Mheshimiwa Moshi S. Kakoso, Mheshimiwa Sylevester M. Kasulumbayi, Mheshimiwa Prof. Peter Mahamudu Msolla, Mheshimiwa Modestus Dickson Kilufi, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mheshimiwa Mansoor Sharif Hiran, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Joyce John Mukya, Mheshimiwa Rose Kamil Sukum, Mheshimiwa Juma Othman Ali, Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mheshimiwa Seleman Said Bungara Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni, Mheshimiwa Dokta Titus Mlengeya Kamani na mimi Mheshimiwa Said J. Nkumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati napenda kuwapongeza Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David - Naibu Waziri, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, kwa ushirikiano wao mzuri waliyoipa Kamati katika kipindi

chote hiki. Aidha, nampongeza Katibu Mkuu Dkt. Charles Nyamrunda pamoja na wataalam wote wa Wizara kwa ushirikiano wao wakati wa kujadili na kuchambua bajeti ya Wizara kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah na Katibu wa Kamati ndugu Elieka Saanya kwa kuiwezesha Kamati kufanikisha shughuli zake na kuratibu taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naliomba Bunge lako Tukufu likubali na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Fungu 99 kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 jumla ya shilingi 57,165,193,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. SILVESTER M. KASULUMBAYI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya aliyonipa nikawa hapa leo hii. Kadhalika, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 99 (7) toleo la 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda hautatosha na kwa sababu hotuba hii ni ndefu, ninaomba yatakayobakia yarekodiwe kwa kuwa yako kwenye hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kutoa shukrani kwa chama changu cha Demokrasia na Maendeleo – *CHADEMA* kwa kuniteua kugombea Kiti cha Ubunge Jimbo la Maswa Mashariki na kushinda kwa kishindo kikubwa. Napenda pia kutoa shukrani za kipekee kwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, kwa kuniteua kuwa Waziri Kivuli wa Wizara hii. Nami natoa ahadi kwake kuwa nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu na kwa jinsi Mwenyezi Mungu atakavyonijalia kutekeleza wajibu wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitakuwa nimetenda haki kwa wananchi wa Jimbo la Maswa Mashariki kama sitawashukuru kwa imani kubwa waliyonayo kwangu na kwa chama changu cha Demokrasia na Maendeleo *(CHADEMA)*, nami nawaahidi kuwa nitaitunza na kuiheshimu imani yao kwangu, na kuendelea kushirikiana nao kuleta maendeleo katika Jimbo letu jipya. Mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa, naishukuru familia yangu, pamoja na ndugu na jamaa wote ambao wamenivumilia sana kutokana na misukosuko mbalimbali ya kisiasa ninayokutana nayo toka mfumo wa siasa za vyama vingi kuanzishwa na uchaguzi wa kwanza wa mwaka 1994, niligombea Kata ya Ipililo na kushinda kwa kishindo kikubwa kupitia *CUF*. Ndugu zangu hawa wamekuwa wakinipa ushauri wakati wote bila kuchoka na hivyo kunitia moyo wa kuendelea kuwawakilisha kwa hali na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mifugo inakabiliwa na matatizo kadhaa yaliyojikita katika sera yenyewe na mfumo mzima wa ufugaji hapa nchini. Maendeleo endelevu katika Sekta ya Mifugo bado hayajawekewa mpango mkakati mahsusi utakaohusisha mahusiano katika matakwa ya kijamii, kiuchumi na kimazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fikra ya viongozi na watunga sera wengi katika nchi yetu ya Tanzania na Afrika ya Mashariki kwa ujumla ni ufugaji wa asili ni wa kizamani, na kuwa hauna tija kwa uchumi wa Taifa. Vilevile kuna fikra kuwa aina hii ya maisha inachangia kuharibu mazingira na hauwakilishi mfumo mzuri wa utumiaji wa maliasili zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji kwa upande mwingine wanaonekana wabishi na wapenda fujo. Miongoni mwa hawa wafugaji pia wanaonekana kuyakataa mabadiliko na maisha ya kisasa na wanang'ang'ania mifugo yao na kurandaranda nayo hovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sera zinazopinga ufugaji wa asili, matamko ya viongozi wakuu wa nchi na utekelezaji wa matamko hayo hauzingatii maslahi ya wafugaji. Hapa

tutatoa mifano michache: Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, tarehe 22 Februari 2006, alisema: *“Ni bora wafugaji wachache wakasirike, lakini tulinde maisha ya kizazi kijacho” na 16 Novemba, 2006: kusisitiza hotuba ya 5 Februari, 2005 kuwa “Nchi nzima haiwezi kugeuzwa kuwa malisho….maasai na blanketi hawezi kuingia Bungeni….ronjo hazitakuwepo (malisho yaliyotengwa kwa misimu).”*

Pili, tarehe 23 Novemba, 2006 Hotuba ya Mheshimiwa Makamu wa Rais katika Wilaya ya Mbarali alisema: *“Nimekuja hapa leo kujionea utekelezaji wa zoezi la kuhamisha wafugaji na ufanisi wake, nimeridhishwa na mafanikio yaliyopatikana na hatuturudi nyuma.”*

Tatu, tarehe 05 Februari, 2009 Mheshimiwa Waziri Mkuu Bungeni alisema: *“Kamwe Serikali haitaruhusu ufugaji kama unavyofanyika na wafugaji wa kuhamahama nchini….” Aliendelea kusema: “Ukiniuliza wafugaji waende wapi, nami nitakuuliza walitoka wapi.”* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limekuwa linawaathiri sana wafugaji hapa nchini, ni ile hatua ya Serikali kuanzisha na kuendelea kupanua Mbuga za Wanyama na Mapori ya Akiba ya Uhifadhi katika maeneo ambayo wafugaji huyatumia kuchungia mifugo yao. Jambo hili linazidi kupunguza eneo la malisho kwa mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kauli hiyo, Waziri Mkuu alikuwa anawaagiza wafugaji warudi katika maeneo yao ya asili ya Arusha, Manyara, Shinyanga, Musoma, Mwanza Kagera na Tabora na kwingineko wanakotoka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshindwa kuyashughulikia matatizo yanayowakabili wafugaji kwa sababu hawajayafahamu kwa mtazamo sahihi matatizo yenyewe. Tatizo kuu ni ongezeko la mifugo ambayo kwa muda mrefu haikuwa na soko la uhakika lililo zuri. Neema hii ilipelekea maeneo ya malisho kutotosha; ndipo hamahama ikatokea. Serikali haikupaswa kulichukulia suala zima kwa mtazamo hasi, ilipaswa kukaa na wafugaji na kutafuta suluhisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya uharibifu wa mazingira uliosababishwa na mifugo katika Bonde la Ihefu hayakuweza kuthibitishwa kisayansi. Taarifa ya Danida/Benki ya Dunia (1995) imeelezea kuwa uharibifu wa mazingira katika Bonde la Usangu na Ihefu ulichangiwa na kilimo cha umwagiliaji. Machibya na Mduma (2005) wameeleza kuwepo kwa matumizi mabaya ya maji kwa ajili ya kilimo katika bonde la Usangu kwa asilimia 70. Mashamba 10 ya umwagiliaji yaliyofadhiliwa na *ADB, WB, CIDA, FAO* kati ya mwaka 1960 na 1990 yalianzishwa na yamesababisha uhaba wa maji katika Bonde la Usangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti uliofanywa na Sokile na wenzake (2002) umeonyesha kuwa maji yamekuwa yakitumiwa vibaya na mfumo wa umwagiliaji. Mifereji ya umwagiliaji imekuwa ikitiririsha maji kwenye mashamba ambayo hayajalimwa kwa mwaka mzima hata wakati maji hayahitajiki kwa umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasema kuwa huu ni ushahidi tosha kuwa Serikali haina mtazamo sahihi wala mipango mizuri ya kuwasaidia wafugaji kutokana na mifugo kuongezeka na malisho kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wa aina zote tulionao katika nchi yetu ni sehemu muhimu sana ya jamii yetu, uhamisho wa sehemu hiyo ya jamii kutoka katika maeneo yao ya kuendeshea maisha yao ya kila siku kwa sababu yoyote bila kujadiliana nao ni kuwanyima haki yao ya msingi, na inatakiwa kulaaniwa na wapenda amani. Kugawiwa wawekezaji maeneo ya wafugaji; mfano, eneo aliojichukulia Mkurugenzi wa Wilaya ya Kilosa wakati tayari ilifahamika hakukuwa na ardhi ya kutosha kwa wafugaj; kuchukuliwa ardhi ya wafugaji wa Hanang na Serikali kama mashamba ya ngano na hivi leo kubinafsishwa kwa wawekezaji toka Kenya haya yote ni matendo ya kionevu, na yanastahiki kulaaniwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha kuwapeleka wafugaji Lindi, Mtwara na Pwani - maeneo ambayo hayafai kwa ufugaji kwa kukosa miundombinu kwa ajili ya mifugo kinaonyesha

kwamba Serikali haikufanya utafiti na matayarisho ya kutosha kabla ya utekelezaji wa zoezi hilo lililogharimu maisha na mali nyingi za wafugaji hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhamishiwa kwa wafugaji Kilosa na maeneo mengine ya nchi ni mwendelezo wa azma ya Serikali kuumaliza ufugaji wa asili Tanzania, kama Mheshimiwa Rais alivyosema kuwa nchi nzima haiwezi kuwa malisho. Hivyo basi, ili kutekeleza kauli hiyo, operesheni "hamisha wafugaji" ikafuatia. Madhara yake ni wafugaji kubakia masikini kwa kupoteza mifugo yao mingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna migogoro mingi na mikubwa ambayo Serikali ndiyo inatakiwa kulaumiwa kwa kushindwa kuwajibika na kulinda raia na mali zao. Hivi sasa kuna migogoro kati ya wafugaji wa Loliondo na Kampuni ya uwekezaji ya *Ortello Business corp*, wafugaji wa Meatu na Kampuni ya *Mwiba Holding*, wafugaji wa Kijiji cha Kimotorok Simanjiro na Mbuga ya Tarangire na migogoro mingine midogo midogo mingi katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani imepata taarifa kuwa Serikali imeingia mkataba wa kumpa mwekezaji toka Marekani *(Agrisol Energy)* ardhi yenye ukubwa wa ekari 327,755, maeneo yaliyokuwa yakikaliwa na wakimbizi toka nchi jirani ili afanye uwekezaji katika kilimo cha mazao ya nafaka, miwa pamoja na mazao mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kuwa kabla ya wakimbizi kukalia eneo hilo, lilikuwa likitumiwa kwa pamoja na wakulima na wafugaji, na hakukuwa na mgogoro wowote baina ya makundi hayo muhimu katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo kilichofanywa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenda Marekani kutafuta Mwekezaji kama alivyokiri mwenyewe wakati akihitimisha majadiliano ya bajeti ya ofisi yake kuwa Septemba, 2010 alikwenda Marekani (Iowa) na kukutana na mmiliki wa makampuni ya *Agrisol Energy* na kummilikisha maeneo hayo, wakati mwaka 2007 alikaa na wawakilishi wa wafugaji Mkoani Rukwa kwa lengo la kutafuta suluhisho la mgogoro baina yao na wakulima, na akaunda Tume iliyopendekeza wahusika wapatiwe maeneo yaliyokuwa yanakaliwa na wakimbizi, lakini kwa sababu zake binafsi akashindwa kuwapatia suluhu wafugaji hao. Huu nao ni mgogoro mwingine mpya unaotengezwa na Serikali.

Kambi ya Upinzani inaona kitendo cha Waziri Mkuu ni cha ajabu sana, kwa sababu badala ya kuwasaidia watu wa eneo hilo, ameisaidia kampuni ya kigeni ili izidi kutajirika kwa raslimali za nchi ya Watanzania. Kitendo hicho cha kushindwa kuwalinda Watanzania na mali zao kinamwondolea moja kwa moja uhalali wa kuwa kiongozi, hivyo kwa lugha rahisi ni yeye kupima uwezo kwa kosa hilo na kufanya uamuzi mgumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inashauri Serikali ifanye mambo yafuatayo ili kuimarisha ufugaji wa asili:-

(a) Operesheni za kuhamisha wafugaji zisimamishwe na wafugaji wasaidiwe na Serikali kugawana maeneo na wakulima kwani miaka yote wafugaji wamekuwa wakiishi pamoja na wakulima na makundi haya yanategemeana katika kuendesha maisha yao ya kila siku.

(b) Serikali itathmini upya sera yake ya kuwamilikisha wanaoitwa wawekezaji maeneo makubwa ambayo tayari yanakaliwa na wafugaji na wakulima. Kama uwekezaji utahitajika katika ardhi za wafugaji usifanyike bila kufanya makubaliano na wafugaji wenyewe.

(c) Ripoti ya Kamati inayohusu kuhamishwa kwa wafugaji Ihefu na ile ya mgogoro wa ardhi kati ya mwekezaji na wafugaji ripoti ziwekwe hadharani na zifanyiwe kazi.

(d) Tume huru iundwe ili kuchunguza kuhamishwa kwa wafugaji kwa nguvu itakayowashirikisha wanaharakati, wadau wa maendeleo, makundi ya haki za binadamu, wafugaji na wakulima pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali.

(e) Serikali itoe taarifa ya kiasi cha fedha kilichokusanywa kutokana na operesheni ya kinyanganyi iliyowatoza wafugaji faini zisizo halali na fedha hiyo irudishwe kwa wafugaji.

(f) Serikali itenge na kupima maeneo ya wafugaji na kuwapatia hatimiliki sambamba na kuchimba malambo na visima vya maji katika maeneo hayo ili kuepusha kuhamahama.

(g) Utaratibu wa utatuzi wa migogoro na mfumo wa Mahakama utumike kutatua matatizo ya ardhi badala ya kufanyia kazi matamko ya kisiasa ambayo hayazingatii utawala wa sheria.

(h) Serikali ifanye tathmini ya ongezeko la mifugo dhidi ya raslimali na mahitaji ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa Sekta ya Mifugo kwa uchumi wa nchi bado siyo mkubwa pamoja na kuwa Tanzania ni ya tatu barani Afrika kwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo, tukiwa na ng'ombe milioni 19.2, mbuzi milioni 13.6, kondoo milioni 3.6, nguruwe milioni 1.7 na kuku wa kienyeji zaidi ya milioni 35, na kuku wa kisasa milioni 23. Lakini bado mchango wa mifugo katika pato la Taifa ni dogo mno. Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2010 inaonyesha mchango wa Sekta hii katika pato la Taifa *(GDP)* kushuka kwa 0.1% kila mwaka katika kipindi cha miaka mitano. Mwaka 2006 ilikuwa 2.8% mpaka kufikia mwaka 2010 ilikuwa 2.4%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa na idadi kubwa ya mifugo isiyowiana na pato ina maana kuwa mifugo tuliyonayo haina ubora unaostahili hasa katika Soko la Mifugo. Zipo nchi zenye idadi ndogo ya mifugo kuliko sisi, lakini mchango wake katika pato la Taifa ni mkubwa mno ukilinganisha na sisi. Nchi hizo zina mifugo bora kuliko sisi. Kwa mfano, Botswana ambayo sehemu kubwa ya nchi ni jangwa, imepata mafanikio makubwa katika uchumi wake kwa kutegemea kwa kiasi kikubwa mifugo michache inayofikia milioni tatu hivi kwa hesabu za mwaka 1999. Ni nchi yenye kutajirika duniani kwa biashara ya nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *NARCO* inakusudia kuuza madume karibu 10,000 ya Boran kwa wafugaji wa ndani ili kuhakikisha kuwa inapata ng'ombe bora wa kuchinjwa wakati wote. Hatua hiyo siyo tu itawahakikishia wateja kupata nyama iliyo bora wakati wote na pia kuwaongezea kipato wafugaji wenyewe. Kambi ya Upinzani inaliona jambo hili kuwa ni la msingi sana, lakini tatizo lililopo ni kwamba, nchi yetu ina wafugaji wengi mno na wameenea nchi nzima ambao sasa wanaitwa "wachungaji." Tunaitaka Serikali itueleze ni kwa vipi madume hayo 10,000 yatawafikia wafugaji hao walioenea nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inashauri Serikali iandae mpango wa kuanzisha ranchi ndogo ndogo za wananchi *(Community mini - ranches)* ili kuweza kusaidia juhudi za *NARCO* katika ngazi ya jamii kuingiza mitamba, madume na mbegu bora kwa ajili ya kuzalisha machotara ambao watamudu mazingira husika. Uanzishaji wa ranchi hizi ndogo ndogo utaleta manufaa mengi kwa jamii kama ambavyo Baba wa Taifa aliweza kuona toka mwanzo baada ya uhuru. Kazi kubwa ya ranchi hizi mbali na kuwa vituo vya kusambaza mitamba na madume kwa vikundi vya wafugaji pia vitahusika na:-

(a) Kukusanya maziwa toka kwa wafugaji na kuyapeleka kwenye vituo vya usindikaji;

(b) Uzalishaji wa ng'ombe chotara wa kwa wafugaji mbalimbali;

(c) Kuboresha matumizi bora ya ardhi kwa wafugaji na uoteshaji wa nyasi mbambali katika mashamba darasa katika maeneo mbalimbali;

(d) Kuanzisha vituo vya kutolea huduma za ugani na kuelimisha juu ya ufugaji wa kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na haya, pia Wizara kwa kupitia ranchi hizi za jamii itaweza pia kushughulikia upatikanaji wa maji kwa urahisi, utengaji wa maeneo na mashamba madogo madogo ya kufugia au kuoteshea majani ya kulisha nyakati za kiangazi na masika (malisho mzunguko).

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine muhimu ambalo Wizara ya maendeleo ya mifugo na Uvuvi haina budi kulitekeleza kwa haraka kwa manufaa ya wafugaji ni tafsiri ya dhana ya Kilimo Kwanza au Mapinduzi ya Kijani ambayo nchi yetu imeanzisha miaka miwili iliyopita. Ieleweke kwamba tafsiri sahihi ya Mapinduzi ya Kijani katika kilimo, kwa Sekta ya Mifugo ni Mapinduzi Meupe kwa maana ya ongezeko la uzalishaji wa maziwa, ambayo yatatoa mazao mbalimbali ya mifugo kwa kusindika. Nchi nyingi zikiongozwa na India, Uholanzi zimeweza kufanikiwa kwa hili, na kuongeza pato la Taifa kutokana na mazao ya mifugo, pamoja na kuondoa umasikini kwa wafugaji wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Biashara ya Mazao ya Mifugo pamoja na kuwa na idadi kubwa ya mifugo, wananchi wa Tanzania bado hawajafaidika na Sekta ya Maziwa kwa kiwango kinachotarajiwa na mchango wake kiuchumi ni mdogo kwa wazalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2010 inaonyesha kuwa lita za maziwa zilizozalishwa mwaka 2010 ni jumla ya lita bilioni 1.65 kutokana na ng'ombe wa maziwa 680,000 kati ya jumla ya ng'ombe milioni 19.2. Hapa inaonesha hakuna uwiano mzuri wa idadi ya lita za maziwa na kiasi cha ng'ombe. Hii ina maana kuwa idadi ya maziwa yanayozalishwa kwa kila ng'ombe ni kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na sekta hiyo ya maziwa kutokuwa tija toshelevu kulinganisha na idadi ya ng'ombe tulizonazo, changamoto kubwa na ya msingi ni ukosefu wa viwanda vya nyama. Kiwanda kilichokuwepo hapo awali cha *Tanganyika Packers* kiliuzwa kabla ya kufanya utaratibu mbadala, jambo ambalo kwa kiasi kikubwa limesababisha wafugaji wasipate soko la uhakika la mifugo wao. Serikali inajenga machinjio tu ambayo hayaongezi ubora wa bidhaa zitokanazo na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwaeleza wafugaji ni lini kiwanda cha nyama cha Shinyanga kitamalizika kujengwa na kuanza kutumika? Kwani ujenzi wake hadi sasa unakaribia miaka 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasisitiza kuimarishwa kwa viwanda vya ngozi vilivyopo katika maeneo ya wafugaji, sambamba na kujenga na kuimarisha machinjio katika kanda zote hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hivi majuzi daktari wa mifugo Wilaya ya Maswa alikuwa anaomba kibali cha kuchoma vipande vya ngozi 18,000 kutokana na kushindwa kupata soko la kuuza ngozi hizo. Pale pale kuna kikundi cha wajasiriamali cha *SENANI GROUP* kinajihusisha na kutengeneza bidhaa za ngozi lakini hawapati ngozi kutokana na ukiritimba usiokuwa na msingi wa sheria ndogo zinazotungwa na Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la kuangalia ni masoko ya uhakika ya mifugo. Pendekezo letu la *NARCO* kuwezesha wafugaji kupitia ushirika na vijiji kuanzisha ranchi ndogo ndogo ndani ya jamii na kuboresha miundombinu ya huduma za mifugo ikiwepo maji na malisho bora, itaongeza unenepeshaji wa mifugo na kuwafanya wafugaji waweze kuvuna mifugo kwa ajili ya kuuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yaliyotengwa kama minada kwa ajili ya kuuzia mifugo hayana huduma yoyote kwa wauzaji na wafugaji. Maeneo mengi hayana vyoo na sehemu ya kupata chakula. Tatizo lingine kubwa linalowakumba wafanyabiashara wa mifugo ni ukosefu wa usalama kwenye minada. Kumekuwa na matukio ya mara kwa mara ya uvamizi wa majambazi ambao hupora fedha za wafanyabiashara hawa wa mifugo na wakati mwingine watu kupoteza maisha. Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuhakikisha kunakuwa na askari wa kutosha ili kulinda usalama siku zote za minada katika maeneo husika.

Kambi ya Upinzani inapendekeza Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI ianzishe mpango wa uboreshaji wa masoko ya msingi *(livestock primary markets)* ndani ya jamii kwa kuweka mizani ili kuweza kupunguza kunyonywa kwa wafugaji kwa bei ndogo ya mifugo wakati bei ya nyama iko juu. Wafugaji wakiwezeshwa kuuza mifugo kwa kilo/mizani bei itakuwa nzuri, na hivyo kushawishi

wafugaji kufuga kibiashara zaidi badala ya kupiga kelele za mara kwa mara kwamba wafugaji hawataki kupunguza mifugo wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la magonjwa ya milipuko ya mifugo limekuwa hadithi ya mara kwa mara ndani ya nchi yetu. Kwa hakika hatutaweza kufikia kwenye Mapinduzi Meupe na ufugaji wa kibiashara wenye tija ya uhakika kama suala la magonjwa ya milipuko halitapewa kipaumbele na Wizara hii. Magonjwa kama Homa ya Midomo na Miguu, Homa ya, Kimeta yamekuwa magonjwa tishio kwa mifugo yetu kwa ujumla.

Kambi ya Upinzani inasema kwamba sasa ni wakati muafaka kwa Wizara kushughulikia haya magonjwa. Vituo vyetu vya utafiti vikiongozwa na Chuo Kikuu cha Sokoine *(SUA),* Vituo vya Utafiti wa Magonjwa ya Mifugo *(VIC)* na Kituo cha Temeke viwezeshwe kufanya utafiti wa kina ili kujua tatizo na hatimaye kupata chanjo ya magonjwa haya ndani ya nchi badala ya kutegemea nchi nyingine. Tunapendekeza kwamba wadau wa nje washirikishwe katika kutimiza hili. Kwa kufanya hivyo, Kambi ya Upinzani inaamini tutakuwa tumepata mafanikio mengi mbali ya kupata chanjo, lakini pia ujuzi na maarifa zitakuwa zimeongezeka ndani ya vituo na tasisi zetu za utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa ya mifugo yaenezwayo na kupe yamekuwa tatizo sugu kwa Taifa hili. Serikali kwa kupitia Wizara hii imekuwa ikijaribu bila mafanikio makubwa kupunguza tatizo liletwalo na kupe kwa kutoa ruzuku kwenye dawa ya kuogeshea.

Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali iongeze ruzuku kwenye madawa ya kuogeshea. Pia ruzuku ya kutosha ielekezwe kwenye chanjo ya magonjwa kama Ndigana Kali kwani ugonjwa huu ndiyo hatari kupita yote yaletwayo na kupe. Kwa bahati, chanjo yake inapatikana ila kwa bei kubwa sana. Hivyo, wafugaji wengi hawawezi kumudu kuinunua kwa wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukame umekuwa ni baa la mara kwa mara ndani ya nchi yetu na umeathiri uzalishaji na ufugaji kwa ujumla. Katika kipindi kisichozidi miaka 10 sasa nchi imeshakumbwa na ukame zaidi ya mara tatu (2005/2006, 2008/2009, 2011/2012). Bila kufanya juhudi za makusudi kupambana na hali hii, hatukuwa na uhakika wa chakula, na maisha ya watu wetu yatakuwa ya kubahatisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwa na mpango maalumu wa kufuatilia matokeo ya ukame, namna ya kupunguza madhara na kuwandaa wananchi kwa matokeo ya majanga ya ukame. Mbinu mbalimbali ziandaliwe na kuanza kutekelezwa kupunguza makali ya ukame kwa kutazama mzunguko wake. Maeneo kama Longido, Ngorongoro, Shinyanga, Kongwa na hata Simanjiro/Monduli hayana budi kuzingatiwa.

Aidha, Kambi ya Upinzani inashauri Wizara ifikirie namna ya kusaidia wafugaji baada ya ukame. Wenzao wakulima, mara nyingi hupatiwa mbegu za mazao. Je, wafugaji sio sehemu ya nchi hii? Nao pia wanahitaji msaada baada ya ukame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ambalo kwa muda mrefu wataalamu na wadau wengi wamekuwa wakilikwepa kwa muda mrefu ni suala la Bima ya Mifugo ili kujikinga na majanga na ajali. Wafugaji ni kundi linalohusika katika harakati nyingi za kuhakikisha upatikanaji wa nyama na maziwa kwa nchi hii. Bila wao, fedha nyingi za kigeni zingetumika kuagiza mazao haya nje ya nchi. Hata hivyo, ufugaji umebaki kuwa njia ya maisha inayokabiliwa na matatizo na changamoto nyingi za kimazingira na hasa, ukame wa mara kwa mara, magonjwa ya mifugo na madhara yatokanayo na wanyama wakali wa pori kama simba.

Kambi ya Upinzani inapendekeza kwamba ili kuweza kuwashawishi wafugaji kuongeza ubora wa mifugo na kupunguza madhara ya magonjwa, ianzishe mkakati wa Bima ya Mifugo ili kukinga mifugo na majanga yaliyotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya hali ya uchumi inaonyesha kuwa uvuvi ulichangia asilimia 1.4 ya pato la Taifa kwa mwaka 2010. Jumla ya tani 347,157 za samaki wenye thamani ya Shilingi milioni 774.5 zilivunwa. Kati ya tani hizo, tani 294,474 sawa na asilimia 84.4 zilitokana na uvuvi katika maji baridi na tani 52,683 sawa na asilimia 15.2 zilivuliwa maji chumvi.

Kambi ya Upinzani inataka kuelewa, tani 52,683 zilizovunwa katika maji chumvi zinahusisha zilizovunwa katika ukanda wa bahari kuu au samaki hao walitokana na uvuvi wa wavuvi wadogo wadogo tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inasema kuwa katika maji ya Tanzania, samaki aina ya jodari hupatikana kwa wingi kuanzia mwezi Julai hadi Novemba. Katika kipindi hicho, wastani wa tani mbili hadi tano za samaki hupatikana kwa meli kwa siku. Aidha, kuanzia mwezi Desemba hadi Juni, katika kipindi hicho wastani wa nusu tani za samaki hupatikana kwa meli kwa siku.

Taarifa hiyo ya Serikali ni kwamba uvuvi wa bahari kuu kwa meli 71 kwa miezi mitano tu zinavunwa tani 53,250. Kambi ya Upinzani inataka kuelewa kwa tani hizo Serikali inapata mrabaha kiasi gani? Tunauliza hili kwani Serikali haina mfumo wa kufuatilia ni kiasi gani kinavunwa na meli hizo kwani meli zikishavuna zinaondoka, hazirudi tena kwetu kutoa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu hizi zinaonyesha kuwa kama tukiwa makini na kuwekeza kwenye viwanda vya samaki ukanda wa Pwani, Ziwa Tanganyika na Nyasa ni dhahiri Sekta hii ya Uvuvi itaweza kuliingizia Taifa pato kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa rasmi za Serikali hapa Bungeni ni kwamba, uvuvi wa Bahari Kuu huliingizia Serikali mapato kutokana na ada za leseni za uvuvi na usajili wa meli zinazovua kwenye eneo husika. Katika mwaka 2010/2011, jumla ya meli 71 za uvuvi zilisajiliwa na kukatiwa leseni za kuvua katika Bahari Kuu, ada ya leseni kwa meli inayovua kwa uvuvi wa *purse seining* ada ni dola za Kimarekani 12,000 kwa miezi mitatu au 35,000 kwa mwaka na usajili wa meli ya kigeni ni dola 2,000 kwa mwaka. Mapato yaliyopatikana ni jumla ya Dola za Kimarekani 2,074,400. Meli za uvuvi katika Bahari Kuu hulenga kuvua samaki aina ya jodari na samaki wengine wa aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasema kuwa ada kwa meli za kigeni zinazovua baharini bado ni ndogo mno kwa kulinganisha na nchi nyingine ambapo ada ya kuvua katika bahari kuu ni dola za Kimarekani kati 60,000 hadi 100,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa vyombo mbalimbali vya habari vya jana tarehe 26 Julai, 2011 imeripotiwa kuwa nchini mwetu wameingizwa samaki aina ya kamongo wanaoaminika kuwa wana mabaki ya sumu ya mionzi ya nyukilia na waliingizwa nchini tarehe 11 Julai, 2011 kwa kibali cha *TFDA Na. TFDA11/F/IPER/0896. (Makofi)*

Kambi ya Upinzani, tunahoji, ilikuwaje kampuni ya *Alphakrust Ltd* ya Dar es Salaam ikaruhusiwa kuingiza samaki hao? Kama *TDFA* ndio waliotoa kibali cha kuingizwa kwa samaki hao baada ya kufanya ukaguzi na kujiridhisha kuwa samaki hao hawana madhara: Je, ni nani au mamlaka gani iliyogundua kuwa wana madhara? Ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya maafisa waliohusika kutoa kibali husika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi inawezekana kweli kwa nchi yenye ukanda mkubwa kama yetu wa Bahari na wa pwani wa bahari wa kilometa 1,424 upana wa kilometa za mraba 64,00, bahari kuu upana wa kilometa za mraba 223,000. Eneo la maji baridi maziwa makubwa matatu na madogo 29, kwa raslimali hii yote tuliyopewa na Mwenyezi Mungu iliyojaa samaki wengi wa kila aina, kama Taifa tuna haja kweli ya kuagiza samaki kutoka nje ya nchi? Kwanini fedha zetu za kigeni zisitumike kununua mahitaji mengine ambayo hayapatikani nchini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Wenje, Wenje alitaka kutumia kanuni ya kudumu namba 45 ya hoja ya dharura ambayo masharti yamebainishwa katika kanuni ya 48. Hoja hii inahusu jambo la dharura lolote likitokea linalogusa na linahitaji hatua za haraka na jambo hili siyo lazima liwe jambo la kivita. Kwa hiyo, kutokana na kifungu hiki, Mheshimiwa Wenje alitaka aweze kuitaka Bunge liweze kuchukua hatua ya kuchukua mjadala dhidi ya jambo hili ambalo tayari litakuwa limewaathiri wananchi wengi sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Samahani, maelezo ambayo umeyatoa, kwenye hotuba yako hayamo: Je, yaingizwe katika *Hansard*?

**MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI:** Yaingizwe.

**MWENYEKITI:** Yaingizwe. Nimeuliza kwa sababu umesoma kitu ambacho hakimo kwenye hotuba yako.

**MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI:** Yaingizwe.

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI:** Tatizo la Tanzania kutonufaika na maliasili zake lipo pia katika sekta hii kama lilivyo katika sekta nyingine. Lipo tatizo kubwa la Serikali kushindwa kusimamia sekta hii na kusababisha kuendelea kuvuliwa kwa samaki wachanga, matukio ya unyanganyi kuendelea kushamiri maeneo ya uvuvi, na tatizo la wavuvi haramu kuendelea kutuibia kwa kushirikiana na wafanyakazi Serikalini wasio waaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero kubwa kwa wavuvi katika maziwa yetu ni leseni za uvuvi kuwa ghali mno kulinganisha na hali halisi ya biashara hiyo. Gharama ya leseni ni kati ya Sh. 80,000/= hadi Sh. 118,000/=. Leseni za mitumbwi ni kubwa, mbali ya hilo ni pale wafanyakazi wanaofanya kazi katika mtumbwi au boti ya uvuvi kuhitajika kukatiwa leseni. Kambi ya Upinzani inaona kama kweli Serikali inajali wangewekewa utaratibu kwa watumishi hao kukatiwa Bima. Kwa njia hii Serikali ingeonekana inajali wananchi wake badala ya utaratibu uliopo sasa wa leseni. Tozo la ushuru wa nyavu ni kuanzia Sh. 13,000/= kwa kila nyavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wavuvi nao wanahitaji kupata huduma zote zinazotolewa na Serikali kama wenzao wakulima au wafanyabiashara wengine, hivyo tunaishauri Serikali kumaliza haraka tatizo la wavuvi kutopata ruzuku na mikopo kwa vifaa wanavyotumia kufanyia kazi zao kama wakulima wanavyopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuifanya sekta hii kuwa na mchango mkubwa kwa uchumi wetu na kuongeza kiwango cha uvunaji wa samaki, Kambi ya upinzani inapendekeza yafuatayo:-

- Badala ya kujihusisha tu na kuwatafuta wavuvi haramu wanaotumia nyavu na njia nyingine, Serikali ijielekeze pia kwenye vyanzo vya uzalishaji na uingizaji wa vifaa hivyo ili kukomesha visiingie kwenye soko. Kupambana na wavuvi huku nyavu ndogo na vifaa vingine vikiendelea kuingia kunakwamisha jitihada zote. Swali la kujiuliza ni: kwa nini upande wa nchi jirani za Kenya na Uganda hawana tatizo la nyavu ndogo? Huu ni mradi haramu wa Maafisa Uvuvi wa Tanzania dhidi ya wavuvi wetu. *(Makofi)*

- Serikali ipige marufuku mtindo wa Maafisa Uvuvi kukamata wafanyabiashara wa samaki sokoni kwa kisingizo cha kuuza samaki ambao wamevuliwa kwa njia zisizo halali. Hii ni kushindwa kazi kwa Maafisa Uvuvi kwani wanapaswa kufanya kazi yao katika mialo na sio sokoni. *(Makofi)*

- Kuimarisha mipaka katika eneo la maji. Hii ni kwa sababu katika maziwa yetu na ukanda wa bahari tumechangia na nchi nyingine. Hii inachangia tatizo la ujambazi majini.

- Badala ya kutegemea samaki kutoka kwenye mito, maziwa na ukanda wa bahari, wananchi wapewe elimu juu ya ufugaji samaki katika mabwawa na kuanzisha vituo vya kutosha nchini kuzalisha vifaranga vya samaki. Hii itasaidia kuongeza upatikanaji wa samaki kwa wananchi hasa maeneo ambayo hayana maziwa na bahari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba sasa kuwasilisha mbele ya meza yako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, kwa taarifa yako.

Waheshimiwa Wabunge, tumepokea hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Wizara hii na taarifa ya Msemaji wa Upinzani. Sasa tunaanza majadiliano. Nitawataja watakaochangia asubuhi hii, tutaanza na Mheshimiwa Saleh Pamba, na Mheshimiwa Kikwembe ajiandae. Mheshimiwa Abdulkarim Ismail Shah, Mheshimiwa Rita Mlaki wote pia wajiandae. Tunaanza na Mheshimiwa Saleh Pamba.

**MHE. SALEH AHMED PAMBA:** Mheshimiwa mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa kwanza katika hoja iliyopo mble yetu. Kabla yakwenda kwenye hoja yenyewe, napenda nichukue nafasi hii nitoe shukurani zangu kwa wapiga kura wa Jimbo la Pangani ambao wamenipa kura za kutosha asilimia 71 na nawaahidi kwamba sitawaangusha. Napenda nichukue nafasi hii pia kukipongeza chama changu cha Mapinduzi kwa ushindi mkubwa kilichoupata na kuunda Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua nafasi hii adimu niwashukuru Wabunge wote kwa umoja wao kwa kunichagua kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Bunge nasema asanteni sana, nasema sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni Serikali sikivu, imesikia hotuba ya Kambi ya Upinzani kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inawanyanyasa wafugaji. Lakini katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri napenda nichukue nafasi hii kumpongeza sana, ametoa hotuba nzuri, ya kina, hotuba yenye takwimu nyingi, ukurasa wa 176 wa hotuba, ni *response* ya Chama cha Mapinduzi na Serikali ya Chama cha Mapinduzi na Wizara hii imetenga hekta milioni 2,282,196.73 kwa ajili ya wafugaji peke yake ili wasiweze kuhamahama. Hiyo ni kazi ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayowajali wafugaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue tena nafasi hii niishukuru sana Wizara. Mchango wa Sekta ya Mifugo na Uvuvi, kwa miaka mitano, kumi iliyopita ulikuwa chini sana 5% mwaka 2005, 3.6% mwaka 2010, na uvuvi vile vile inaonekana sekta hii ni sekta isiyokua. Lakini napenda nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Wizara kwa kuleta mpango maalum unaoitwa *livestock development program.*

Huu ni mpango ambao utatuondoa katika hali ambayo tunayo hivi sasa ili sekta hii ya mifugo na uvuvi iweze kuchangia katika pato la Taifa. Naishukuru sana Wizara kwa kuleta pia mpango wa maendeleo ya uvuvi, *Fisheries Development Program* ambayo itatuondoa katika 2% tuliyopata mwaka 2000, 1.4% na kutuleta kwenye mpango wa 5% ambayo ndiyo mategemeo yaliyopo katika mpango wa maendeleo ya Taifa. Nasema Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Mifugo, nasema hongereni sana kwa kuleta program hizo, zina matumaini makubwa, zitatusaidia sana katika kuleta maendeleo katika sekta hii ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia bajeti inayotolewa kwa Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi, kwa malengo haya na kwa kawaida tunapoanza bajeti moja, ni mwanzo wa bajeti nyingine. Ninaamini kabisa Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu na ili kuikwamua sekta hii, bajeti inayotolewa sasa hivi ya Shilingi bilioni 20 haitoshi, lazima twende kwenye bajeti ambayo iko kwenye mipango ya kutoa kipaumbele katika sekta hii na bajeti iliyotengwa ni Shilingi bilioni 345.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kwamba, tutakapoingia kwenye Bajeti ijayo ya mwaka 2012/2013, Serikali itatilia maanani ili kuhakikisha kwamba, Sekta hii inapewa rasilimali na nyenzo za kutosha ili iweze kuleta mchango katika Pato la Taifa.

Nimefarijika sana na Hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Katika Hotuba yake amesema kwamba, lengo kubwa la Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Uvuvi, kwanza ni ku-*modernise Fishing and Fishing Industry through value addition*. Hilo ndiyo muhimu sana kwamba; ni lazima Sekta ya Uvuvi iendelee na ihakikishe kwamba, inaongeza thamani kwa mazao ambayo tunauza. Mazao tunayouza nje kama ni Samaki basi tuyaongezee thamani, kama ni minofu basi ni lazima tuiongezee thamani na kuhakikisha kwamba, tunaiendeleza Sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuchangia, nilikuwa ninaangalia nchi ndogo tu kwa takwimu, Nchi ya Vietnam, siyo kubwa kama Tanzania. Nilikuwa ninaangalia Sekta yake ya Uvuvi ina-*perform* vipi. Nchi yetu ya Tanzania ina Mito, Maziwa makubwa matatu; Victoria, Tanganyika na Nyasa na mengine mengi madogomadogo, lakini bado hatujatumia rasilimali hizi kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mwaka 2010, Nchi kama Thailand na Vietnam, mapato yake ya samaki peke yake yalikuwa ni dola bilioni 4.5. Mapato ya Tanzania ya samaki hayajafikia hata dola milioni tatu. Kwa hiyo, tuna kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba, mipango hii ambayo tumeiandaa na kuweka tunaitekeleza kwa haraka sana na kikubwa ambacho tunatakiwa tukifanye ni kama alivyosema Mheshimiwa Waziri katika Hotuba yake kwamba, lazima tu-*modernise Fisheries Industry* na *Livestock Industry* hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaangalia tena kwa mazao ya baharini, ambayo yanatoka maeneo ya Pwani. Mazao ya baharini kama Ngisi, *Octopus* au Pweza, kwa Vietnam peke yake, mwaka 2010 dola milioni 113 ndizo zilizopatikana kwa samaki hawa tu. Tunayo Bahari kubwa sana, tuna ukanda wa maili 200 sasa hivi, Umoja wa Mataifa utatuongezea tena maili nyingine 200, kisha tutakuwa na Ukanda wa Bahari wa maili 400. Kwa hiyo, *potential* ni kubwa sana kwa ajili ya suala hili la uvuvi. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali kwamba; ni lazima tujizatiti na kujipanga vizuri ili kuhakikisha kwamba, tunaweza kuinua uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nikiangalia pia suala lingine ambalo ni muhimu kwa nchi yetu, kama nilivyosema suala linalohusu samaki; Maziwa, Mito, Bahari na kadhalika, nalo ni la ufugaji wa samaki. Thailand wanapata zaidi ya dola bilioni tatu kwa ajili ya ufugaji wa samaki peke yake katika Mito na Maziwa. Kwa hiyo, tuna changamoto kubwa kama Taifa, kuhakikisha kwamba, tunafanikiwa katika suala hili. Matumaini yangu ni kwamba, kwa mipango iliyopo, ninadhani Serikali itahakikisha kwamba, tunasonga mbele ili kuiinua Sekta hii. Tufanye kazi kwa bidii ili tuhakikishe kwamba, tunatekeleza hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala moja ambalo ninataka nilizungumzie nalo ni suala la *Deep Sea Fishing Authority*. Tunaipongeza Serikali kwa kuanzisha Mamlaka hii. Mamlaka hii ndiyo itakayosimamia Bahari Kuu na kuhakikisha kwamba, inatuletea uzalishaji wa kutosha. Kwa hiyo, ninachoomba ni kwamba, tudhibiti na kuhakikisha kwamba, meli zote zinapata leseni na tuhakikishe pia kwamba, tunajenga bandari ya uvuvi ili tuweze ku-*benefit* katika maeneo ya mahusiano na uvuvi, kwa sababu bandari ya uvuvi itatusaidia katika meli zitakazokuja pale, itatupa takwimu za samaki waliovuliwa katika maeneo yetu na tuta-*charge* ushuru. Kwa hiyo, dola milioni tatu za leseni ninaziona kama ni kidogo, tunaweza tukapata fedha nyingi zaidi kama tutaimarisha eneo hili la *Deep Sea Fishing Authority.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wananchi wa Pangani, ninapenda nichukue nafasi hii, niipongeze sana Serikali kwa Mradi wa *MACEMP. MACEMP* ni Mradi mmoja ambao umemwokoa mvuvi, umefanya kazi vizuri katika miaka mitano ya Mradi huu. Ninaelewa kwamba, sasa hivi mna-*negotiate* na *World Bank* ili muwe na Mradi mwingine wa *MACEMP.* Ninachosema ni kwamba, katika Mradi huu wa Pili, hakikisheni kwamba, sasa mnawafikia wale ambao mlishindwa kuwafikia wakati ule. Maeneo ya mikopo kwa wavuvi wadogo wadogo, vifaa vya uvuvi vya kisasa na kadhalika ni maeneo ambayo ninaamini kabisa kwamba, katika *MACEMP II* mtayatilia maanani na kuhakikisha kwamba, wavuvi wa nchi yetu wanafaidika na tunaondoka kwenye umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala moja ambalo ninataka niipongeze Wizara hii, nalo ni suala la wafugaji wadogowadogo. Kwa niaba ya Wananchi wa Pangani, ninapenda nichukue nafasi hii kuishukuru sana Wizara, kwa kuanzisha Kituo cha Maziwa katika Wilaya ya Pangani hasa kwa wafugaji wadogowadogo. Wananchi wa Pangani ni maskini, lakini kila mwezi wafugaji wadogowadogo wanapata zaidi ya shilingi milioni 130 kutokana na kuuza maziwa na ufugaji mdogomdogo. Hili ni suala zuri sana na ninapenda nichukue nafasi hii kuwapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ambalo ningependa kulizungumzia, ninaamini Mheshimiwa Waziri analifahamu, nimeshakutana naye mara nyingi, tumeshalijadili na ninaamini

kwamba, Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu; hili ni suala linalohusu Wafugaji wa Ng'ombe wa Maziwa wa Mkoa wa Tanga.

Tumezungumza na Mheshimiwa Waziri kuhusu eneo la Buhuri, tuhakikishe kwamba wafugaji wanapewa lile eneo ili waweze kuendelea kuzalisha mitamba. Kulikuwa na kesi Mahakamani imekwisha, ninaamini kwamba, Waziri atakapokuwa anatoa majumuisho, atawapa matumaini Wafugaji hawa wa Mkoa wa Tanga, ambao wanaendelea vizuri sana katika suala la ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa yako ni kwamba, Kiwanda cha *Tanga Fresh,* asilimia 40 ya hisa ni za wafugaji wadogowadogo. Ninaamini kwamba, Serikali yetu ni sikivu, suala hili Mheshimiwa Waziri analifahamu, ataweza kutoa hilo eneo la ekari 200 tu kwa nchi yetu, siyo eneo kubwa sana, wafugaji hawa waweze kuendelea kuweka mitamba ya kuzalisha maziwa ya kutosha ambapo kiwanda hiki kina mahitaji makubwa sana ya maziwa. Bado maziwa hayatoshi, kiwanda hiki mahitaji yake kwa siku ni lita 60,000, lakini yanayopatikana kwa Mkoa wa Tanga na Mikoa ya jirani ni lita 30,000 tu. Kwa hiyo, bado soko ni kubwa na bado kuna nafasi ya kuwasaidia Wananchi hawa ili kuhakikisha kwamba, wanaondokana na umaskini katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa ninamwita Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe.

**MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika Wizara hii.

Kwanza kabisa, kama ilivyo ada ni wajibu kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa yale yote anayotujaalia.

Pili, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa Hotuba yake aliyoiandaa pamoja na timu yake yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea na mchango wangu, ninapenda niongelee suala la samaki kutoka Japan. Kwa kweli mimi baada ya kusikia kwenye vyombo vya habari imenishtua sana, kama hawa samaki kweli inasemekana wamekwishafika hata hotelini, basi ina maana kuna watu wameshaanza kula na tunaelewa madhara ya Nyuklia yalivyo makubwa hasa katika mwili wa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachoiomba na kuitaka Serikali mpaka jioni ya leo, kama inawezekana wawe wameshatoa tamko linaloongelea ukweli kuhusiana na jambo hili na kwa sababu ninachangia suala la ufugaji na uvuvi, inanishangaza kwani hatujafikia mahali tuanze kuagiza samaki kutoka nje ya nchi kwa ajili ya chakula cha kila siku cha binadamu. Samaki tunao wengi wa kutosha, wavuvi wetu wanatakiwa kupata elimu ya kutosha ili kuweza kuzalisha samaki kwa kiasi kikubwa kabisa. Tuna maeneo makubwa sana yanayoweza kutoa samaki wengi na siyo kuagiza kutoka nje ya nchi, kwa sababu tunaelewa kabisa madhara yaliyoipata Japan na mpaka sasa hivi inasemekana na inaaminika kwamba, ile Nyuklia bado inaendelea kuvuja, ndiyo maana hata nchi zilizo jirani na Japan zimeweza kuchukua tahadhari si kwa vyakula tu bali kwa vitu vyote vinavyotoka Japan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niongelee suala la ufugaji. Suala la ufugaji ukianza kuliongelea haliwezi kuepukika na masuala ya ardhi, ina maana kwamba ni suala ambalo ni mtambuka. Tunapoongelea migogoro ya wafugaji, tunaongelea na migogoro ya ardhi ambayo ni lazima itamgusa mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri katika maelezo yake, alieleze kwamba, wataendelea kutoa elimu kwa wafugaji ili angalau waweze kuwa na ufugaji wenye tija, ambao unaweza kuleta maendeleo ya kifamilia na taifa kwa ujumla ili kuweza kuondokana na umaskini. Elimu hii Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba, inaweza kutolewa kwa

njia ya televisheni pamoja na redio. Ninapenda kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba, kwa mtindo huu, Wananchi waliopo Katavi ni vigumu sana kupata hiyo elimu kwa njia ya runinga ama kwa njia ya redio, kwa kuwa miundombinu inatakiwa iimarishwe kwa njia ya vyombo vya habari na mengineyo. Kwa hiyo basi, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, kama kuna njia mbadala ya kuwapa elimu Wananchi hasa waliopo vijijini, hili suala aliangalie kwa umakini. Pia aangalie ni namna gani Wananchi wa Vijijini wanaweza kupata habari sahihi hasa kuhusiana na ufugaji, waweze kufanya maamuzi sahihi kutokana na rasilimali walizonazo kujiletea maendeleo na kuongeza pato la familia na taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeisoma hii hotuba kwa mapana na nimesikitika kidogo, kwa sababu kuna eneo umesema kwamba, Serikali kupitia Wizara, itahimiza shughuli mbadala za kiuchumi kwa jamii za wavuvi ili kupunguza nguvu ya uvuvi kwenye maji ya asili na maeneo tengefu, kwa maana kwamba, shughuli mbadala kama ufugaji wa kuku, samaki na kadhalika. Nikiangalia hizi shughuli zote zimetengwa kwa Mikoa ya Pwani, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba, Rukwa na Katavi tuna neema ya maji; tuna Ziwa Tanganyika, Rukwa, Mto Ugala, Maporomoko ya Maji Mamba, Majimoto, Ugala na tuna maeneo chepechepe mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nilieleze hili kwa kirefu kwamba, Mkoa wetu wa Rukwa na Katavi wakulima ni asilimia 85, ina maana tukishavuna hatuna shughuli mbadala ya kufanya. Wanaofuga ng'ombe wanawauza kwenye magulio na kadhalika. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, kama Pwani na Mikoa mingineyo imeweza kutengewa maeneo kwa ajili ya kuchimba mabwawa ya kufugia samaki na kwa ajili ya kuanzisha vikundi na miradi ya ufugaji wa kuku, kwa ajili ya kuanzisha vikundi na kwa ajili ya miradi ya ufugaji wa mwani; ninamwomba Mheshimiwa Waziri akubaliane na mimi kwamba, katika huo mpango alionao, kuna vikundi kama 20 vya Pwani na vinginevyo; ninaomba arudi na kule Rukwa na Katavi hasa Mpanda, akawahakikishie Wananchi kwamba, wanaingia kwenye hivyo vikundi na wanaanza ufugaji wa samaki, kwani ufugaji wa samaki kule kwetu ndani ya miezi sita, mtu anaweza akaanza kuvua wale na akajipatia kipato, akaweza kupeleka watoto wake shule na kuendesha maisha yake bila wasiwasi huku akisubiri msimu ujao wa kilimo. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri, awahakikishie Wanakatavi kwamba, hilo utalifanya ili na wao wawe na shughuli mbadala baada ya kuvuna mazao yao waweze kushiriki katika shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nitakuwa mchoyo wa fadhila bila kumshukuru pamoja na kwamba, hajaainisha ufugaji wa samaki kwetu. Ninapenda kumshukuru mwanakijiji mmoja anaitwa Sunchila, anatoka katika Kijiji cha Katumba, Sumbawanga, amekuwa akitoa mchango mkubwa sana. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri amtumie huyu bwana ili aweze kutengeneza mabwawa ya samaki kule kwetu. Amekuwa akitoa mchango wa hali na mali kusaidia wajane katika maeneo ya Sumbawanga, kusaidia akina mama na wazee, ambao amewajengea mabwawa ya samaki na wanavuna samaki sasa hivi ninavyosema hata wewe ukienda kule leo utapata samaki watamu kabisa wa kula, ambao wanafugwa na akina mama pamoja na wazee na wajane.

Mheshimiwa Waziri ninaomba sana huyu mwanakijiji anayeitwa Sunchilam anapatikana katika Kijiji cha Katumba Sumbawanga, unaweza ukawasiliana naye na ukamsaidia nyenzo za kutendea kazi ambazo anaweza akawasaidia Wananchi walio wengi ambao ni maskini katika Mkoa wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia niongelee kuhusu suala la uvuvi na nyavu. Tumekuwa mara nyingi tukiwakamata wavuvi kwa sababu wanavua samaki wadogo kwa kutumia nyavu ndogo. Mimi ninaomba nimwulize Mheshimiwa Waziri kwamba; hizi nyavu zinaagizwa na nani au zinatengenezwa na nani kwa sababu tuna Sheria na kama hili suala limepitishwa kwamba watu wasingeneze nyavu ndogo lakini bado zinatengenezwa kwenye viwanda; matokeo yake yule mvuvi ataipata anakwenda kuitumia anavua samaki; akikamatwa wale samaki ananyang'anywa na havui samaki wengi labda beseni moja tu, lakini atanyang'anywa. Je, anaponyang'anywa wale samaki wanapelekwa wapi; na wanaotengeneza hivi nyavu ndogo wanachukuliwa hatua gani ili tuweze kunusuru mazalia ya samaki na tuweze kunusuru vifaranga wa Samaki na tuweze kupata samaki wengi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba pia Mheshimiwa Waziri anipatie ufafanuzi kuhusiana na suala la nyavu ndogo ambazo zimeonekana kwamba ni tatizo sana hasa kwa upande wa wavuvi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi ya kusema, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Ninaomba uketi kwanza, tuendelee. Ninaomba nimwite Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa na mimi fursa hii ya kuweza kuchangia Sekta hii adhimu ya Wizara ya Mifugo na Maendeleo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, sina budi kuipongeza Serikali. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa maelezo mazuri yaliyoandikwa na mipango mizuri ambayo imeandaliwa katika kitabu cha mwaka huu. Sitakuwa na maneno mengi, kwa sababu hii ni awamu ya kwanza ambayo tumeanzia tangu uchaguzi. Ninafahamu uzito wa Serikali kwa majukumu yaliyopita, lakini ninaamini bajeti ijayo ndiyo itakuwa nzuri zaidi katika mpango mzima wa kuisaidia Sekta hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji waliopita wengi wametoa maelezo mazuri sana. Maelezo mazuri kwa maana ya mkakati mzima wa maendeleo katika Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Mimi nitajikita zaidi kwa upande wa uvuvi kwa sababu mifugo ni jambo ambalo mnaliona, wenzetu wamelalamika, wengine wanaona tabu, lakini ninasema liko jambo moja kupitia bajeti ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine na sisi roho zinatuuma pale yanapotokea maafa kama yale yaliyotokea kwa ndugu zetu wafugaji wa ng'ombe. Kipindi cha ukame kilichopita, Serikali imeweza kutoa ruzuku kwa wafugaji kwa kuwapa ng'ombe, halafu mtu anakuja kukejeli kwamba, Serikali haijafanya jambo lolote! Hakika lazima tukae kiubinadamu na tuweze kuelewa. Hakuna jambo zuri na kwa kuwa wengi sisi ninaamini ndani ya Bunge hili ni wacha Mungu, kuna neno moja nitalitamka kwa Kiarabu lakini tafsiri yake kwa Kiswahili ni kwamba; malipo ya wema ni wema. Kwa hiyo, pale anapotokea mtu kuja kuchangia jambo ambalo limekutokeeni kwa maafa, basi yule amesaidia, mshukuruni japo kwa uchache ule ambao amejitahidi kuutoa. Mimi ninasema kwa hili, Serikali ninawapongezeni kwa kuwasaidia ndugu zetu kwa masaibu yaliyowapata ya ukame. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, ninataka nizungumzie suala la uvuvi. Kuhusiana na mipango mingi ya uvuvi, bado mpango mzima wa bajeti ya maendeleo ni shilingi 4,700,000,000 kwa nchi nzima; hebu nieleze Wizara hii itafanyaje kazi? Hakika ni danganya toto; pesa hakuna lakini utamlaumu nani; nimlaumu Waziri; nizuie shilingi; nimlaumu Naibu Waziri; Katibu Mkuu au Watendaji? Ninasema kwa kuwa bajeti hii ni ya kwanza, ninaunga mkono lakini bado Wizara ya Fedha iiangalie sana Sekta hii. Uvuvi siyo kitoweo, uvuvi ni uchumi wa nchi. Nchi nyingi sana mapato makubwa yanatokana na uvuvi na Serikali nyingi zinaendeshwa kwa uvuvi peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano; nchi ya Myanmar, uvuvi peke yake unachangia zaidi ya asilimia ishirini na moja ya pato la taifa. Pia katika Maldives uvuvi unachangia zaidi ya asilimia kumi na nane. Leo Tanzania uvuvi unachangia asilimia 1.4, hakika ni jambo la kusikitisha; bahari tunayo na wavuvi tunao, lakini nini kinachotusibu? Ninaona haya kurudia kusema tena kwamba, tatizo ni ndugu zetu watendaji. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri ajaribu sana kuangalia, hata kifikra ninaamini Sekta ya Mifugo imeboreka zaidi baada ya kuona kwamba, Mawaziri wote mmetokea kwenye asili ya mifugo. Sasa hakuna msemaji mzuri, hakuna msimamizi mzuri zaidi wa *field* siyo maandiko, anayeweza kujua athari na faida za bahari. (*Makofi*)

Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri aliangalie hili na yapo maelezo aliniambia, lakini aliseniambia nisiseme na mimi sisemi kwa heshima yake, lakini ninachosema ni kwamba, ninaomba sana hili mliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba, leo nimebanwa sana kwa sababu mengine nilikuwa nimeshazungumza katika kipindi cha asubuhi. Nilichokuwa ninataka kusema; ikiwa tumeweza kutoa maji kutoka Ziwa Victoria mpaka Kahama, ikiwa tumeweza kujenga Shule za Kata nchi nzima, ikiwa hata wenyeji wa Barabara ya Shekilango ile wameweza kuhakikisha kwamba hupiti nyumba bila kukuta baa, leo tunashindwa nini kuiendeleza Sekta hii na kuwasaidia wazawa wa nchi hii kwa kuwawezesha waweze kwenda kuvua katika maji ya kina kirefu ili tuweze kupata tija kwao na kwa Taifa? Ninaomba mnieleze ni nini ambacho kinatusibu sisi Watanzania, Wizara au Serikali kushindwa kuwasaidia wazawa kwenda kuvua katika Bahari Kuu? Tutakuwa tunagombana kila siku na wavuvi wadogo wadogo, wengi wamezungumza, Mheshimiwa pale amezungumza kutokea Rukwa kwamba, kazi yetu ni kuchoma nyavu. Wakati mwingine kweli zinatuchanganya kwa sababu uharamu wa nyavu hata mimi ninalalamika, lakini ninajiuliza uharamu wa nyavu ni nyavu yenyewe au matumizi yake ndiyo yanakuwa haramu? Sasa hapo napo pia mjaribu kutuweka sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, wavuvi wadogo wadogo wa Ukanda mzima wa Pwani, Mradi huu wa *MACEMP II* umetusaidia. Ninaomba niipongeze sana *MACEMP* kwa kuweza kutusaidia sisi wa Ukanda wa Pwani, ingawa ilikwenda sana katika Wilaya tatu; Mafia, Kilwa na Rufiji; ninaomba sasa hivi katika Programu nzima za Wilaya zote 16 kama mlivyoandika, muwasaidie wavuvi hawa kwa sababu mazingira ya wavuvi nchi nzima yako sawa, yanafanana kwa wavuvi wa Pwani, wa Maziwani, wa Mabwawani na hata katika Mito. Ninaomba sana tuangalie wavuvi hawa waweze kupata tija katika shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale unapotengeneza mbadala basi mpe mvuvi mbadala wa kuweza kumzuia asiende kuvua. Ukimpa mvuvi mizinga ya nyuki, hebu niambie nyuki hao watatoa asali ile kwa miezi mingapi mpaka ijae chupa aende kuuza na aache uvuvi ambao anaufanya kila siku, asubiri ile chupa mpaka ijae na aifikishe sokoni aweze kuiuza iweze kumsomesha mtoto wake au kumwendeshea maisha yake? Kwa hiyo, ninaomba vitu mbadala mkivifanya hakikisheni kwamba ni vile ambavyo ni vya kuridhisha, lakini siyo hivi vidogo vidogo ambavyo vinamfanya mvuvi baadaye aache na kurejea tena baharini na kuendelea na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaomba kuishauri Serikali kupitia Mradi huu wa *MACEMP* na ninawatakieni kila la kheri, Mungu awajalie muweze kupata *MACEMP II* ili Watanzania tuweze kufaidika. Hebu jaribuni safari hii kuwawezesha Watanzania kwani ni aibu leo kuona Tanzania tunaagiza samaki kutoka nje, kweli! Hili jambo ni aibu kwa sababu samaki tunao na wavuvi tunao. Ninaomba mkae mliangalie hili. Hili ni jambo la kushangaza hata kama mnatoa vibali na kwa nini mnafanya hivyo?

Mimi niliongea na Meneja wa Kampuni iliyoleta samaki kwa sababu kiwanda chake kipo Mafia, nikamwuliza hivi kwa nini wewe unaagiza samaki? Akasema kwamba, tatizo *licence* yetu ya kuvua na kuuza samaki nje imezuiwa. Aah! Nikamwambia mbona *licences* ziliruhusiwa? Mheshimiwa Waziri sasa hapa ninaomba ujaribu kuliweka sawa ili jamii iweze kufahamu. Masuala ya Nyuklia wenzangu wameshayaeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri; katika Wilaya ya Mafia kweli uharibifu wa mazingira ulikuwepo, lakini kuna baadhi ya watu walikubali kwenda kusalimisha nyavu zao wenyewe. Ninaomba sana, kwa heshimima zote, ninamwombea Mzee Haji Hassan kutoka Kijiji cha Jojo, yeye alikuwa na nyavu akazirejesha mwenyewe pale Wilayani, akasema ninakiri matatizo ninazirejesha hizi nyavu kabla sijakwenda kuharibu, lakini ninaomba basi mnirejeshee zile nyingine au nipeni zile za kuweza kunisaidia katika maisha yangu. Hakika mpaka leo, yule mzee bado hajakabidhiwa nyavu hizo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, ninaomba tumwonee huruma mzee huyu aweze kufaidika na wale ambao wataamua kusalimisha wenyewe nyavu zao, ambazo zinaharibu mazingira, basi tuangalie uwezekano wa kuwabadilishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sina mengi, nimebanwa sana kwa sababu mengi nilikwishayazungumza asubuhi na Mheshimiwa Waziri ameyasikia; ninaamini yale ambayo yametolewa kama ushauri na wenzangu kwa niaba ya Wavuvi wote nchini, kama Mwenyekiti wa Wavuvi wa Bunge, ninasema tunaomba sana muwaangalie Wavuvi wa hali ya chini, muweze kuwasaidia na kuwapa nyavu ambazo zitaweza kusaidia zisiharibu mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamtaarifu Mheshimiwa Waziri kwamba, bomu bado linaendelea. Bomu linatoka Dar es Salaam na linapigwa Dar es Salaam. Ninaomba hili mliangalie sana katika boti zinazotoka Dar es Salaam, sasa hivi hata sisi Mafia kupitia Kitengo chetu cha Hifadhi ya Bahari na Halmashauri yetu, tutahakikisha tunalinda Hifadhi yetu ya Bahari na pia maeneo yetu yanayotuzunguka katika Bahari ya Mafia, Rufiji, Mkuranga, Kilwa na mengine ili yasizidi kuathiriwa na uharibifu mkubwa wa mazingira uliopo katika bahari yetu, kwa sababu tegemeo letu ni hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ninarejea tena kumwomba Mheshimiwa Waziri atuwezeshe Watanzania kupata zana za kutuwezesha kuvua katika maji makuu. Leseni hizi tulizopata kwa meli 77 zilizokuwa zimetolewa pesa ni ndogo kulingana na uchumi wanaoondoka nao, kwa sababu ninaamini siyo wakweli na wanaweza kutoa taarifa sahihi. Nilikuwa ninataka kushauri jambo moja kwamba, kile kituo kilichokuwa pale *TAFICO* ambacho safari hii mmesema kitakuwa kituo cha doria, ninaomba sana ikiwezekana pale ilipokuwa *TAFICO* basi ndiyo kiwe kituo cha kuletea samaki kwa hizo meli ambazo zimepata *licences* ili tuweze kujua ni tani ngapi walizovua na tuweze kujua kipato kama ushuru tutapata kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi, wakati umekuwa mzito, ninaunga mkono hoja hii na kuwatakia kila la kheri timu nzima ya Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Ninaamini kwamba, Mradi wa *MACEMP* utakuja kutukomboa Ukanda wa Pwani, lakini pia angalieni katika Maziwa yote matatu na ninaomba sana muwatafutie Miradi ya pesa ili iweze kwenda kuwasaidia wavuvi katika Maziwa ya Victoria, Tanganyika, Nyasa na Maziwa madogo madogo pamoja na mabwawa yaliyoko nchini. Hali ya wavuvi siyo nzuri, lakini mkituwezesha tutaondokana na umaskini na Tanzania itapata tija kubwa kupitia kipato ambacho kitakusanywa kama ushuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninarudikia kusema kuwa, ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kwa vile muda uliobakia ni mchahe sana, sitaweza kumwita mchangiaji mwingine. Hata hivyo, ninapenda nitoe maelezo yafuatayo:-

Tulikuwa na hoja mbili hapa; hoja ambayo ilianzia kwa Mheshimiwa Tundu Lissu, ikaleta malumbano marefu sana na hata kuonesha picha mbaya kwa Wananchi ambao wametutuma tuje tujadili hoja ambazo zinaathiri ustawi wa maisha yao na kuzitafutia ufumbuzi kwa kuiagiza Serikali kama Wabunge, iangalie nini cha kufanya kwa ajili ya kuboresha ustawi wa maisha yao.

Waheshimiwa Wabunge, niseme kwamba, utaratibu tulionao sasa hivi hauleti heshima ya Bunge, unapoteza heshima na hadhi ya Bunge letu machoni mwa Wananchi wa nchi yetu. Ninaomba sana, tulipoanza tulipata semina elekezi ambazo hazipungui tatu mpaka nne, kwamba; tupitie Kanuni ambazo zinaongoza mambo yote yahusuyo Bunge. Ninaamini baada ya muda wote huu, kila mmoja amechukua juhudi ya kusoma Kanuni za Bunge. Ninawahimiza sana; kama huna uhakika ni bora umwulize mwenzio kuliko kuchukua uamuzi ambao mwisho wa siku wewe mwenyewe unakuvunjia heshima machoni pa Wananchi.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 67(1) – (2), inaagiza kwamba; na ninaomba niisome: “Spika anaweza kulihutubia Bunge wakati wowote na kwa ajili hiyo anaweza kumkatiza Mbunge yeyote anayezungumza.” Spika na sisi wafuasi wake; Naibu Spika, Mwenyekiti, nikisimama hapa kama Mbunge alikuwa anaongea au Waziri itabidi anyamaze kimya na aketi.

Fasili ndogo ya (2) inasema: “Endapo Spika atasimama wakati wa mjadala na kuanza kuzungumza, Mbunge yeyote ambaye atakuwa anazungumza wakati huo au ambaye atakuwa

amesimama mahali pake akisubiri kuanza kuzungumza, ataketi mahali pake na Bunge litabaki kimya ili Spika aweze kutoa maelekezo au taarifa yake." Ninadhani eneo hili tunalielewa vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, wakati nilipomhitaji Mheshimiwa Ezekia Wenje aketi, aliendelea kuzungumza, kukaidi Kiti na pia kushindwa kuitii Kanuni hii ya 67 kama nilivyoisoma. Mheshimiwa Ezekia Wenje, aliendelea kuzungumza kinyume cha Kanuni zetu. Pia Kanuni ya 59 na sehemu zake zote inasema hivi; ninaomba noisome:-

"Kwa idhini ya Spika, Mbunge yeyote anaweza kusimama na kuchangia Bungeni katika nyakati zifuatazo; kwa idhini ya Spika, nina- *underline;* ili uweze kuzungumza humu ndani ni lazima uwe umepata idhini ya Spika." Ninaomba msome sehemu ambazo zinafuatia na kisha mlinganishe, Mheshimiwa Ezekia Wenje, alikuwa ameruhusiwa kuongea humu ndani; sikuwa nimemruhusu! Kwa hiyo, ninaomba tuzingatie, maana kuna hoja hapa kwamba, tunaoketi hapa juu tuna *bias*.

Kanuni ya nane, ninaomba niisome pia inasema; "Uadilifu kwa Kiongozi wa Bunge, Spika na Wafuasi wake. Kwa kuzingatia matakwa na masharti yaliyowekwa na kiapo cha kazi zake na kwa madhumuni ya utoaji wa maamuzi na uendeshaji wa shughuli za Bunge kwa haki na bila ya upendeleo, Spika ataendesha shughuli za Bunge na kutoa maamuzi kwa haki, uadilifu na bila ya chuki, wala upendeleo wowote kwa kuongozwa na Katiba, Sheria za Nchi, Kanuni nyingine zilizopo, maamuzi ya Maspika wa Bunge waliotangulia na pia kwa kuzingatia uzoefu, pamoja na mila na desturi za Mabunge mengine yanayofuata utaratibu wa Kibunge unaofanana na unaofuatwa na Bunge la Tanzania."

Waheshimiwa Wabunge, ninawaomba muamini wanaoongoza vikao hivi. Kama Kanuni hii inavyoonesha, tunapaswa tuwatendee haki kwa uadilifu mkubwa sana bila kuwa na *bias* kwa mtu yeyote, kwa sababu kazi yetu hapa tukiwa *biased* tunaweza kuivuruga nchi. Kwa kuogopa hilo, tunajitahidi kwa msaada wa Mungu, tunasali sana Mungu atupe roho wake Mtakatifu. (*Makofi*)

Ninaomba pia niendelee kusema kwamba, kwa sababu Mheshimiwa Ezekia Wenje nilipomtaka atoke nje hakukaidi alitoka; kwa mamlaka niliyonayo, Kanuni inaniagiza asihudhurie siku nzima ya leo, lakini ninampunguzia adhabu hiyo, kwa hiyo, saa kumi na moja, ahudhurie Vikao vya Bunge. (*Makofi*)

Ninapenda pia nitoe maelezo yafuatayo: Wakati Mheshimiwa Ezekia Wenje, akihitaji kutoa maelezo aliyodai kuwa ni ya dharura na kwa mazingira yalivyokuwa na mlikuwa mnayaona pale isingekuwa rahisi kutofautisha hoja ambayo alitaka kuileta na hali halisi ilivyokuwa; hivyo, ninaomba pia tuangalie mazingira ambayo yalipelekea hata uamuzi ule ukafanyika kwa sababu hali halisi isingekuwa rahisi kutofautisha.

Baada ya kutoa maelezo haya na muda wa kusitisha shughuli za Bunge umekwishafika, ninaomba kusitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni. Ahsanteni. *(Makofi)*

*(Saa 07.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11. 00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na kikao chetu. Kama alivyokuwa ametoa taarifa Mheshimiwa Mwenyekiiti wa Bunge kwamba, msemaji wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Rita Mlaki, kwa hiyo, ninaomba nimpe nafasi Mheshimiwa Rita Mlaki.

**MHE. RITA L. MLAKI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hii, niweze kuchangia hoja ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Kwanza, ninachukua nafasi

hii kumpongeza Waziri na Wataalamu wake, kwa hotuba nzuri sana ambayo ina *data* za kutosha; hongera sana Mheshimiwa Waziri. Nitapenda kuongelea sana kuhusiana na ngozi ambayo ni zao la mifugo, ngozi za ng'ombe, mbuzi na kondoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ya Tanzania ni ya tatu katika *Sub Saharan Africa* kwa wingi wa mifugo. Kutokana na *data* ambazo nimezipata jana kwenye *internet,* inaonesha kwamba, tuna mifugo 20,000,000 ambayo ni nusu ya *population* ya nchi yetu, tunaweza tukagawana hawa wanyama watu wawili kila mmoja akapata mnyama mmoja. Hii ni mojawapo ya hazina ya nchi yetu na ni rasilimali kubwa sana, ambayo tungeweza kuifananisha na dhahabu, tungeweza kuifananisha na madini mbalimbali, tungeweza kufananisha mazao ya kilimo pamoja na utalii katika kuingiza fedha katika nchi yetu. Kwa maana hiyo, Wizara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu na ingepaswa kuchangia katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na *data* ambazo nimezipata kwenye *internet* na *website* yao, Sekta hii kwa sasa imeajiri watu 2,000; ina maana katika viwanda vilivyopo sasa hivi a ingeweza kuajiri zaidi ya watu 15,000 kama yafuatayo yangefanywa:-

Kabla sijaeleza au kutoa mawazo yangu, Hotuba haikutofautiana sana na *data* ambazo pia nimekuja nazo. Tuna uwezo wa kuzalisha vipande vya ngozi 2,800,000, hii ni ngozi ya ng'ombe tu. Kwa *data* zangu inaonesha pia za mbuzi 13,000,000 na kondoo 1,000,000 kwa mwaka na tungeweza kupata 150,000,000,000 kama Serikali ingesaidia katika Sekta hii ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa Serikali imeongea hapa katika bajeti, wameelezea wanavyohamasisha bidhaa hii ya ngozi iongezwe thamani, ina maana ngozi iwe *processed* kabla ya kupelekwa nje na ikaonesha kwamba, itasimamia ushuru wa bidhaa hizi ili kuhakikisha kwamba, malighafi nikiwa na maana ngozi ghafi haipelekwi nje kwa wingi. Ninaomba kusema kwa masikitiko makubwa sana na ninaongea hapa nikiwa na *data* kutoka *Tanzania Tanneries Association* pamoja na *LAT;* wanakosa malighafi ya kutumia katika viwanda vyao. Wastani wa asilimia 80 ya ngozi inayozalishwa hapa nchini inakwenda nje ikiwa ghafi kabla haijawa *processed.* Asilimia 20 tu ndiyo ambayo inabaki kuwa *processed. Data* za Waziri zinakaribiana na hizi, kwa hiyo, ninaamini haya ninayoyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni balaa; hii ni mali nyingi sana kwa nchi yetu na Serikali ingekuwa na uwezo kabisa wa kuhakikisha kwamba, tunafaidi kutokana na bidhaa hii kwa kuwasaidia hawa wenye viwanda waweze kuzalisha zaidi na tupeleke mali iliyoongezwa thamani na hiki ni kilio kikubwa cha wale wenye viwanda. Kwa wale wanaopeleka malighafi nje nikisema *raw hides and skin,* wanafurahia sana, lakini kwa wale wenye viwanda wanapata tabu sana. Tukumbuke kwamba, wao wamefanya *investment.* Tunazo *Tanneries* nane kama ilivyosemwa kwenye Hotuba na hizo zote kwa sasa nina uhakika, kwa sababu nimetembelea kadhaa kabla ya kuja Bungeni, zinafanya kazi katika *capacity* ya asilimia 50 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na *data* za *Tanzania Tanneries Association,* hivi viwanda vingeweza kuzalisha ngozi 1,500,000 za ngozi, lakini kwa sasa inazalisha theluthi moja tu ya hizo wanasema hawana malighafi ya kutosha. Mimi binafsi nimekwenda Morogoro juzi kwenye kiwanda kinachoitwa *East Hides,* nimekwenda pia *Himo Tanneries,* kote huko nimekwenda kutazama hali inavyoendelea kwa sababu ya *interest* ambayo nimekuwa nayo na zao hili. Wanasema wanapokwenda kufuatilia ngozi kule kwa wafugaji, wanamkuta mnunuzi anayeuza ghafi nje amekwenda pale ametoa fedha za ziada ili kuweza kama kum-*cut* ile *price* aweze kupeleka nje na wale wenye mifugo wanakubali wanampa yule ambaye anatoa pesa nyingi, kwa hiyo, viwanda vinakuwa havina malighafi. *East Hides Tanneries* au *Morogoro Tanneries* ya zamani, nimekuta mashine ziko pale hazifanyi kazi na alikuwa hana malighafi.

Ninamwomba Mheshimiwa Waziri alitazame hili ili tuone katika mapendekezo nitakayotoa tutafanyaje kuweza kudhibiti kupeleka malighafi ya ngozi nje na tuwasaidie hao wenye viwanda waweze kuzalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri sana katika hotuba kwamba, tulikusanya ngozi 2,500,000 kati ya hizo tukauza nje zile *raw* 1,700,000, ina maana ambazo zilikwenda viwandani ni 800,000 na zile ambazo tumepeleka nje bila kuwa *processed* tumepata shilingi 17,000,000,000. Fikiria tumepeleka tukapata shilingi 17,000,000,000 na nyingi kuliko zile ambazo tuli-*process,* zile ambazo tumefanyia *process* tukapata shilingi 16,000,000,000. Ina maana tunge-*process* tungepata zaidi. Serikali tunawaomba mchukue hatua za kuvilinda viwanda vyetu na hii ni kwa viwanda vyote vya ngozi vikiwemo *Himo Tanneries, East Hides, Moshi Tanneries, Afro Leather, Kibaha Tanneries, Salex* na *Petrocity* ambayo imeanza juzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi za wenzetu kama Uganda, Sudan, Zambia, Ethiopia na Nigeria, wamepiga marufuku kupeleka hizo ghafi nje ili viwanda vyao vipate malighafi na wanavilinda. Kama haiwezekani kupiga moja kwa moja marufuku basi tuongeze *levy.* Nina hakika mnafahamu kwamba, *Tanzania Tanneries Association* pamoja na *LART* waliomba waongezewe *levy* wale wanaopeleka malighafi ya ngozi nje mpaka asilimia 90. Maskini ya Mungu, wamekuja ninadhani walikuwa wamechelewa hawakuwa na mwakilishi wa kuwasaidia, walipofika huku wanaambiwa hiki, kwa hiyo, baadae kwenye Hotuba sioni mahali inapoongelea hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ofisa mmoja nimemwona kwenye *internet,* simfahamu, yuko Wizarani, sijui alikuwepo zamani au yupo sasa, anaitwa Nelson Kilongozi. Yeye amesema Serikali itaruhusu ngozi ghafi iendelee kuuzwa nje, kwani viwanda vya ndani havina uwezo wa kutosha. Kuna *surplus* ya *1.5 metric tones* na tusipouza nchi itanuka uvundo. Serikali haipaswi kusema hivyo kabisa, ambacho tungekifanya tungeongeza tuwasaidie viwanda ili waweze ku-*process*. Kuna kiwanda kipo pale Mwanza, ambacho hakifanyi kazi kwa zaidi ya miaka kadhaa, ninadhani itakuwa imefika 20 sasa.

Kile kiwanda kimekosa *treatment plant* ya ku-*treat* yale maji machafu; hiyo tu, ndiyo ilifanya kiwanda kifungwa mashine, nilipotembelea zilikuwa mpya kabisa. *UNIDO* wamefanya utafiti wakati nikiwa Serikalini na walikuwa tayari kutusaidia kutununulia mitambo ya ku-*treat* maji machafu yanayotoka katika viwanda vya ngozi wafuateni. *UNIDO* wapo tayari kabisa labda kama sasa hivi wamebadilisha mawazo, tuwaombe tena upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tujaribu kama tunashindwa kuweka hiyo ban sasa hivi, basi tu-*control* ushuru ambao wanapaswa kulipa. Sitaki kusema ushahidi nilionao, lakini kutokana na *data* za hao wahusika, wanasema kuna uwezekano kabisa, *container* linawekwa ngozi ghafi, mfano bola 20,000, 30,000 au 40,000 lakini wana *under declare* kwamba, ni dola 2,000 na Afisa wa Serikali anakubali linapita tunapoteza ushuru mkubwa sana. Tunaiomba Serikali izingatie hilo ili iweze kukusanya ushuru wetu ambao unapotea kutokana na hayo. Tungeomba basi kuna *government guarantee loans,* Serikali ijaribu kuwapatia wawekezaji zaidi wa hivi viwanda ili waweze ku-*process* ngozi yetu kuongeza thamani. Hilo nitaliomba sana na vilevile viwanda kama hiki cha *Himo Tanneries* wanahitaji msaada mkubwa sana wa Serikali.

Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri ulifika pale, kila kiwanda nikienda ninakuta Waziri ulishafika; wanakupongeza na wanakushukuru sana. Tunakuomba ujitahidi kuiomba Serikali wawasaidie viwanda vidogo vidogo kama hivi vya *Himo Tanneries,* ambavyo vinahitaji mashine mpya, vinahitaji mashine za ku-*process* ngozi zao kuwa ngozi ambayo inafaa kutengeneza viatu, mabegi na kadhalika ili waweze kuendelea. Ninaomba kabla sijamalizia, nizidi kusisitiza kwamba, tunaiomba sana Serikali waongeze huo ushuru ufike asilimia 90 na tunaomba vilevile Serikali iwasaidie mikopo viwanda hivi ili waweze kujiendeleza na tunaomba Serikali idhibiti ushuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa niongelee kuhusu bidhaa za ngozi. Ukilitazama hili begi hapa limetengenezwa *Himo Tanneries;* hii ni *Suede Leather* kwa mashine za zamani sana. Tunaomba muwasaidie hawa. Yupo kijana mdogo pale anaitwa Woiso, ametengeneza ngozi ziko pale na kiwanda ni kizuri, tunaomba msaada wa Serikali. Nitakuomba sana Mheshimiwa Waziri uende tena na kutazama jinsi unavyoweza kuwasaidia hawa watu. Vilevile wamsaidie *treatment plant* kwa kupitia *UNIDO* au Mashirika mengine ambayo yanajali mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru mnashirikiana na Wizara ya Viwanda na Masoko, tunaomba muwatafutie masoko. Kule China, Pakistani, India kuna masoko mengi sana ya ngozi, tutumie ngozi ambayo ni rasilimali ya nchi yetu kuuza nje tuweze kupata fedha. Tunalo Soko la *AGOA*, bidhaa zilizopitishwa za mwanzo zilikuwa za nguo na ngozi; tunaomba fursa hii tuitumie tena vizuri tupeleke ngozi; mabegi kama haya, mikanda, *wallet* zile wanatengeneza sana, nimeziona kule *Himo Tanneries.* Wanaomba mashine mpya ili waweze kufanyia *finishing* nzuri, waweze kuhakikisha kwamba, wanaweza kuzipeleka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali isaidie viwanda vyake, nchi zingine wangeweza kuamua kwamba, kuanzia sasa hivi viatu vinavyotengenezwa katika viwanda vyetu viboreshwe na viuzwe kwa wanafunzi wa shule za msingi na inawezekana kabisa kwa sababu tunafanya kila *effort* kujaribu kuvisaidia hivi viwanda ili viweze kutusaidia. Tutakuwa na soko kubwa hapa karibuni, ninadhani tuliliongelea kwenye bajeti kuu, ambalo litaanzia Cape Town mpaka Cairo. Tungeweza kuchukua hii Sekta ya Ngozi ambayo itatusaidia tukauza vitu, kwa sababu sisi ni wa tatu, labda Ethiopia ndiyo inatushinda. Jukumu la Serikali pamoja na mambo mengine ni kusaidia ku-*facilitate* mikopo, masoko na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninapenda ku-*declare interest* kwamba, ninahusika sana na mambo ya uvuvi. Ninaomba kuiuliza Serikali; ilifunga uvuvi wa kamba zaidi ya miaka mitatu iliyopita wakasema kamba wamekwisha; hivi bado hawajazaliana jamani? Sasa hivi kuna mwenzangu ameniambia hapa kwamba, kama kuna kitu kinazaa kuliko chochote ni samaki. Tunaomba kama kamba wamekwishazaliana mfungue, watu wamenunua meli zao zimekaa, zile *trawler* huwezi kuvulia kitu kingine, tungeomba mtusaidie ili tuweze kuhakikisha angalau imefunguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie kwa kulia kilio hicho na ninaomba niseme kwa hivi sasa …

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ni kengele ya pili.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Siungi mkono hoja mpaka nitakapopata ufunguzi wa zao la ngozi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na wachangiaji wanaofuata. Kabla hatujaendelea, ninaomba niseme yafuatayo: Kwa mujibu wa Kanuni ya 60, kifungu kidogo kinachojadili mwongozo wa majadiliano, kinaniruhusu kuangalia uwiano wa wachangiaji hapa ulivyo ili kuwaruhusu hata Wabunge wengine wenye taaluma katika hoja hiyo kuweza kuchangia.

Sasa kwa kadiri ya orodha yangu niliyonayo, kwanza, nitampa nafasi Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, halafu nitaendelea na Wabunge wengine wawili, atafuatiwa na Mheshimiwa Lekule Laizer, atafuatiwa na Mheshimiwa Rose Sukum, halafu nitaangalia kama muda wangu unatosha tunaweza kuongeza mchangiaji mmoja.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Kwanza, ni-*declare interest,* nilikuwa mvuvi na sasa hivi ni mkereketwa wa wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na swali tu kwa Waziri; ninakumbuka Mheshimiwa Waziri Magufuli alituambia kwamba, aliingia Mkataba na *Japanese Tunner Corporation Association* wa kwamba wao wangeweza kuleta meli 30 na watatulipa dola 200,000,000 kila mwaka na Mkataba huu ulikuwa umesainiwa na wao walikuwa walete meli 30 hapa nchini. Ninataka kujua huo Mkataba una-*stand* vipi katika uvuvi wa Bahari Kuu? Ninajua kuna asilimia 40 ya mgawano baina ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Zanzibar katika hapo na watu wale watafaidika. Kama unavyofahamu, *Deep Sea* sehemu kubwa sana iko kwenye Jimbo langu la Wawi. Kwa hiyo, ninataka ufafanuzi wa hilo na kwamba huu Mkataba upo na umesainiwa na utekelezaji wake ukoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitaka tu ni-*caution* kidogo kwamba, Wajapani wamekubali kutoa shilingi 200,000,000 kwa mwaka na wanaleta vyombo 30. Sasa ukifanya mahesabu ya haraka haraka, ukichukua na zile *overhead costs* za kuzalisha samaki, chombo kimoja lazima kizalishe si chini ya dola 1,700,000 ili waweze kulipa hizo pesa na wao wapate na faida. Sasa lazima *over-fishing* itatokea tu ili waweze kufanikiwa hilo. Je, Serikali imejipanga vipi katika Mkataba huo ili kuhakikisha kwamba meli hizo hazivui ziada kiasi ya kwamba wanatuharibia mazao yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuhusu suala zima la kuendeleza uvuvi. Nimeona katika Hotuba ya Waziri na nilikuwa ninafuatilia katika majarida mbalimbali na hasa ya *FAO* kwamba, tunazo *prawns* nyingi; Ruvuma kule kwa Mwenyekiti ziko 1,192, Iringa 3,137, Mbeya 1,186 na Kilimanjaro 1,660. Sasa ukichukua wastani wa uzalishaji wa tani saba ambao wenzetu wanazalisha mpaka 30 kwa paundi moja, tungeweza kupunguza hili tatizo la samaki. Sina hakika kama *prawns* zinafanya kazi hivi sasa. Tunataka Waziri atusaidie kutuambia je; hizi *prawns* zipo tu kitakwimu lakini hazipo katika uhalisi au vipi? Pia atusaidie hapa angalau tuondoke tulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni suala la uvunaji au upandaji wa kamba. Katika eneo ambalo tungeweza kupata mapato ya haraka sana na kwa muda mfupi sana ni upandaji wa kamba na hasa katika mashamba haya ya mpunga na kadhalika. Wenzetu wa Bangladesh wanafanya hivyo, Indonesia, Malaysia, lakini Tanzania tumekuwa tukitoa hadithi kila siku juu ya jambo hili na hatujafika pahali pazuri. Nilitaka Waziri vilevile atusaidie kutueleza ni hatua gani hasa zinazochukuliwa katika suala zima la *fish farming* kwa ujumla?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikielezee kitu kingine ambacho ningependa sana tubadilike; ukichukua takwimu za Waziri alizotupatia sasa hivi hapa; Zao la Dagaa Kavu limeingiza shilingi milioni 600. Ukichukua mazao mengine yote ya baharini, jumla ni shilingi bilioni tano, lakini *component* ya dagaa peke yake imechukua *portion* kubwa sana. Kama kungekuwa na *concentration,* kama kungekuwa na mpango mzuri ukafanywa kwa sababu dagaa wanapatikana kwa wingi, lakini hakuna matunzo mazuri. Kwanza, watu wangepata chakula, tungepata bidhaa ya kutengenezea chakula cha mifugo, *at the same time* tungeweza ku-*earn a lot of foreign exchange*, lakini halijashughulikiwa, watu wanajifanyia kienyeji tu. Wenzetu wameweza kupata *revenue* hiyo iliyopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni kwamba, inasikitisha Serikali inatoza ada kwenye leseni ya chombo, lakini vilevile inamtoza leseni mvuvi. Mimi sijawahi kuona abiria anakatiwa leseni. Gari linakatiwa leseni lakini wale wanaofanya kazi ukiacha dereva anakuwa na leseni, lakini wafanyakazi wa kawaida hawatozwi leseni. Sasa hapa kumekuwa na kodi ambayo mimi ninafikiri siyo sahihi kwa wavuvi wadogo wadogo hata kidogo, wakati unaona wale wavuvi wakubwa hawatozwi leseni ya aina yoyote, hawa wanatozwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne, ninakwenda kwa haraka; Mheshimiwa Waziri anasema, kuna meli kama 77 za kigeni. Kwa taarifa ya *FAO* kuna meli kama 200 na hizi *technique* za *fishing* ziko kama 51. Wengine wanatumia hizo *pool and line* na wengine hizo *long line and so forth.* Sasa ukitumia hizo *long line* wanazotumia ambazo zinakwenda kama kilomita tatu, wanakokoa mazalia ya samaki yote. Ninafikiri Serikali ifikie mahali, katika wavuvi tulionao kama 175,000 hivi sasa, ambao ni *traditionalist,* hawawezi kubadilika; tuwachukue vijana wetu wanaomaliza Vyuo Vikuu ambao wamesomea uvuvi na ufugaji, tuwaanzishie Miradi ya kuweza kubadilika kutoka uvuvi tulionao kuwaingiza katika uvuvi wa kisasa. Bila ya hiyo, mvuvi na mfugaji hawezi kubadilika. Lazima umchukue mtoto wa mfugaji aliyepata elimu, umchukue mtoto wa mvuvi aliyepata elimu, umfundishe *techniques* mpya za uvuvi ambazo zitaweza kutunza rasilimali zetu, ambazo zitaweza kutupatia mapato zaidi na ambazo zitawezesha hata bidhaa zetu zinazotokana na mazao ya mifugo na uvuvi basi zinatunzwe vizuri. Bila ya hiyo, hakutatokea mabadiliko yoyote. Ndiyo maana ukaona Kenya uvuvi unachangia asilimia 12 ya *GDP,* lakini wamekuwa na hekta 330,000 kwa muda wa miaka kumi ya malisho. Sisi wafugaji wetu hawa wanahangaika tu, hakuna mahali maalum wanapojua hapa pameandaliwa kwa ajili ya malisho yao. Ardhi tunayo kubwa; inashindikana nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni kwamba, hatujaandaa vijana walioelimika, tukawaambia ninyi tunataka mtuanzishie ufugaji wa kisasa na uvuvi wa kisasa. Hawa tuwapatie nyenzo na fedha, hizi fedha za *MACEMP* zingeelekezwa huko tungeona mabadiliko hivi sasa. Fedha hii kwa taarifa yako ni nyingi, inamalizikia kwa *administration* kununua pikipiki, kufanya *workshop*, fanya nini, lakini hazimfikii mtu wa kawaida.

Nitakupa mfano; boti moja inaweza kuvua tani 40 kwa kutumia *pool and line* kwa muda wa saa kumi na mbili na thamani yake ni dola laki nane. Ukizichukua dola milioni 61, wakichukua milioni kumi tu wakanunua zile boti wakapata utaalam wa kuvulia, leo tusingekuwa na tatizo la ku-*export* samaki wa aina mbalimbali, kwa sababu samaki hao hawaharibiki wala hawapati madhara yoyote kwa kutumia *pool and line*. Pesa hizi zinatumika ovyo na ninasema ovyo kwa sababu haziko *focused*, zinatawanywa kila pahala. Ukienda ukauliza katika Jimbo langu la Wawi leo nani alifaidika na *MACEMP* huwezi kukuta watu wawili, watatu. Sasa ninasema bado matumizi ya rasilimali hii siyo mazuri hata kidogo. Hizi fedha siyo ndogo, ninaomba Serikali iwatumie vijana wetu wanaomaliza Vyuo Vikuu ambao hawana ajira waweze kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilikwenda *VETA,* wanayo machinji ya ng'ombe ya ku-*process* nyama, wanapata mafunzo pale, lakini wakitoka pale wale vijana hawana kazi. Wamefundishwa namna ya kuchinja, ku-*pack,* ku-*export*, lakini wakitoka pale hawana kazi. Mimi nilifikiri Serikali ingetafuta dola laki tano wakawafungulia mahali pengine wakajiendeleza, leo tungepata soko la nyama na tungepata ngozi safi kabisa. Kwa utaratibu huu tunaokwenda nao sasa hivi, kwa kutegemea wavuvi hawa l75,000 wabadilike, hawatabdilika hata siku moja, kwa sababu kwanza tunatawanya elimu yetu kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ni suala zima la mapato yanayotokana na samaki. Nimewasikiliza Mheshimiwa Waziri, Msemaji wa Kamati na Kambi ya Upinzani; kama kuna *area* ambayo Mheshimiwa Waziri tunahitaji tuletee Sheria, ni kupiga marufuku haraka uvuvi haramu unaofanywa kwenye bahari kuu. Nimesema kuna meli 200 zinazovua kwa mujibu wa taarifa ya *FAO,* hizi meli zinachukua si chini ya tani mia tano au mia sita kwa meli moja. Hizi ni fedha nyingi sana wanazochukua. Sasa kwanza tupige marufuku, tuseme meli yoyote tutakayoikuta tutaifilisi; hakuna kesi, Sheria iwe *very clear.* Ukiikuta meli hakuna kesi ya kwenda Mahakamani wala kuulizana, umeingia kwenye *zone* yetu wewe tunakufilisi hadithi imekwisha. Wenzetu wanafanya hivyo; hiyo ni njia moja ya kuweza ku-*protect* hizi *area*. Nimeona hapa umeandika muda mrefu wa kwenda kulinda; vifaa vya kufanyia kazi hiyo viko wapi Mheshimiwa Waziri? Hakuna. Angalau ikitokea meli mbili, tatu, kufilisiwa mimi ninakwambia watu hawatakwenda. Kwa utaratibu huu tulionao pale, sisi Wawi kila siku tunashuhudia meli kubwa zinakuja kuvua zinachukua samaki zinaondokea. Mimi nilifikiri Mheshimiwa Waziri akifanya hivyo, ingeweza kusaidia haya mazao mengine yaweze kupata faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ni mazao haya mengine ya bahari, kwenye Ripoti sikuona *live fish* wanasafirishwa hapa nchini. Nilitegemea na hilo nalo ungelisoma kama ambavyo sikuona taarifa hata kidogo ya nyuki humu ndani, sijui kama hawako kwako au siku hizi wamehama? Hawako kwako bahati mbaya wako kwa Waziri wa Utalii. Kwa hiyo, nilifikiria kwamba, mngeangalia hayo maeneo mengine vilevile ambayo mngeweza kutupatia mapato haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. ROSE K. SUKUM**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia Hotuba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Kabla ya yote, sina budi ku-*declare interest* kwa kusema kwamba, mimi ni mfugaji.

La pili, pia mimi ni Mkurugenzi wa Bodi ya Mashirika yanayowasaidia wafugaji. Tatu, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji. Kwa hali hiyo, ninaomba kutambua uwepo na umuhimu wa wafugaji hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji pia hapa nchini wanastahili kutambuliwa, wanastahili kujulikana na pia ni Watanzania na Serikali hii ni ya kwao. Wafugaji wamekuwa wakidharauliwa

sana, wakikejeliwa, wakinyanyaswa, pia wakiporwa hata mali zao. Vilevile hawashirikishwi kwenye masuala ya maendeleo, nikimaanisha kwamba, huwa hatuwajali kuweza kuwapatia namna gani pato la nchi hii na wao washiriki. Nimelizungumza hivyo, kwa sababu linanigusa sana na ninapata uchungu kusema kwamba, wafugaji ni kama chumvi; chumvi haijawahi kusifiwa hata siku moja kusema chumvi ni tamu. Mwanadamu hali mboga bila chumvi, hali wali bila chumvi na hata viazi vitamu vinawekwa chumvi ndiyo vinakuwa vitamu zaidi. Sasa na sisi wafugaji huwa hawatambuliwi hata siku moja, lakini nyama mezani haikosekani, maziwa yanatafutwa kwa hali na mali hata kuagizwa nje ya nchi. Hata sisi humu ndani tunakula sana au tunakunywa maziwa ya Nido, lakini tunasahau maziwa ya Watanzania, ambayo ni mazuri zaidi yanatokana na ng'ombe wetu wa asili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashangaa kuona hatuwawezeshi wafugaji kwa kuwapatia ardhi, kwa sababu mgogoro wote unatokana na ardhi. Nimeona kwenye Hotuba ya Waziri ameainisha kwamba wataendeleza maeneo ya ufugaji endelevu na pia watayapima na ardhi hiyo, ninaomba kuwauliza pia nimeona kwenye jedwali mmepima hekari milioni mbili. Inafahamika wazi kwa taarifa ya awali kwamba, kuna hekari zaidi ya milioni sitini ambazo zinafaa kwa ajili ya ufugaji hapa Tanzania. Sasa kwa nini basi tusiwekeze kupima hiyo ardhi ili wafugaji wasihangaike na wasiteseke ndani ya nchi hii. Hili limesahaulika sana; nimeshindwa kuelewa tatizo liko wapi? Mawaziri hawa ni wapya hata kuwalaumu ninashindwa na wameteuliwa na Mheshimiwa Rais ili waweze kumshauri Rais watutetee. Bahati nzuri amewekwa Waziri kijana na Naibu Waziri naye pia ni mfugaji. Ukiangalia kwenye hii Hotuba, sijaona namna ya pekee ya kuwasaidia wafugaji wa asili ambao ni wengi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona wazi kabisa kwamba, sasa tuendelee kueleza kwamba, msaidieni Mheshimiwa Rais kwa kumshauri vizuri ili wafugaji wasihangaike. Migogo ya ardhi kati ya wafugaji na wakulima na wawekezaji pia iishe na kama lipo tatizo kwa Katibu Mkuu, basi Katibu Mkuu kama umeshindwa kuwashauri, kaa pembeni atusaidie sisi wafugaji wa asili tuweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ng'ombe au mifugo hiyo ina thamani kubwa sana kwetu. Kwanza, kiatu kizuri duniani ukikitaka ni cha ngozi na ngozi lazima itokane na mnyama na ni aghali. Begi zuri alilolionesha Mheshimiwa Mbunge aliyetangulia ni la ngozi na bei yake ni ghali, inapatikana na mnyama huyo huyo. *Jacket* zuri la ngozi linatokana na mnyama huyo huyo, kama siyo ngozi ya kondoo ni ya mbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nielezee kwa nini tunasahau hawa wafugaji, ndiyo maana ninasema mnapenda vitu vizuri kutokana na wafugaji kama vile chumvi inavyopendwa, lakini haisifiwi, ndicho hicho ninachokizungumzia. Maziwa yanahitajika kwenye meza zote ndani ya ofisi zetu, kwenye majumba yetu na tunajaribu kuboresha wanafunzi wote wapate maziwa tufanane na wenzetu, lakini sisi bado tumesahau. Nyama; tunaletewa karatasi hapa nani anahitaji nyama ambazo zinatoka Kongwa ajiorodheshe, kumbe nyama inahitajika. Sasa wafugaji tunawachukia nini na hawa ngombe wa asili tunawachukia kwa nini? Tanzania nzima hatutakula nyama ya *ranch* lazima twende kwa wafugaji wa asili ili tuweze kugawana kile kilichopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wafugaji wa Kilosa walinyanyaswa, Wafugaji wa Ihefu walinyanyaswa, Wafugaji wa Serengeti na Loliondo walinyanyaswa, Ngorongoro hata Karagwe. Wanakuja kutoka Burundi wanaingia kule Karagwe, wananyanyasika, lakini Serikali haijaribu kuangalia ni jinsi gani sasa tuwalipe hawa wafugaji. Ninaomba nielezee kwa kifupi, wafugaji waliokuwa Kilosa pamoja na mimi kwa sababu ng'ombe wangu 60 walichukuliwa na mpaka leo sijarudishiwa sijui wako wapi na kuna wenzangu pia; lakini kuna wengine walichukuliwa ng'ombe 143, Watumishi wa Serikali ya Halmashauri ya Kilosa wanakwenda kuswaga Dumila wasiwarudishie wale ng'ombe na yule baba amebaki maskini mpaka leo, watoto wake hawasomi, leo wake zake wanalia kila wakati. Kwa nini wafugaji tutiwe umaskini? Wakati ule wa oparesheni, ng'ombe mmoja akilala anatakiwa alipiwe shilingi 30,000 kwa siku moja. Mimi nina risiti hapa; amelala kwenye godoro gani; amefunikwa blanketi gani na ameoga na maji ya moto ya wapi; na amelala hoteli gani ya kitalii? Kwa nini tunyanyasike kiasi hicho? Mimi ninapenda kufahamu hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni matatizo makubwa na ni kero kubwa ambayo imeshindikana kwisha. Msiwaone wafugaji wamekuja hapa, wamekuja kusikiliza mnasema nini. Ninaomba kauli ya Serikali itoke na itamkwe wazi kwamba, ardhi ipimwe, wafugaji wapate ardhi yao hawatahangaika. Nina uhakika, hawatahangaika kwa sababu wao wamejua kujitegemea miaka yote.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MHE. ROSE K. SUKUM**: Ninajua umewahi sana, lakini hakuna neno nitaandika kwa maandishi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji hawa wanaweza kuleta pato la nchi hii kuliko madini. Hebu tuwatumie na sasa Serikali igeuke kuwatumia wafugaji kwa kuwapa ardhi na ipate mapato kutokana ng'ombe waliopo. Ng'ombe mmoja ukimwuliza ni laki tano kwenda juu, hakuna chini ya hapo labda ndama. Sasa je, Serikali ingekusanya kodi kiasi gani? Kwenye maandishi hapa wametuandikia kwamba, ng'ombe waliopo nchini ni milioni 21. Watanzania tuko milioni 43. Wakati ule ng'ombe na wanadamu tulikuwa sawa kwa idadi, milioni tisa tisa; hivi hawa ng'ombe walikufa au hawazai? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ng'ombe anazaa kila mwaka, walau sisi tunakula hata dawa za uzazi wa mpango kupunguza watoto. Kwa nini ng'ombe wawe wachache halafu wanadamu tuwe wengi? Ninasema siyo kweli na hesabu yenu siyo sahihi. Mimi kama mfugaji, nina ng'ombe Kibaigwa, sijaona Mtendaji aliyekuja kuhesabu ng'ombe kwenye boma langu; nina ng'ombe Dosidosi, sijaona Mtendaji aliyekuja kuhesabu ng'ombe wangu; nina ng'ombe Muguch Wilaya ya Hanang, sijaona Mtendaji akija kuhesabu ng'ombe wangu moja, mbili, tatu. Je, hii idadi mmeitoa wapi kama siyo ya kukisia mezani? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tuna ng'ombe wengi sana, hamtaki kutusaidia, wanatosha kuchinjwa na kuwa na viwanda vya kutosha na kuwasindika tuweze kupandisha pato la wafugaji na Serikali ipate mapato. Mimi ninaomba sasa Serikali ijikite mahali ambapo tunapenda sisi wafugaji tusikilizwe pia. (*Makofi*)

Kwanza, tujengewe viwanda vya kutosha kila Kanda za Wafugaji, halafu wafugaji ndiyo wabinafsishiwe kwa sababu wao ndiyo wana uchungu na hawa wanyama ili waweze kupata kipato. Msilete watu wengine kuja kubinafsishiwa. Tuambieni kwa nini Kiwanda cha Shinyanga kimekufa? Kwa nini Kiwanda cha Mbeya kimekufa? Kwa nini Kiwanda cha Arusha kimekufa? Kwa nini Kiwanda cha *Tanganyika Packers* mmekiuza; na kama mmekiuza kwa nini kisijengwe kiwanda cha nyama mahala pengine ili sisi tuweze kufaidi? Ukisindika nyama nina uhakika umeuza nyama kwenye kopo badala ya kuuza kwenye kilo inaoza. Ukisindika maziwa tayari umeuza maziwa ambayo hayaharibiki na tunaweza kuuza nje ya nchi. Tunaomba hiyo fursa wafugaji tupewe, tubinafsishiwe hayo mashamba, tubinafsishiwe ardhi na maeneo yote yenye viwanda, wafugaji wanaweza na vile viwanda vya ngozi virudi kwa Watanzania, hatutaki watu wa nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wana uwezo, wana akili na wana hela; hebu waambieni wafugaji wauze ng'ombe mmoja mmoja kama watashindwa. Kama ng'ombe mmoja ni laki tano na kuna zaidi ya milioni 40 kwa nini wasiweze? Kwa sababu hesabu iliyotolewa siyo sahihi kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie ujenzi wa malambo na majosho. Kweli tumepeleka madaraka kwa Wananchi kwa maana ya *D by D*, kwa maana ya kwamba, Halmashauri zetu ziweze kufanya; lakini naomba niseme hilo ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MHE. ROSE K. SUKUM**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nitaandika mengine kwa maandishi. (*Makofi*)

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja hii lakini niseme naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sistahili kuwa mkali leo katika bajeti hii kutokana na jambo zuri ambalo Serikali imetusaidia Wilaya ya Longido lakini Kamati ya Uongozi kwa kweli haijatutendea haki kutupangia siku moja. Wakulima wa korosho wamezungumzia korosho watu zaidi ya 10, pamba watu zaidi ya 10 lakini sisi wafugaji, ni wawili tu ndio watapata nafasi ya kuchangia mifugo, kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uongozi haijatendea wafugaji haki kuwapangia siku moja. Tulitaka nasi tungepangiwa siku mbili, tuchangie mifugo, tuchangie uvuvi. Mamilioni ya wananchi wanategemea uvuvi, mamilioni ya wananchi wanategemea mifugo, lakini hawana nafasi ya kuchangia kwa sababu mmetupa siku moja. Ni ajabu! Siku nyingine mkitupangia siku moja, wafugaji wote tutatoka, mbaki kuchangia wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali, namshukuru Rais, namshukuru Waziri Mkuu kwa kutupa shilingi bilioni 8.7 kwa ajili ya kuwapa wafugaji ambao mifugo yao ilikufa. Nawapongeza sana. Mimi tangu nikue sijawahi kuona umaskini mkubwa katika Jimbo langu kama ulioko sasa. Sijawahi kuona akinamama wakiokota kuni na kupeleka kwenda kuuza, sijawahi kuona akinamama wakichoma mkaa, sijawahi kuona akinamama wakizunguka kwenye mashine kuokota punje za mahindi na kufukuzana na kuku ili apate kibaba cha kwenda kuwapikia watoto, sijawahi kuona maishani mwangu, ndiyo sasa nimeona lakini, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeona na imesikia kilio chetu, ikatupa fedha kwa ajili ya kununua mifugo, nawashukuru sana. Wanafunzi wametoroka shuleni, wamehamia Kenya kwa ajili ya umaskini. Vijana mnaowaona katika Miji yote wanazunguka wamekwenda mpaka Mombasa kutokana na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya muda, kwa sababu kwanza hakuna wenzangu ambao watanifuatia kusemea wafugaji, ni mimi peke yangu na dada yangu pale aliyezungumza, namshukuru sana na nampongeza kwa hayo aliyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii inayoitwa ya mifugo, kila siku nasema kwamba hakuna Wizara ya Mifugo, ni kejeli tu. Kwa sababu, pesa za mabwawa hazipo katika Wizara hii, pesa za machinjio haziko katika Wizara hii, vibanio, majosho, birika za ng'ombe kunywea maji, haziko katika Wizara hii, kwa nini? Kwa nini ipelekwe katika Wizara nyingine? Jana imesomwa kwenye Wizara ya Kilimo, ndiyo ziko huko, angalieni kwenye kitabu, hotuba ya jana ndiyo ziko huko, kwa nini zitolewe huku? Wizara hii imebaki na sensa, imebaki na utafiti. Naomba bajeti nyingine, fedha zote za miradi ya mifugo zirudishwe katika Wizara hii, wataalam wanafanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni migogoro ya wafugaji na wakulima. Serikali ichukue uamuzi katika Mikoa ambayo ina vurugu za wafugaji na wakulima, itenge maeneo ya wafugaji, wakulima wasiende na wafugaji wasiende tena Vijiji vya wakulima, inawezekana! Wafugaji siyo kwamba wamezaliwa juzi hapa Tanzania, walikuwepo miaka ya nyuma lakini tatizo limekuja, juzi Serikali ilipoondoa kodi ya mifugo, wakulima wakachukia mifugo, wakasema waondoke kwa sababu hawana faida tena kwetu. Ndiyo sababu! Walipokuwa wakilipisha kodi ya mifugo, hakuna Halmashauri hata moja ambayo ilichukia mifugo. Wanataka waje tena wengi, sasa hawalipi kodi ndiyo maana wanafukuzwa, Serikali iangalie jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Wasukuma walioko Shinyanga, walioko Maswa wana mashamba na mifugo, kwa nini wasigombane? Wamasai walioko Kiteto na wakulima wako, kwa nini wasigombane? Kwa nini iwe hawa wa Morogoro? Kuna tatizo! Serikali iangalie tatizo hili! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tunahitaji ushirika wa wafugaji. Wafugaji Tanzania hatuna chombo cha kutusemea, hakuna chombo cha kutafuta masoko, hakuna chombo cha kutafuta dawa. Tunataka chombo chetu, tunataka chombo ambacho kitawakilisha matakwa ya wafugaji kwa Serikali na Serikali iwaite ikibidi kuja kukaa nao na kuzungumza mambo ya mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ranchi za Taifa, hizi Ranchi nyingi zilikuwa za wafugaji, nashangaa sasa wanatafuta wawekezaji. Mwekezaji ni nani? Mwekezaji ni mtu kutoka nje au mwekezaji tajiri? Ardhi aliyonyang'anywa mlalahoi, ndiyo anakuja kupewa tajiri au mwekezaji kutoka nje? Hao wawekezaji muangalie kwa sababu wamekuwa mzigo kwa wanyonge. Kwa hiyo, naomba hizo Ranchi, kwanza katika Wilaya yangu tumeanza kunenepesha mifugo, tuna vikundi vingi vya kunenepesha mifugo, Ranchi ya Kilimanjaro asipewe mwekezaji yoyote, wapewe wafugaji wanaozunguka katika eneo hilo, kwa sababu ilikuwa kwanza ni yao, tunashangaa mkimwita mwekezaji, sijui mwekezaji kutoka wapi kuja kumpa eneo letu huku tuna umaskini wa kutupwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji wa mifugo, sisi tuna Ranchi, tunahitaji kuwa na mbegu bora lakini, Ranchi zilizoko Tanzania hazitusaidii, hawana mbegu bora kwa sababu wanaachwa tu hivi, ni mbegu ambayo siyo bora tena. Tunakwenda Kenya kununua madume kwa shilingi milioni mbili, milioni tatu kwa dume moja. Ng'ombe walioko hapa Kongwa, hakuna mfugaji wa kwetu, wa Jimbo langu anayetaka madume ya hapa Kongwa ni wadogo sana. Wamekuja kuangalia, wamekataa, wamerudi kwenda kununua madume sehemu nyingine. Ni afadhali hata Kongwa waende Longido kununua madume kuja kuboresha mifugo yao. Kwa hiyo, tunataka Ranchi ziboreshwe, wananchi waweze kununua mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dawa za mifugo za ruzuku. Kuna dawa za ruzuku ambazo zinahitajika sana kwa wafugaji lakini katika dawa za ruzuku, dawa hizo haziwekwi. Kwa mfano, dawa ya *ECF* hailetwi, tunanunua, ndama mmoja ni shilingi 8,000/=, ng'ombe mkubwa ni shilingi 12,000/= kwa dozi. Kwa nini dawa hii isiwekwe kwenye dawa za ruzuku? Hizi dawa za *Foot and Mouth Disease*, ndizo ziwekwe kwenye ruzuku lakini hazipo. Naomba dawa hizi ziwekwe ili tuweze kupata dawa hizo kwa unafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri Mkuu, katika fedha za kununua mifugo, tunaomba tuchanganye na mbuzi kwa sababu mbuzi ni rahisi sana kukua na kuwa wengi na kumsaidia huyu mtu ambaye hana chochote kuliko ng'ombe ambaye atachukua muda mrefu. Kwa hiyo, tunaomba tuchanganye mbuzi na ng'ombe kuliko kununua ng'ombe peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni upimaji wa maeneo ya wafugaji. Mpaka sasa wafugaji wa Morogoro na Kilosa hawana maeneo waliyopimiwa ambayo unaweza ukawaambia kwamba mkae hapa kwa sababu hapa ndiyo eneo lenu. Vijiji vyao vimepelekwa tena kwa wakulima, malisho yao yamepewa wakulima, kwa nini vita isitokee? Hivi watakwenda wapi? Hivi wafugaji, kwa mfano kwangu Kiteto, Simanjiro, wakisema kwamba hii ardhi ni ya kwetu, wakulima waondoke, jamani si vita itatokea! Itatokea vita kubwa sana kwa sababu hakuna mkulima atakayeacha shamba lake, ni eneo lake na ana haki. Mfugaji aliyeko Kilosa ana haki kuishi pale, aliyeko popote, aliyeko Mpanda, ana haki kama mkulima. Naomba Serikali isibague, mkulima na mfugaji wote ni Watanzania na wapewe haki sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapito ya mifugo, wakulima wanakwenda kuweka mashamba kwenye mapito ya mifugo kwenda kwenye maji, hivi mifugo wataruka mashamba? Wana mabawa ya kuruka shamba? Wamekuja kuweka mashamba yao kwenye njia za mifugo, kwa nini vita isitokee? Naomba mgogoro huu wa wafugaji na wakulima, kuna wenzangu ambao wanataka kuifanya siasa, hii siyo siasa, tusiweke katika siasa, mkiweka katika siasa tutagombana, vita itatokea. Naomba na Mheshimiwa Waziri Mkuu alitambue hilo, nashukuru jana umekaa kimya! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, narudia kusema kwamba naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapa nitaruhusu msemaji mmoja wa mwisho aseme, halafu niwape ruhusa Mawaziri waweze kujibu.

Waheshimiwa Wabunge, lakini naomba nizungumzie suala moja kwa mujibu wa madaraka ya Kikanuni niliyonayo, na nikishatoa maelekezo hayo, nitaomba Serikali itusaidie kufanya hayo nitakayosema.

Waheshimiwa Wabunge, hapa asubuhi leo wakati Msemaji wa Kamati inayochambua bajeti hii alisema kwa uchungu sana kuhusu suala lililojitokeza siku hizi mbili/tatu zilizopita na kuripotiwa na magazeti linalohusu samaki walioingizwa kutoka Japan, wanaosemekana kuwa na chembechembe za nyuklia ndani yake ambao wanaweza kuwa wana hatari kubwa kwa maisha na afya ya Watanzania lakini suala hilo pia lilizungumzwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, lakini likazungumzwa na Wabunge waliochangia mjadala huu kwa kipindi cha asubuhi kwa hisia kali sana. Wakati Msemaji wa Kamati alipokuwa anasema aliiomba Serikali itoe ufafanuzi wa jambo hilo leo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba niseme kwa mujibu wa Kanuni ya 49, naomba wote tukubaliane jambo hii ni nyeti na ni zito na linatakiwa kwa kweli litolewe maelekezo ya kina na Serikali. Naomba Waziri atakapokuwa anaeleza kwa kuwa anabanwa kwa mujibu wa Kanuni, atalizungumza kwa namna yake lakini, ningeiomba Serikali kwa mujibu wa Kanuni ya 49, isimame mbele ya Bunge hili kesho na itoe Kauli za Mawaziri kutoa ufafanuzi angalau wa kueleza kwa kina yale yaliyokwishakufanyika na yale ambayo yanaweza kutoa ufafanuzi wa kutosha kuhusiana na sakata hili ili wote kwa pamoja na Watanzania wote tupate kuelewa lililojiri. Hii itatusaidia sasa kuona ni namna gani Serikali imelishughulikia suala hili kwa kina na kuona namna gani tutafanya kama Watanzania ili kuokoa jambo hili na kuliweka wazi kwa manufaa ya Watanzania wote.

Kwa hiyo, baada ya kusema haya, simfungi Mheshimiwa Waziri kulijibu kwa kuwa tayari Waheshimiwa Wabunge walishauliza, lakini tungependa Serikali ipate muda wa kutosha iweze kusoma na kugawa nakala kwa mujibu wa Kanuni, Wabunge wote watapata nakala ya maelezo hayo kwa kina zaidi.

Baada ya kusema hayo, naomba nimwite msemaji wa mwisho Mheshimiwa Mwijage.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipatia nafasi nichangie bajeti hii muhimu ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Mimi ni mkulima, lakini mimi natoka katika sehemu ambako nusu ya Jimbo langu ni maji. Kwa niaba ya Wabunge wanaozunguka Ziwa Victoria ambao ni wavuvi na kwa niaba ya Wabunge ambao maeneo yao yanahusisha ufugaji, naomba nichukue fursa hii kuwazungumzia au kuwasilisha hoja zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvuvi wa Ziwa Victoria, natoa ushauri kwa Serikali yangu, ufanisi katika uvuvi umeanza kupungua. *Unit cost* ya kumpata samaki kwa kila kilo inapanda, samaki wanaovuliwa sehemu zile gharama zake zinapanda, kuna tatizo la uvuvi kupita kiasi *(overfishing)*. Tunaishauri Wizara hii na Serikali kwa sababu kiasi cha pesa iliyopangiwa Wizara hii, haiwezi kubeba mzigo huu. Tunawashauri, Ziwa Victoria liangaliwe, kuna hatari ya samaki kuisha katika Ziwa Victoria lakini wanapokwisha samaki, samaki waliochangia pesa nyingi, mapato makubwa ambayo tumeyaona kwenye hesabu, nimesimama hapa kuwalilia wazazi wangu, kuwalilia ndugu zangu ambao wao uvuvi ni sehemu ya asili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hesabu zinazozungumziwa hapa zinahusu wavuvi wakubwa, wavuvi wanaotumia *trolley* wanaosababisha *overfishing*, lakini hakuna kinachozungumziwa kwa wavuvi wa asili wa Vijiji vya Bumbile, Vijiji vya Maiaga, watu wa Kome na wale wajukuu zangu wa Musoma, havijazungumziwa. Hawa watu wameshuhudia samaki wakiondoka, wao wanabaki na umaskini. Naomba Serikali iwaangalie. Serikali iwaangalie kwa sababu siwezi kumtupia mzigo Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi nilivyoiona bajeti yake na kwa falsafa ile ya kasungura, haka umepewa kasungura kadogo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii, sisi baada ya kuona matatizo, baada ya kusakamwa na kuisha kwa samaki tumekwenda kwenye ufugaji wa samaki kwenye mabwawa. Hapa kwenye jukwaa yuko bwana Bushiri Hussein, mfugaji wa samaki kwenye mabwawa ambaye Serikali imempatia nafasi ya kwenda Vietnam ili akajue namna ya kufuga samaki, tuweze kuondokana na hii dhahama ya kula kwa macho. Unakula kwa macho wakati

wenzako wanapeleka minofu Ulaya. Unajua sisi watu wa Bukoba tunaamini kwamba samaki ndiye anayeongeza akili kichwani, tumeamua kwenda kwenye mabwawa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi, ufugaji wa samaki kwenye mabwawa una tija na nawashauri wenzangu muangalie sekta hiyo. Naiomba Serikali yangu iongeze pesa kusudi wananchi waweze kuandaa hiyo miundombinu ya ufugaji wa samaki kwenye mabwawa. Kuna mahitaji ya maabara, kuna mahitaji maalum ya Maafisa Ugani waliopata elimu maalum namna ya kufuga samaki. Samaki wanafugika mahali popote, kwenye Maziwa unafuga, kwenye Bahari unafuga, kwenye Mito unafuga. Taifa la Vietnam, asilimia 70 ya pato lake linatokana na samaki lakini sisi tuna mito, sisi tuna mabwawa, tunaangalia, mimi naiona sehemu ya ufugaji wa samaki ni njia nyingine ya kuweza kutuokoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye mifugo, mimi mifugo naianzia mbali. Kwangu, kuku ni mfugo na falsafa rahisi ya mfugo, nilimwona rafiki yangu mmoja wakati anapigana akihangaika kwamba kwa nini wananchi wanachangia shule; ukifuga kuku wanne wa kienyeji, ukawauza, unapata shilingi 20,000/=, unaweza kumpeleka mtoto wako shule ukamlipia karo. Hivi kweli Watanzania ni maskini wa kushindwa kufuga kuku wanne? Unaona uchungu wa kufuga kuku wanne kuchangia majengo ya shule? Tumefika hapo? Ndiko ninakouanzia ufugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo la malisho. Nimemwona mkulima mmoja wa malisho pale Chalinze. Tunaweza kuandaa malisho ya kisayansi tukaacha huu ugomvi wa wakulima na wafugaji, tukapunguza idadi ya mifugo. Msemaji mmoja akitetea wafugaji ametoa mfano wa wafugaji wa Burundi walionyanyaswa Karagwe, walinyanyaswa kule walikotoka, Rwanda, Kagame anazuia *overgrazing*. Sasa kama walifukuzwa Rwanda, iweje waje Karagwe? Nasema jambo hili kwa niaba ya Wabunge wa Mkoa wa Kagera na sisi hatukubali, hatuwezi kukubali! Malisho bora ndiyo falsafa ya Kagame, iweje Kagame awafukuze kwao waje kwetu Karagwe mseme tunawafukuza? Haiwekezani! Tusiwatetee hivyo, tusiwatetee watu bila hoja, ujue ni kwa nini walikuja Karagwe, walikuja Karagwe baada ya Kagame kuwaambia waondoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze maswahibu ambayo yananinyima usingizi, kuna jamaa mmoja yupo Masaka alikuwa anazungumza Kiingereza cha nchi ya huko akawa anasema *this MP has got a price tag on his face*, ananisema mimi eti mimi kwenye uso wangu kuna bei yangu mimi. Nawaambia ndugu zangu kuna mateso makubwa tunayopata Mkoani Kagera. Kuna maelefu ya ng'ombe wameingia Mkoani Kagera. Muulize Waziri wa Mambo ya Siri anajua. Mifugo maelfu kwa maelfu imeingia kwenye hifadhi, wanyama kama vile tembo wanatuvamia sisi sasa. Wanyama hawa wameingiliwa kwenye hifadhi yao wanatuingilia sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lilianza vipi, nimemueleza Waziri anayehusika, lakini na yeye limemzidi, hili jambo ni la Serikali nzima, nimemueleza mtu wa Mambo ya Ndani na nilikuwa namtania Mheshimiwa Nahodha, nikamwambia Waziri wa Ulinzi mimi ni rafiki yangu, nitakufanyia mpango, Kagera tunaomba Jeshi tukapambane na ule uvamizi wa wafugaji waliotoka Uganda, Rwanda na Congo. Wafugaji waliotuvamia sisi siyo hawa wa akina Mzee Laizer, Mzee Laizer ni Mzee wangu, tumevamiwa, tatizo lilitokana na maamuzi ya Serikali, wakati mashamba ya *NARCO* yalipogawiwa kutengeneza *block*, nazungumza mbele ya Mwenyezi Mungu kwamba zoezi lile halikuwa sahihi, halikuwa wazi, kuna watu walipewa maeneo hawawezi hata kupata ng'ombe mmoja. Kuna watu walipewa maeneo kwa mgongo wa watu kutoka Rwanda na Uganda, ndiyo hayo aliyosema Mzee Laizer kwamba inakuwaje mnagawa maeneo msiwape watu wa asili mnakwenda kumtafuta mtu kutoka nje kwa sababu ana pesa, kwa sababu ni mtu wa nje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanateseka, Rutoro watu wanalala nje, nyumba zinachomwa, wanawake wamebakwa, wamenituma niwasemee. Kuna Walimu wanapigwa risasi kule, kuna majengo ya shule matofali yanaharibiwa na wafugaji hao, ndiyo mnasimama kuwatetea? Siyo hao!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugawaji wa ranchi haukuzingatia mipaka ya asili, ugawaji wa ranchi haukuzingatia wenyeji wa asili, lakini zaidi ya hapo hata viongozi wa vijiji ambao wamekuwa wakijifanya madalali wakiagiza ng'ombe kutoka nchi za nje na kuja kuwasumbua,

napenda kukiri kwamba wapo watu wana ranchi, wana *blocks* wanaweza kufanya vizuri, ni Watanzania wenzetu. Kwanza mimi napenda sana nyama ya ng'ombe lakini mimi ninao ndugu zangu wana *blocks,* wenye ranchi, lakini huu udalali, wingi wa ng'ombe walioingia ukiongozwa na watu wenye dharau, wakija wanatutishia, mimi wanasema wataninunua, wakapeleleze wajue bei yangu. Nimewaambia sifanyi biashara ile siyo rahisi kuninunua, ningependa iwe kumbukumbu kwa nchi hii kwamba nimelizungumzia suala hili. Naishauri Serikali migogoro ya ranchi kwa Mkoa wa Kagera Serikali ikae upya na katika Tume zenu mnazounda muwaite Wabunge wa Kagera, bahati Mbaya Mheshimiwa Blandes hayupo, tumekaa vikao, kila siku vikao mara mbili, tunataka mtuite tuwape majawabu. Kuna misingi ya haki mliyokiuka mojawapo amenikumbusha Mzee wangu Laizer, utagawaje eneo maelfu kwa maelfu unawasahau watu wa palepale, watakusumbua tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini utampaje mtu hekta elfu mbili, hekta elfu mbili ni ekari karibu elfu nne, mtu mmoja anapewa anaweka ng'ombe watatu, wanafanya udalali kwa kutafuta ng'ombe mpaka Congo. Ngombe wanatoka Congo DRC wa Wanyamlenge, wanatoka Rwanda, wanatoka Uganda wanakuja hapa, wanatukana, ninazo video, wametukana hata kiongozi wa Nchi yangu. Katika Kijiji kimoja walibandua picha zangu zote na za Mwenyekiti Kikwete, watu hawa ni wabaya sana. Kwa hiyo, naiomba Serikali yangu itusaidie, tukae chini sisi Wabunge wa Kagera, tukae na wataalamu wa Serikali, mmeunda Tume nyingi, hizo Tume tukae tuzichambue, tutoe muafaka. Tunahitaji wafugaji na tunahitaji ufugaji wa kisasa. Tunahitaji malisho, malisho yapo, tutengeneze *way* watu wafuge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisikose shukrani, nishukuru mtindo wa kutoa ng'ombe kwa wakulima, kuna ng'ombe mnagawa inasaidia na naomba kuunga mkono hoja kwa sababu naona hii dozi niliyotoa ni lazima tupate majibu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuwasikiliza wachangiaji hao wote, kweli mchango wa jioni hii umekuwa moto. Sasa naomba niwape taarifa niliyopewa na Mawaziri, Naibu Waziri yeye atachangia mada hii kwa dakika ishirini na Waziri yeye atatumia dakika 55. Kwa hiyo, naomba nimwite Mheshimiwa Naibu Waziri.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika sekta ya mifugo. Mkoa wa Mara hususan Wilaya ya Bunda, Serengeti, Tarime na Musoma Vijijini, cha kusikitisha hamna mabwawa ya kutosha kunywesha mifugo hii ukizingatia mabadiliko ya hali ya hewa ya ukame hasa katika Wilaya ya Serengeti na Bunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majosho ya kuoshea mifugo (ng'ombe) ni michache sana na mengine yalishachakaa hatua ya kufikia Kata na hata Tarafa kukosa josho la kuoshea ng'ombe na ku-*treat* hawa mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai kwa Serikali iweke suala kama kipaumbele kwa kuhakikisha maeneo ya ufugaji yanapata josho za kisasa, mabwawa ya kuoshea mifugo ya kisasa yawepo na pia kuwepo na usambazaji wa dawa za mifugo kwa mujibu wa afya ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekti, katika kutia moyo na kuendeleza sekta hii ya mifugo, ni vema Serikali itoe mikopo kwa wafugaji ili waweze kufuga kisasa. Pia waweze kudhaminiwa kujihusisha na ufugaji wa kuku, bata, samaki, vitu ambayo vinaongeza kipato kwa wananchi na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kuhusiana na *security* kwa wafugaji kutokana na wavamizi na watu wenye nia mbaya ambao huiba mifugo hususan Wilaya ya Tarime na Serengeti kutoka nchi jirani. Hii inakatisha tamaa sana wafugaji wetu. Hivyo basi sina budi kuitaka Serikali ichukue hatua kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ili kukomesha uhalifu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa pili ni kuhusiana na taarifa za kuingizwa nchini samaki toka Japan, samaki zinazosadikika kuwa na sumu. Kwa kweli hii ni fedheha kwa Taifa. Taifa

ambalo linafanya jitihada za kuimarisha miundombinu ili iweze kurahisisha usafirishaji wa zao la samaki nje leo nchi hiyohiyo au Serikali hiyohiyo inatoa vibali vya *importation* ya *junk fish as if* sisi tuna-*scarcity* ya samaki. Mbaya zaidi samaki hao wanapatikana katika Ziwa Vicktoria na maziwa mengine. Hii ni aibu sana tena sana. Naomba kuungana na wenzangu kupata majumuisho yakijibu jambo hili la fedheha kwa Taifa letu.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Tanzania ni moja katika nchi ambazo zimejaliwa kuwa na ukanda mrefu wa Bahari lakini imejaliwa vilevile kuwa mshirika wa Maziwa makuu matatu yalimo katika Bara la Afrika zaidi ya hayo Tanzania ina Maziwa kadhaa pamoja na Mito ikiwemo Bahari ya Hindi. Ni dhahiri kwamba Maziwa, Mito na Bahari tuliyonayo Tanzania ni rasilimali na utajiri mkubwa tuliopewa Watanzania na Mungu kwani thamani na bidhaa nyingine za majini ni miongoni mwa maendeleo makubwa tuliyopewa Watanzania. Kwa Taifa la Tanzania sekta ya uvuvi pekee inaweza ikatoa pato kubwa kwa Taifa ilimradi sekta hii iweze kuendelezwa na Serikali kwa kuwapatia wavuvi wetu vifaa na zana za kisasa ili kuwaendeleza katika shughuli za uvuvi. Ukiacha samaki ambao tunao kwa wingi katika Maziwa, Mito na Bahari lakini kuna Matumbawe kwa wingi ambayo nayo ni vivutio na pia ni sehemu ya mazalio ya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya uvuvi kwa sasa haijapata msukumo wa kutosha ili wavuvi wetu waweze kuondokana na uvuvi wa kale na kujiingiza katika uvuvi wa kisasa wenye tija na uhifadhi wa mazingira. Uharibifu mkubwa wa kutumia mabomu na sumu na nyavu za uvuvi zisizokidhi viwango, ni miongoni mwa matukio yanayoendelea hadi sasa nchini. Sio tu kwamba mabomu na sumu yanafanya uharibifu mkubwa wa mazingira na kuhatarisha walaji wa samaki, lakini ni wazi kuwa uvuvi wa namna hii ukiendela baada ya miaka michache ijayo hatutakuwa tena na sekta ya uvuvi nchini kwetu. Ni wazi kwamba kama hakujafanywa juhudi za kutosha za kuwasaidia wananchi katika sekta ya uvuvi, sekta ya uvuvi itaendelea kuwa chini.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo (Mb) kwa uwasilishaji wake wa hoja hii. Pia napenda kumshurukuru Naibu Waziri na Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wao wote kwa kazi nzuri za kumsaidia Waziri katika utendaji wao wa kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi Bahari Kuu (*Deep Sea Fishing Authority – DSFA)*. Kutoka mwaka 2009 mpaka 2011, Wizara ilitoa leseni za uvuvi katika Bahari Kuu ambapo leseni 72 zilitolewa na jumla ya shilingi 3,339,354,000/= zilipatikana. Napenda kujua mgao ukoje kati ya pande mbili za Muungano, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepata shilingi ngapi na Tanzania Bara imepata shilingi ngapi kwa kipindi hicho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna malalamiko ya Wajenzi wa Ofisi ya Mamlaka inayojengwa Fumba, Zanzibar kuwa upande wa Bara kuna ucheleweshwaji wa malipo. Je, kwa nini linafanyika hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia 100.

**MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa njia ya maandishi nachangia bajeti ya Wizara hii ambayo kwa imani yangu, sekta hii ndiyo njia rahisi ya kupitia katika kuukimbia umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ni uvuvi na uendeshaji wa Ziwa Victoria. Naishauri Serikali iongeze nguvu ili kuhakikisha kuwa tunapata pato kutokana na samaki wanaovuliwa katika Ziwa Victoria. Wavuvi toka nchi jirani wanavua upande wa Tanzania na kupeleka mavuno sehemu za upande wa kwao Uganda na Kenya. Aidha nchi tatu zinazohusika na Ziwa hili zinapaswa kukaa pamoja na kutafuta suluhu ya uvuvi kupita kiasi *(over fishing).* Lipo tatizo la wavuvi haramu ambalo tunalipa nguvu sana lakini uvuvi kupita kiasi una madhara. Gharama ya uvuvi kwa kilo inayopatikana inaongezeka kila kukicha, eneo hili liangaliwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na pendekezo hilo hapo juu ipo haja ya kuwaangalia kwa jicho la huruma wavuvi asili wa Ziwa Victoria. Wakati tukifurahia mapato

yatokanayo na uvuvi katika Ziwa hili, hali ya wavuvi asili imeendelea kuwa duni kila kukicha. Kada hii inapaswa kusaidiwa kama tunavyofanya kwa wachimbaji wadogowadogo. Jamii ya wavuvi katika Visiwa vya Ziwa Victoria wanaendelea kula kwa macho, ipo fursa ya jinsi ya kuwasaidia watu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni ufugaji wa samaki kwa kutumia Mabwawa au Mito, Maziwa na Bahari kwa kutumia "*cages*". Samaki ni dhahabu hai. Ufugaji wa samaki una faida iliyo wazi na kubwa zaidi kuliko biashara zilizo nyingi. Pendekezo langu ni kuwa Serikali iendelee kuhamasisha na kuwekeza katika sekta ya hii, kuwepo Maafisa Ugani, maabara, elimu ya ushirika wa mikopo nafuu ni mambo mahimu katika kuendeleza sekta hii. Sera madhubuti juu ya ufugaji wa samaki itasaidia juhudi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati naanza kuchangia nimeeleza kuwa sekta hii ndiyo njia rahisi ya kutumia kukimbia umaskini. Ada ya shule ya sekondari ni shilingi 20,000 kwa mwaka. Kuku wa kienyeji wanne kwa bei ya kijijini inatosha kulipa karo. Je, ni mtoto gani anayeweza kumudu masomo ya msingi na ashindwe kufuga kuku 16 kwa miaka minne, au mbuzi wanne kwa kipindi hicho? Napendekeza jitihada ziongezwe katika kuhamasisha ufugaji wa Kuku, Bata, Mbuzi, Kondoo na Ng'ombe. Ufugaji huu sasa uelekezwe katika ufugaji wa kisasa unaotumia eneo dogo na kuleta ufanisi mkubwa. Kutokana na faida niliyoainisha katika sekta hii, vyombo vya fedha na Idara za Ushirika zisaidie sekta hii ili ikue na kuleta maendeleo kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na uendelezaji wa ufugaji wa Mbuzi, Ng'ombe na Kondoo ipo haja ya kuendeleza Sera ya Malisho. Kuna faida nyingi tukiweza kuhamasisha kilimo cha malisho kwa ajili ya kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nielezee masikitiko yangu juu ya shughuli za mifugo Mkoani Kagera. Bahati mbaya mifugo Mkoani Kagera imeturudisha katika vita mara ya pili. Tofauti na mara ya kwanza tulipovamiwa na Nduli Amin, safari hii adha ya mifugo imetuletea uvamizi ambao Serikali inachelewa kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la mifugo Mkoani Kagera lina sehemu kuu mbili na katika mchango huu nitazungumzia Ranchi za *NARCO*. Bila kupepesa macho, makosa makubwa yalifanyika wakati wa kugawa Ranchi zilizokuwa chini ya *NARCO*. Kulikuwepo na mazingira ambayo mtu anayefikiria nchi hii na vizazi vijavyo angelipa zoezi hili jina ambalo mimi nashindwa kulitamka au hata kuliandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii na uongozi wa Wizara hii kwa namna yoyote haihusiki na dhambi hii. Hivyo sasa wakati umefika kufanya marekebisho. Tume zote zisitishwe, maandiko ya Tume zilizopita yawekwe mezani na watu wenye miwani ya busara yaziangalie na kutoa maamuzi. Kwa Kagera, sisi Wabunge wa Kagera tunadai kwa niaba ya wananchi wetu tuhusishwe katika kutafuta suluhu. Jambo lililo wazi ni kuwa si wakulima, wananchi wa kawaida na wale waliopewa *blocks* anayefaidi katika hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasoro katika ugawaji wa Ranchi za *NARCO* Mkoani Kagera ni kama ifuatavyo:-

1. Zoezi la ugawaji *block* halikuwa safi.

2. Waliopewa *blocks* walipewa maeneo makubwa sana kuliko uwezo wa kawaida, 2,000 – 3,000.

3. Waliopewa *blocks* wengine si raia wa Tanzania ni Wanyarwanda na Waganda.

4. Ugawaji ulizaa udalali ambapo waliopewa *blocks* wanazitumia kupangisha wafugaji haramu wa Rwanda na Uganda. Watu hawa hawana uwezo wa kuziendesha au kuziendeleza.

5. Baadhi ya waliopewa *blocks* wanazimiliki kwa niaba ya wageni kinyume cha taratibu za uwekezaji.

6. *NARCO* ilipoamua kwenda kwenye Nyalubanja haikuzingatia mahitaji ya ardhi kwa vijiji na wananchi wa Kagera bila kujali kuwa *NARCO* ni Shirika la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suluhisho la tatizo hili lipo na ni rahisi sana. Wataalam wa Wizara wakae na Wabunge wa Kagera tuwape maoni ya wadau.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo, Naibu Waziri, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo kwa utendaji wao mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze kuhusu ufugaji wa kuku. Wanawake wamehamasika na baadhi yao wameanza kufuga, lakini bado wengi wao wanalo tatizo la ukosefu wa miundombinu ya ufugaji, hawana pembejeo, hawana fedha kwa ajili ya kununulia dawa na hawana fedha kwa ajili ya kununulia mashine za kutotolea vifaranga. Naomba Serikali iwasaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya chakula cha kuku inapanda kila siku. Naomba Serikali iangalie suala hili ili iweze kufuatilia bei za vyakula zishuke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweze kutenga fedha kwa ajili ya kwenda kutoa elimu kwa wafugaji wa Kuku, Mbuzi na Ng'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo inayotolewa kwenye Halmashauri kuhusu ufugaji wa Kuku bado haijaweza kukidhi haja ya wananchi hasa wanawake na vijana, kwa sababu, sehemu kubwa wanachangia nguvu zao na kujenga mabanda ya kuku lakini hawapati pesa za kununulia mashine za kutotolea vifaranaga, tunaomba Serikali iangalie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wengi wanahangaika, hawana vifaa vya kisasa vya kuvulia samaki. Naomba Serikali iweze kuwasaidia sana kama vile wanavyokopeshwa wakulima pembejeo kwa kukopeshwa vocha za mbolea na wavuvi nao waweze kukopeshwa vifaa vya kuvulia samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maeneo haya, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. David Mathayo (Mb) – Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa hotuba nzuri ya kuvutia ambayo ameitoa asubuhi hii. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Ole-Nangoro kwa msaada mkubwa anaompa Waziri na hivyo kuleta ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukumbusha tu kwamba Wilaya ya Siha nayo ilipata maafa makubwa yaliyosababishwa na ukame na hivyo ng'ombe wengi na mbuzi na mifugo iliteketea. Tunaomba Serikali itusaidie mitamba na madume ili kurudisha mifugo mipya na kuinua kipato cha wananchi.

**MHE. UMMY A. MWALIMU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja.

Pili napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara, kwa hotuba nzuri yenye kuleta matumaini kwa wavuvi wakiwamo wa Wilaya za Tanga Mjini, Pangani, Muheza na Mkinga – Mkoani Tanga. Hata hivyo, napenda kutoa maoni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi ndio shughuli kuu ya kiuchumi ya wakazi wa Vijiji vya Mwambao/Bahari katika Wilaya Muheza, Mkinga, Pangani na Tanga Mjini. Uvuvi ndio maisha ya wakazi wa maeneo haya kwa sababu unawapatia ajira, kipato na lishe (chakula). Bahati mbaya,

sekta hii inakabiliwa na changamoto kubwa ambayo ni uvuvi haramu. Natambua jitihada mbalimbali za Wizara katika tatizo hili. Hata hivyo, bado kunahitajika kuwepo mikakati maalum ya kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara iwabane wanaohusika na kusambaza zana haramu za uvuvi. Wizara iwapatie wavuvi wadogowadogo mikopo yenye masharti nafuu ili waweze kununua zana bora za uvuvi. Miradi kama ya *MACEMP* yenye lengo la kuboresha maisha ya wananchi waishio maeneo ya Ukanda wa Pwani ihakikishe inawafikia wananchi wengi zaidi wakiwemo wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa Kiwanda cha Maziwa *(Tanga Fresh*) umesaidia kuboresha maisha ya wananchi (wafugaj) wengi katika Mkoa wa Tanga. Hata hivyo, kiwanda hiki kinakabiliwa na mgogoro wa ardhi (hekta 200) katika eneo la Buhuri. Kuna kurushiana mpira kati ya uongozi wa Wilaya/Mkoa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, hivyo kukiweka kiwanda katika hali ya wasiwasi. Wizara ifuatilie suala hili ili kukiwezesha kiwanda kuendelea na uwekezaji/uzalishaji wa maziwa kwa faida ya maendeleo ya wakazi wa Jiji la Tanga, Wilaya ya Pangani, Muheza na maeneo mengine ya Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza hotuba nzuri iliyosomwa mbele yetu na Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Naishukuru Wizara kwa kuweka mpango wa kukarabati Kituo cha Mafunzo Mabuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naiomba Wizara iweze kukarabati Taasisi ya Uzalishaji Mitamba Mabuki ili irudi katika hali yake ya zamani kabla ya uamuzi wa Serikali kuibinafsisha. Ukarabati uhusishe majengo ya ofisi, mabwawa ya kunyweshea mifugo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri yenye matumaini kwa wafugaji iwapo mipango kama ilivyo kwenye kitabu cha bajeti itatekelzwa kwa mwaka 2011/12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ni-*declare interest* kuwa mimi ni mdau wa ufugaji ninayejishughulisha na utotoaji wa vifaranga chotara, ufugaji wa kuku chotara wa nyama na mayai ya kuku na kwa ajili ya kutotoa vifaranga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji wa kuku una tija kubwa sana kama ukifanywa kwa kisasa na ufanisi. Ni mradi ambao akinamama wengi wanafanya ili kujikimu maisha yao. Kumekuwa na matatizo makubwa sana hasa katika kuboresha utotoaji wa kitaalam kutokana na ukosefu wa pembejeo kama vitotozi *(incubator*) ambapo kuna vitotozi vya kutumia mafuta ya taa ambavyo vinaweza kutumika hata Vijijini. Kwa kutumia vitotozi, kuku anaweza kutoa vifaranga mara nne ya kama atatumia hali ya kawaida ya kuku kulalia. Mitaji imekuwa adimu, utaalam kwa wafugaji wadogo hakuna, chakula kimekuwa kikipanda bei siku hadi siku hata baada ya Serikali kupunguza kodi ya virutubisho vinavyotumika katika kutengeneza chakula cha kuku. Naomba Serikali iyaangalie matatizo haya ili ufugaji wa kuku uwe na tija na kuweza kuchangia pato la wafugaji na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona hotuba na mpango umezumgumzia uvuvi na hasa uvuvi katika Bahari na Maziwa. Wizara ina mpango hafifu wa kuendeleza uvuvi wa mabwawa ambao unaweza kuleta tija zaidi na kutoa ajira kwa vijana wengi. Hata alipozungumzia ufugaji wa Mabwawa, wafugaji wa asili wa Tanga, Dar es Salaam, Mafia, Pwani, Kilwa haikutajwa ambapo kote huko kuna Pwani nzuri ambapo hata maji ya Bahari yanaweza kutumika kutengeneza Mabwawa. Siyo hiyo tu, bali samaki ambao wametajwa kuendelezwa ni Perege na Kambare lakini Mabwawa haya kwenye Ukanda wa Pwani wanaweza kufuga samaki wa maji chumvi na samaki aina ya Kamba na Kambakochi ambao wana soko zuri ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vijana wengi sana katika Miji na Vijiji vya ufukweni ambao kama wangesaidiwa kupewa mafunzo na miradi ya Mabwawa ingesaidia sana kutoa ajira kwa vijana. Vijana wengi katika fukwe mbalimbali katika Mwambao wa Pwani zetu toka Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Kilwa, Lindi na Mtwara wana ujuzi wa kuvua lakini wamebaki kuwa vibarua kwnye boti za matajiri. Umefika wakati Serikali iwasaidie kuwapatia vijana hawa mitaji hata kama kuwakopesha boti ili waweze kukuza uchumi wao. Hii siyo tu itawasaidia wao bali pia Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ufugaji wa ng'ombe, takwimu zinaonyesha Tanzania kuna ng'ombe, mbuzi na kondoo zaidi ya milioni 30, lakini ukiangalia hali ya mifugo na wafugaji wote wana hali mbaya. Mimi nimeshakula na kuona ng'ombe wa *NARCO,* wana mbegu nzuri, wenye ladha nzuri na wanafugwa kwa kutulia yaani eneo dogo lakini wana utaalam wa kunenepesha ng'ombe wao. Kwa nini basi utaalam huu usisambazwe kwa wafugaji wengine wadogowadogo? Hii itasaidia kuongeza tija ya mfugaji, kuzuia uharibifu wa mazingira, migogoro ya ardhi isiyokwisha na kuwapatia vijana wetu ajira. Tunaweza kufanya kama kwenye kilimo cha wakulima wadogowadogo wanaosaidiwa na wakulima wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA M. MLATA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza shukrani kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa taarifa/hotuba nzuri ya Wizara hii. Ni kweli Wizara hii imekuwa ikisahaulika sana hasa katika masuala ya fedha ukizingatia kuwa hapo awali ilikuwa ni sehemu tu katika Wizara zingine na hivyo kushindwa kupata fursa ya kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais wa Awamu hii ya Nne kwa kuliona na kuamua kuunda Wizara ya kushughulikia Mifugo na Uvuvi. Hivyo niwaombe tu, Waziri na timu yake yote kukaza buti na kuhakikisha sekta ya uvuvi na ufugaji vinaleta faida kwa Taifa, kwa wafugaji na wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Singida, tumejaliwa ufugaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe, kuku pia uvuvi lakini naona nguvu ya kuwainua wahusika imekuwa ndogo sana kwani hapo zamani nilishuhudia nikiwa mdogo majosho na Mabwana ya Mifugo wakiwa kazini kwenye maeneo husika. Pia walihakikisha wanasimamia ipasavyo suala la mabwawa ya kunyweshea mifugo, je, siku hizi wako wapi? Je, Waziri anaweza akanipa orodha au idadi ya majosho yaliyo hai katika Mkoa wa Singida? Je, kuna mabwawa mangapi yanayokidhi ufugaji Mkoani Singida? Nauliza hivyo kwa sababu naona Mkoa wetu umewekwa kando kana kwamba hatuna mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo linguine, suala la ufugaji wa kuku Serikali imesema itaendelea kuhamasisha uzalishaji wa mayai na matumizi ya teknolojia sahihi ya ufugaji wa kuku, lakini swali, unahamasishaje bila vitendea kazi? Bila soko, *funds* na kadhalika? Je, Wizara itakuwa tayari kuleta wataalam Mkoani Singida ili kutoa hayo mafunzo ya ufugaji sahihi wa kuku wa asili na pia kusaidia upatikanaji wa mikopo ya wafugaji hao watakaokuwa wameshapata mafunzo? Je, Serikali itakuwa tayari kusaidia upatikanaji wa soko la kuku na ikiwezekana kijengwe Kiwanda cha Soseji Singida?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni juu ya uvuvi wa Ziwa Kitangiri, je, Serikali inafahamu kwamba kuna mgogoro kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Iramba na Wilaya ya Meatu kuhusu uhalali wa Ziwa liko wapi kwa maana ya mpaka? Je, sasa Serikali ipo tayari kutoa tamko kuwa leseni ya wavuvi katika Ziwa Kitangiri zikatiwe Doromon na watozwe ushuri kwenye Halmashauri zao na kwamba Serikali itangaze Ziwa Kitangiri liko Wilaya ya Iramba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ANDREW J. CHENGE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David (Mb), Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, kwa hotuba nzuri inayotoa mwelekeo mzuri na matumaini kwa ukuaji wa sekta za mifugo na uvuvi hapa nchini. Aidha nampongeza Mheshimiwa Ole-Nangoro, Naibu Waziri, Katibu Mkuu Dkt. Charles Nyamrunda

na timu yake ya wataalam kwa mchango wao katika maandalizi ya hotuba hii na kwa kazi nzuri ambayo wanafanya. Kazeni buti twende mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitamke kuwa naunga mkono hoja hii kwa asilimia moja. Hata hivyo, nina machache ya kuchangia. Sekta ya Mifugo na Uvuvi zina nafasi kubwa za muhimu katika kuchagia katika pato la Taifa, katika kutoa lishe bora, ajira na kipato kwa wavuvi na wafugaji. Hata hivyo, uwekezaji katika sekta hizi bado hauridhishi. Kwa mfano, sekta ya uvuvi ikisimamiwa vizuri (kwa kujenga mazingira mazuri kwa wawekezaji wa ndani na wa nje), ina uwezo mkubwa wa kuchangia pato ya Taifa. Ni suala la kuvua rasilimali ambazo tayari zipo zikisubiri kuvunwa (katika Maziwa na Bahari). Ni vema tukajiulize kwa nini hadi sasa sekta hii haichangii kwa kiasi kikubwa katika pato la Taifa kama nchi ya Mozambique na Seychelles?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tuangalie mfumo wa ada zinazotozwa kwa leseni, lakini pia Serikali iangalie uwezekano (kupitia Sheria) kupiga marufuku uvuvi unaofanywa katika Ukanda wa Uchumi na meli kubwa zinazovua samaki na kusindika samaki huko huko Baharini. Meli zote zitakiwe kuvua na kurejea Bandarini kwa madhumuni ya kusindika samaki kama inavyofanyika katika nchi nyingine. Hii itatoa ajira, mapato ya uhakika kwa Serikali na kuweza kudhibiti uvuvi unaofanywa hivi sasa. Naelewa hatua hii itahitaji uwekezaji mkubwa kwa upande wa Serikali wa kuwa na meli kubwa za doria. Hili haliepukiki kama sekta hii tunataka ikue na itoe mchango wake stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali katika sekta ya mifugo haitofautiani sana na sekta ya uvuvi, ina changamoto nyingi. Hata hivyo, kwa idadi ya mifugo tuliyo nayo (ng'ombe milioni 21.3, mbuzi milioni 15 na kadhalika) bado tuna kazi kubwa ya kuendeleza sekta hii muhimu. Uwekezaji katika sekta hii bado ni mdogo mno. Naipongeza Serikali kwa jitihada zake za kujenga mazingira mazuri ya kuvutia uwekezaji katika viwanda vya kuongeza thamani mazao ya mifugo kama vile ukataji wa nyama, utengenezaji wa bidhaa za ngozi na usindikaji wa maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iongeze kasi ya kushirikiana na wadau wa nyama ili kuendeleza kwa haraka sekta hii. Sekta ndogo ya nyama inahusisha ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku na nguruwe kwa soko la ndani na la nje. Nashauri Serikali ijenge machinjio ya kisasa ya kutosha kwenye maeneo yenye mifugo mingi kama vile Shinyanga, Mwanza, Singida, Arusha na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahishwa sana na hotuba za Waziri katika Ibara ya 90 hadi 95 ya Hotuba yake. Naipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayofanya ila napenda kutoa angalizo. Namwomba Mheshimiwa Waziri afuatilie kwa karibu Machinjio ya Kisasa yaliyopo hapa Dodoma – yameanza kukumbwa na changamoto ambazo iwapo hazitashughulikiwa mapema yatavuruga soko letu la nyama hasa katika nchi ya Kiarabu. Tuna tatizo la *pump* ya maji na *cold rooms*. Pili kuna malalamiko mengi kuhusu utaratibu wa kupata vibali vya *exports* kutoka Wizarani. Yadaiwa kuwa kuna urasimu usio na ulazima wowote. Namwomba Waziri wakati anahitimisha hoja yake alisemee suala hili ili wote tufahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS**: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kuwa hai na uzima pamoja na Wabunge wengine tuliopo katika ukumbi huu wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye mifugo mingi ndani ya Bara la Afrika lakini bado haisaidii Taifa ipasavyo. Mifugo haijatoa mchango wa kutosha katika pato la Mfuko wa Taifa. Kwa kuwa ufugaji hausimamiwi vizuri na kuendelezwa kwa vitendo bado wafugaji wanaendelea na ufugaji ule ule wa zama za babu zetu waliopita. Mfano wafugaji wengi wanakusanya makundi makubwamakubwa ya Ngombe, Mbuzi na Kondoo pasipo kuzingatia malisho bora, matibabu na majosho vitu ambavyo ni lazima katika ufugaji bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naiomba Serikali ipange mipango endelevu ya kusimamia ufugaji utakaokuwa na tija kwa Taifa. Wafugaji wasimamiwe wafuge ng'ombe wachache ambao

ataweza kuwahudumia kwa huduma zote muhimu. Tukimudu kupunguza idadi ya mifugo mingi, matatizo ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji yatapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba Serikali kutafuta mbegu bora za ng'ombe ambao wana tija kubwa na kuwapa wafugaji wetu waendeleze ufugaji bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvuvi, bado Serikali yetu haijasimamia uvuvi wa kiuchumi bali uvuvi tulionao ni uvuvi wa kupata mboga tu. Mungu katubariki tuna Bahari, Maziwa na Mito ambayo yana rasilimali lakini wavuvi hawajawezeshwa. Wavuvi wadogowadogo ambao ndio wengi wanasumbuliwa na kuchomewa nyavu zao na kero mbalimbali. Serikali ipange mipango bora kuwapatia vifaa bora vya uvuvi wavuvi wetu wadogowadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania mpaka muda huu samaki wa Bahari Kuu hawajavuliwa. Naiomba Serikali iwapatie meli za uvuvi wavuvi wetu wavue samaki wa bahari Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayofanya kukuza uvuvi na mifugo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kuu la kuunda Wizara hii ni kufanya sekta hizi mbili kuchangia kwa kiasi kikubwa pato la Taifa kupitia wafugaji na wavuvi lakini bado suala hili halijapiga hatua kubwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ufinyu wa bajeti kuu na bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi kati ya wafugaji na wakulima ni dosari kwa nchi yetu kwa sababu sote ni Watanzania. Kuna haja kwa Serikali kupima maeneo yote ili yale ya mifugo yatenganishwe na ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, azma ya kufanya Tanzania nchi ya wafugaji na sio ya wachungaji bado haijafikiwa kwa sababu bado wafugaji hawajakuwa wa elimu pana ya mageuzi katika Sera ya Mifugo. Kwa kuwa jambo hili linagusa mila za watu, itachukua muda mrefu kutekelezwa. Hata hivyo, elimu ya ufugaji kwa vitendo itolewe ili kubainisha faida na tija inayopatikana kwa kufuga kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya nyama ni budi iboreshwe kwa kuhamasisha unenepeshaji wa ng'ombe ili kupata nyama nyingi na yenye ubora wa Kitaifa na Kimataifa kwa kuuza nyama nyingi nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya uvuvi ina nafasi ya pekee katika kukuza uchumi wetu hasa kwa sababu tumezungukwa na ukanda mkubwa wa Bahari lakini bado uvuvi haujachangia pato la Taifa kwa kiwango cha kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ianze kuandaa vikundi vya wavuvi wapewe zana za kuvulia – boti, nyavu na utaalam wa mbinu mbalimbali za uvuvi. Vikundi hivi ndivyo vitakavyokuwa dira kwa Watanzania (wavuvi) wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zana za kilimo zimekuwa tatizo kwa kuharibu mazalio ya samaki. Hata hivyo, mbinu inayotumika kupambana na wanaoharibu mazalio ya samaki sio ya kiungwana, tukitilia maanani kuwa hatujatoa mbinu mbadala za uvuvi na tukitilia maanani kuwa uvuvi ndio chanzo cha maisha cha Watanzania waishio Ukanda wa Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu kwa Wizara hii kwa ushirikiano na Wizara ya Viwanda iboreshe usindikaji wa samaki, nyama na maziwa ili viweze kuwafikia hata wale Watanzania walioko mbali na maeneo ya uzalishaji.

**MHE. REGIA E. MTEMA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi itiliwe mkazo zaidi ili kuongeza pato la Taifa. Tuna kila sababu ya kujivunia rasilimali hii Mungu aliyotupa kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe tamko kuhusu Samaki walioingizwa nchini, hao samaki wenye sumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kujua ni kwa jinsi gani wavuvi wadogowadogo watakavyonufaika kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaona kwenye hotuba mahali popote wavuvi wa Kilombero wakitajwa ni jinsi gani watakavyowezeshwa. Napendekeza wavuvi hawa wapate elimu ya ujasiliamali, namna bora ya uvuvi pamoja na kupata mikopo yenye masharti nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaoingiza nyavu haramu nchini wawajibishwe na sio kumwajibisha mvuvi ambaye yeye hana hatia kwani amenunua tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wana malalamiko ya muda mrefu kuhusu migogoro yao na wakulima. Serikali *has to pay attention to this issue at least once in life time*. Wafugaji Mkoani Morogoro wasikilizwe kero zao na migogoro yao iishe basi.

**MHE. SUBIRA K. MGALU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunipa uhai unaoniwezesha kuendelea kutimiza majukumu yangu ya Kibunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa utekelezaji wa mpango wa maendeleo wa mwaka 2010/2011 uliopelekea kufanikiwa katika maandalizi ya hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu katika hotuba ya Wizara hii utajikita katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, migogoro ya ardhi kati ya wafugaji, wakulima na watumiaji wengine wa ardhi. Mkoa wetu wa Pwani umepokea wafugaji hasa Wamasai katika maeneo mbalimbali mfano Bagamoyo eneo la Kijiji cha Mapinga na Chamakweza, Rufiji, Mkuranga na Kibaha eneo la Magindu. Hata hivyo, tumeshuhudia mapigano ya mara kwa mara baina ya wafugaji na wakulima katika kugombea ardhi. Mapigano hayo yanayohatarisha usalama wa wananchi yamejitokeza katika maeneo ya Kata ya Makindu, Wilayani Kibaha na maeneo ya Bonde la Rufiji, Wilayani Rufiji. Hivi karibuni tumeshuhudia mapigano kati ya wafugaji na wakulima katika Kijiji cha Mapinga, Wilaya ya Bagamoyo. Naishauri Serikali ichukue hatua za haraka kukomesha ugomvi wa ardhi kati ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Sekta ya Uvuvi ina mchango mkubwa katika pato la Taifa na ingekuwa na uwezo mkubwa wa kuchangia kwa kiasi kikubwa kama Serikali ingewekeza kiasi cha kutosha. Ninayo masikitiko sekta hii ya uvuvi kutengewa kiasi kidogo cha pesa za maendeleo kulinganisha na mwaka 2010/2011 kwa mujibu wa Takwimu za Kitabu cha Maendeleo, ukurasa wa 283 ambapo mwaka 2010/2011, *Sub-Vote* 9001, *(Fisheries Development Division),* Kifungu 6501, *Marine Coast Environment Management Project* zilitengwa jumla ya Shs.9,175,071,600 wakati mwaka huu kifungu hicho kimetengewa kiasi cha Shs.4,771,079,000. Kinachonishangaza kwa upande wa makusanyo, Wizara inategemea makusanyo zaidi toka kwenye uvuvi kuliko kwenye ufugaji. Kwa mfano kwa mwaka 2010/2011, Wizara ilitarajia kukusanya shilingi bilioni 13,,633,400,000 kati ya hizo, shilingi 3,528,502,000 (26%) ni kutoka sekta ya mifugo na shilingi 10,104,898,000 (74%) kutoka sekta ya uvuvi, hadi mwezi Juni 2010 kiasi kilichokusanywa ni shilingi 13,721,094,895. Ni kwa nini kama Wizara inategemea asilimia 74% ya mapato yake toka kwenye sekta ya uvuvi, Serikali hiyohiyo imeitengea kiasi kidogo cha pesa katika Bajeti ya Maendeleo? Maeneo ya Ukanda wa Pwani na kwenye Mito, Maziwa, sekta ya uvuvi inatoa ajira kwa kiasi kikubwa. Hivyo kuinyonga Bajeti ya Maendeleo hasa pesa za ndani ni kutotenda haki kwa wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana utekelezaji wa miradi ya *MACEMP* katika maeneo ya Ukanda wa Pwani. Ujenzi wa vituo vya jamii tumeona, ujenzi wa mialo tumeona na

kadhalika. Tunaomba tathmini ya kina ifanyike kubaini mafanikio na matatizo ya mradi huo wa *MACEMP* ili awamu ya pili mradi huo ufanyike kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. REBECCA M. MNGODO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kutoa mchango wangu kuhusu hotuba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David (Mb) aliyowasilisha Bungeni juu ya Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania walio wengi, wafugaji na wasio wafugaji wanaitegemea sana sekta ya mifugo na uvuvi kwa maendeleo yao. Makadirio ya matumizi ya Wizara hii yaliyoombwa ya shilingi 57,165,193,000.00 na kutoka kiasi hicho cha fedha shilingi bilioni 20,853,683.000.00 kwa ajili ya maendeleo, kati ya hizo shilingi bilioni 4,358,694.000.00 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 16,494,989.000.00 ni fedha za nje. Kiwango cha fedha zinazotarajiwa kutoka nje ni kikubwa ukilinganisha na kiwango cha fedha za ndani. Hii ni hatari kutegemea fedha za nje kwa kiasi kikubwa kwa ajili ya kufanikisha shughuli za Wizara hii. Endapo fedha za nje hazitapatikana, je, itakuwaje? Ni muhimu Serikali iwe makini kwa jambo hili. Fedha ya maendeleo iongezwe, kiasi kilichotengwa ni kidogo mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa uvuvi, hivi karibuni tumesikia kwamba samaki kutoka Japan wameingizwa nchini, aina ya Kamongo ambao inasadikiwa kuwa wana sumu ya nyuklia. Athari za nyuklia zinafahamika ni pamoja na watu kupoteza maisha au mimba kuharibika kwa wanawake wajawazito. Athari ya walaji wa samaki hao kupata kansa, kunyonyoka nywele na kadhalika. Serikali idhibiti uingizwaji wa nyama, samaki kutoka nje. Aidha, samaki kutoka Japan wateketezwe na mauzo yake yasimamishwe mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuichangia hoja hii, nianze na uvuvi wetu. Kwanza, tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia Bahari, Mito na Maziwa ambayo yote haya kwa njia moja au nyingine uchumi wetu tunategemea hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini basi tusitumie rasilimali hii ya Bahari, Mito na Maziwa ili kukuza uchumi wetu? Kwa nini kusiweko Kampuni ya Samaki ambayo itakuwa ni kampuni ya Serikali ambayo itakuwa na Viwanda vya Kusindika Samaki wa aina zote ambao wamo katika Bahari, Maziwa, Mito yetu ambazo ni rasilimali zetu na pia ajira zitakuwepo kwa vijana ambao hawana pa kukimbilia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bahari yetu, mara nyingi utasikia kunaonekana meli za uvuvi ambazo zinatoka nje. Je, Serikali imechukua hatua gani ili kuzuia hali hii ya wizi wa samaki wetu katika mwambao wa bahari yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vyombo vya habari vimetoa taarifa kuhusu samaki walioingia nchini, samaki hao wanatoka China na wana mionzi ya nyuklia ambayo ni sumu kwa binadamu. Cha kusikitisha samaki hao wamepita katika ukaguzi wa kitaalamu na kwa nini hawakuonekana kwamba ni hatari? Hapa pana hujuma ya makusudi kabisa na hili msilifumbie macho waliohusika wawajibishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania hatuna shida ya samaki kutoka nchi za nje kwani tumejaliwa, tuna samaki wa kutosha katika nchi yetu wa Baharini, wa maji chumvi na Mito, wa maji baridi, sasa iweje leo tunaletewa samaki kutoka nje? Serikali hapa iwe makini kutetea hali ya wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija katiaka suala la nyavu za matundu madogo, hapa wasilaumiwe wananchi tu bali viwanda vinavyotengeneza nyavu hizi vipigwe marufuku ili kunusuru huo uvuvi haramu usitokee tena. Tuboreshe uvuvi wetu kwani ni uchumi ambao utatuletea pato kubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mifugo, ng'ombe ni mnyama na nyama yake ni chakula, ngozi yake mali tunatengenezea viatu, vigoda, viti na tunasafirisha nje na mavi yake ni mbolea, maziwa tunakunywa mtindi na samli yake ni dawa. Naomba sekta hii iboreshwe kwani nayo pia uchumi wetu wa Taifa unatoka hapa. Tulikuwa tuna viwanda vingi hapa vya ngozi ambavyo vinatengeneza viatu, sasa sekta hii ikiboreshwa mambo yote yale yatarudi kama zamani ila kusiwe na ubinafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kwa Wizara tajwa hapo juu na kwa hoja ya uvuvi nitapenda nifafanuliwe hoja zangu vinginevyo nitachukua hatua ya kuzuia mshahara wa Waziri na pia naweza kutoa shilingi katika bajeti husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii inakabiliwa na matatizo mengi hasa katika Jimbo langu la Nkasi Kusini. Changamoto hizo ni pamoja na:-

(i) Leseni za uvuvi nyingi katika seti moja ya kukamilisha chombo cha uvuvi ambapo wanaoshiriki katika kukamilisha utendaji halisi wa chombo kama *Ring Net* inatakiwa kati ya watu kumi na kumi na mbili, washiriki wote lazima wawe na leseni kila mmoja na kwa vile mara nyingi hawana uwezo wa kulipia hulazimika kulipiwa na mmiliki wa chombo na huwa wamebaki vijakazi wake bila hiari, hii ni kuanzisha aina ya utumwa nyingine.

(ii) Leseni hizi hulipwa licha ya kila chombo kinachotumika kulazimika kulipiwa leseni pia tena kwa mlinganisho wa thamani ya dola ya Marekani. Wavuvi wamekuwa hawafanyi shughuli zao badala yake wamekuwa wakikamatwa kila mara na hapajajengeka mahusiano baina ya wavuvi na wataalam wa uvuvi.

(iii) Wavuvi hawajapata aina yoyote ya msaada wa kuweza kuboresha shughuli zao za uvuvi kutoka Serikalini kama ilivyo kwa kilimo na wafugaji ambapo ruzuku zimetolewa.

Kwenye bajeti msamaha katika ushuru wa nyavu haiwezi kuleta badiliko kubwa la kutambulika sanasana itaweza kuwanufaisha wafanyabiashara wa nyavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya samaki wabichi nje ya nchi. Katika Ziwa Tanganyika pamekuwepo na biashara inayovunja Sheria ya Kuuza Samaki Wabichi nje ya nchi yaani samaki wabichi wanaovuliwa eneo la Ziwa Tanganyika, Kata za Ninde, Wampembe na Kala hupelekwa moja kwa moja kwenye soko la samaki wabichi kule Zambia wakiwa hawajachakachua kama Sheria inavyohitaji na watumishi wa Wizara wamekuwa wakitumika kukusanya ushuru bila kujali kuwa wanavunja Sheria na hakuna hatua zozote zimechukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Wizara kubadili Sheria hizi zinazonyanyasa wavuvi. Pia kutochana nyavu ambazo zinanunuliwa kwa fedha nyingi sana badala yake kuwaelimisha wavuvi kubadili aina ya uvuvi ambao utakuwa endelevu badala ya kuchoma nyavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ziwa Tanganyika eneo lote la Nkasi Kusini hakuna kabisa masoko ya samaki wala hakuna mipango endelevu ya kuhakikisha wananchi wana mahali safi pa kwenda kupata samaki wakiwa kwenye mazingira masafi yaliyoandaliwa.

Biashara ya Samaki wabichi imeleta athari zifuatazo:-

(i) Wananchi hawapati kitoweo cha samaki kwa vile wafanyabisahara wananunua samaki wakiwa majini licha ya kuishi pembezoni mwa ziwa.

(ii) Wananchi wamebaki hawana ajira ndogondogo za kuwaandaa samaki hasa akinamama na kuleta malalamiko mengi ya kupoteza aina ya kazi walizozizoea.

(iii) Wananchi sasa kupitia Halmashauri yao wanakosa mapato ya Halmashauri yao kwani samaki huuzwa majini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo inaharibu sana mazingira, ardhi inaharibika sana kila mahali. Wafugaji ni wababe kupita kiasi kwa jamii ya wakulima. Inaonekana Serikali imechelewa kuchukua hatua ya kutunza mazingira. Serikali iwasaidie wananchi wanyonge wanaonyanyaswa na jamii ya wafugaji. Jambo hili linawaumiza wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za dawa/malisho. Majosho ya kutosha yapo, lakini bei ni kubwa, bei za dawa zipunguzwe. Machinjio yatengenezwe ili kutoa huduma ya nyama kwa ubora. Idadi ya mifugo ilingane na eneo linalohusika. Uhamishaji mifugo kiholela haufai, unasababisha maeneo mengine kuzidiwa kama Nkasi.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa namna alivyowasilisha kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shughuli zinazowapatia vipato wananchi wa nchi hii na Taifa hili ni pamoja na ufugaji na uvuvi. Kutokana na mifugo, tunapata chakula kwa maana ya nyama, maziwa na siagi. Vingine ni ngozi pamoja na samadi. Mifugo inatusaidia katika shughuli za uzalishaji kwa maana ya wanyama kazi ambao hutumika katika shughuli za kilimo pamoja na usafirishaji. Kwa upande wa samaki pia ni chanzo cha chakula chenye *protein* na pia ni chanzo cha mapato kwa mwananchi wa kawaida na Taifa kwa ujumla. Tuombe Serikali kuwasaidia wafugaji kutoa huduma ya chanjo pamoja na masoko ya uhakika kwa ajili ya kuuza mazao yatokanayo na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, tuiombe Wizara kuwapatia mikopo na masoko wavuvi wetu. Aidha, viwanda vya nyama pamoja na samaki kwa ajili ya usindikaji ni muhimu ili kuboresha ubora wa nyama na samaki. Tuiombe Serikali isikie kilio cha wavuvi.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutanguliza shukrani zangu kuhusu jambo muhimu ambalo Serikali imechukua jukumu la kuwapa wafugaji kifuta machozi. Namshukuru Rais, Mheshimiwa Dkt. Jakaya M. Kikwete kukubali kuwapa wananchi mifugo watano (5) kwa ajili ya kufuga baada ya ng'ombe wao kufa. Ahsante sana. Ombi langu, kwa kuwa mbuzi ni muhimu sana na ni rahisi kuzaliana na kusaidia familia, naomba wakati wa kununua ng'ombe wanunuliwe na mbuzi wagawanywe kwa hao waathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwenye bajeti hii kuna miradi ya mifugo ambayo haiko kwenye Wizara hii mfano fedha za *DADPs* za mabwawa, machinjio, vibanio, majosho na birika za ng'ombe kunywea maji, ziko chini ya Wizara nyingine na hakuna usimamizi. Ukiangalia miradi yote iko chini ya kiwango, fedha zinaliwa, hili ni jambo ambalo halivumiliki, ni *EPA* nyingine kwenye Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, mifugo ni zao kama mazao mengine lakini cha kusikitisha hakuna utaratibu wa mauzo ya mifugo. Ng'ombe wanauzwa kiholela hata idadi iliyouzwa hakuna ukweli kwani hakuna soko maalum linalotegemewa kuuza mifugo. Naomba Serikali watafute masoko ya kuuzia mifugo na viwanda kwa ajili ya kuchinja mifugo na kuuza nyama nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, migogoro ya wafugaji na wakulima. Ni kweli migogoro imedumu na inaendelea kuwa mikubwa. Jambo hili lisiwe la kisiasa kwa ajili ya Chama fulani kutumia mgogoro huu kutafuta kura, siyo jambo la busara. Naiomba Serikali iangalie kwa nini wakulima na wafugaji wawe na mgogoro katika maeneo ya Kusini tu? Mbona Wasukuma wa Shinyanga ni wakulima na wafugaji, kwa nini wasipigane? Mbona wakulima na wafugaji walioko Mkoa wa Manyara na Arusha wanakaa kwa amani? Mbona wakati ule kabla kodi ya mifugo haijafutwa, Halmashauri za Mkoa wa Morogoro, Mpanda walikuwa wakiwatetea wafugaji? Kwa sasa kwa kuwa mifugo hailipiwi kodi ndiyo maana wamechukiwa na wakulima? Naomba Serikali itenge vijiji vya wakulima na wafugaji na wakulima wasiruhusiwe kulima maeneo ya malisho na kufunga mapito ya mifugo kwenda kunywa maji au kwenda kwenye malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, maeneo ya Ranchi ya Serikali. Katika hotuba ya Waziri, ukurasa wa 36 alisema kununua ng'ombe 3,453 kutoka kwa wafugaji wanaozunguka maeneo ya Ranchi kwa ajili ya Programu ya Unenepeshaji. Ununuzi huu haujawahi kufanyika, ni muhimu na ni faida kwa wafugaji. Naomba Ranchi ya Kilimanjaro washirikishe wafugaji wanaoishi kandokando ya Ranchi hiyo ili nao wawe kwenye watakaopewa maeneo ya kunenepesha mifugo na kuuza ng'ombe, mbuzi na nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, kuanzisha Ushirika wa Wafugaji. Wafugaji wanahitaji kuwa na ushirika wao ili wawe na chombo ambacho kitawasaidia wafugaji kibiashara. Kwa muda mrefu biashara ya ufugaji imekuwa inafanyika kiholela na hakuna sauti ambayo inawawezesha kutafuta masoko, bei na mifugo haina utaratibu inauzwa kwa kuangalia tu lakini baada ya ng'ombe kuuzwa nyama inapimwa kwa kilo. Hii ni biashara na udanganyifu. Wafugaji wa Wilaya ya Longido wameanza utaratibu wa kuanzisha ushirika, kinachohitajika ni elimu pamoja na kanuni za kuanzisha ushirika. Naomba msaada huo wa kuanzisha Ushirika wa Wafugaji Wilaya ya Longido.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, dawa za mifugo. Utaratibu huu wa dawa za ruzuku ni mzuri lakini kuna dawa ambayo ni muhimu sana wafugaji wapate kila mwaka tena kwa bei nafuu dawa ya *E.C.F*. Dawa hii ni chanjo, Serikali ijitahidi kuleta dawa hii na kuchanja ndama kila mwaka wanapozaliwa. Dawa nyingine muhimu ni dawa ya miguu na midomo, ugonjwa huu unatokea kila mwaka lakini dawa haipatikani, tunafuata Kenya, hii ni dawa muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nane, mbegu ya ng'ombe bora. Kwenye Ranchi zetu hawakuboresha tena, mbegu ile imepitwa na wakati. Mifugo hao watafutiwe mbegu nyingine wa kuboresha, haiwezekani tukafuatilia mbegu kwenye Ranchi za Kenya huku kwetu tuna Ranchi. Longido tumeboresha ng'ombe kutoka maeneo ya Kenya, kufuata ubora wa Ranchi zote zilizoko Kenya, naomba tuboreshewe mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumalizia kwa kushukuru na kuomba kwamba wakati wa kununua mifugo ya kufuta machozi, Kiongozi wa Serikali aje kuzindua mradi huo kwani ni muhimu na haijawahi kutokea. Ahsante.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri kwa hotuba nzuri aliyowasilisha. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda kuzungumzia sekta ya uvuvi ambayo ni muhimu sana kwa wananchi waishio kandokando ya Ziwa Victoria. Jimbo la Busanda lina maeneo yaliyoko kandokando ya Ziwa Victoria. Kwa kutaja ni Vijiji vya Bukondo, Kasanghwa, Kageye na Nungwe. Ili kuweza kuinua hali za maisha ya wananchi waishio katika maeneo haya, naomba Serikali inipe mpango mkakati wa namna itakavyoweza kuwawezesha wananchi hawa. Wavuvi waliopo Vijijini wana uwezo mdogo sana kiasi kwamba hawana uwezo wa kununua nyenzo muhimu za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia MKUKUTA inakusudia kuongeza kipato na kupunguza umasikini. Hivyo basi hata wananchi hawa wavuvi waandaliwe mpango maalum wa MKUKUTA ili waweze nao kunufaika na kuboresha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti nimeona miradi mingi sana inayolenga Ukanda wa Bahari ya Hindi wakati Ukanda wa Ziwa umeachwa bila mradi. Naomba Serikali pia iangalie Ukandz wa Ziwa Victoria kwani kuna wavuvi wengi sana ambao wakiwezeshwa, nina uhakika wataboresha maisha yao na uchumi wao kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba Wizara iweke mkakati wa kuanzisha miradi ya maendeleo kwa wananchi wavuvi kandokando ya Ziwa Victoria na hasa katika Jimbo langu la Busanda ambapo wengi wanalia kilio kikubwa hawana vifaa vya uvuvi. Naamini Serikali ikiwawezesha wananchi hawa watafaidika na watainuka kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imefanya kazi nzuri kwa kipindi kilichopita na pia ina mipango mizuri kwa mwaka 2011/2012. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, utekelezaji wa mradi wa *MACEMP* unasuasua kutokana na masharti ya kuzitaka *BMUs* kuwa na pesa kwenye akaunti zao kabla ya kupewa pesa za mradi. Ni vyema sharti hili liondolewe na vikundi hivyo vitakiwe kuchangia nguvukazi kwani wengi wanashindwa kutoa michango ya fedha kutokana na hali ngumu ya uchumi Vijijini. Jambo la msingi hapa ni usimamizi mzuri wa pesa ya mradi ili zifanye kazi iliyokusudiwa. Baadhi ya *BMU* kwa mfano Mkoani Mtwara zilitaka kujenga vyoo katika maeneo ya fukwe ili kuzuia uchafuzi lakini kutokana na masharti na ucheleweshaji, vyoo hivi havijajengwa na hivyo uchafuzi wa fukwe unaendelea. Tafadhali Serikali iangalie kwa karibu vikwazo vyote vya utekelezaji wa *MACEMP* ili tuharakishe maendeleo katika jamii za wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, uchomaji nyavu zisizofaa umeongeza shughuli za uvuvi usio endelevu. Kwa mfano utumiaji wa baruti katika baadhi ya maeneo umeongezeka ambapo huu ndio hatari zaidi kwa viumbe wa majini. Hili linatokana na sababu kwamba wavuvi huchomewa nyavu bila maandalizi yoyote ya kuwawezesha kufanya shughuli mbadala za kuwapatia kipato. Hivyo wavuvi wakichomewa nyavu hujikuta wakilazimika kujiingiza kwenye uvuvi wa baruti ili wapate chakula, gharama za matibabu, kusomesha watoto na kupata mavazi. Naishauri Wizara ijikite zaidi katika elimu kwa wavuvi na kuwaandaa kuyamudu maisha kabla ya kuchoma nyavu, wapewe nyenzo mbadala za uvuvi (nyenzo bora).

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, wafugaji wapewe elimu juu ya mazao bora ya mifugo kama maziwa, nyama na ngozi. Waelimishwe zaidi wasipende kuwajeruhi mifugo kwa kuwapiga kwani huku kunaathiri nyama na ngozi pia utoaji wa maziwa. Elimu hii ni muhimu na izingatiwe sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Dirisha la Kilimo la Mikopo katika Benki ya *TIB* kuwepo na fungu maalum kwa ajili ya kuwakopesha akinamama wafugaji wa ng'ombe wa maziwa na kuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. JUMA OTHMAN ALLY**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie upande wa uvuvi haramu. Hii itasaidia sana pindi Wizara ikitenga fedha na kuwaelimisha wavuvi wasinunue pia kutumia zana zisizokubalika na baadaye kufanya uvuvi haramu. Naiomba Serikali ikemee pia hatua kali ziwekwe na zifanyiwe kazi ili wanaoagiza nyavu ndogo wasiweze kuziingiza hapa nchini na baadaye kuvua uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara isimamie sana mradi wa *MACEMP* utakapomaliza mkataba wake iombe uendelee tena kwani umetusaidia sana hata kule Visiwani Zanzibar, nawapongeza sana kwa kutusaidia pia utaporudi utupe mafunzo na elimu ya uvuvi halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naiomba Serikali iongeze bajeti ya Wizara hii kwani ni Wizara kubwa na ina mambo mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara iangalie sana upande wa Zanzibar kwani kuna Bahari kubwa ya kuvua pia kuleta maendeleo ya Bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pindi mradi wa *MACEMP* utaporudi tena ufikishwe haraka pia watupatie elimu zaidi ya ufugaji wa samaki wa aina mbalimbali mfano Chaza na vitu vingine vya baharini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri aweke sheria kali ili nyavu ndogo zisiagizwe pia zisiingie nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono. Ahsante.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David (Mb) Waziri na Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro (Mb), Naibu Waziri kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara hii muhimu kwa ustawi na maendeleo ya Taifa letu. Nampongeza pia Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya kusimamia utekelezaji wa mipango ya sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu fidia kwa wafugaji wa Arumeru. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri (Uk.29) imeeleza kuwa wafugaji wa Wilaya za Monduli, Longido na Ngorongoro waliopoteza mifugo kwa sababu ya ukame mwaka 2008/2009 watafidiwa. Hata hivyo, nasikitika sana kwamba uamuzi wa kulipa fidia wafugaji walioathiriwa na ukame huo umekuwa na upungufu. Hii ni kwa sababu wafugaji wa Jimbo langu waliathirika sana kwani ng'ombe wachache waliokuwa nao kwa ajili ya maziwa na wanyamakazi walikufa karibu wote na kuwaacha fukara. Nimeambatisha hapa nakala ya barua ya *DED* yenye idadi ya wanyama waliokufa. Naomba Serikali ilipe fidia kwani wananchi walipata matumaini wakati wataalam walipofika kufanya tathmini ya hasara iliyopatikana. Ni matumaini hayo ndiyo yaliyowezesha Chama cha Mapinduzi kushinda Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010. Wananchi wa Arumeru wameanza kujenga hisia kuwa Serikali inawabagua kwani jirani zao wa Longido na Monduli wanapata huduma nyingi nao wakitazama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, uboreshaji wa malisho na maji kwa mifugo. Eneo la malisho kwa ajili ya mifugo linazidi kupungua kwa sababu ya maamuzi yanayochukuliwa kuongeza maeneo ya wanyamapori na kilimo bila kutathmini athari zake mifugo. Ni vizuri Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Maliasili na Utalii, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira washirikiane na Wizara ya Ardhi kuweka mipango bora ya matumizi ya ardhi na kutenga eneo kwa ajili ya malisho ya mifugo kila Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji kwa ajili ya mifugo ni tatizo kubwa kwenye Jimbo langu na limekuwa sugu, hakuna lambo hata moja. Hotuba ya Waziri imeonesha kuwa malambo yalijengwa mwaka 2010/2011 katika Wilaya mbalimbali nchini. Bahati mbaya Wilaya yangu si mojawapo. Naomba Wizara itusaidie kujenga malambo kwenye Kata za Oldonyosambu, Mwandet, Olkokola, Musa, Kisongo, Mateves, Oljoro na Bwawani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ufugaji wa samaki. Wilaya ya Arumeru inayo maeneo mazuri ambayo ufugaji wa samaki ungeweza kufanyika kwa mafanikio makubwa kama Serikali ingehamasisha wananchi na kutoa ruzuku na elimu ya kutosha, wangefaidika kiuchumi na kiafya kwa kupata chanzo cha *protein* na pia kujipatia fedha. Eneo la Themi ya Simba kwenye Kata ya Bwawani panafaa sana kwa samaki. Pia malambo yanayojengwa kwa ajili ya kunywesha mifugo yajengwe kwa namna ambayo yatatumika pia kufuga samaki. Naomba Wizara itusaidie kuanzisha na kuendeleza ufugaji wa samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo furaha kubwa kuchangia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Pia mimi ni mjumbe wa Kamati ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipewe majibu juu ya mikakati iliyoandaliwa ili kupunguza au kumaliza migogoro kati ya wakulima na wafugaji. Je, Wizara imejipanga kupima na kuainisha maeneo ya wafugaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Wizara hii ndiyo inaanza, sina cha kulaumu juu ya utendaji wa Wizara. Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuja Mbarali ili akutane na wafugaji ili aweze kusikiliza kero zao moja kwa moja kutoka kwao? Ni lini wafugaji wa (Mbarali) Tanzania wataacha kuishi kama wakimbizi? Kwani kila wanakokwenda wanaonekana hawatakiwi lakini kila siku tunapata kitoweo buchani. Kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kutatua kero za wafugaji nchini? Naomba kupata maelezo ya kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilifanya jambo jema kuwaondoa wafugaji kutoka Bonde la Ihefu ambalo ni muhimu kwa kuhifadhi maji ambayo hatimaye huingia Mto Ruaha na kufika bwawa la Mtera kwa ajili ya kuzalisha umeme. Kwa bahati mbaya, wafugaji walioondolewa Bonde la Ihefu hawakutendewa haki kabisa na Serikali. Kulikuwa na sababu gani kwa wafugaji kutozwa faini ya Tshs.10,000/= (Elfu Kumi) kwa kila mfugo uliohamishwa kutoka Ihefu? Lilikuwa ni agizo la nani? Naiomba Serikali iwarudishie wafugaji wote waliolipia mifugo inapohamishwa kwani hawakutendewa haki. Naomba nipewe majibu kabla sijatoa shilingi au mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati zoezi la kuhamisha wafugaji, Mkuu wa Wilaya, Hawa Ngulume alisababisha mifugo mingi ya wafugaji kufa kwa kuifungia bila kuruhusiwa kwenda malishoni na hivyo maelfu ya ng'ombe kufa na kusababisha hasara kubwa kwa wafugaji. Naiomba Serikali iwalipe fidia wafugaji wote waliopoteza mifugo yao. Naomba maelezo ya kuridhisha vinginevyo sitaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji waliokuwa wanategemea kunywesha maji maeneo ambayo kwa sasa ni hifadhi, wanaomba kuchimbiwa malambo.

**MHE. DKT. SEIF SELEMAN RASHIDI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, natoa shukrani za dhati kwa Warufiji kwa kunipa nafasi ya kuwawakilisha Bungeni na kwa niaba yao, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi nzuri yenye nia ya kuboresha maisha ya Watanzania. Pamoja na pongezi, nitoe shukrani kwa kuainisha mpango wa maendeleo ya mifugo na uvuvi katika nchi yetu na hususani Wilaya ya Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Viwanda yote haya ni ya msingi katika kuongeza mapato na kumnufaisha Mtanzania. Hatuwezi kufanya kila eneo la nchi hii kutumika kwa kilimo na mifugo ya ng'ombe kutumika kwa pamoja. Naamini Shinyanga, Singida, Mwanza, Tabora na Manyara ilikuwa ina misitu na ilikuwa karibu sawa na Mkoa wa Pwani. Bila ya kuficha, ukataji wa miti na ufugaji mkubwa kuliko uwezo wa eneo husika umesababisha nusu jangwa, ukame, mafuriko na njaa. Pamoja na mambo mengine kilichosababisha hayo ni kukata miti na kuchunga ng'ombe bila ya uwekezaji wa kupanda miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inanishangaza kuona Serikali kwa uwezo wake mkubwa wa kuona mbali zaidi imetekeleza mpango mbovu sana wa kuwahamisha wafugaji kuwapeleka kwenye maeneo ya miti na mabonde ya kilimo hususani bonde la Mto Rufiji bila ya kujali athari zake kama zilivyo sasa katika Mkoa wa Shinyanga na kadhalika. Hivi leo maeneo mengi makubwa ya Wilaya ya Rufiji ikiwemo Bonde la Mto umevamiwa na ufugaji ambao hauna mpango na udhibiti kwa kuhakikisha kwamba idadi ya mifugo inawiana na eneo, kwamba maeneo ya kilimo asiwepo mfugaji, maeneo ya wafugaji yawe yameandaliwa vya kutosha kumvutia mfugaji kukaa hapo, lakini pia maeneo ya misitu yanahifadhiwa kwa kupunguza kasi ya ukataji wa miti unaofanywa na wafugaji. Cha msingi pia usalama wa Watanzania hawa unalindwa kwa usawa sio kwa ubabe wa kiuchumi wa wafugaji kuwadhalilisha na kuwanyima haki na kwa kurubuni vyombo vya dola, lazima udhibitiwe kwa nguvu zote. Namtaka Waziri atoe msimamo wa Serikali juu ya watendaji wasio waaminifu wanaoogemea upande wa wenye fedha na kuwanyima haki wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya yote, naiomba Serikali pia kuendelea na mpango *MACEMP* na kuongeza juhudi za kuwawezesha wafugaji wa samaki katika upande wa Pwani ikiwa pamoja na Wilaya ya Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David (Mb), Waziri wa Maendeleo Mifugo na Uvuvi. Pia shukrani kwa Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro (Mb), Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Pia natoa shukrani za dhati kwa Watendaji Wakuu wa Wizara husika kwa uandaaji mzuri wa bajeti husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu katika Wizara hii utakuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji kwa wafugaji. Hili tatizo limeathiri kwa kiasi kikubwa wafugaji ambao wako mbali na Bahari au Maziwa. Kwa mfano wananchi wangu wa Jimbo la Tarime ni waathirika wakubwa wa suala hili. Naishauri Serikali itemize wajibu wake kwa kuwasaidia wafugaji uchimbaji wa malambo na mabwawa kwa ajili ya kunyweshea mifugo. Kwa mfano katika Jimbo langu la Tarime, kuna maeneo maalum ya wafugaji hasa Kata za Nyarokoba, Gorongia, Komaswa, Manga na Kibasuka. Ifahamike wazi kuwa sehemu hizi ni kame hivyo ni bora Serikali ikasaidia sana kuwachimbia malambo na mabwawa watu wangu ili wasiendelee kutaabika kutokana na suala la ukame linalowakabili wakazi wa Wilaya yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la majosho pia huathiri kwa kiasi kikubwa suala la maendeleo ya mifugo hapa nchini. Serikali pia isaidie kutoa huduma hii pamoja na kutoa dawa na wataalam wa sekta hii kwa ajili ya kuboresha mifugo yetu. Ni vizuri kila kijiji kikawa na josho kwa ajili ya kuogesha mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la malisho, naishauri Serikali kuhakikisha inatenga eneo kwa ajili ya malisho ya wafugaji. Katika Jimbo langu la Tarime, Serikali iangalie kwa makini suala la mbuga ya Serengeti ili iweze kupatikana nafasi ya malisho katika Vijiji vya Kata za Nyarokoba, Gorongia na Nyamungu. Ikumbukwe na ifahamike wazi kuwa maeneo ya malisho ya mifugo ya watu wa Kata hizi yalichukuliwa na Mamlaka ya Serengeti (SENAPA) kwa nguvu bila kuwashirikisha wananchi wa eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanda vya Nyama Tanzania. Hii ni changamoto kwa Serikali. Ijenge viwanda vingi na hata ikiwezekana ijenge kiwanda kila Mkoa ili kuwawezesha wafugaji kujikomboa kimapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujiulize ni kwa nini sekta ya uvuvi katika nchi yetu haitoi nafuu kwa wavuvi wa nchi hii? Je, sekta ya uvuvi inachangia asilimia ngapi katika pato la Taifa? Tufikiri Zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na kuunga mkono hoja.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa kazi nzuri wanayofanya. Pamoja na pongezi hizo naomba katika kufanya majumuisho ya hotuba yake anisaidie yafuatayo:-

Kwanza, Kiwanda cha Himo *Tanneries* cha Kusindika Ngozi kutoa harufu mbaya. Kiwanda hicho kimekuwa kero kwa wakazi wa Himo kwa muda mrefu kwa sababu kinatoa harufu mbaya. Jitihada za kuomba msaada kutoka kwa Wizara ya Viwanda na Wizara ya Mazingira bila msaada wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kuhusu ng'ombe wa maziwa. Wafugaji wengi wa Vunjo wana ujuzi na uwezo wa kufuga ng'ombe wa maziwa. Lakini ng'ombe wa maziwa anapatikana kwa bei ya Sh. 600,000/=. Fedha hizi ni nyingi kwa watu wanyonge. Kama Serikali inatoa ruzuku kwa pembejeo kwa nini Serikali isichukue mkopo kutoka kwa Benki ya Dunia ikawakopesha wakulima au wafugaji wa Vunjo wakapata ng'ombe wa maziwa kwa Sh. 200,000/= wakaendelea kulipa mkopo huo kidogo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kuhusu mbuzi wa maziwa. Kanisa la KKKT linasambaza mbuzi wa maziwa kutoka Israel kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu na yatima. Mbuzi hao ni wazuri na wanatoa maziwa mengi kama ng'ombe. Je, Wizara ina mpango gani wa kuimarisha miradi kama huu ambao una manufaa makubwa kwa wananchi maskini wa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, Jimbo langu lina mbwa wengi wazururaji ambao hawapati chanjo. Mbwa hawa waking'ata watu madawa ni ghali ya kuwatibu wahusika na wengi wanapoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara ieleze ina mikakati gani ya kuondosha kero hii katika Jimbo la Vunjo.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri sana, sasa ni kumwomba Mwenyezi Mungu yaliyoandikwa humu yatekelezwe itakuwa ni faraja kubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia kwa kuanza kutaja maslahi binafsi. Mimi ni mtu wa Pwani, Tanga nimetoka katika familia ya wavuvi hivyo na mimi ni mvuvi. Kijijini kwetu shughuli kuu katika eneo hilo ni uvuvi. Hivyo najua ugumu wa uvuvi hasa wa jadi ni mgumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi miongoni mwa watu wa Mikoa hii ya Pwani (Ukanda wa bahari) umeangamia kabisa, kiasi kwamba wavuvi wana fikra potofu kuwa kazi ya uvuvi imelaaniwa na Mwenyezi Mungu, kusema kweli sio sahihi kwani mifano hai tunayo kama *Norway Fishing Industry* wanaitegemea sana, ni ya pili kwa ukubwa katika kuwaingizia pesa za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili Jeshi la *Marine* ambalo linalinda uvuvi haramu. Kwa kweli wanayoyafanya huko *site* ni zaidi ya waliyotumwa, wanawadhalilisha sana wavuvi kupita kiasi. Sina uhakika kama sheria zao ndivyo zinavyowaruhusu kufanya hivyo na zinawalinda, naomba Mheshimiwa Waziri, anifafanulie katika majumuisho yako hayo, majukumu yao na endapo wakiwaua raia wanachukuliwa hatua gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi mambo wanayoyafanya ambayo ni kinyume na sheria ninavyohisi ni haya:-

- Kuwakamatia wavuvi vyombo vyao na kuvichukua;

- Kuchukua matanga yao ya madau na wakati mwingine kuchukua madau yao wakiwa maji marefu na kuhatarisha sana maisha ya wavuvi hawa;

- Huwapiga sana wavuvi na kuwakanyaga kanyaga na mabuti yao, wengine wanaathirika sana, nami ni mmoja wapo kwani watu hawa wameniulia kaka yangu (mtoto wa shangazi yangu) walimpiga kama jambazi sugu wakamuumiza kifuani na hakuchukua muda mrefu katika maisha yake akafariki. Pia kuna Mzee mmoja Kijiji cha Tongoni walimpiga Mzee Khalidi Aboud, walimpiga magongo na risasi juu amepona kwa kudra za *Allah* tu, lakini si mzima mpaka leo akili zake sio nzuri.

- Tukio la tatu sasa, mwaka jana kati ya mwezi Agosti na Septemba askari wa Jeshi la *Marine* hao hao waliwashuti watoto Kijiji cha Tongoni kwenye ufukwe wa bahari bila sababu za msingi, watoto hao ni:-

    - Mzonge Abdallah miaka 14 -15, huyu alikufa *on the spot* hakuomba hata maji ya kunywa.

    - Ilali Abdu walimpiga risasi ya mkono alikimbizwa Bombo Hospitali kutibiwa na kulazwa hakuna msaada wowote uliotolewa na watu hao.

    - Huyu aliwahi kujificha nyuma ya mti na risasi ilimpitia karibu na sikio, sasa cha kushangaza hakuna hatua zozote walizochukuliwa wauaji hawa ndio maana wanajiona wako juu ya Sheria kiasi kwamba ukiwauliza ninyi na Mungu nani mkubwa watasema sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kitengo kinachoshughulika na askari wa *Marine* hawa wawasimamie ili wafanye lile lililokusudiwa tu na sio kuwatesa wananchi wakazi wa maeneo hayo.

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuchangia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali halisi ya ufugaji hapa nchini. Suala hili limekuwa ni kero kwa wafugaji wengi. Je, Serikali na Wizara haioni sasa umefika wakati muafaka kutatua kero hizi za wafugaji na wakulima ili wafugaji hawa watengewe maeneo yao. Wizara ya Maliasili nao wamekuwa wakichangia katika migogoro hii ya wafugaji. Wanachukua maeneo bila ridhaa ya wafugaji na kuendelea kupanua maeneo ya mbuga za wanyamapori na kuweka mapori ya akiba ambayo wafugaji wanayatumia kuchungia mifugo yao. Jambo hili linazidi kupunguza eneo la malisho kwa mifugo. Je, Serikali na Wizara haioni kwamba wafugaji hawa vijijini hawatendewi haki. Kwa mfano, kabila la Wamasai wengi wao hawajasoma na wanategemea ufugaji kama kitega uchumi chao na maisha yao yote wanategemea ufugaji tu.

Hivyo basi wafugaji hawa hawana makazi ya kudumu kuhusu ufugaji wao. Wamekuwa na makazi ya kuhamahama. Je, Serikali na Wizara husika haioni kwamba kuna umuhimu wa kuwatengea wafugaji hawa makazi yao ya kudumu ili waweze kujikimu kimaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la migogoro ya ardhi kwa wafugaji na watumiaji wengine. Naishauri Serikali na Wizara husika kuangalia kwa makini hawa wawekezaji wanaokuja kuwekeza Tanzania. Wawekezaji wengi wamekuwa wakifaidika na rasilimali za Taifa letu na kuwaacha watanzania wengi katika hali ya umaskini. Mbona sisi Watanzania hatufaidiki na rasilimali za nje? Kwa hiyo, migogoro mingi na mikubwa ambayo Serikali ndiyo inatakiwa kulaumiwa kwa kushindwa kuwajibika na kulinda raia na mali zao. Hivi sasa kuna migogoro kati ya wafugaji wa Loliondo na Kampuni ya uwekezaji ya *Oritelo Business Corp*oration. Wafugaji wa Meatu na Kampuni ya *Mwiba Holding*, wafugaji wa Kijiji cha Kimotorola, Simanjiro na Mbuga ya Tarangire na migogoro mingine midogo midogo mingi katika maeneo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuangalia kuhusu wafugaji hawa. Wapatiwe semina endelevu kwa ajili ya utunzaji wa mifugo yao. Wafugaji hawa waanzishe ushirika wa vijiji, kuanzisha ranchi ndogo ndogo ndani ya jamii na kuboresha miundombinu ya huduma za mifugo ikiwemo maji na malisho bora. Hii itaongeza unenepeshaji wa mifugo na kuwafanya wafugaji waweze kuvuna mifugo kwa ajili ya kuuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji hawa inatakiwa wajengewe machinjio bora ya kisasa na wajengewe viwanda kwa ajili ya usindikaji nyama na vile viwanda vya zamani vifufuliwe kwa ajili ya usindikaji nyama na kuimarisha kwa viwanda vya ngozi vilivyopo katika maeneo ya wafugaji sambamba na kujenga na kuimarisha machinjio kanda zote hapa nchini. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo itachangia pia kuongezeka kwa uchumi wa Taifa letu na kuliingizia Taifa letu fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la uvuvi. Taarifa ya hali ya uchumi inaonesha kuwa uvuvi ulichangia asilimia 1.4 ya pato la Taifa kwa mwaka 2010. Jumla ya tani 347,157 za samaki wenye thamani ya shilingi milioni 774.5 zilivunwa, kati ya tani hizo tani 294,474 sawa na asilimia 84.4 zilitokana na uvuvi katika maji baridi na tani 52,683 sawa na asilimia 15.2 zilivunwa maji chumvi. Ni kwa nini Serikali haiwathamini hawa wavuvi wadogo wadogo na wakawapatia zana za kisasa na wavuvi hawa pia wapatiwe leseni na semina endelevu kuhusu matumbao ya vyanzo vya samaki na kuwadhibiti wale wanaotumia uvuvi haramu. Tuhakikishe Serikali inadhibiti uvuvi wa bahari kuu ili kuingiza Serikali mapato kutokana na ada za leseni za uvuvi na usajili wa meli zinazovua kwenye eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu ametupenda sana Tanzania, ametupa rasilimali za kutosha, maziwa makuu na bahari kuu. Kweli neema hizi Mungu alizotupa hatuwezi kuzitumia mpaka tuagize samaki kutoka Japan na tuliingia lini mkataba huo wa Japan kutuletea samaki Tanzania? Kwa akili yangu kama Mheshimiwa ninalolijua najua tuna mikataba ya kuingiza magari, baiskeli, cha kunishangaza kwa mujibu wa vyombo vya habari vya jana tarehe 26/07/2011 imeripotiwa kuwa nchini mwetu wameingizwa samaki aina ya Kamongo wanaoaminika kuwa wana mabaki ya sumu ya mionzi ya nyuklia na waliingizwa hapa nchini tarehe 11/07/2011 kwa kibali cha *TFDA* na. *TFDA II/F/IPER*/0896.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ichunguze kwa makini ni akina nani waliohusika kutoa kibali hiki cha kuingiza hawa samaki na waliohusika wachukuliwe hatua za kisheria. Hawa Wajapan kama walikuwa wanaona samaki hawa ni wazuri kwa nini wasile wao? Inaonesha kwamba wameshachoka kutuibia rasilimali zetu na sasa wanataka kutuua kwa njia hii ya samaki hawa wenye mabaki ya sumu ya nyuklia. Wajapan hawa hawatutakii mema Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi inawezekana kweli kwa nchi yenye ukanda wa Pwani wa bahari wa kilometa 1,424 upana wa kilomita za mraba 6,400, bahari kuu upana wa kilomita za mraba 223,000. Eneo la maji baridi maziwa makubwa matatu na madogo 29 kwa rasilimali hii yote tuliyopewa na Mwenyezi Mungu iliyojaa samaki wengi kila aina. Kama Taifa tuna haja kweli ya kuagiza samaki kutoka nje ya nchi? Kwa nini fedha zetu za kigeni zisitumike kununua mahitaji mengine ambayo hayapatikani hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaunga mkono hoja hii mpaka haya yote niliyoyachangia hapo juu nipatiwe majibu.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mimi ni mdau wa mifugo, naomba ku-*declare interest* kuwa mimi ni Mjumbe wa Bodi ya *PINGOS* (Mashirika yanayotetea wafugaji) mwanachama na mwanaharakati wa haki za binadamu (*LHRC*) pia ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji.

Kwanza, naomba kutambua uwepo na umuhimu wa wafugaji hapa nchini. Wengi wetu tumesoma, tumetibiwa na kukimu maisha yetu kupitia mifugo. Wafugaji pia wa nchi hii ni Watanzania na Serikali hii ni yao, wana haki ya kikatiba inayomruhusu Mtanzania kwenda popote nchini bila kuvunja sheria. Lakini wafugaji wamekuwa wakidharauliwa, wakiwekwa pembeni katika masuala ya maendeleo, kuhamishwa ovyo bila kujali haki za kibinadamu wala za kikatiba, bila kupewa fidia, wakati mwingine kutopewa kabisa na kuporwa mifugo yao, je, Serikali haioni kuwa haiwatendei haki wafugaji? Serikali sasa itoe tamko la kuwapatia ardhi wafugaji hawa ili waepuke unyanyasaji wanayofanyiwa na watendaji wa Serikali na wawekezaji wengine kama wa Kapunga Mbarali.

Pili, Serikali imekuwa ikiipigia debe sera za uwekezaji na huku ikitangaza lazima uwekezaji huo uwe na maslahi kwa umma, hususan jamii inayoizunguka. Lakini Serikali hiyo hiyo kupitia watendaji wake imekuwa ikitwaa ardhi ambayo imekuwa ikitumika kwa ufugaji kupitia mgongo wa dhana ya uwekezaji na kwa maslahi ya mwekezaji na siyo uwekezaji kwa maslahi ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kuwa na mkakati maalum wa kuibua uwekezaji miongoni mwa jamii za wafugaji ambao wameonesha uzoefu mkubwa katika ufugaji tangu enzi za mababu? Ama dhana ya uwekezaji inabadilika inapokuwa kwa mzawa hasa mfugaji na kuwa na mantiki zaidi kwa wageni tu au wakulima wa mazao tu? Je, Serikali inapinga kuwa ufugaji ni uwekezaji ambao ardhi inayotengwa kwa ufugaji huwa kwa ajili ya maslahi ya umma?

Tatu, *FAO* inasema tule nyama kilo 50 kwa mtu kwa mwaka na tunywe maziwa lita 200 kwa mtu kwa mwaka. Lakini sisi Tanzania hivi sasa tunakula nyama ni kilo 12 na tunakunywa maziwa lita 44 tu kwa mtu kwa mwaka. Ili ushauri wa *FAO* ufanyiwe kazi, kwa mwaka Watanzania wote (chukulia tupo milioni 43 na zaidi) tutahitaji kula nyama tani milioni 2.15, lakini sasa tunakula tani laki 516 tu (sawa na 24% ya mahitaji halisi). Kwa upande wa maziwa tunahitaji kunywa lita bilioni 8.60, lakini sasa tunakunywa lita bilioni 1.89 tu (sawa na 22% ya mahitaji halisi). Ni dhahiri kuwa tunahitaji mifugo zaidi ili kujitosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni kwa nini inang'ang'ana na Sera ya kupunguza mifugo wakati mahitaji ya nyama na maziwa bado ni makubwa hivyo? Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kuongeza mifugo hasa ukizingatia tuna maeneo makubwa zaidi ya hekta milioni 60 yanayofaa kwa ufugaji?

Nne, pamoja na kuwa nyama ni chanzo muhimu cha protini, bado kasi ya Serikali katika uzalishaji wa mifugo bora kwa ajili ya nyama hakiridhishi. Katika mwaka 2010/2011, kati ya ng'ombe wote waliopo nchini, ni wastani wa ng'ombe kati ya 90,000 na laki moja (kama

mlivyotueleza kwenye Kamati) tu ndio walionenepeshwa. Hiki ni kiasi kidogo ukilinganisha na mahitaji ya machinjio hapa nchini. Ruvu pekee itahitaji ng'ombe bora takriban 146,000 kwa mwaka. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzalisha mifugo bora ya kutosha na ili kukidhi mahitaji ya machinjio hayo ya kisasa? Je, Serikali hadi sasa imesambaza mbegu na madume bora ya nyama kiasi gani kwa wafugaji na katika Wilaya gani (wachungaji wa kiasili)? Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kununua mifugo kwa bei nzuri kutoka kwa wafugaji na kuiboresha kwa lengo la kukidhi mahitaji machinjio yetu na pia kuwatafutia masoko nje ya nchi ili kuongeza tija katika ufugaji na kipato kwa wafugaji?

Tano, chini ya uongozi wa Baba wa Taifa katika miaka ya nyuma tulikuwa na Viwanda vikubwa vya Maziwa katika maeneo ya Musoma, Dar es Salaam, Tanga, Mbeya, Utegi, Arusha na kadhalika. Viwanda hivyo vilibinafsishwa lakini ghafla vikafa ama kupunguza uzalishaji. Hali hii imeshusha usindikaji wa maziwa nchini badala ya kukua kama ilivyotarajiwa na Watanzania pamoja na Baba wa Taifa letu aliyejenga viwanda hivyo. Wizara kama msimamizi wa maendeleo ya Sekta itueleze:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini viwanda vingi vimekufa au kudorora ufanisi? Viwanda hivyo vyote vipo katika hali gani na uwekezaji umeendelezwa kwa kiasi gani? Serikali ina mpango gani wa kuvifufua au kunyang'anya na kutoa kwa wawekezaji wengine wakiwemo vikundi vikundi vya wafugaji? Je, Serikali haioni haja ya kusamehe mzigo na pia kikwazo cha kodi za *VAT* kwenye bidhaa za maziwa za Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kujenga usawa katika soko la maziwa hapa nchini, Serikali haioni haja sasa ya kudhibiti uingizaji wa bidhaa za maziwa kutoka nje ya nchi? Basi kama Serikali haiwezi kuwafanya lolote, iwasaidie na kujenga uwezo wa wanachi wake ili waweze kuwa washindani wazuri kwenye soko letu la maziwa?

Sita, hata kabla ya zama hizi za sasa za diplomasia ya kiuchumi, ushirikiano Serikali na mashirika ya Kimataifa ni muhimu kwa maendeleo. Hata bajeti ya Serikali kwa 20% inategemea misaada kutoka nchi za nje na Mashirika ya Kimataifa. Lakini hivi karibuni tumesikia kuwa shirika kubwa kama la *Heifer* ambalo limesaidia sana kutoa ng'ombe wa maziwa wamepunguza msaada wao. Kwanza, nataka Serikali itambue michango ya mashirika yanayoisaidia sekta hii kama *Heifer*, *land o lakes* na mengine mengi. Tusipowajali marafiki hawa na kushirikiana nao, wataondoka na wala hatutakuwa na nafasi ya kuwapata tena na zaidi itatia doa kwa jina zuri la Tanzania. Je, Serikali haioni *Heifer* na mashirika mengine ni kuwa wabia muhimu na marafiki wakubwa wa maendeleo? Je, ni kwa nini isiwe nao karibu na kuwashawishi wasiendelee kupunguza au kufunga kazi zao hapa nchini? Je, Serikali kupitia Wizara hii ina mkakati gani wa kushirikiana na kuweka mazingira bora hasa ya ushirikiano kwa wabia hao ili maendeleo ya sekta hii yasikwazike?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa majirani zetu wanachangamkia sana fursa za upatikanaji wa miradi kama hii na hivyo wabia kuvutika kwao zaidi, je, Serikali kupitia Wizara hii na zile za Mambo ya Nje, Afrika Mashariki na kadhalika hazioni kuwa zinatakiwa kuwa tayari na kuweka mbinu mkakati maalum wa ku-*lobby* ili kupata fursa za mashirika hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu inatufananisha au inafananisha wafugaji kama chumvi. Chumvi hata siku moja haiambiwi tamu bali chungu. Lakini chumvi lazima itumike kwenye chakula vitafunwa hata maji ya baraka na mifugo daima ni wabaya, waharibifu lakini kila meza ya Mkuu ina nyama na maziwa.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge la Tisa, mwezi Aprili, 2009 Serikali ilitoa Tamko baada ya mgogoro wa wakulima au wafugaji na *operation* ambayo haikuwa halali ya kupunguza mifugo katika Mkoa wa Rukwa na Morogoro na kuahidi kuunda Kamati ya Uchunguzi na itakapothibitika wafugaji watalipwa fidia juu ya hasara waliyopata, hadi sasa Serikali haijatoa taarifa ndani ya Bunge. Ningependa kufahamu taarifa hii itatolewa lini na kwa nini imechelewa kutolewa na hali sasa waathirika wa zoezi hilo wanaendelea kuteseka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nchi hii haina utaratibu na mpango rasmi wa matumizi ya ardhi wafugaji wamekuwa wakihama toka eneo moja hadi lingine hali hii itaendelea mpaka lini, umefika wakati sasa wa kuwa na majawabu juu ya uhamaji huu na kunusuru nchi na uharibifu wa mazingira.

Hata hivyo Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuwepo na jawabu juu ya kadhia, hii siyo sababu ya askari wetu kuchukua sheria mkononi kwa kuwaadhibu wafugaji kwa kuua mifugo yao kama ilivyotokea katika kijiji cha Kashishi Namalendi, Kata ya Ikuba, Wilayani Mpanda ng'ombe 65 waliuawa kwa kupigwa risasi kati ya tarehe 15 na 18 mwezi Mei 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata maelezo aidha, huduma za msingi na ugani kwa wafugaji hazipo au hazitoshelezi madawa na majosho pia. Hakuna utaratibu bora wa ukusanyaji wa maziwa kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natarajia Wizara inayo majibu ya hoja zangu na mkakati wa kuendeleza mifugo na uvuvi nchini na hususan mpango wa kusaidia wavuvi wadogo wadogo katika Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kuhusu msaada kwa wavuvi walioacha uvuvi haramu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1998 kulifanyika kampeni ya Kitaifa ya kukomesha uvuvi haramu katika Ukanda wa Pwani, Tanga, Dar es Salaam, Mafia, Kilwa, Lindi na Mtwara. Wavuvi 300 walipatikana Mtwara na wavuvi 100 walipatikana Lindi. Wavuvi hawa waliapa kuacha kabisa uvuvi haramu, lakini sasa wavuvi hawa hawajapata zana mbadala ili waweze kujiajiri. Je, Serikali inawasaidiaje? Tunaomba maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba *Speed Boat* kwa Lindi na Mtwara ili kuzuia wavuvi haramu wa nje na wa ndani, ni ahadi ya Serikali. Ahsante.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake lakini nina jambo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifugo mingi katika Wilaya ya Kibondo, siungi mkono hoja hii kwa sababu kumekuwa na mifugo mingi kwenye hifadhi ya Moyowosi hasa maeneo ya Busungu, Kifura, Mgongwe na maeneo ya Murungu. Pia mifugo mingi hii imeleta migongano ya wakulima na wafugaji. Napenda kupata majibu ni lini mifugo hii itaondoka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni uvuvi, ningependa kujua na kupata majibu kwa nini Serikali inazuia wananchi wa Kibondo kufanya uvuvi katika mabwawa kwenye maeneo ya hifadhi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja mpaka nipatiwe majibu haya na kauli ya Serikali.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuwachimbia wafugaji mabwawa ya maji kwa ajili ya mifugo yao. Wilaya ya Nkasi ina ng'ombe wengi sana lakini wakati wa msimu wa kiangazi ng'ombe wanasumbuka sana na wafugaji wanazidi kufuata mito na wanachangia kuharibu vyanzo vya maji katika Wilaya yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi ndiyo balaa tupu kila mvuvi lazima awe na leseni na mtumbwi uwe na leseni, nyavu ziwe na leseni na wanasumbuka sana maana hata uvuvi wao wa kizamani hawapati chochote, hali yao wavuvi ya tangu miaka ya 1960 mpaka leo ni ile ile, naiomba Wizara yako kuwatolea hizo leseni maana hawana wanachopata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nakuomba wewe au Naibu wako watembelee mwambao wa Ziwa Tanganyika hasa katika Miji ya Kirando au Kabwe katika Wilaya ya Nkasi Kaskazini kwa macho yako hali ya wavuvi hao wana hali mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MHE. KULTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuleta hotuba ya Wizara hii katika Bunge lako Tukufu ili nasi tupate kuchangia. Nami napenda kuchangia katika vipengele vifuatavyo:-

Kwanza, migogoro kati ya wakulima na wafugaji. Serikali mwaka 2008 ilihamisha mifugo kutoka Ihefu kuja Rufiji na yalipangwa maeneo maalum kwa ajili ya wafugaji kama vile Loliondo–Chumbi, Siasa–Utete, Mbilinganye, Ngorongo, Bungu, Kipugira na kadhalika na Serikali iliahidi kujenga miundombinu kama vile malambo, majosho, shule, mitego ya kuulia mbung'o na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hadi leo Serikali imeshindwa kutimiza ahadi yake kwa kiasi kikubwa hivyo kusababisha wafugaji kuhamia katika Vijiji kama vile Umwe, Mgomba na eneo la Bonde la Mto Rufiji ambalo ni maalum kwa shughuli za kilimo, hivyo, kusababisha mwingiliano baina ya wafugaji na wakulima ambao unasababisha migogoro. Kwa mfano, kuna baadhi ya wakulima wamepata majeraha baada ya kupigwa na wafugaji na pia kuna Mzee wetu amepoteza maisha baada ya kupigwa na wafugaji, Mzee Abdulrahman Mtibo na kesi ilifikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Rufiji tulipangiwa kupokea mifugo 45,000, lakini hadi sasa takwimu zinaonesha kuwa tuna mifugo zaidi ya 200,000. Je, Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani na wakazi wa Wilaya ya Rufiji kama si kukuza migogoro kati ya wakulima na wafugaji? Kwani idadi ya mifugo imekuwa kubwa kuliko eneo la malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia wafugaji wengi wanaoendelea kuja Rufiji hawana vibali halali vya kuingiza mifugo yao, je, huu si ukiukwaji wa sheria? Mapendekezo na ushauri wangu ni kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ihakikishe inachukua hatua za haraka kutuma timu ya kwenda kuangalia hali ilivyo tete ili wananchi wa Rufiji wasiendelee kupigana na wafugaji kama ilivyo sasa.

(ii) Serikali ihakikishe inatimiza ahadi ya kutengeneza miundombinu katika maeneo maalum yaliyotengwa ili kusiwepo na mwingiliano kati ya wakulima na wafugaji katika eneo la bonde la Mto Rufiji ambalo ni eneo maalum kwa shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni uvuvi. Tanzania tumejaliwa kuwa na ukanda mrefu wa Bahari na mshiriki katika maziwa makuu matatu ambayo ni Victoria, Tanganyika na Nyasa na tuna utajiri mkubwa wa samaki katika bahari na maziwa haya, lakini leo hii Tanzania inaagiza samaki kutoka nje ya nchi na hatimaye tunaambulia kuletewa samaki wenye sumu kama hawa walioingia kutoka Japan na hatimaye kuzorotesha afya za Watanzania. Je, Serikali imeshindwa kuwasaidia wavuvi wa Tanzania kupata vitendea kazi vya kisasa ili kwenda kuvua bahari kuu na kuwaacha wageni kuvua samaki wetu kwa njia haramu kama vile kutokuwa na leseni halali na kusababisha nchi yetu kukosa mapato?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ushauri na mapendekezo:-

(i) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe kwa wingi mikopo ya masharti nafuu kwa wavuvi na wananchi wengine wenye nia ya kujiajiri kwenye sekta hiyo kwa ajili ya kununulia vifaa vya kisasa vya uvuvi na hifadhi na kuanzisha ufugaji wa samaki katika maeneo mengine ya maziwa ukiacha ukanda wa Pwani tu.

(ii) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha shughuli za doria katika maeneo ya uvuvi ili kuhakikisha kuwa wavuvi wachache hawaendelei na utaratibu wa uvuvi unaoharibu mazingira na kuleta mangamizi makubwa kwa samaki na viumbe wengine wa majini. Ahsante.

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kuipongeza Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Pia naomba nichangie upande wa mifugo hasa mashamba ya ufugaji wa kuku hususan kuku wa kienyeji. Mkoa wa Singida hasa Iramba Mashariki, ni wafugaji wa kuku wa kienyeji ambao hutoa soko la ajira kwa wakulima na vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa, Serikali haijatambua umuhimu wa wanyama hawa. Madawa ya kuwasaidia wakulima hawa hakuna, wanafuga bila usimamizi wa wataalam wala madawa ya chanjo ya kuwatibu hawa kuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara hii iwatazame wafugaji wadogo wadogo ili waweze kuinua soko na kuongeza kipato chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa kutokana na soko huria kila mtu anauza madawa ya mifugo, awe na utaalam au hana anatembeza kwenye magulio. Hii ni hatari sana kwani dawa hizo za wanyama zinahitaji wataalam sawa na za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara na Serikali irejeshe tena utaratibu wa kuwasaidia wafugaji wafuge wanyama ambao wataongeza pato lao. Sasa kila mkulima anahitaji kuboresha kilimo kwa kuongezea na ufugaji mdogo wa ng’ombe mbuzi, nguruwe, kuku na kadhalika kwani anaboresha lishe ya familia yake na kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna nchi zinazoongeza pato la Taifa kwa wanyama hawa wadogo wadogo. Tusipuuze hata ufugaji wa kuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. HUSSEIN NASSOR AMAR**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nasikitika kuwa, kitabu cha bajeti kimetusahau wafugaji wa Jimbo la Nyang’hwale kwa vipaumbele vyote. Kama mabwana, malambo, majosho, soko la ngozi na ng’ombe wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna bwawa kubwa huko Nyamgogwa, Kata ya Shabaka, linahitaji kusafishwa na ukarabati mkubwa. Kuna bwawa kubwa Nyang’hwale, Kata ya Nyang’hwale lilibomoka na kumwaga maji yote karibu miaka 15 iliyopita, linahitaji ukarabati mkubwa. Kuna lambo kubwa eneo la Kitongo, Kata ya Kakora, linahitaji ukarabati mkubwa. Kuna lambo kubwa eneo la Khalumwa, Kata ya Khalumwa, linahitaji ukarabati mdogo wa kusafishwa tope tu. Kuna lambo kubwa eneo la Bulangale, Kata ya Bukwimba, linahitaji ukarabati mdogo tu. Naomba Wizara ituangalie kuturekebishia haya ili mifugo yetu ipate maji na pia binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu majosho. Majosho hayatoshi na yaliyopo hayafanyi kazi sababu maji hakuna kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu dawa za mifugo, hazitoshi kwani zipo chache zikipatikana zinauzwa kwa bei ya juu sana na Maafisa mifugo waliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hoja hii. Naipongeza Wizara kwa hotuba nzuri ambayo imeambatana na takwimu mbalimbali ambazo zitasaidia katika ufuatiliaji. Baada ya maelezo yangu hapo juu, naomba nichangie yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze kuchangia kuhusu samaki wenye mionzi. Taifa kupitia vyombo vya habari wametangaza kuingizwa shehena za samaki toka Japan ambazo inasemekana zina sumu ya mionzi. Madhara yake ni kuwa walemavu na kutoa mimba. Je, ni kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kuhusu mgogoro wa ardhi. Wafugaji wanahitaji ardhi ya kutosha tena kubwa. Hii ni kwa sababu baadhi yao kwa makabila mbalimbali kama Wasukuma, Wagogo na Wamasai wana ng'ombe wengi, tena wengi sana kwa maelfu. Wafugaji hawa wanabaki kuhamahama bila milki ya ardhi ya machungo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iwatengee maeneo rasmi ya malisho kwa mifugo yao. Pili, wawachimbie malambo au mabwawa ya kutosha katika maeneo yao wanayoishi. Tatu, majosho kwa ajili ya mifugo yao yajengwe mengi kwa kinga ya mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa kuleta hotuba nzuri sana ya bajeti ya Wizara hii. Pia nawapongeza watendaji wote wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi naomba nitoe maoni yangu machache kuhusu hotuba ya Waziri. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 na ya 2010 imekuwa ikiongelea kuhusu uzalishaji wa mifugo bora kwa njia ya uhamilishaji *(Artificial Insermination)* na madume bora. Nia na madhumuni ni kuwapatia wafugaji mbegu bora za mifugo hasa ng'ombe bora wa maziwa na nyama. Napongeza juhudi za Serikali za kuanzisha Kituo cha Uhamilishaji cha Usa River, Arusha eneo la Tengeru. Huu ni mwanzo mzuri lakini jambo la kusikitisha kituo chetu cha uhamilishaji hakijakidhi haja hata kidogo. Mwaka 2008 nilipata mbegu zaidi ya mia mbili (200) nilipandisha ng'ombe zaidi ya mia moja kwenye shamba langu huko Karagwe lakini kwa bahati hakuna ng'ombe hata mmoja aliyepata mimba. Hali hii ilinivunja moyo sana mimi na wananchi wangu wote wa jimbo la Karagwe ambao walitamani kujifunza kutoka kwa Mbunge wao. Hadi leo hii sijajua tatizo lilikuwa nini. Hadithi kama hii iko sehemu mbalimbali za nchi hii. Hoja inayotolewa na wafugaji wengi ni kwamba kituo cha Arusha (*NIC*) hakina mitambo mizuri ya kisasa kwa ajili ya kutunzia mbegu bora. Serikali ilifanyie kazi suala hili kwa haraka iwezekanavyo kwani wafugaji wanahangaika kufuata mbegu Kampala (Entebe), Nairobi, Botswana, Afrika Kusini, Uholanzi na kadhalika kwa wale wasiokuwa na uwezo wanaishia kuzalisha mifugo isiyo na ubora wowote hivyo kudumaza kipato cha wafugaji wetu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu chanjo ya *FMD*. Ugonjwa wa miguu na midomo ya ng'ombe ni tishio kwa wafugaji. Chanjo hii ni ya ghali sana kiasi kwamba wafugaji wengi hawaimudu kuinunua. Ni kwa nini Serikali haitoi ruzuku au bure kwa wafugaji chanjo hizi muhimu. Bila chanjo muhimu kama hizi mifugo itakufa na haiwezi kupata soko la nje. Kwa hali hii Kilimo Kwanza hakitawanufaisha wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera hasa Wilaya ya Karagwe, Muleba, Ngara na Biharamulo zimevamiwa na wahamiaji haramu kutoka Rwanda na Uganda wakiingiza mifugo mingi katika nchi yetu bila kibali maalum. Wahamiaji haramu hawa wamechukua malisho yote kwa ajili ya mifugo yao na kuwafanya wafugaji wazalendo kukosa malisho ya mifugo yao. Hawa wahamiaji haramu wanawapiga na kuwaua Watanzania wenzetu kisa wanajifanya hii ni nchi yao, wao ndio wenye haki. Kwa nini Serikali haiwadhibiti watu hawa, kuwaondoa na kuwarudisha kwao, wao wenyewe na mifugo yao? Mwaka 2006/2007 Serikali iliendesha zoezi la kukamata na wahamiaji haramu na mifugo yao, wengi wao walirudishwa kwao na mifugo yao na hiyo Karagwe kupata malisho angalau kwa kipindi cha miaka kama mitatu hivi. Sasa wahamiaji haramu hao na mifugo yao wamerudi kwa kasi ya ajabu! Hadi wanaua wananchi wetu na kutuibia mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo Raia wengi wa Rwanda wanaoishi Rwanda na ni watumishi wa Serikali ya Rwanda lakini wanafuga mifugo yao nchini Tanzania. Ni kwa nini Serikali inakaa kimya na kuruhusu nchi yetu inaporwa na wageni na kufanywa shamba la bibi? Serikali

iache woga, iache kuwaogopa raia wa kigeni, iamke ilinde rasilimali za nchi yake kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wa mifugo walio kwenye Kata hawana tija yoyote. Hawatembelei wafugaji, hawatoi ushauri bali huonekana siku ya kutoza fedha za chanjo ya mifugo, baada ya hapo hupotea. Je, ni nini sababu za wao kuwepo. Kwa nini walipwe kwa kazi ambayo haimnufaishi mfugaji. Kama Wizara ya Mifugo kimuundo haiwezi kuwapa maelekezo mazuri kwa kuwa wako TAMISEMI, jambo hili liangaliwe vizuri maana hawana la maana wanalolifanya kuendeleza mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanda vya Maziwa na Nyama vinahitajika, Serikali itutafutie wawekezaji waje wawekeze kwenye viwanda vya nyama na maziwa. Serikali iingilie haraka fukuto la mgogoro wa wafugaji na wakulima Kata ya Kihanga Wilayani Karagwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua jitihada nzuri ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya kukomesha uvuvi haramu na mimi kama sehemu ya uongozi wa nchi hii naunga mkono hizi jitihada. Katika utekelezaji wa azma hii kuna mtindo wa Maafisa Uvuvi kwa kushirikiana na Polisi kufuata samaki sokoni na kunyang'anya wauzaji kwa kisingizio kwamba ni samaki wadogo na lazima wachukuliwe kukomesha uvuvi haramu. Je, Serikali haioni kwamba ni muda muafaka wa Serikali kukomesha tabia hii inayoweza kusababisha fujo masokoni na badala yake kujikita katika kuzuia uzalishaji wa zana haramu katika viwanda na kukamata wavuvi kwenye mialo wanaovua na kuuza samaki wadogo chini ya kiwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kauli ya Serikali kuhusu kukomesha tabia hii.

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina changamoto chache juu ya uvuvi ambazo naomba Wizara izitilie maanani na kuzitolea majibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mfumo wa leseni ya uvuvi una matatizo yafuatayo:- Leseni ya mtumbwi ikitozwa Wilaya moja tena hutozwa leseni, mtumbwi ukienda Wilaya nyingine ndani ya mwezi huo huo. Mbona magari hukata leseni moja tu na hata gari liende Wilaya yoyote ndani ya nchi linatumia leseni hiyo hiyo. Mfano, Mtumbi Na. *BME* 2900 ulikatiwa leseni ya mtumbwi Irugwa Wilaya ya Ukerewe mnamo 9/2/2011 kwa stakabadhi Na.HW5 Na 713766 kwa Sh.75,000?= ambapo na leseni ya uvuvi pamoja na leseni ya wavuvi watano zililipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo 3/6/2011 mtumbwi huo kutokana na utafutaji wa samaki ndani ya Ziwa Victoria ulikwenda Kayenze, Wilaya ya Ilemela na kulipia leseni ya mtumbwi, leseni ya uvuvi na wavuvi watano upya Sh. 75,000/= kwa Stakabadhi Na. *MCC/GRR/A* 341941. Mfumo huu uliathiri pia mtumbwi Na. *TZMUK* 147 kwa kulipia leseni Irugwa, Wilayani Ukerewe Stakabadhi Na. *HW5* 692848 ya 78,000 mnamo 9/1/2011 na ulipokwenda Kayenze Wilayani Ilemela mnamo 3/6/2011 ulilipa tena Sh. 75,000/= kwa stakabadhi Na. *MCC/GRR/A*341940. Naamini utakubaliana na mimi kuwa huu mfumo siyo mzuri. Nauliza mbona muuza duka halipiwi leseni? Naomba maelezo ya kina kwa nini mfumo huu wa leseni usifutwe?

Pili, Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri leseni za uvuvi wa wavuvi wadogo zisiwe katika viwango vya dola za Kimarekani kwani kutokana na kuporomoka kwa shilingi yetu kila kukicha wavuvi hawa huingia hasara kubwa. Tutumie fedha zetu na hili litolewe kauli ya Serikali katika mkutano huu.

Tatu, Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Ziwa Victoria nako tunahitaji mradi kama wa *MACEMP* wa kubadilishana zana haramu kwa zana halali kama ambavyo imefanyika katika bahari na ukanda wa Pwani.

Nne, Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mikopo kwa wavuvi umekuwa wimbo wa porojo za kila bajeti mwaka hadi mwaka. Wavuvi wapi wamewahi kupata mkopo? Mbona wavuvi wa Mwibara hawapati mkopo? Naomba maelezo ya kina vinginevyo hakitaeleweka.

Tano, Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuongezeka kwa samaki ndani ya Ziwa kwa nini wavuvi wakubwa wasipewe leseni zenye ukomo wa idadi ya tani ili tusi-*overfish*?

Sita, Mheshimiwa Mwenyekiti, kupungua kwa samaki ndani ya Ziwa Victoria kwa nini kunahusishwa na uvuvi haramu kwa kiasi kikubwa kuliko athari zitokanazo na mabadiliko ya tabia nchi na uvuvi usio na ukomo. Dhana hii imeifanya Wizara kutumia fedha nyingi sana zikiwemo doria zisizo na tija kupambana na uvuvi haramu. Naomba maelezo ya kina juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. MWIGULU L. NCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kupongeza Serikali kwa umakini mkubwa na dhamira ya dhati ya kuendeleza sekta ya mifugo na uvuvi. Hii imedhihirishwa na kupunguzwa kwa kodi katika nyuzi za kuvulia. Kadhalika mazingira ya uvuvi yanapoboreshwa yanasaidia watu wengi kujihusisha na shughuli hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali kuboresha taratibu za kiutawala yaani katika maeneo ya uvuvi kusiwepo na unyanyasaji wa wavuvi usio na tija wala ulazima unaofanywa na baadhi ya wahusika kwa maslahi binafsi. Pia udhibiti wa zana za uvuvi zilizo haramu udhibitiwe kuanzia zinapotengenezewa na uuzwaji au usambazaji wake ili kupunguza migogoro inayotokea dhidi ya Serikali na wavuvi. Upande wa mifugo ni vema kero ya matumizi ya ardhi ikatatuliwa kuondoa athari zinazoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, upatikanaji wa maji ni muhimu sana, hivyo ni lazima mabwawa yachimbwe kwa ajili ya maji. Bei za mifugo ni lazima zilindwe isishuke kiwango cha kuwafanya wafugaji wasipate hasara. Vilevile wataalam wa mifugo warudishwe ngazi ya vijiji ili kutibu mifugo inapopatwa na magonjwa. Majosho yatengenezwe na yaliyoharibika ya kukarabatiwa ili kutoa huduma za matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. RASHID ALI OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa dhati kuniwezesha kuwepo katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima ya Bunge lako, sasa naomba nichukue nafasi hii ili nichangie kwa njia hii ya maandishi kwa baaadhi ya maeneo ya hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sekta ya Mifugo. Nianze na Maziwa. Matumizi ya maziwa bado yako katika kiwango cha chini kwa takwimu zinavyoonyesha. Mtanzania kwa mujibu wa Shirika la Chakula (*FAO)* inashauri unywaji wa maziwa lita mia mbili (200) kwa mtu mmoja kwa mwaka. Lakini takwimu za wataalam zinaonesha mtu mmoja anakunywa lita 44 tu za maziwa, jambo ambalo ni kiwango kidogo sana kutokana na umuhimu wa maziwa kwa mpango wa lishe ya mwanadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu huu unasababishwa na mambo mbalimbali bei kubwa ya maziwa, uhaba wa Viwanda vya Kusindikia Maziwa na kutokuwepo miundombinu ya kufikisha maziwa kwenye masoko. Naishauri Serikali mambo yafuatayo:-

(a) Bajeti ya Wizara iongezwe ili shughuli zake ziende kwa uhakika

(b) Wizara hii haijitegemei kutokana na Serikali kutoa fungu dogo kwenye bajeti kwa kutegemea sana fungu la ruzuku kutoka mashirika ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maziwa na bahari zetu, tunao samaki wengi, lakini la kushangaza tunafanya biashara na nchi nyingine kutuuzia samaki. Kwa mfano, samaki aina ya Vibua kutoka Afrika ya Kusini, samaki hawa katika bahari yetu wapo wa kutosha badala yake tunakuza uchumi wa wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wavuvi wetu wananyanyaswa ndani ya nchi yao kwa kukosa kuendelezwa:-

- Hakuna utaratibu wa kupewa mikopo nafuu ya fedha taslimu ya kujiendeleza;

- Hapana mikopo ya vyombo na zana nyingine za uvuvi jambo ambalo ni sehemu moja ya kupunguza wimbi la ukosefu wa ajira hapa nchini petu;

- Serikali inawatoza kodi wavuvi wadogo wadogo badala ya kutozwa leseni ya vyombo vya uvuvi; na

- Wavuvi wadogo wadogo wenye kujitafutia riziki zao, zana zao kupigwa moto na walinzi kwa madai ya kuwa wanaharibu mazingira, lakini wawekezaji wa nje ya nchi hawachukuliwi hatua yoyote wanapoharibu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvuvi haramu. Ziko meli nyingi kubwa zinavua katika bahari yetu kuu, lakini hakuna ulinzi wowote unaofanyika. Wavuvi hao wanahamisha samaki na mali nyingi nyingine za baharini wala hakuna hatua zozote zinazochukuliwa za ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naishauri Serikali, wavuvi wetu wadogo wadogo walegezewe masharti ya sheria kwani wimbi kubwa la ukosefu wa ajira linapungua kutokana na bahari yetu na vilevile wavuvi wadogo wadogo wapatiwe mikopo ili wajiendeleze katika kujitafutia riziki zao. Ahsante.

**MHE. RITTA E. KABATI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Dokta David Mathayo; Naibu Waziri, Mheshimiwa Ole Nangoro; Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa hotuba nzuri aliyoisainisha hapa Bungeni.
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufafanuzi kwa mambo yafuatayo:-

Ujenzi wa machinjio ya Kata ya Mwangaza, Jimbo la Iringa Mjini. Mradi huu wa machinjio ulipo katika Kata hiyo. Mradi huo, Halmashauri ya Manispaa ya Iringa Mjini, Jimbo la Iringa ilileta andiko katika Wizara yako ya Sh. 600,000,000/=. Tayari Halmashauri imeshafanya ujenzi wa machinjio hiyo yenye gharama ya Sh.113,000,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe nimeshafuatilia na Mheshimiwa Waziri aliahidi kuja kutembelea machinjio, hivyo naomba leo nipatiwe jibu, naogopa machinjio hayo yasije kugeuka kuwa hofu kabla haijakwisha maana imeshachukua muda mrefu. Leo hii nisipopata jibu nipo tayari kushikilia mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja lakini nipatiwe jibu.

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanah Wataala* kwa ukarimu na rehema zake nyingi kwangu anazoendelea kuniruzuku, *Alhamdulillah*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imejaaliwa sana rasilimali ya mifugo na uvuvi. Tunao ng'ombe, mbuzi, kondoo na hata kuku wengi kiasi cha kushika nafasi ya tatu barani Afrika kwa kuwa na mifugo mingi baada ya Ethiopia na Sudan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na neema hiyo Serikali bado haijafanya juhudi za makusudi katika kuboresha maisha ya wafugaji kutokana na mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati umefika kwa Serikali kuyaona mapato yanayoweza kupatikana kutokana na mifugo. Serikali yenye machinjio ya kisasa ili kuongeza thamani ya nyama sambamba na kujenga Viwanda vya Kusindika nyama kwa ajili ya soko la Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja pia kwa Balozi zetu popote zilipo kutangaza ubora wa mifugo yetu, kutafuta masoko nje ya nchi kwa ajili ya kusafirisha nyama *fresh* iliyochinjwa na kufungwa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kuwa lipo soko kubwa la bidhaa za mifugo hasa nyama nje ya nchi. Tatizo ni miundombinu na elimu kwa wafugaji ili nyama iwe katika viwango vinavyokubalika Kimataifa hasa kuepusha mifugo na maradhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi ni neema nyingine aliyotujaalia Mwenyezi Mungu ambayo Serikali haijaipa umuhimu. Ni aibu kwa sekta ya uvuvi kuchangia asilimia moja ya pato la Taifa (1%) wakati nchi yetu imezungukwa na Bahari kubwa ya Hindi, Maziwa makubwa, Mito na kadhalika. Ipo haja sasa Serikali kuweka nia, azma na dhamira ya dhati kuinua sekta ya uvuvi nchini ili kuinua vipato vya wavuvi na nchi pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya Serikali kuwakamata na kuwanyang'anya zana zao za uvuvi wavuvi wadogo wadogo, sasa iwapange, iwape elimu na iwapatie vifaa bora zaidi vya uvuvi, aidha, kwa kuwapa misaada au kuwakopesha. Wavuvi hawa wakipewa elimu na vifaa watavua kisasa na kuhifadhi mazingira. Faida itakuwa ni mara mbili, kupata samaki wengi na kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, samaki ni chakula bora kabisa na hivyo ni biashara isiyokosa mnunuzi!! Wavuvi wetu wajengewe uwezo ili kuinua vipato vyao na kupunguza umaskini. Uvuvi ni uchumi! Rasilimali kubwa ya samaki iko katika uvuvi wa bahari kuu. Wakati umefika sasa Serikali kuwajengea uwezo wavuvi wetu wazalendo ili wavue katika bahari kuu na kuongeza pato lao, pato la Taifa na pia kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa zilizopo ni kuwa kuna meli 70 zinazovua bahari kuu, meli hizi zinavua wastani wa tani mbili hadi tano kwa siku. Hii maana yake ni kuwa meli hizi zinavua wastani wa tani milioni mia za samaki (100,000,000) *M/Tons.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni mali nyingi sana ambayo haitoi mchango kwa uchumi wa Taifa letu bali unanufaisha Mataifa yanayoleta meli zao kuvua. Thamani ya samaki ni zaidi ya 500,000,000,000/=! Ni aibu kwa Taifa, utajiri huu kuvunwa kiholela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ada ya leseni wanazolipishwa wavuvi hawa wageni ni kidogo sana. Naishauri Serikali itoze ada ya leseni ya dola za Marekani 60,000 mpaka 80,000 kwa mwaka, wakati Serikali ikijipanga kuwapa wazalendo uwezo sekta ya uvuvi wa bahari kuu. Kwa kuwawezesha wazalendo wavue kisasa kwenye uvuvi mdogo na wa bahari kuu kutasaidia nchi yetu mambo mengi ikiwa ni pamoja na kuinua vipato vya wananchi wetu, kuinua pato la Taifa, kuongeza lishe bora ya samaki kwa wananchi wetu, kuongeza ajira kwa vijana wetu na haya yatachangia kwa kiasi kikubwa kudumisha amani na utulivu wa Taifa letu, kwani wananchi watakuwa na imani kubwa zaidi na Serikali yao. Na pia itasaidia kuhifadhi mazingira yetu mazuri ya bahari yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Mchango wangu uko katika uvuvi wa Bahari kuu, kwanza mapato yanayopatikana katika uvuvi wa Bahari kuu ni kidogo sana katika kusaidia uchumi wa Taifa letu kwa kawaida nchi nyingi zinazotoa leseni za uvuvi wa Bahari kuu lazima katika nchi inayotoa leseni iwe na Kiwanda cha Samaki ili kila wanapokwenda kuvua bahari kuu inabidi samaki warejeshwe kwenye hicho kiwanda ambacho kiko kwenye ile nchi iliyotoa leseni hii inasaidia kujua samaki wa tani ngapi zimetoka kwa ajili ya uvuvi wa Bahari kuu. Pili, katika meli zinazofanya shughuli za uvuvi wa Bahari kuu zinatakiwa na wafanyakazi wazalendo, baadhi ya nchi zinashurutisha wawe wafanyakazi nusu kwa nusu, hii inasaidia kupatikana ajira kwa wazalendo ambao hao wanasaidia pia katika uangalizi wa uvuvi huo.

Tatu, kuwa na Afisa mmoja wa Idara ya Uvuvi katika kila meli iliyopewa leseni maana itasaidia kujua samaki gani wanaovuliwa. Pia kwa vile samaki wote waliovuliwa wanarejeshwa nchini kwanza watachukuliwa samaki waliowataka kwenye leseni zao na waliobakia watatumika katika soko la ndani, ambalo litasaidia kupunguza mahitaji ya samaki humu ndani, haya yakifuatwa katika nchi yetu yatasaidia kuongeza mapato ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mikoa ambayo imeathirika na utendaji mbovu wa watendaji wa Wizara hii ni Mkoa wa Morogoro. Mkoa wa Morogoro ni wa wakulima, lakini baada ya Serikali kuruhusu wafugaji kuingia Mkoa huo na mifugo yao bila utaratibu, maandalizi ya miundombinu pia upimaji wa ardhi na kuwaelekeza mahali pa kupeleka mifugo hiyo. Serikali imeruhusu kiholela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya wafugaji na wakulima ni ya miaka mingi na inasababishwa na watendaji wa Serikali. Mauaji na umaskini unaowapata wakulima na wafugaji wa kulaumiwa ni Serikali na inapaswa kuwajibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe tamko kuhusu mauaji yaliyotokea Wilaya ya Kilombero katika Kata ya Chita na Chisano ambapo Mkuu wa Wilaya ya Kilombero kumtuma Mtendaji wa Serikali akawaamuru wafugaji waondoke, matokeo yake mtendaji huyo ameuawa na wanaosemekana ni wachungaji. Je, Serikali inatoa kauli gani? Inangoja hadi watu wangapi wauawe ili waokoe maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mabwana Samaki huenda sokoni na barabarani kukamata wauza samaki kwa kisingizio, ni samaki wadogo na wamevuliwa kwa makorokoro. Je, kwa nini Maafisa hao wasiwakamate wanaoingiza nyavu hizo na badala yake kuwakandamiza walala hoi hasa akinamama wanaobangaiza kwa biashara ndogondogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke mipango madhubuti ya kuandaa miundombinu ya wafugaji na chumvi.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niipongeze Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa kazi ngumu wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu mnayoitoa kwenye *T.V* na redioni haitusaidii sana sisi watu wa Rukwa, tunahitaji wataalam waje *Site* waone kwanza tulivyofanya na kisha watuelekeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabwawa ya samaki yako mengi na samaki ni wengi mno wasioweza kuingia sokoni kwa sababu ya kuchomana wao kwa wao na kisha hudhoofika, mjini hatujui hata jinsi ya kuvua kwenye mabwawa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Rukwa tuna Ziwa Tanganyika na Ziwa Rukwa lakini samaki wengi hupelekwa Burundi, Zaire na Zambia na hivyo kufanya kipato cha Serikali kushuka na kutoa taarifa isiyo sahihi ya samaki wakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Rukwa naamini ni Mkoa wa watu maskini hata ufugaji wa kuku haupo isipokuwa kuku waliopo wanaishi kwa mpango wa Mwenyezi Mungu tu. Naiomba Serikali yako kuelekeza nguvu Rukwa kwa mafunzo zaidi ya ufugaji na hasa kwa akinamama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa Hotuba nzuri ambayo imelenga kuinua mchango wa mifugo na uvuvi kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi ya tatu Barani Afrika kwa wingi wa mifugo hususan ng'ombe lakini mchango wake katika pato la Taifa haulingani na wingi huo. Je, Serikali

ina mkakati gani wa uhakika ili sekta ya mifugo iweze kuchangia kwa kiasi kikubwa katika pato la Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti ni muhimu katika kuleta maendeleo endelevu na kuongeza tija katika uzalishaji. Hata hivyo, utafiti katika Wizara hii ni kitengo kidogo sana na ambacho hakijitegemei (*Non-autonomous*), itakumbukwa vile vile kwamba, katika mkutano wa watafiti wote uliofanyika *Kunduchi Beach Hotel*, Dar es Salaam tarehe 18-19/03/2010 chini ya Uenyekiti wa Waziri Mkuu, moja ya maazimio ilikuwa ni kuanzisha upya *TARO* na *TALILO* ili utafiti uweze kuchangia vizuri katika sekta za kilimo na mifugo. Je, Wizara imefikia wapi katika azma hii?

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie hoja ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Wizara hii kwanza ina Bajeti ndogo sana kuliko mahitaji ya Wizara. Naishauri Serikali iweze kutenga bajeti ya kutosha ili iweze kwenda na hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia juu ya migogoro ya wakulima na wafugaji. Eneo hili lisipoangaliwa vizuri tutasababisha maafa makubwa sana kati ya wakulima na wafugaji, ni vema Serikali ikachukua hatua za dharura kuhakikisha kunatengwa maeneo ya wafugaji ya kulishia mifugo yao kuliko ilivyo sasa, maeneo ya wakulima yanatumika na shughuli za ufugaji jambo ambalo linaleta sana migogoro ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Serikali iwaandalie wafugaji kwa kuwachimbia mabwawa, malambo na majosho sambamba na madawa ya mifugo. Kwani wafugaji wakitengewa maeneo yao na kuandaliwa miundombinu hiyo ya mabwawa, malambo, majosho na madawa wataacha tabia ya kuhamahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali katika Jimbo la Mpanda Vijijini nina matatizo ya ukosefu wa malambo na majosho katika Kata ya Mpandandogo, Kabungu, Katuma, Mwese na Ikola, maeneo haya tunaomba sana huduma hii ielekezwe kwani kuna mifugo mingi na mahali pa kunyweshea mifugo hakuna. Endapo Serikali itawasaidia kuchimba malambo katika Kata hii mtakuwa mmewasaidia sana wafugaji hawa wanaotangatanga kwa ajili ya kufuata malisho na mahali pa kunyweshea mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uvuvi halijapewa msukumo mkubwa kwani katika eneo la Jimbo langu la Mpanda Vijijini kuna Ziwa Tanganyika ambako kuna shughuli za uvuvi. Lakini uvuvi uliopo Ziwa Tanganyika ni mdogo mdogo na hauna mafanikio ya kumsaidia mvuvi. Kwani Ziwa Tanganyika lina kina kirefu zaidi kwenda chini ukizingatia kuwa ziwa hili linapitiwa na bonde la ufa. Hivyo, kuifanya shughuli ya uvuvi katika eneo hili kuwa ya kusuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali kuwasaidia wavuvi hawa wa Ziwa Tanganyika kwa kuwapa mikopo ya kununulia zana za uvuvi, ambazo zitawasaidia wavuvi wadogo wadogo ambao ndio shughuli zao huko ziwani. Vile vile lazima tuwasaidie wavuvi wa Ziwa Tanganyika kuwaunganisha katika vikundi vya ushirika ili waweze kukopesheka na vyombo vya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ina utajiri mwingi kwa sababu ya mifugo mingi iliyo nayo na eneo la Bahari na Maziwa Makuu kama Ziwa Victoria Tanganyika na Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tatizo ni wafugaji kutokuhamishwa ipasavyo ili kufanya biashara na mifugo waliyo nayo. Nashauri Serikali itunge sheria, iwatake wafugaji kuwa na kiwango fulani cha mifugo, ili awe na kiwango cha kuweza kuhamilishwa ili apate ng'ombe bora au anenepeshe ili kupata *beef* nzuri ambayo anaweza ku-*export* nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Serikali ihamishe wafugaji hawa wapewe wigo wa biashara (*diversity*), wafanye biashara mfano, *Real Estate*, badala ya kuhodhi ng'ombe wengi wasiokuwa na faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nashauri Serikali iwasaidie wafugaji kwa kujenga Viwanda vya Nyama kikanda hasa Mikoa ya Shinyanga, Tabora, Mwanza na Arusha. Hii itasaidia kuuza nyama ndani na nje ya nchi na itaongeza thamani ya nyama. Linaweza kufanyika kwa kushirikiana na sekta binafsi (*PPP*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, Serikali ihamasishe na kutoa elimu *seriously* kuhusu faida za ngozi na wafugaji wapewe elimu ya kutokuweka alama katika miili ya mifugo ili kutoharibu ngozi. Serikali pia ijenge viwanda vya ngozi (ifufue viwanda vya ngozi mfano, Kiwanda cha Ngozi, Mjini Moshi – Kilimanjaro), ili ngozi zisiuzwe *raw* badala yake ziwe tayari zimesindikwa na hivyo zitakuwa na thamani zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, Serikali isaidie kuboresha Viwanda vya Maziwa. Badala ya wafugaji kuhangaika kupata soko la maziwa, maziwa haya yauzwe katika viwanda vyetu, viwanda hivi vitengeneze pia siagi (*butter*) na jibini (*cheese*). Hili na la viwanda vya ngozi linaweza kufanyika kwa kushirikisha sekta binafsi (*PPP*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, Serikali iendelee kuweka doria na sheria kali zichukuliwe kwa wavuvi wanaotumia makokoro na *net* za mbu kuvua samaki katika mabwawa. Mfano, ni uvuvi unaofanyika Bwawa la Nyumba ya Mungu Mkoani Kilimanjaro, katika Wilaya ya Mwanga. Muhimu kanuni na sheria zifuatwe ili samaki waweze kuuzwa na kuinua kipato cha mvuvi na wananchi wengine. Serikali pia ilinde *Deep Sea Fishery* na wageni walipie vibali vya kuvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, ipo pia haja Maziwa kama Jipe (Wilayani Mwanga) ambayo yameachwa yakajaa magugu, ziwa hili lililo *shared* na Kenya. Upande wa Kenya ziwa ni jeupe halina magugu. Serikali (Wizara ya Mifugo na Mazingira) walifanyie kazi, Ziwa hili liwe msaada kwa kuwapa kipato Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke mkazo matunzo ya maziwa mengine yote nchini yawe ni kipaumbele ili kuyanusuru na mazingira mabaya na wahalifu wa makokoro. Nashauri Serikali iendelee na mkakati wa kuwakamata wahalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAKIA H. MEGHJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Wizara hii ningependa kuchangia katika sekta ya uvuvi. Pamoja na pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na wataalam wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma Tanzania imekuwa ikisafirisha minofu ya samaki nje hasa nchi za Europe na hii ilikuwa inachangia fedha za kigeni. Hivi sasa hakuna hata ndege moja inayotua pale Mwanza. Wenye Viwanda vya Samaki husafirisha mazao kwenda Kenya, kwa maana hiyo, sehemu kubwa ya uchumi huu unanufaisha nchi jirani. Wizara iliangalie suala hili na nashauri Wizara ifanye kikao na wawekezaji wote wa samaki. *MACEMP* umekuwa ni mradi wenye manufaa makubwa hasa kwa wananchi wa kipato cha chini na kati, kwa hiyo hivi sasa kufanya tathmini ya mradi huu kwa nia ya kuimarisha *MACEMP II.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ushirika wa wavuvi lazima nalo litiwe mkazo ili kuwasaidia wavuvi hasa wavuvi wadogo wadogo. Kuna haja pia, kwa Wizara kama wataalam hawajafanya hivyo waende kujifunza Maldives. Mfano, leseni za *Deep Sea Fishery* hazitolewi kwa watu ambao si raia wa huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. STEPHEN N. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Wizara hii naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja ila kuna matatizo kwenye mifugo, ni lini wafugaji waliokuja kwenye Jimbo langu wataondoka. Wapo kwenye Kata ya Makuyuni, Muyuzi, Kwagunda wameingia katika eneo hili na kuvuruga maeneo ya wakulima, wametoka Mkoa wa Arusha na Manyara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tatizo katika Mji wa Mombo hauna machinjio ya kisasa, naomba Serikali iangalie huu mji ambao unakuwa kwa kasi sana. Naomba Serikali iangalie

mji huu. Pili, kulikuwa na majosho kwenye maeneo ambayo hayapo kwa sasa, naomba lijengwe Josho Mswaha Darajani, Mnyizi na Mkomazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kukopa ng'ombe kwenye Jimbo langu haujafika kabisa, hivyo, naomba Serikali iangalie huo mradi kwa sababu wananchi wanaupenda. Nina ziwa ambalo lina samaki linaitwa Ziwa Manga. Naomba Serikali iangalie hiyo kazi ya bwawa na naomba nichimbiwe lambo kwenye Jimbo langu.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa fursa hii ili kuweza kuchangia bajeti ya Wizara ya Uvuvi ya mwaka 2011/2012. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ya kuhamasisha na kusimamia ufugaji wa kisasa na kudhibiti vitendo vya uvuvi haramu ili sekta ya mazao ya uvuvi kuwa endelevu. Ilani ya Chama cha Mapinduzi imeweka msisitizo wa kuimarisha mikakati madhubuti ya kuhakikisha wafugaji na wavuvi wanafuga kwa kutumia njia za kisasa ili wapate mazao bora ili kupata bei nzuri za mifugo yao na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini ni wadau wakubwa wa Wizara hii kwa maana wengi ni wafugaji na wavuvi katika Mto Ruvu. Mheshimiwa nipende kuchangia kwamba, kuna haja ya kuendelea kuboresha huduma inayotolewa na wataalam wa mifugo na uvuvi ya kutoa elimu ya ufugaji wa kisasa kwa kupunguza wingi wa mifugo ili waweze kuihudumia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa juhudi zake za kuimarisha mashamba ya kuzalisha mitambo na mbegu bora za uhamilishaji. Pia kutoa ruzuku ya dawa ya kuogeshea mifugo na kujenga au kukarabati majosho. Pamoja na juhudi zote hizo zinazofanywa na Serikali kuboresha sekta ya ufugaji lakini mifugo yetu haijaweza kupata soko la nje kwa kuwa haijafikia viwango vinavyotakiwa soko la nje, hata ranchi zetu za Ruvu na Kongwa zinatumia mifugo wanayotunza wenyewe, hawajanunua mifugo ya wananchi. Serikali yetu imeelimisha wataalam wengi katika sekta ya mifugo, pia tunacho Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine. Chuo hiki kina wataalam na tafiti nyingi sana zimefanyika kuhusu njia bora za ufugaji na jinsi ya kutunza mifugo kwa kiwango cha Mataifa. Wengi wa wataalam hawa wasomi wako maofisini na wanasikika tu katika makongomano na semina zinazowahusu wenyewe kwa wenyewe. Natumaini ni wakati muafaka sasa watalaam hawa waende vijijini waliko wafugaji na wavuvi kuwaelimisha njia bora za kutunza mifugo na uvuvi wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa duniani (*Global Climate Changes*) duniani kote mvua zimekuwa adimu sana. Wafugaji wetu wanategemea sana ufugaji wa kienyeji wa kuwa na mifugo mingi ambayo hawana uwezo wa kuwalisha vizuri. Kuna tatizo kubwa la ukame, hivyo, wafugaji wanategemea kuhamahama kutafuta maeneo yenye unafuu kidogo wa malisho. Katika kuhamishahamisha mifugo hii, wanaingia katika maeneo ya wakulima na kusababisha ugomvi wa kugombea ardhi katika ya makundi haya. Tatizo hili ni kubwa sana na liko katika mikoa mingi hapa nchini. Nashauri wataalam wa ufugaji wapelekwe vijijini kuwaelimisha wafugaji kupunguza mifugo yao na kuwaelekeza jinsi ya kufuga kwa njia za kisasa *(zero grazing).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mikakati hii ya kusaidia kuboresha ufugaji, Halmashauri ziainishe maeneo ya ufugaji na kufanya sensa ya mifugo iliyoko katika Halmashauri zao. Baada ya zoezi hili mifugo itafahamika iko mingapi na kupitisha sheria ya kila mfugaji awe na eneo kubwa kiasi gani na mifugo itunzwe namna gani. Kwa kufanya hivi kutasaidia sana wafugaji kupata malisho ya mifugo yao na kuzalisha mifugo bora bila usumbufu na itakuwa rahisi kupata soko lenye bei nzuri kwa mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi nyingine zinaweza kuchukuliwa kwa Serikali kufungua mashamba mengi ya majani bora ya malisho ili wafugaji waweze kuyanunua na kulisha mifugo yao. Hapa pia sekta binafsi inaweza kuhamasishwa kupewa ardhi ya kupanda majani ya malisho kwa ajili ya kuuza majani na mbegu ya majani kwa wafugaji. Mfano, katika Jimbo la Kibaha Vijijini kuna shamba la mfano la malisho ya Mifugo lililoko Vikuge. Eneo la shamba hili ni kubwa lakini

nasita kusema kwamba shamba hili halitumiki kikamilifu. Nashauri kwa kuwa ni shamba la mfano, basi litumike kufundisha wafugaji ili waweze kupata ujuzi wa kuanzisha mashamba ya malisho ya mifugo yao. Hii itasaidia pia kuondoa tatizo la ugomvi wa ardhi kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa uvuvi naipongeza sana Serikali kwa kuwa makini katika kuzuia ujangili unaofanyika wa uvuvi haramu katika maziwa, mito na bahari ambao ulikuwa unaathiri sana upatikanaji wa mazao ya uvuvi. Pamoja na kwamba samaki wanaopatikana katika nchi yetu lakini wana bei kubwa kiasi kwamba si wananchi wengi wanaweza kununua na kula samaki labda walioko katika maeneo ya uvuvi. Hii inachangiwa na kutokuwepo na uwezo wa wavuvi wetu kununua zana za kisasa za kuvua pamoja na njia za kuhifadhi samaki kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ingechukua hatua za kuona kwamba samaki ni chakula bora na hawana madhara kwa afya. Hivyo, kama sekta ya uvuvi ikiimarishwa kwa kuwawezesha wavuvi kupata elimu ya kuvua, mitaji ya kununua vifaa bora vya kuvua na kuhifadhi samaki, samaki watapatikana kwa wingi na wataweza kuuzwa katika soko la nje na la ndani na kwa wingi wa upatikanaji wa samaki hawa, wananchi wataweza kununua kwa bei nafuu. Kwa kuwa samaki ni lishe bora, ulaji wake kwa wingi utasaidia kuboresha afya za wanachi kuwa katika hali nzuri na matumizi ya taasisi za afya yatapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali Jimbo la Kibaha Vijijini lina mifugo mingi na pia kuna samaki wengi wa aina ya kambale wanaopatikana katika Mto Ruvu. Serikali inaweza kuwasaidia wananchi wa Jimbo hili hasa wale walioko kando kando ya Mto Ruvu, kuwajengea Chuo au Taasisi ya Utafiti wa kutotoa vifaranga vya samaki aina ya kambale na kuwafundisha wananchi jinsi ya kufuga samaki kwa kuwaelekeza kuchimba au kujenga mabwawa ya kufugia samaki. Kwa kuwa uwezo wa wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini ni mdogo, Serikali ingeweza kuunga mkono juhudi za wananchi wale kwa kuwajengea Kiwanda cha Kusindika au Kuhifadhi Samaki ili waweze kunufaika kwa vijana kupata ajira na kuondoa umaskini uliopo kwa jamii hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. *ENG.* CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa hotuba nzuri. Naomba kuchangia eneo moja la uzalishaji wa vifaranga vya samaki. Kwa kuwa vifaranga wa samaki wanazalishwa katika mabwawa, napenda kushauri jambo moja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mipango ya pamoja ya matumizi ya maji. Mabwawa yanahitaji gharama kubwa kuyajenga. Aidha, mabwawa yanatumia eneo kubwa la ardhi kuhifadhi maji. Ili kupunguza gharama ya ujenzi wa mabwawa ni vizuri tukawa na utaratibu wa kuibua miradi ya pamoja ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji (mabwawa na mifugo) ambayo inajumuisha maji ya kunywa, maji ya kumwagilia, maji ya majosho na mabirika ya kunywesha mifugo. Utaratibu huu siyo tu kwamba utaongeza ufanisi lakini pia utasaidia kupunguza gharama za ujenzi na kutatua baadhi migogoro kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ombi maalumu katika Jimbo langu la Buyungu, nimejenga bwawa la umwagiliaji ambalo sasa lina samaki aina ya sato ambao hatujui walikotoka. Aliyekuwa Waziri wa Mifugo Mheshimiwa Dkt. John Magufuli alituahidi kutuletea vifaranga wa samaki. Naomba Wizara itimize ahadi yake, nilikwishaleta maombi kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuchangia katika hotuba ya Bajeti hii, kwani ni Wizara nyeti na ina umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kufahamu fedha ya ruzuku ya Maswa inayotolewa kila mwaka, pamoja na kwamba haitoshelezi mahitaji, lakini hakuna tathmini yoyote iliyofanywa kujua athari yake. Ni lini basi tathmini hiyo itafanyika? Pamoja na kwamba Serikali

inahimiza suala la ufugaji ni kidogo mno, haliendani na mahitaji. Serikali imekuwa haiwekezi kwenye mashamba ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu tumekuwa tunaishauri Serikali, kufanya sensa ya mifugo nchini. Kwa sababu ni zaidi ya miaka 25 haijafanyiwa takwimu za mifugo tunazopewa ni za makisio tu inayotokana na *survey* ya sampuli kwenye baadhi ya kaya. Takwimu hizi hazitupi hali halisi ukizingatia matokeo ya asili na yale ya kibinadamu kama vile ukame, maradhi na mauzo kwa ajili ya kitoweo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Suma JKT wamepewa *tender* kujenga machinjio ya Ruvu, lakini cha ajabu wanatumia *Engineer* wa Wizara, kwa nini? Kama walikuwa hawana *Engineer* ni kwa nini walichukua *tender* hiyo? Hivi mkataba huo wa ujenzi uliongelea kama hawana mtaalamu huyo? Kama hiyo haitoshi machinjio hayo hayajakamilika mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kugusia kidogo kuhusu uvuvi. Wizara inaposema wavuvi wajikusanye vikundi ili wawezeshwe, hebu Serikali ituambie ni uwezeshwaji upi huo? Kama ni pesa ni shilingi ngapi kwa vikundi vinavyokidhi vigezo. Napenda kutoa ushauri Serikali iwawezeshe wavuvi hata kama ni vikundi vinne au vitano tu na viwe vikundi vya mfano. Kwa kuwapa boti ambazo zinaweza kuvua maji marefu pamoja na zana zilizokamilika ndani ya boti hizo ili kupima uwezo wao wa kuvua na kipato chao. Wizara inaweza fanya hivyo kwa kuwa utakua ni uwezesho wa mkopo, wakati wakifanya marejesho Serikali itaona ni jinsi gani ya marejesho hayo, yataweza nunua boti zingine kwa ajili ya vikundi vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi tulionao ni lazima tuwapongeze kwani wanatumia uvuvi wao wa asili na kuliletea Taifa mapato kama tukiwawezesha. Je, Taifa letu litatuingizia kipato kikubwa? Ni lazima tubuni, tuwezeshe, ndipo tuvune. Tuige nchi za Sychelles na nyinginezo. Ahsante.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika hoja hii iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi katika eneo mahsusi la uvuvi wa baharini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko makubwa kutokana na wavuvi wadogo wadogo ambao hulazishwa kukata leseni pamoja na ukweli kwamba wavuvi hawa ni mabaharia tu na chombo husika na mmiliki wa chombo hicho huwa na leseni na vibali vyote stahiki. Kwa kweli suala hili ni zito na limekuwa kero kubwa kwa vijana hawa ambao hujipatia riziki zao halali kutokana na kibarua chao hicho. Naomba Serikali iliangalie kwa umakini mkubwa na kulipatia suluhisho la kudumu jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali baada ya kulazimisha vibarua hawa (mabaharia) kukata leseni ihamishie gharama hizi kwa mmiliki wa chombo ili vijana hawa waweze kufanya kazi katika chombo chochote watakachopenda kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchangia katika suala la uvuvi wa maliasili za baharini. Wizara imepiga marufuku kwa uvuvi wa majongoo bahari. Hili jambo nafikiri Serikali ingeliangalia upya kwani kufanya hivyo sidhani kwamba Serikali inafaidika vipi na uzuiaji wa kuvuliwa kwa majongoo bahari. Majongoo bahari ni bidhaa ambayo ina soko kubwa duniani na hata hapa ndani ya nchi linaleta kipato kizuri kwa wananchi wanaojishughulisha na uvuvi huo. Hivyo ni vyema Serikali ikaweka utaratibu mzuri utakaowezesha uvuvi huo kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vigumu kumzuia mwanadamu kutenda kile ambacho kinampatia kipato kinachomwezesha kuishi. Hivyo ni vizuri Serikali ikaelewa kwamba pamoja na zuio hilo, uvuvi huo unaendelea kwa njia za siri wa kufanya Serikali kukosa mapato makubwa yanayotokana na maliasili hiyo adimu duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ingawa si kwa umuhimu, naomba Wizara na wizi mkubwa unaofanywa na nchi za nje zinazokuja kuvuna mazao bahari yetu na kuikosesha Serikali mapato. Hili ni muhimu kwa kulinda rasilimali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. *ENG.* STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nampongeza Waziri pamoja na Naibu wake na timu nzima ya Wizara hii. Mchango wangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, fukwe nyingi za Ziwa Nyasa zinaharibika kutokana na ukataji wa miti katika milima iliyopo kando ya ziwa na hivyo kufanya mchango kuingia kwenye ziwa hasa katika maeneo ya Njombe ambapo pia pana bandari. Hii inasababisha kuharibu mazalio ya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zana za uvuvi kama nyavu *standard* zijulikane na zitolewe kodi na ushuru ili kuwawezesha wavuvi badala ya kuchoma tu zile za makokolo. Wavuvi hawana masoko ya uhakika kwa ajili ya kuuzia na kuhifadhi dagaa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwalika Mheshimiwa Waziri apange ziara katika Kata ya Kihegera – Mbinga ili wavuvi nao wapate moyo kuwa wanakumbukwa na ni muhimu kwa jamii, ndio maana wakatengewa Wizara, nami nitakuwa mwenyeji wako pamoja na Mheshimiwa John Komba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vya kutibia mifugo vijijini havipo, ni vema kuwaendeleza wajasiriamali, wataalamu huduma vijijini ili watoe huduma hiyo. Nawasilisha.

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la kero ya kutopatiwa ekari 5,000 za wakulima wa asili Wami Sokoine.

Mheshimiwa Waziri nilimuandikia barua kumjulisha tatizo la muda mrefu la kutopatiwa ekari 5,000 wafugaji wa asili Wami Sokoine. Uamuzi wa Baraza la Mawaziri wa mwaka 2002 uligawa iliyokuwa Ranchi ya Dakawa kwa makundi mbalimbali wakiwemo wafugaji wa kisasa, wakulima wa Lukindo, *Mtibwa Sugar* na ujenzi wa Makao Makuu ya Wilaya ya Mvomero walipewa ekari 3,000 cha kushangaza wafugaji wa asili hawakupewa ekari 5,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Waziri atoe majibu hadharani ndani ya Bunge hili wakati anahitimisha hoja yake bila hivyo nitaondoa shilingi hii. Naomba niambiwe yafuatayo:-

Je, ardhi hiyo ekari 5,000 zipo na watapewa lini? Kwa nini suala hili la kuwapatia ekari 5,000 limechukua muda mrefu na endapo ekari hizo hazipo zilienda wapi, alipewa nani na kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni maombi ya kutenga fedha kwa ajili ya kujenga malambo na majoshoo maeneo ya wafugaji Wami Sokoine, Kambala, Masimba, Kibati, Matate, Melela na Doma. Naomba Serikali ijenge malambo na majosho ya kutosha kwa ajili ya wafugaji. Pia ni vema sasa Serikali itenge fedha kuboresha minada ya mifugo ya Mongeni na Hoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa usimamizi wa uvuvi katika ukanda wa bahari ya Tanzania haupo madhubuti na ndio maana tunashindwa kupata samaki wengi na wa kutosha wakati tuna samaki wengi katika bahari yetu. Serikali bado haijajipanga kwenye uvuvi inashughulika zaidi kwenye mifugo na samaki waliokuwepo kwenye maziwa, wavuvi wanaovua hivi sasa ni wale wadogo wadogo tu wanaotumia mishipi, nyavu za kawaida na madema. Wale wanaovua samaki wakubwa ni wageni na kisha kuondoka na samaki wao na baadaye huwaleta hapa hapa Tanzania kuja kutuuzia kwa kisingizio wanatoka Japan na Yemen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi katika nchi yetu tumeingiziwa samaki kutoka Japan ambao wanaonekana wana mionzi ya *nuclear* na kuna samaki ambao wanatoka Afrika ya Kusini ambao wanatengenezwa kwa *plastic* na sio kuvuliwa, na hawa pia wameingia Tanzania na

asilimia kubwa ya samaki wanaouzwa wanatoka Yemen, cha kushangaza sisi tuna bahari kubwa kuliko nchi hizi, kama tuna mipango endelevu tusingekula samaki kutoka nje ambao hatuna uhakika nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa gari ikija kutoka Japan inakaguliwa na bila ya *certificate* ya Ukaguzi huwezi kutoa, je inakuwaje samaki mpaka wanafika sokoni na kwa walaji hawajakaguliwa? Hivi sasa Watanzani wanahofu juu ya maisha yao kwa sababu watu wengi wameshakula hao samaki waliotoka Japan wenye mionzi ya *nuclear*, kwa kuwa Serikali imetoa tamko lao samaki waende wakapimwe na ambao Serikali itoe tamko kwa wale ambao wameshawala hao samaki dalili gani wataziona kwenye miili yao ikiwa wamedhurika ili wafike hospitali haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iwe na mikakati madhubuti wa kuendeleza uvuvi katika bahari zetu za mwambao wa Tanzania ili tuweze kupata samaki wa hapa nyumbani na wengine kuwauza nchi za nje ili tupate kuongeza Pato la Taifa. Iweje samaki wetu wavuliwe na wageni na sisi wenyewe tushindwe kuwavua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naiomba Serikali kupita Wizara hii sekta ya uvuvi ipewe kipaumbele.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji wa kisasa wa kuku umeonekana kwamba unaendelea kukua kwa kasi kubwa sana, hivyo basi kuna ukweli kwamba kuku wa kienyeji kuna uwezekano mkubwa wa kutoweka baada ya muda wa miaka michache ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasemekana pia kwamba wafugaji hawa wa kuku wa kienyeji wanatumia dawa ambazo zinatumiwa kwa kuongeza uwezo wa kuishi kwa wale wagonjwa wa UKIMWI, dawa ambazo zinasemekana kwamba zinawafanya kuku kukua haraka haraka sana, lakini pia kuku hawa mlaji anapovunja mifupa wakati anapowatumia kuku hawa kama kitoweo pia kuna uwezekano wa kupata matatizo yatokanayo na dawa zinazotumiaka kulisha kuku hao, lakini pia hata mayai ya kuku hawa wa kizungu inasemekana kwamba yana tatizo na sio mazuri ukilinganisha na yale ya kuku wa kienyeji. Kama jambo hili ni kweli, Serikali inasema nini juu ya kulitanabalisha Taifa juu ya jambo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tumesoma katika magazeti lakini pia tumesikia katika vyombo vya habari vya hapa nchini kwamba samaki wenye uzito wa matani kwa matani wameingizwa hapa nchini wakitokea Japan na kwamba hivi sasa samaki hao tayari wameshasambazwa ndani ya nchi yetu, kama kitoweo. Samaki hao wanasemekana wana mionzi ya sumu ambayo ni hatari kwa mlaji, jambo linaloweza kutupatia athari wananchi kwa wale wote ambao watakula samaki hao, hivi sasa hata vizazi vyao vinaweza kuathirika (kuzaa vizazi vyenye athari) zilizotokana na sumu hiyo iliyo katika samaki hao. Je, Serikali inayo taarifa hii, kama inayo wamechukua hatua gani ya kulitahadharisha Taifa juu ya jambo hilo hatari kwa afya na maisha ya Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Ahsante.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kusema kwamba ninaunga mkono hoja. Pamoja na kuunga mkono hoja, kuna maeneo kadhaa ambapo ninahitaji ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Kiwanda cha Nyama Shinyanga. Katika siku za karibuni kumekuwa na taarifa za mara kwa mara zinazotolewa na vyombo vya Serikali kwamba Kiwanda cha Nyama cha Shinyanga ambacho kilibinafsishwa na kununuliwa na kampuni ya *TRIPPLE'S* aliyekinunua ameshindwa kukiendeleza. Taarifa nyingine inasema *TRIPPLE'S* yupo katika hatua za mwisho kupata mkopo toka *TIB* ambayo ni Benki ya Serikali na taarifa zinasema amekwishapata mkopo. Sasa hali ya matamshi yanayopigana inawasababishia usumbufu wananchi ambao tayari wana mkataba wa *TRIPPLE'S* wa kuwauzia ng'ombe na hususani wafugaji wa Jimbo la Kahama. Ninaomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Shinyanga kimsingi ni mkoa wa wakulima na wafugaji ni miongoni mwa mikoa inayoongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo. Wilaya ya Kahama ni miongoni mwa Wilaya za Mkoa wa Shinyanga ambayo ina mifugo mingi hasa ng'ombe. Hata hivyo, pamoja na kuwapo kwa ng'ombe wengi wafugaji na mifugo wanatangatanga bila kuwa na eneo mahsusi la malisho. Ukiangalia katika jedwali namba sita maeneo yaliyopimwa na kutengwa kwa ajili ya ufugaji utaona kwamba katika Mkoa wa Shinyanga ni Wilaya ya Bariadi tu ndio ina eneo kwa ajili ya ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua ni kwa sababu gani maeneo kama hayo hayajatengwa katika Wilaya za Kahama, Kishapu, Shinyanga Vijijini, Maswa na Bukombe? Kukosekana kwa maeneo rasmi ya ufugaji kunasababisha wafugaji wenye maelfu ya ng'ombe kuvamia pori la akiba la Kigosi/Moyowosi ambako kumekuwa na matatizo makubwa ambayo yamesababisha hadi vifo. Naomba ufafanuzi.

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie katika Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Katika mpango wa mwaka 2011/2012 Serikali imeweka vipaumbele kadhaa katika mifugo, hii ni pamoja na kutenga maeneo ya malisho, kuhamasisha ufugaji wa kisasa na kujenga viwanda vya kusindika mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutenga maeneo ya wafugaji kutatatua matatizo mengi yanayotokea kati ya wafugaji na wakulima. Katika jambo hili Serikali ilichukulie umuhimu wa pekee ili kero inayosababisha magomvi isiwepo. Wakati mwingine viongozi wa vijiji pamoja na watendaji wa Serikali ndiyo husababisha mapambano kwa kuomba fedha kutoka kwa wachungaji wa mifugo kwa kudai wao watawapatia sehemu za kuchungia hivyo wachungaji wanapokataa kutoa fedha ndipo magomvi hutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano dhahiri ni mwezi wa tano, 2011 ng'ombe zaidi ya 56 walikuwa katika vijiji vya Ikuba, Chamalendi na Kashishi. Ng'ombe hao walikuwa na askari wa *TANAPA*. Je, kulikuwa na sababu yoyote ya kuwapiga risasi ng'ombe hao, badala ya kuwashika wahusika wa mifugo hiyo na kuwafungulia mashtaka? Huo ni uonevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali itoe mafunzo kwa wafugaji ili waelewe mipaka yao na sheria za nchi. Kwa suala la uvuvi hususani Mkoa wa Rukwa na Katavi, uvuvi ni kitu muhimu sana kwani tumezungukwa na maziwa mawili ambayo ni Ziwa Rukwa na Ziwa Tanganyika. Lakini wavuvi wamekuwa wakivua samaki na dagaa katika mazingira magumu kutokana na ukosefu wa vifaa vya kisasa vya kuvulia. Tunaiomba Serikali iwaangalie wavuvi wadogo wadogo kwa kuwakopesha vitendea kazi kama nyavu na vinginevyo vinavyohusu uvuvi. Hii itawafaya wapate mapato mazuri ya kujikimu katika maisha yao kwa uhakika, tofauti na ilivyo sasa ambapo katika Mto Ugala wavuvi hawa wadogo wadogo kwa kutumia nyavu zenye matundu madogo wamekuwa wakivua samaki wale wadogo ambao walihitaji kukua na hivyo kusababisha samaki kutoweka muda mfupi ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anifahamishe Serikali imechukua hatua ipi kwa ng'ombe 56 waliouawa mwezi wa tano, mwaka 2011 na askari wa *TANAPA* katika vijiji hivyo nilivyovitaja huko Mpimbwe Mkoani Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa ufugaji wa kuenea nchi nzima haukubaliki na hivi sasa ndio unaofanyika. Matokeo yake ufugaji wa aina hiyo kumetokea mapigano baina ya wakulima na wafugaji katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Mfano hai ni hivi majuzi huko Bagamoyo kumetokea mapigano baina ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuondoa tatizo la wafugaji, Bunge la Tisa limetunga sheria inayohusiana na namna ufugaji bora. Sheria hiyo pamoja na mengine inataka wafugaji wawe na maeneo maalum ya ufugaji na maeneo hayo yawepo miundombinu itakayokidhi kuwepo mifugo

katika eneo husika. Pia katika sheria hiyo imeweka inapotokea mifugo kuzidi eneo husika mhusika auze mifugo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha mpaka leo sheria hiyo haijaanza kufanya kazi kwa sababu kanuni hazijatungwa au kumaliza kutungwa. Wizara ielewe haiwezekani wananchi kuendelea kuumia kwa sababu kanuni za Sheria ya Mifugo hazijatungwa. Naona ipo haja kuiga kazi iliyotumika katika kutunga kanuni za Sheria Gharama za Uchaguzi. Sasa ni lini sheria hiyo ya mifugo itaanza kufanya kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha kuwepo mradi wa *MACEMP* kwa wavuvi wa ukanda wa bahari bado maisha ya wavuvi hali yao ipo katika umaskini na mazingira ya bahari bado yanachafuliwa kwa kukatwa mikoko. Mradi wa *MACEMP* umo katika kumaliza muda wake na kama wavuvi ukanda wa bahari wamefaidika vipi? Je, mradi huu wa *MACEMP* utapofikia mwisho Wizara umejizatiti vipi katika kuendeleza yale yaliyoanzishwa na *MACEMP?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado wavuvi wetu waliopo kwenye mito, maziwa na bahari wanasumbuliwa sana na zana wanazotumia hasa nyavu. Bado lugha ya nyavu haramu imetawala, wavuvi wengi wamechomewa nyavu zao. Ieleweke kuwa na nyavu zenye macho madogo pekee yake sio inayotambulisha uharamu wa nyavu peke yake, dagaa haziwezi kuvuliwa kwa nyavu zenye macho makubwa na pengine hata macho madogo. Kwa hivyo, katika kuvua dagaa inabidi papatikane chandarua. Nionavyo nyavu haramu ihusishwe na samaki anayevuliwa, kwa hiyo, Wizara ipo hapa suala hili tuliangalie upya la nyavu haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. GREGORY G. TEU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya ahadi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete wakati wa kampeni za urais, Mheshimiwa Rais aliahidi kusaidia juhudi za kukipandisha hadhi Chuo cha Utafiti wa Mifugo cha Mpwapwa *(LITI)* kuwa Chuo Kikuu Kishiriki chini ya Chuo Kikuu cha Kilimo na Mifugo cha Sokoine Morogoro yaani *Affiliated University,* vilevile ahadi hii ni kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi (2010) Ibara ya 6(85)(e) & (iv).

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Wizara ina mkakati gani wa kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais kukipandisha Chuo cha Utafiti wa Mifugo *(LITI)* Mpwapwa kuwa Chuo Kikuu Kishiriki *(Affiliated University).*

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mfumo mzuri kwa wananchi wa Wilaya ya Tanga kujihusisha katika shughuli za ufugaji na Serikali imepanga watengewe sehemu za kuendeleza ufugaji huo. Serikali ishughulikie ugawaji wa maeneo hayo kwa ufugaji huo ili wananchi waondokane na adha ya kufuga wanyama ndani ya Jiji la Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo cha maziwa cha *Tanga Fresh* ni mradi unaowezesha wananchi wengi wa Tanga kujiajiri kiufugaji ng'ombe wa maziwa kwa kukopa ng'ombe kulipa maziwa. Kiwanda hiki kinapata usumbufu wa ardhi waliyokodishwa kufanyia kazi ya uchunguzi sehemu ya Buhuri. Ninaomba Wizara iwasaidie ili waendelee kuzitumia hekta zao walizonazo kwa sasa kwa kufanyia kazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wanahitaji kupewa elimu zaidi juu ya madhara ya uvuvi unaoharibu mazingira, sambamba na kupewa mikopo ya kununulia nyenzo za uvuvi. Kama haiwezekani kuanzisha mfuko maalum wa kuwapatia mikopo wavuvi basi angalau waruhusiwe kukopa kupitia mfuko wa pembejeo za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utarataibu wa kuwapatia wavuvi leseni ya kufanyia kazi hizo uboreshwe na kuweka wazi kuwa leseni zielekezwe kwa chombo na si kwa mvuvi mmoja aliomo kwenye chombo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji wavutiwe na kuanzisha mashamba ya mazao ya baharini, kama kamba na kamba mti ili wananchi wapewe uwezo na ushiriki katika kufuga aina hizo za samaki ambazo zinaweza kuwapatia wananchi kipato kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja asilimia mia.

**MHE. PEREIRA AME SILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia kwenye hoja hii ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Awali ya yote nachukua fursa hii kuwapongeza kwa hotuba nzuri na yenye taarifa na tarakimu za kutosha. Pamoja na pongeze hizo naomba nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvuvi wa bahari kuu, ni lazima tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema kubwa ya rasilimali za asili alizoturuzuku. Kati ya rasilimali hizo ni maliasili za bahari, mito na maziwa ikijumuisha samaki na mazao mengine. Nasikitika sana kwamba pamoja na rasilimali hizi nchi yetu bado imeshindwa kuzivuna na kupata faida kwa ajili ya mwananchi mmoja mmoja, vikundi na Taifa kwa jumla, ni kwa manufaa makubwa kuliwezesha Taifa kupata manufaa kutokana na *endowment* hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba mpaka leo hii rasilimali zetu za bahari kuu zinavunwa na nchi za Mataifa ya nje bila ya idhini. Naelewa kwamba bado nchi yetu bado haina uwezo na vifaa vya kuhakikisha ulinzi imara wa eneo hili la *EEZ*. Hata hivyo nashauri yafutayo:-

(a) Serikali kupitia Wizara hii ijipange kuhakikisha tunajenga uwezo na kwa haraka ili kudhibiti matumizi ya eneo la *EEZ* pamoja na uvunaji wa rasilimali zilizoko.

(b) Ingawa hatua kwenye (a) zitasaidia kupata mapato ya leseni na pia kudhibiti uharibifu wa mazingira, faida hasa ya ukanda huu tutaipata. Kwa sisi wenyewe kujipanga kiuwezo ili tuweze kuvuna rasilimali hizo. Sehemu kubwa ya vijana wetu hawana ajira na hatuna budi kuwatayarisha kwa ajili ya kushiriki kwenye uvuvi kwa kuwapatia vifaa vinavyohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni moja ya nchi yenye mifugo mingi katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Wingi wa mifugo, katika hali ya kawaida ungetusaidia kupata mapato kwa mauzo ya mazao ya mifugo hiyo. Hata hivyo katika siku za hivi karibuni tumeona kwamba wingi huu wa mifugo ni kikwazo katika juhudi zetu za kujenga umoja na uthibiti wa uharibifu wa mazingira. Jambo hili ni hatari kubwa na mvutano kati ya wafugaji na wakulima imekuwa jambo la kawaida. Suluhisho ya tatizo hili ni elimu ya ugani, utafiti – kuangalia vipi tunaweza kuchanganya na mipango wapi na vipi tufuge na tulime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi unaoharibu mazingira, upungufu wa mapato kwa wavuvi inapelekea kila mvuvi kutafuta mbinu za kuweza kupata samaki wengi leo bila kufikiri wavuvi wa kesho watavua nini. Lazima tuelewe kwamba Tanzania haiwezi ikaachwa bila ya uvuvi na wavuvi. Kwa sababu hii ni lazima sheria na mbinu mbadala zitumike ili kuhakikisha kwamba wavuvi wa leo hawapunguzi uwezo wa wavuvi wa kesho, kukimu maisha yao. Ili kulitimiza lengo hili la lazima mbinu zifuatazo nashauri zipewe nafasi yao.

Kwanza elimu ya wavuvi ili kuelewa athari ya vitendo vyao pamoja na faida ya kutumia mbinu na vifaa vinavyoheshimu mipaka ya kimazingira, pili, kusimamia sheria ziliopo na kuzirekebisha iwapo inahitajika, tatu, kufanya utafiti juu ya mbinu na vifaa vya uvuvi vitakavyoongeza tija na bila kuathiri mazingira na nne, kueneza mbinu na vifaa vya ufugaji wa samaki kama njia mbadala wa mapato na chanzo cha protini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SELEMAN S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iangalie kwa umakini suala la Bajeti ya Wizara kwani Wizara hii ina Bajeti ndogo mno ambayo haiendani na mahitaji ya Kiwizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ijenge machinjio makubwa Jijini Dar es Salaam ili kuwezesha kukua kwa uchumi wa nchi yetu kwa kuuza nyama nje ya nchi. Naomba suala la mifugo lipewe utaratibu mzuri ili kuzuia migogoro mingi inayojitokeza baina ya wafugaji na wakulima hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iweke nguvu ya kutosha katika kuimarisha ulinzi na usalama katika bahari yetu kwa kuzuia waporaji wa mali zetu (samaki) katika eneo hili la nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalamu wa mifugo ni wachache sana. Naiomba Serikali iweke Bajeti ya kutosha ya kuviwezesha vyuo vyetu vya mifugo viweze kufundisha wanafunzi wengi wa fani ya mifugo ili kupunguza tatizo la upungufu wa wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dawa za mifugo zipo juu sana. Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka wa kuangaliwa mchakato mzima wa utengenezaji na uingizaji wa dawa za mifugo ili dawa hizo zipatikane kwa bei nafuu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naipongeza Serikali kwa juhudi mbalimbali zinazofanya katika kuendeleza sekta ya mifugo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Mifugo Mheshimiwa Dkt. David Mathayo, Naibu Waziri Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro na timu nzima ya Wizara kwa uwasilishaji mzuri wa Bajeti ya Wizara yao. Naomba nichangie maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya wafugaji na wakulima, hii ni kero kubwa sana, si tu kwa wakulima bali kwa wafugaji na wananchi kwa ujumla. Ikumbukwe kuwa wafugaji wanaohamahama siyo ridhaa yao kuhama, bali wanafanya hivyo ili kunusuru maisha ya mifugo yao ambayo wanategemea kama chakula na uchumi wa familia zao na huko nyuma maeneo wanakoacha, ni maeneo yao ya asili ni kwa vile tu hakuna malisho na maji na kwa kuwa Serikali pia imewanyanyasa wafugaji na kuwapa (kutoa) maeneo yao kwa wawekezaji kwa madai kuwa wawekezaji hao wanaletea Taifa faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ushauri kwa Serikali. Kwanza kutoa elimu ya uelewa kwa wafugaji ili maeneo yao yasimilikishwe wakulima na pindi wanaorudi wakute maeneo yao ili nao wamilikishwe kulingana na sera ya Taifa ya ardhi na pili, iwe ni marufuku kuwapa wawekezaji maeneo mazuri ya malisho na maji kwa wafugaji kwa kuwa wafugaji pia hawapendi kutangatanga kutafuta malisho, wakiishia kwenye mogogoro, matusi na hata mauaji ya wafugaji huko Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mikubwa ya Kitaifa inayoanzishwa hainufaishi wafugaji kama *ASDP,* Benki ya Wakulina na kadhalika. Miradi hii, ama mipango hii ya Kitaifa yanabeba pia mipango ya kunufaisha wafugaji kinadharia tu. Ukweli mifugo hailengwi hata kidogo isitoshe hakuna mfumo wowote unaoeleweka wa kuwakopesha wafugaji, kama ilivyo ruzuku ya pembejeo na zana kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naitaka Serikali sasa itueleze ni lini itaanzisha mradi/mpango mahususi kwa ajili tu ya mifugo? Naomba Serikali ianzishe Benki ya Wafugaji, kwa sababu taratibu za kukopesha wakulima ni tofauti kabisa na taratibu za kuwakopesha wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja Wizara hii mpaka maelezo niliyotoa yafafanuliwe. Serikali imezidi, siku hadi siku bila hata huruma ku-*neglect* wafugaji. Wafugaji watambuliwe pia kama na wao ni Watanzania. Pia wapewe elimu ya uelewa, sasa hivi wanajua ardhi hii ni ya Mungu na si ya mtu ndiyo maana wanaweza kutoka Dongobesh mpaka Tunduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wamilikishwe ardhi, tusipofanya hivyo watakuwa watu wasio na kwao. Ni marufuku ardhi ya wafugaji kupewa wawekezaji, Tanzania ina maeneo mengi mengine. Mbona mabonde, maziwa ya wakulima hawapewi wawekezaji, ikibidi wapewe basi iwe kwa muda mfupi. Nashukuru.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu kwa muda mrefu sana imekuwa na migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wa ardhi hii inatokana na kutokuwepo kwa mpango madhubuti katika utumiaji wa ardhi maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo sababu kwa Wizara kuangalia upya ni namna gani ufumbuzi wa huduma za kutumia maeneo ya wafugaji ili vilevile watuamiaji wengine wa ardhi waweze kutumia katika shughuli zao za kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyoelewa mchango wa sekta ya mifugo kwa Watanzania bado siyo mkubwa pamoja na kuwa Tanzania ni ya tatu Barani Afrika kwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Serikali haijachukua hatua madhubuti kuhusiana na uvuvi haramu nchini katika maeneo mbalimbali hapa nchini, wavuvi wamekuwa wakiharibu neema ambayo Mwenyezi Mungu ametujaalia katika kutuwezesha kuweza kumudu maisha yetu ya kila siku. Hivyo naiomba Serikali ichukue hatua za makusudi katika kushughulikia masuala ya uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyopendekezwa na kamati Serikali iendelee kutoa elimu kwa wavuvi juu ya umuhimu wa kutumia zana bora za uvuvi na hii iende sambamba na kupatiwa wavuvi mikopo yenye masharti nafuu ili waweze kununua zana bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. FELSTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. David Mathayo, Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa maandalizi mazuri ya Bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufahamishwa hatima ya mafao ya waliokuwa wafanyakazi wa Wizara hii katika machinjio ya kisasa yaliopo Mkoani Dodoma baada ya machinjio kubinafsishwa, walielezwa kuwa wataendelea kuwa watumishi wa Wizara (rejea barua ya Wizara ya tarehe 09/11/2008) na Serikali iliwaahidi kwamba hawatapoteza haki zao za kisheria, cha ajabu ni kwamba wengi wao wamekwishaachishwa kazi na mwajiri mpya bila kupewa kitu chochote. Mheshimiwa Waziri aliwahi kutembelea machinjio hayo na kuelezwa matatizo yaliyopo hapo lakini mpaka sasa Wizara yake haijajali maslahi ya waliokuwa watumishi wa Wizara yake. Watu hao wanasubiri kujua hatima ya mafao yao kutoka kwake leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuona kwamba tuna mifugo mingi sana na Tanzania ni nchi ya tatu katika Bara la Afrika kuwa na mifugo mingi lakini hakuna hata kiwanda kimoja cha kusindika nyama. Naishauri Serikali kutafuta wabia kwa ajili ya kujenga viwanda vya nyama wakishirikiana na ranchi zetu za Taifa. Ranchi zetu ziwe vituo vya mafunzo kwa wananchi wanaoishi jirani na ranchi hizo katika suala la unenepeshaji mifugo, ukimilishaji na kadhalika. Ranchi zetu hazina hatimiliki hivyo ufuatiliaji wa hatimiliki ni jambo la muhimu na la kuwekewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji ni watu yatima katika nchi yao, ni wakimbizi kila wanapokwenda wanafukuzwa kwamba wanaharibu mazingira, hii siyo haki mbona wachoma mkaa, wanaokata miti ovyo hawafukuzwi kama wafugaji? Wanaofyeka misitu kwa ajili ya kilimo mbona hawafukuzwi? Nadhani kinachohitajika kwa wafugaji ni elimu ya namna ya kupunguza mifugo yao na pia kuwapatia soko la uhakika kwa mifugo yao na jinsi mifugo hiyo inavyoweza kuwafaidisha kimaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji sasa waruhusiwe kuuza mifugo yao kwa kilo ili wafaidike na bei ya mifugo yao. Kumpima mnyama, mifugo kwa macho kuwa ndio mizani siyo kuwatendea haki wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni vyombo vya habari vimetangaza juu ya samaki walioingizwa nchini kutoka Japan na wenye sumu hatari kwa matumizi ya binadamu, samaki hao inaaminika walikufa kutokana na milipuko ya *nuclear* iliyotokea kule Japan. Tunaomba maelezo ya ukweli wa jambo hili kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoani Mara na Mwanza kuna wafanyabiashara wengi wanoasafirisha samaki kwenda nchi jirani ya Kenya kupitia mpaka wa jirani na njia nyingine za panya katika mipaka yetu. Je, Wizara hii inafanya ufuatiliaji kujua kama wasafirishaji hao wana leseni na tani wanazosafirisha zinahusiana na leseni husika? Je, kuna utafiti unaofanywa na Wizara kuhusu uvuvi unaendelea maeneo mbalimbali ya nchi katika maziwa, bahari na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na uwasilishaji makini. Nawapongeza pia Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara kwa uandaaji mzuri wa Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za mifugo, sekta ya mifugo ni tegemeo la wananchi wengi wa Tanzania. Wizara imetekeleza mengi mazuri, lakini katika Jimbo la Bagamoyo tunaendelea kuathirika na huduma finyu za mifugo. Wafugaji wanaathirika na kutohudumiwa na Maafisa Ugani, kutokuwepo majosho na kutopata ruzuku za dawa. Wizara iongeze juhudi ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya sekta katika Wilaya mbalimbali. Maafisa Ugani waongezwe na kazi zao zihakikiwe na Wizara ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, machinjio ya Ruvu, pamoja na kuipongeza Serikali kwa kubuni mradi wa machinjio Ruvu, naomba kuchukua nafasi hii kusema wasiwasi wangu kuhusu kasi ya ujenzi wa mradi huo na baadae ubora wa machinjio hayo. Mradi unasuasua sana, ujenzi una zaidi ya miaka mitatu sasa, kuna tatizo gani? Pamoja na hoja hizo, nashauri Wizara ijipange kuhakiki mpango mzima wa mradi ili kujihakikishia kuwa na machinjio bora mradi utakapokamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa *MACEMP* umewakomboa vijana wengi katika Wilaya ya Bagamoyo. Takribani vikundi 42 vilipata ufadhili wa miradi yo. Kuna ambao wamefanya vizuri sana na kama wachache ambao wamepata changamoto. Ombi langu kwa Waziri, ni kuwa Serikali iharakishe awamu ya pili ya *MACEMP* na mfuko uongezwe nguvu, ili vijana wengi zaidi wawezeshwe. Pia mafunzo ya ujasiriamali yaongezwe katika mradi wa *MACEMP.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya wafugaji yanatokana na soko zuri la nyama na wanyama. Katika maeneo mengi ikiwemo Bagamoyo, soko la nyama/wanyama bado ni duni. Bei za wanyama hazifanani na gharama za ukuzaji na unenepashaji wanyama. Serikali iendeleze juhudi ya kupata masoko ya nje ya nyama na hasa yale ya nchi za Kiarabu *(UAE,* Saudia, Iran na kadhalika) na Comoro. Masoko mazuri yatahamasisha sana ufugaji wa kisasa nchini kwetu. Somalia na Ethiopia wanauza mbuzi kwa idadi kubwa sana Saudia, kwa nini sisi tusiuze?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu pamoja na wataalam wote walioshiriki kuiandaa hotuba hii ambayo ipo makini iliyojaa takwimu ambazo ndio kielelezo cha utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, naomba kupongeza Wizara yako kwa kushirikiana na Zanzibar kuhusu Mradi wa *MACEMP*, mradi huu kwa Zanzibar umeweza kusaidia wavuvi na vijana kujiendeshea shughuli zao za uvuvi pamoja na kujiondoshea umaskini. Misaada iliyotolewa ya kupewa *boat* za

uvuvi, nyavu na hata mashine ya kuendeshea boti hizo, pamoja na kutoa elimu kwa wadau wa Unguja na Pemba (Zanzibar).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa 47 (iii) inayoelezea katika mstari wa nne nanukuu; "Taasisi imejenga kituo cha hali ya bahari *(Satellite Receiving Station)* ambacho kitatumika kubaini maeneo yenye samaki wengi katika tabaka la juu la maji kwenye bahari ya Kitaifa *(Territorial Sea)* na ukanda wa uchumi wa bahari. Kituo hiki kimejengwa *TAFIRI* Makao Makuu, Kunduchi Dar es Salaam." Kila kitu kizuri kinahitaji kupongezwa na kilicho kizuri msaidie na mwenzio kwa kumuelewesha hadi nae afanikiwe.

Ninaiomba Wizara yako kwa kushirikisha Wizara ya Zanzibar inahusika na uvuvi na wao kuna kituo kama hicho kwa Zanzibar. Serikali ya Mapinduzi na Wizara zake ni sikivu na kwa jambo zuri kama hili italipokea kama ilivyo kwa *MACEMP* jinsi ilivyopokewa na Wazanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kuishukuru tena Wizara kwa jinsi inavyoshirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhusu uvuvi wa bahari kuu, kwa ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya Mamlaka zinazojengwa eneo la Fumba Zanzibar. Vilevile kwa kushirikiana na Jeshi la Wanamaji, Polisi na Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM), ninapongeza na huo ndio mwanzo mwema, na ndio mbinu ya kudhibiti uvuvi haramu, baharini kwa Tanzania (Bara/Visiwani).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa suingi mkono hoja ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa sababu kuu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliamua kuondoa mifugo Ihefu na kupeleka Mkoa wa Lindi, nadhani Wizara haikuwa imejipanga katika zoezi hili. Hivyo mifugo iliyopelekwa Mkoa wa Lindi imetelekezwa. Wilaya ya Kilwa na Lindi Vijijini haipati Bajeti ya kutosha hivyo kuleta uharibifu wa mazingira kama vile hakuna marambo ya kutosha kukidhi haja ya mifugo iliyopeleka na hakuna majosho, je, kwa kutoweka miundombinu ya marambo na majosho, wafugaji wanahamahama na kukausha mito yote mikubwa ikiwemo Mto Mbwemkuru na Mto Matandu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kupitia Wizara ya Mifugo inaonekana mipango yao kuwa sio mizuri na kuwa inakurupuka na kuwaacha wananchi wakiwa katika migogoro ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha kuona Mkoa wa Lindi haumo katika ujenzi wa malambo wala majosho, huu ni uonevu na dharau za makusudi za kurudisha nyuma maendeleo ya mifugo katika Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwasilisha na suingi mkono hoja.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika hoja ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei kubwa ya nyama ya ng'ombe, pamoja na ng'ombe wengi waliopo nchini lakini bado bei ya nyama ya ng'ombe na mifugo mingine kama vile nguruwe, mbuzi, kondoo, kuku pamoja na samaki ipo juu sana. Hali hii huwafanya Watanzania wengi washindwe kumudu bei. Kwa mfano, leo bei ya nyama ya ng'ombe huuzwa kati ya shilingi 4,000/= hadi shilingi 6,000/= kwa kilo moja. Katika hali hiyo ni Watanzania wachache sana watakaomudu bei hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ushauri ufuatao, kwanza Serikali kupitia Wizara isimamie kwa karibu zaidi bei za nyama pamoja na mazao yake ili Watanzania wengi hasa waliopo vijijini waweze kumudu bei hizo. Lakini pia nataka kujua hivi bei za nyama, kama vile ng'ombe, nguruwe, mbuzi, samaki na kadhalika hupangwa na chombo gani? Ongezeko la zao la nyama (ng'ombe) hakuna manufaa sana kwa Watanzania wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tetesi za kuwepo samaki wa sumu kutoka Japan. Zipo tetesi kwamba hivi karibuni kumekuwepo tetesi za kukamatwa samaki walioathirika na mionzi ya sumu *(nuclear)* kutoka Japan. Nataka kujua jambo hili lina ukweli gani? Kama kuna ukweli Serikali imechukua hatua gani? Na kama hakuna ukweli na kwa kuwa jambo linalosemwa linaweza kutokea, je, Serikali inachukua hatua gani madhubuti kuhakikisha samaki wenye sumu hawaingizwi nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugonjwa wa homa ya nguruwe *(African Swine Fever – ASF).* Ugonjwa huo ambao uliikumba mikoa kadhaa nchini Mbeya ukiwepo na Jimbo langu la Mbozi Mashariki likiathirika, umewasababishia wafugaji wa nguruwe na wafanyabiashara hasara kubwa sana. Uchumi wa makundi hayo umeharibika sana. Nataka kujua je,hadi leo karantini iliyowekwa katika mikoa hiyo hususani Mbeya na Wilaya ya Mbozi bado ipo? Kama ipo itaondolewa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo juu wapo wafugaji wa nguruwe ambao walipotelewa (kwa kufiwa) na mifugo yao yote na kwa ujumla maisha yao yote yalitegemea ufugaji wa nguruwe. Leo Serikali inazungumzia kutoa, kifuta machozi kwa wafugaji wa ng'ombe waliopotewa (kufa) na ng'ombe wapo. Kwa nini pia Serikali kwa huruma hiyo wafugaji wa nguruwe waliothirika wasipewe kifuta machozi kama ilivyofanya kwa wafugaji wa ng'ombe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha na naunga mkono.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote wa Wizara pamoja na watendaji wake wote wa Wizara kwa hotuba yao nzuri na namna walivyojiandaa kwa nia ya kuisadia Serikali na Watanzania kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi wa bahari kuu bado tumeshindwa kuitumia ipasavyo bahari yetu kwani rasilimali zetu inaonekana bado zinachukuliwa na wageni. Samaki wengi wakubwa bado hatujaweza kuvua na matokeo yake wanaendelea kuvuliwa na meli za kigeni na hatimaye wanaletwa kwetu kama biashara ya samaki kutoka nje ya nchi kama vile Japan na Yemen.

Naiomba Serikali itoe kipaumbele katika sekta hii ya uvuvi kwa kuwapatia zana za kisasa wavuvi wetu nchini ili waweze kufika mbali katika ukanda wa bahari kuu na waweze kuvua samaki wakubwa ili waweze kusafirisha nje na Taifa liweze kuingiza fedha nyingi za kigeni. Hadi sasa samaki wanaovuliwa kwenye bahari ni wale wadogo tu, kuna samaki wakubwa hawajafikiwa na wavuvi wetu na matokeo yake maharamia wanatuibia. Wavuvi wetu wawezeshwe kwa kupatiwa zana za kisasa na waache kutumia mishipi na nyavu ndogo. Bila kuwawezesha wataendelea kutumia zana haramu, watakamatwa na Serikali, wataendelea kuwa maskini na familia zao kuteseka. Ili kukuza uchumi wa nchi na kumpa fursa ya kujiajiri Mtanzania, hebu tumuwezeshe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata maziwa yetu hatujayatumia ipasavyo. Tanzania ni tajiri sana imezungukwa na bahari, maziwa na mito lakini inashangaza tunaendelea kuvua dagaa huku samaki wakubwa wakichukuliwa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugomvi usiokwisha baina ya wafugaji na wakulima ni jambo linalosononesha sana. Kwa nini Serikali isichukue hatua ya kukosa na wafugaji na wakulima kwa pamoja katika maeneo husika wapewe taaluma ya kutosha ili kila mmoja ajue haki zake na mipaka yake ili kila mmoja aweze kutumia uhuru wake alionao katika Taifa lake bila kuathiri uhuru wa mwenzake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauaji yanayosababishwa na ugomvi huu wa wafugaji na wakulima lichukuliwe hatua za haraka ili likomeshwe kwani wanaouawa ni Watanzania na sio wageni. Kwa mfano, mzozo wa Ihefu nao unaendelea kuwaathiri Watanzania/wafugaji hadi leo kwa kuwahamisha wafugaji bila kukaa nao kwanza na kufanya mazungumzo nao hadi pale ambapo muafaka ungepatikana.

**MHE. LAMECK O. AIRO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hii Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika Wilaya ya Rorya. Napenda kuijulisha Wizara kuhusu wizi wa mifugo iliyoibiwa toka tarehe 17/05/2007 hadi 01/01/2009 Tarafa ya Girango kata za Goribe, Koryo, Mirare, Ikoma, ng'ombe walioibiwa 504 waliorudishwa ni 108, watu waliopoteza maisha ni wanne, Goribe ng'ombe walioibiwa 662 walioruhudishwa 51, watu waliouawa ni watano, Mirare ng'ombe walioibiwa 614 waliorudishwa ni 51, watu waliuawa ni 21, Kata ya Bukwe ng'ombe walioibiwa 540 waliorudisha 50, waliopotea 100, watu walipoteza maisha ni wawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii ilibainika na kusomewa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 01/07/2009. Kwa kuwa hawa wananchi wa Tanzania walikuwa wanategemea sana hawa ng'ombe waliobiwa kwenye kilimo na kukamua maziwa ili kupata fedha ya kujikimu na mahitaji mengine muhimu. Sasa tunaomba Serikali iwasaidie hawa wananchi na matrekta kwa ajili ya kilimo kwani hawa wananchi wamebaki maskini wa kutupwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wilaya yetu ya Rorya hatuna zao la biashara tunachotegemea wilayani kwetu ni uvuvi katika Ziwa Victoria. Kwa sasa hivi maeneo mengi ya Ziwa Victoria hasa wilayani kwetu mialo mingi imevamiwa na magugu maji hasa maeneo ya Shirali kote na maeneo mengine ya uvuvi kwani tunaomba Serikali itusaidie kwa njia ya haraka sana, bila kupata msaada wa haraka basi Rorya itakuwa kwenye hali mbaya sana maana hata Halmashauri inategemea kwa asilimia zaidi ya 80 kwenye mapato yake. Tunaipongeza Serikali imetusaidia sana kwenye wizi wa mifugo kwa kutumia nguvu ya silaha, tunashukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja hiyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa mifugo hauna ubishi, kwa hiyo nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wetu wa mifugo kwa kazi nzuri sana ya kuhakikisha mifugo inawanufaisha wananchi wetu kabla ya kuunga mkono hoja hii, nina maswali machache. Naomba nipatiwe ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zuio la kufuga mifugo yote isipokuwa kuku kwa Tarafa ya Mvumi tangu mwaka 1980 naomba liondolewe. Linakiuka haki za binadamu na kuwanyima haki ya kula nyama na maziwa kwa viwango vinavyotakiwa hizo kilo 50 za nyama kwa mwaka anazotakiwa kula mtu, kwa Jimbo langu wataziba wapi. Kama hawaruhusiwi kufuga, sembuse hayo maziwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sensa ya mifugo ifanywe walau mara mbili kila baada ya miaka mitano. Naomba ufafanuzi ili niunge mkono hoja. Nawasilisha.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichangie kwa maandishi katika Wizara hii ambayo imebeba dhima ya kuwapunguzia wananchi umaskini wa kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sote tutambue kuwa bahari ni rasilimali muhimu ambayo kama itatumika vyema inaweza ikatupunguzia umaskini kwa watu wetu lakini hii inaenda sanjari na mipango na mikakati ambayo inalenga kufanikisha dhima hii ya kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi wa kutumia mabomu ni miongoni mwa uvuvi haramu kutokana na athari zake kwa mazingira ya uhai wa viumbe vilivyomo. Lakini na sisi watumiaji wa viumbe ni jambo la kusikitisha kuwa uvuvi huu unaendelea kufanywa tena sio katika maeneo ya mbali ya bahari yetu ni karibu na macho yetu eneo la feri na ushahidi wa kimazingira unaonyesha kuwa Maofisa wa Wizara hii wanahusika. Kwa nini niseme hivyo, nasema hivyo kwa sababu siku ambayo wapiga doria kutoka Wizara hii hawaendi kufanya doria ndio uvuvi huu haramu wa mabomu ndio unafanyika yaani ni kama wanapewa taarifa na maafisa husika na ndio maana wanaenda kufanya uhalifu huo na baada ya hapo hata samaki wanaopatikana wanauzwa bandarini hapo baina ya saa moja usiku hadi saa tatu usiku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kutokana na hilo naiomba Wizara kulifuatilia hilo kwa usalama wa viumbe wa baharini na usalama wa mazingira ya bahari na usalama wetu pia, kwani sidhani samaki hawa ni salama sana kwa matumizi ya binadamu. Naomba Waziri kulifuatilia hili na kuchukua hatua kwa maslahi ya Taifa letu ili kupunguza watumishi wanongezeka kila siku kutaka kujinufaisha binafsi badala ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi hawa Watanzania wanaendelea kufanya juhudi za kujiondolea umaskini hivyo Serikali ionyeshe juhudi za kuwasaidia katika harakati hizo, ni jambo la kusikitisha kwa suala la leseni limekuwa ni tatizo, wavuvi wanasumbuliwa na hili linatokana na sula la leseni kuwekwa katika Mamlaka mbili *SUMATRA* na Wizara husika. Tunaiomba Serikali moja tu, ili kuwapunguzia usumbufu wananchi wetu, kwani urasimu mara nyingi katika nchi zetu maskini unahusisha utoaji wa fedha nyingi zaidi na kupelekea mazingira ya rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa kuwa Wizara hii ilipata msaada wa shilinig bilioni 50 na zikaahidiwa shilingi bilioni 18 kupelekwa Zanzibar na shilingi bilioni 32 kubakia Bara na kugaiwa kwa wavuvi, lakini hadi sasa wavuvi hawajafaidika na msaada huo na zipo kauli fedha hizo zimefanyiwa shughuli tofauti na iliyokusudiwa, kama kununua vyerehani na vifaa vingine badala ya kuwasaidia wavuvi. Naomba Waziri anipatie ufafanuzi wa suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo nakushukuru.

**MHE. SULEIMA NASSIB OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi haramu umeshamiri sana katika nchi. Serikali imejitahidi kujaribu kudhibiti uvuvi huu lakini bado hali haijaridhisha. Ili kudhibiti uvuvi huu Serikali lazima idhibiti utumiaji wa baruti. Bado baruti inapatikana kwa urahisi na kwa bei ndogo. Lazima baruti yote iliyomo nchini ihakikiwe na idhibitiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi wa samaki wadogo na uharibifu wa mazalio ya samaki. Nyavu zenye macho madogo na nyavu za kuburura zinapunguza samaki. Ingawa Serikali ina kamata nyavu hizi lakini bado uharibifu huu unaendelea tena kwa kasi. Hatua za kuchukuliwa ni kuwapatia mikopo yenye riba nafuu wavuvi kama wanayopata wakulima. Pia zana za uvuvi zipunguzwe bei ili wavuvi washawishike kununua vifaa vya uvuvi halali. Kadhalika elimu itolewe kwa wavuvi ili waelewe kuwa kuna umuhimu wa kuacha uvuvi haramu.

**MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya Wizarani. Sasa naomba nitoe mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwezo wa kumiliki idadi ya mifugo *(manageable size).* Moja ya changamoto ambazo Wizara inapata ni tatizo la kuhangaika na kuainisha, kupima na kuendeleza maeneo ya ufugaji endelevu. Tatizo hili litaendelea ikiwa mambo yafuatayo muhimu hayafanyiki mapema.

Kwanza kuweka kiwango *(manageable size)* cha mifugo ambayo familia moja moja waweze kutunza kulingana na *land size* (ardhi waliyonayo) kila familia, pili, kutenga maeneo rasmi ambayo mtu aliye na mifugo zaidi ya *manageable size* atatakiwa kuchungia, tatu, kuhakikisha kwamba maeneo ya wafugaji wakubwa yapo mbali na wakulima ili kuondoa uwezekano wa kuwa na migogoro ya mapambano ya makundi haya mawili na nne, kujenga *(investiment)* kiwanda au viwanda vya kutosha vya nyama *(meat owning industry)* jirani na maeneo ya wafugaji wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinganishi kati ya wingi wa mifugo Tanzania na manufaa ya mifugo kwa Watanzania *(the relationship/correlation between quantitative data and qualitative benefits).* Tanzania inasifikia kwa wingi wa mifugo *(quantitative data)* lakini ipo karibu ya mwisho kwa *data* za manufaa ya mifugo hiyo kwa Taifa, kwa vipimo vyote vya uzalishaji nyama bora, maziwa na ngozi. Kama ni suala la uchambuzi ningesema kuna *strong negative relationship* ambayo ni *negative correlation coefficient*. Hali hii lazima tuisahihishe mapema ili Taifa liweze

kunufaika na mifugo hii. Nashauri Serikali ihamasishe ujenzi wa viwanda vya nyama, maziwa na ngozi.

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri yenye mchanganuo wa takwimu zinazoonyesha kukua kwa sekta ya mifugo na changamoto zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu shamba la ng'ombe wa maziwa Kitulo, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania alitembelea shamba la ng'ombe wa maziwa lilopo Makete hapo mwaka 2009. Katika ziara hiyo, Rais aliahidi kulifufua shamba la ng'ombe la Kitulo katika muda usiozidi miaka mitatu. Tayari sasa huu ni mwaka wa pili toka agizo hilo litolewe hapo Oktoba, 2009 na shamba hili bado lipo katika mazingira yale yale. Ningependa kufahamu ni lini ahadi hii ya Rais itatekelezwa. Serikali ionyeshe mkakati wa kufufua shamba hili na hatua ambazo sasa zinachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kufahamu soko la maziwa yanayotoka shamba la ng'ombe la Kitulo na kama shamba la ng'ombe Kitulo linakidhi mahitaji ya soko. Bei ya maziwa ya Kitulo ni shilingi ngapi kwa lita moja sasa hivi? Je, Serikali inafanya nini ili kuona kwamba thamani ya maziwa inapanda na hivyo kuchangia Pato la Taifa. Nashauri Serikali iborehse barabara za Mbeya - Makete ipetike kwa kiwango cha lami. Hatua hii itaongeza thamani ya maziwa kutoka shamba hili la Kitulo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kupongeza kazi nzuri na hotuba ambayo imetolewa na Mheshimiwa Waziri. Nampongeza pia Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote katika Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo kubwa la kuhamahama kwa wafugaji kutoka katika maeneo yao. Tatizo hili linawaingiza katika mgogoro mkubwa wafugaji na wakulima. Nchi yetu ina maeneo mengi ambayo yanafaa kwa ufugaji. Ni vema ili kuepusha vita ya wafugaji na wakulima kutenga maeneo maalumu ya wafugaji. Inaelekea kwamba Serikali ipo tayari kupanua maeneo ya wanyamapori, lakini ipo kimya katika kutatua tatizo hili. Umefika wakati sasa kulipa kipaumbele na kushirikiana na Wizara ya Ardhi kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu majosho ya mifugo, hivi sasa katika Halmashauri nyingi kuna uhaba mkubwa wa majosho na dawa za kuogeshea mifugo. Hili ni tatizo kubwa kwani kama jitihada hazitachukuliwa ili upatikanaji wa dawa hizo uwe rahisi, milipuko ya magonjwa kwa mifugo na hata yale yanayotoka kwa mifugo kwenda kwa binadamu kama kichaa cha mbwa yanaweza kuleta janga kubwa kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vya uhamilishaji na madume bora, hapo zamani katika maeneo mengi, Serikali iliweka vituo vya uhamilishaji na kugawa madume bora kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji wa ng'ombe bora/mbuzi bora, upatikanaji wa maziwa ya kutosha na nyma bora kwa walaji. Hivi sasa vituo vingi vimefungwa au havifanyi kazi iliyokusudiwa, mfano mzuri ni katika Jimbo la Rombo. Naiomba Serikali kufufua vituo hivyo katika Wilaya ya Rombo ili wafugaji wapate manufaa na faida itokanayo na kazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bei ya dawa za mifugo na chakula cha mifugo. Ni ukweli kwamba baadhi ya dawa na chakula cha mifugo ni ghali sana. Ili kulinda mifugo yetu bei za vyakula vya mifugo na dawa lazima ziangaliwe ili wakulima waweze kuzimudu. Vinginevyo tutapoteza mifugo mingi na kuwakatiksha tamaa wafugaji na hivyo kuliingizia Taifa hasara kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wataalamu wa mifugo, Serikali haina budi kuongeza udahili wa wanafunzi katika fani za sayansi ya mifugo. Hivi sasa wataalamu waliopo ni wachache sana katika Kata nyingi kwa mfano, Wilayani Rombo hakuna Maafisa wa Mifugo. Katika hali hii ni kujidanganya kuhubiri kuhusu maendeleo ya mifugo bila wataalamu wa mifugo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mifugo inyochungwa ovyo mijini, kwa muda mrefu wafanyakazi wanaona kwamba ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, nguruwe, mbuzi na kadhalika mijini ni njia mojawapo ya kuwaongezea kipato. Hata hivyo mifugo hiyo inateseka kwa kukosa lishe ya kutosha, pamoja na kuzurura ovyo mijini. Napendekeza kwamba Wizara iangalie na itoe ushauri juu ya njia inayofaa kunusuru wanyama hawa kwa kushirikiana na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nashukuru na kama nilivyoeleza mwanzo napenda kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri na watendaji wote katika Wizara hii na naunga mkono hoja hii.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa mwakilishi wa wafugaji naomba nijikite katika sekta ya mifugo kwa kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uboreshaji wa mifugo, nashauri Serikali iongeze Bajeti na juhudi katika kuhakikisha kwa kila Kata inapata Afisa Mifugo na *stock* ya dawa ya mifugo ikiwepo dawa za chanjo za kichaa cha mbwa na magonjwa ya mara kwa mara ya ng'ombe hasa kuhusu homa ya mapafu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu minada ya ng'ombe naomba nishauri Serikali kwamba ili wafugaji wapate bei halali ya mifugo yao wanyama wauzwe kwa mizani wakiwa hai badala ya thamani yao kukadiriwa kwa macho. Ili wanyama hao wawe na afya majosho ya kuogesha mifugo yajengwe katika kila kijiji au vijiji viwili josho moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usafirishaji wa ng'ombe, kwa muda mrefu ng'ombe wa minada wanakuwa wakisafirishwa kwa miguu au malori mabovu. Nashauri gari moshi itumike au magari yatengenezwe kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, soko la nyama, ili kufaidi soko la nje Serikali iweke usafiri wa kuaminika kati ya uwanja wa ndege wa Kilimanjaro na nchi za Kiarabu ambayo ndio soko la nyama la karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nashauri Serikali iwe inatoa bei elekezi ya mifugo katika minada yote nchini kila mwaka bila kusahau kuwepo kwa usafi minadani kwa afya ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itafute ufumbuzi wa kudumu kwa tatizo kubwa la wafugaji kuhamahama na hata vita kati yao na wakulima. Mkakati wa mabadiliko katika suala zima la ufugaji, kutengwe maeneo maalum ya malisho kwa wafugaji. Kujengwe mabwawa ya kutosha katika maeneo ya wafugaji. Majosho na dawa za mifugo, hili ni tatizo kubwa sana, Serikali ifanye juhudi zaidi katika huhakikisha dawa zinapatikana na wawepo wataalamu wa mifugo katika kila kijiji/kata ili mifugo iwapatie wafugaji tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihakikishe kwamba wafugaji wananufaika na mazao ya mifugo kama nyama, ngozi, maziwa, mafuta na kadhalima kuwa na viwanda vya nyama/ngozi. Inashangaza sana kuona kwamba nyama yetu haina kiwango. Hii si kweli ndugu zetu (wazungu) waliopo hapa wanafurahia sana nyama yetu, iweje sasa nchi zao zidai kuwa nyama yetu haina kiwango?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itafute ufumbuzi wa kudumu wa vijiji vya Buger, Marang, Kansay katika Kata ya Kansay inayopakana na hifadhi ya Ziwa Manyara. Pia wafugaji wa vijiji vya Endamaghana, Olpiro, Makhoromba vinavyopakana na Hifadhi ya Ngorongoro. Matatizo makubwa ni malisho na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwapatie maji nje ya hifadhi kwa ajili ya mifugo yao. Uvuvi katika Ziwa Eyasi uwekewe utaratibu mzuri.

**MHE. AMINA MWIDAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina ukanda mrefu wa bahari na imejaaliwa vilevile kuwa ni mshirika katika maziwa makuu matatu yaliyomo kwenye Bara la Afrika. Zaidi ya hayo, ina maziwa mengi madogo madogo mengi na mito kadhaa mikubwa. Maji yote haya yana utajiri mkubwa wa samaki na bidhaa nyingine za majini. Bila shaka Sekta ya Uvuvi pekee ingeliweza kuchangia kiasi kikubwa katika katika pato la Taifa na kupunguza kwa kiasi kikubwa kabisa umasikini unaoikabili jamii ya wavuvi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi miongoni mwa watu wa ukanda wa Pwani umeangamia kabisa. Wavuvi wa maeneo haya bado wanajishughulisha na uvuvi mdogo sana *(subsistence fishing)* na wanapambana na matatizo mengi. Mfano, Mkoa wa Tanga, kama Wilaya ya Tanga, Nkinga, Pangani na Muheza ukiangalia utaona kwamba Wilaya hizo hazijanufaika kutokana na uvuvi. Naomba tujiulize, tangu tupate uhuru mpaka leo, uvuvi kwa ujumla wake, uchumi wake unashuka siku hadi siku, kwanini? Jibu la haraka haraka ni kuwa wavuvi wa maeneo haya hawana wataalam wanaowasaidia, hawana vifaa vya uvuvi wa kisasa na hawapewi mikopo ili wajiendeleze. Je, tutaondoa umaskini kwa njia gani katika eneo hili la Pwani na tegemeo lao kubwa ni uvuvi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema tunataka kuondoa umasikini miongoni mwa watu wetu: Je, tuko tayari kuangalia kazi za jadi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi nchini ni mashahidi kwamba Sekta ya Uvuvi haijapata msukumo wa kutoka ili iondokane na ukale, na kujiingiza katika uvuvi wa kisasa wenye tija na uhifadhi wa mazingira. Uharibifu mkubwa kwa kutumia mabomu na sumu na nyavu za uvuvi zisizokidhi viwango ni miongoni mwa matukio yanayoendelea hivi sasa nchini. Siyo tu kwamba mabomu ya sumu yanafanya uharibifu mkubwa wa mazingira na kuhatarisha maisha ya walaji wa samaki, lakini ni wazi pia kuwa uvuvi wa namna hii ukiendelea baada ya miaka michache ijayo hakutakuwa tena na Sekta ya Uvuvi wa ndani, na wavuvi waliokuwa wanadhani wanaupiga vita umaskini watajikuta ni maskini maradufu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haijafanya juhudi za kutoka za makusudi kuwasaidia wavuvi wetu kuingia katika uvuvi wa kisasa. Hali hii imesababisha Taifa lishindwe kufaidika na utajiri mkubwa wa samaki tulionao katika eneo letu la bahari. Wavuvi wa kizalendo kutokana na kuwa na vyombo duni wamekuwa hawawezi kwenda katika maeneo ya mbali na mwambao yenye kina kikubwa cha bahari wanakopatikana samaki wengi zaidi. Hali hiyo inasababisha uvuvi katika maeneo haya kungiliwa na wavuvi wa kigeni ambao wamekuwa wakiendesha shughuli za uvuvi kinyume cha sheria na kuliibia Taifa letu utajiri wa raslimali hii ya asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa na utajiri mkubwa wa samaki, kutokana na uchache wa samaki wanaovuliwa, bei ya samaki katika soko ni ya juu kuliko inayopaswa kuwa na vilevile wakazi wa kandokando na raslimali hizi hawapati samaki wa kutosha kama chakula. Serikali imeacha wafanyabiashara wakubwa kununua kila samaki anayevuliwa na hivyo wenyeji hawawezi bei ghali ya samaki walioko katika ushindani wa bei badala yake kuambulia kula vidagaa na mapanki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kuwa, Serikali ianzishe mfuko rasmi wa kudumu wa mikopo ya masharti nafuu kwa wavuvi na wananchi wengine wenye nia ya kujiajiri kwenye sekta hiyo kwa ajili ya kununulia vifaa vya kisasa vya uvuvi na hifadhi, na kuanzisha ufugaji wa samaki *(fish farming).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashaui Serikali itoe mafunzo kwa wavuvi na kwa kiasi kikubwa mafunzo hayo yalenge katika matumizi ya njia bora za hifadhi ili kuhakikisha kuwa mavuno ya wavuvi hayapotezi ubora wake kabla ya kufika kwenye soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iimarishe shughuli za doria katika maeneo ya uvuvi ili kuhakikisha kuwa wavuvi wachache hawaendelei na utaratibu wa uvuvi unaoharibu mazingira na kuleta maangamizi makubwa kwa samaki na viumbe wengine wa majini, na ambao una mwelekeo wa kuhatarisha ajira kwenye Sekta ya Uvuvi. Lakini doria hiyo isiwe ya kuwadhalilisha watu wa Pwani kwa kuwapiga, kuwavua nguo na kuchukua samaki wao na hata kuwatesa na kuangamiza vyombo vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Serikali iweke utaratibu wenye tija kwa wavuvi wadogo na wasindikaji wa mazao ya uvuvi kwa kuhakikisha kuwa wenye viwanda hawajishughulishi na shughuli za uvuvi na badala yake watapaswa kununua samaki kutoka kwa wavuvi wadogo wadogo. Mgawanyo huu utasaidia uwepo wa mzunguko wa fedha kwa kutoa ajira kwa wananchi wetu. Wenye viwanda, watasaidia kununua zana za uvuvi za kisasa na kutoa mikopo kwa wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi maalum zifanywe kuhakikisha kuwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi wanafungua viwanda vya kusindikia minofu ya samaki katika maeneo yote yenye mavuno makubwa ya samaki, hususan katika mwambao wa bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri za Miji na Wilaya zilizoko kwenye maeneo ya wavuvi zihamasishwe kuingia ubia na Makampuni binafsi kujenga maghala ya hifadhi baridi *(cold storage facilities)* kwa ajili ya kuwasaidia wavuvi kuhifadhi mavuno ya ziada kwa kulipa ushuru kidogo.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia katika maeneo yafuatayo:-

(1) Matatizo yanayowakabili wafugaji katika Jimbo langu la Bukombe;

(2) Mambo ambayo Wizara inapaswa kuyapa kipaumbele; na

(3) Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi za Serikali kujitahidi kuwasaidia wafugaji, hasa kwa madawa, bado kuna changamoto nyingi zinazowakabili wafugaji katika Jimbo la Bukombe. Baadhi ya matatizo hayo ambayo hayatofautiani na yale yanayowakabili wafugaji wengi wa Tanzania ni:-

(1) Ongezeko la mifugo huku malisho bora yakiwa hayatoshi;

(2) Uhaba wa maji kwa mifugo, hasa kwa kuwa, kwa ujumla hakuna malambo. Lengo la Serikali la uvunaji wa maji ya mvua na kujenga/kukarabati malambo kila mahali penye mifugo halijafanikiwa. Bukombe hakuna majosho pia;

(3) Soko ni tatizo. Hakuna machinjio wala kiwanda cha kusindika nyama au mazao ya mifugo;

(4) Wafugaji hawana elimu kuhusu magonjwa au hata maana ya kufuga kisasa na kibiashara;

(5) Wataalam wa mifugo waliopo hawatoshi kwa kuwa mifugo ni wengi; na

(6) Migogoro isiyokwisha baina ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa matatizo makubwa ni ongezeko la mifugo, huku maeneo ya malisho yakizidi kuwa finyu, na uhaba wa maji kwa mifugo, Serikali ichukue hatua zifuatazo haraka:-

(1) Iharakishe michakato ya kubadilisha ufugaji wa asili uwe ufugaji wa kisasa, ambao unajumuisha hatua zifuatazo:-

(a) Kwa kushirikiana na Halmashauri, kuanzisha maeneo ya malisho ya kisasa. Itabidi kuzalisha mbegu za malisho ya kutosha na kuzisambaza katika maeneo yote yenye mifugo ili zipandwe;

(b) Ijenge malambo na majosho kwa ajili ya mifugo. Malengo ya miaka ya nyuma hayajafikiwa;

(c) Ijenge machinjio katika kila Wilaya (mfano Bukonge, Biharamulo, Geita) ili kuunda soko la wafugaji.

(d) Kuwahamasisha wafugaji kuuza mifugo yao mingi ya kiasili yenye ukosefu duni, na kuanza kuingia kwenye ufugaji wa kisasa; na

(e) Kiwanda cha kusindika nyama cha Shinyanga kijengwe haraka ili kutatua tatizo la soko la mifugo.

(2) Ili kutatua tatizo la wataalam wa mifugo, Serikali iongeze udahili wa wanafunzi katika vyuo vyake. Kadhalika, Vyuo vya Mifugo viimarishwe kwa kuifanya mitaala iwe ya kisasa zaidi na kutumia vifaa vya kisasa katika mafunzo na utafiti.

(3) Zoezi la kutenga maeneo kwa ajili ya wafugaji liharakishwe. Huko Bukombe zoezi hili liko nyuma Sana. Hali hii inachangia sana migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bukombe ina nafasi nzuri ya kufuga samaki kwa kuwa inayo maeneo mengi ambako mabwawa ya kufugia samaki yanaweza kuchimbwa. Hata hivyo, jambo hili halijafanyiwa kazi. Nina mapendekezo yafuatayo:-

(1) Serikali kupitia Halmashauri ihamasishe ufugaji wa samaki kama shughuli ya kibiashara;

(2) Serikali ihamasishe uundaji wa vikundi vya ushirika ili baadhi ya wawakilishi, wapewe elimu ya ufugaji wa samaki kutumia mabwawa; na

(3) Vikundi vya ushirika vifundishwe namna ya kuchimba na kuandaa bwawa la samaki. Lengo liwe kila Kata kuwa na mabwawa kadhaa yanayomilikiwa na makundi ya ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri maswali yafuatayo:-

(1) Wizara imefaulu kutenga maeneo ya malisho kwa ajili ya ufugaji wa asili katika Wilaya ngapi? Bado Wilaya ngapi?

(2) Tatizo la malisho bora limeendelea kuisakama Sekta ya Mifugo. Wizara inalikabilije tatizo hili? Mbegu za malisho (mfano zinazozalishwa Kituo cha Kongwa) zimesambazwa katika Wilaya ngapi na matokeo yamekuwaje?

(3) Wataalam wangapi wa mifugo walioajiriwa katika Wilaya 133 za Tanzania?

(4) Wafugaji wangapi ambao hadi sasa wamepata mafunzo ya ufugaji wa kisasa?

(5) Ni malambo ya majosho mangapi yamepangwa kujengwa katika mwaka 2011/2012?

(6) Lengo la Serikali ni ufugaji wa kisasa na wa kibiashara. Je, mbegu za mifugo bora yenye tija kubwa imeelekezwa katika Wilaya ngapi?

**MHE. EUSTACE KATAGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu nzima ya Wizara kwa kuandaa mpango mzuri na uwasilishaji mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa uendeshaji mzuri wa Wizara ambayo ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni sekta iliyolala. Hakuna Mtanzania nayejihusisha na hata kuwekeza kwenye uvuvi. Uvuvi umeendelea kuwa mdogo na wa zana duni mno *(the old canoe).* Watanzania wahamisishwe kujituma katika sekta hii. Kidogo wakazi wa maeneo ya Ziwa Victoria wanajaribu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na *resistance* iliyopo, lazima tuendelee kuangalia mwelekeo wa ufugaji wa kisasa – ng'ombe wachache kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NARCO* inawasaidia na kuwashauri wafugaji wadogo hasa wanaozunguka ranchi zao, kwa mfano Misenyi Ranchi waendelee kufanya hivyo ili ufugaji wa hawa wafugaji wadogo uboreke. Wawasaidie kupata mbegu bora, utibabu na kadhalika.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mungu kwa baraka zake kwetu. Naomba nichukue fursa hii kuchangia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Kwanza kabisa, naomba nimpongeze Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda kwa juhudi yao kubwa kuleta mabadiliko katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi ili kuongeza tija kwa wafugaji na wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri pamoja na Naibu Waziri pia kwa juhudi na jitihada yao wakishirikiana na wataalam wa Wizara ili kuleta mabadiliko katika Sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Wizara na Serikali kuangalia upya suala la Mifugo na Uvuvi. Ni sekta muhimu sana katika nchi yetu na inagusa maisha ya wananchi wengi, wafugaji, wavuvi, na wananchi wanaotumia mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naishauri Serikali iongeze Bajeti katika Wizara hii, bajeti inayoombwa ni ndogo sana ukilinganisha na changamoto zilizopo katika sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ufugaji wa aina nyingi, ng'ombe wa nyama na maziwa, mbuzi wa nyama/maziwa, kondoo, kuku, bata, nguruwe, samaki, nyuki, bata mzinga, mbwa, farasi na ufugaji nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu wake, tungesema wataalam wengi zaidi waandaliwe, waliopo ni wachache sana hasa madaktari wa mifugo *(vegetarians)* na wataalam wengine ambao watasaidia kutoa huduma na kutoa elimu ya ufugaji bora yenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ingewekeza zaidi katika Chuo Kikuu cha Sokoine ili kiweze kutoa wataalam zaidi waliobobea katika sekta hiyo. Kwa sasa chuo kinahitaji kukarabatiwa miundombinu na Maabara inahitaji kufanyiwa kazi zaidi, vifaa vilivyopo haikidhi mahitaji ya wanafunzi waliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iwekeze zaidi katika mabwawa yenye matumizi mchanganyiko *(multi purpose dams)* katika maeneo ya mifugo hasa jimboni kwangu Babati Vijijini na katika Mkoa wa Manyara ambao ni Mkoa wa wafugaji na kilimo. Kuna maeneo ya vilima vitatu, Manori, Manyara (ya Magara) Manie, Gidas, Utana, Dabil vingepewa kipaumbele cha mabwawa ya mifugo ili wasihamehame kutafuta maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aina bora za dume zingetolewa katika kila kaya ya ufugaji ili tuboreshe mifugo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ingeweka mkazo wa kuanzisha vikundi vilivyosajiliwa vya wafugaji ili wao pia waweze kupata mikopo yenye riba nafuu. Leo hii wafugaji wengi hawapati mikopo ya aina yoyote. Wanalazimika kuuza mifugo kwa bei ya chini kwa ajili ya shida ndogo ndogo na akiba yao ni mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali na Taasisi ya kifedha *(TIB)* Benki ya Raslimali nchini iangalie namna ya kumkopesha mfugaji mifugo ikiwa ndiyo dhamana. Mifugo hiyo inaweza kuwekewa bima kama wanavyofanya huko India. Hii itawezesha wafugaji kukopa na kuendeleza ufugaji wa kisasa na kuongeza tija katika ufugaji wa ngombe wa maziwa, kuku wa nyama na wa mayai ambapo tunaagiza kuku na mayai kutoka nje ya nchi. Pia ufugaji wa bata mzinga *(Turkey),* bata msemano *(gees)* samaki wa kufuga *(Aquaculture)* na ufugaji wa nyuki. Elimu ingetolewa kwa wafugaji ya kujiendesha kibiashara zaidi na wawe wanavuna mazao yao, yaani mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika kuendeleza uvuvi na ufugaji wa samaki, nashauri Serikali iangalie maeneo muhimu ya kufuga samaki yenye tija, pawe na majaribio ili wananchi waweze kuiga katika Jimbo la Babati Vijijini, katika Bonde la Kivu maarufu kwa kilimo cha mpunga. Tunaiomba Wizara na Serikali kuangalia namna ya kutupatia elimu na mafunzo ya ufugaji wa samaki katika maeneo hayo ya Tindiga na yenye maji. Pia kutoa msaada wa kitaalam ili eneo hilo ambako kuna Gereza dogo la Magugu pia wapate kisima cha maji ili wawe mfano wa ufugaji wa samaki na kilimo cha mpunga. Ufugaji huu naamini unafanyika katika nchi za China, Indonesia, na Thailand.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri msukumo uwekwe zaidi katika ufugaji wa nyuki nchini. Hii itawapatia wananchi wengi zaidi mapato, lishe bora na pia itapunguza uharibifu wa mazingira. Misitu mingi inaharibiwa kwa ajili ya wanaoishi hapa jirani kukosa mapato na faida kutokana na misitu jirani na kwao. Elimu zaidi itolewe na vikundi viwezeshwe kupata mkopo ili waweze kufuga kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo ya Pwani, Visiwa vya Mafia, Zanzibar na Pemba tunashauri Serikali itoe elimu na mafunzo ya vitendo kwa ufugaji wa (*oysters*) samaki wanaozalisha lulu *(pears)* nchi za *South East Asia* wanapata faida kubwa sana kutokana na biashara hii ni mabilioni ya dola katika biashara ya lulu. Tunaweza kuwaondolea umasikini kabisa wavuvi wetu na wananchi wanaoshi Pwani na jirani na bahari. Pia ufugaji wa samaki wa maji baridi *(trout)* na aina nyingine ya samaki ingewekewa mkazo na umuhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ya mifugo na uvuvi inaweza kuchangia kwa sehemu kubwa pato la Taifa kwa njia moja au nyingine. Tunaomba Wizara hii ishirikiane na Wizara nyingine kama za Kilimo, Maliasili na Utalii, Ardhi, Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais, Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Viwanda na Biashara pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI na Uwekezaji wa uzalishaji ili kwa pamoja kwa kushirikana na wadau, sekta hii ipate umuhimu wake na iwe na mchango kwa pato la Taifa na kuwaondolea umaskini na pia kuleta tija kwa lishe bora kupatikana nchini kwa kupata mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu zaidi itolewe kwa wananchi wetu ili mgogoro baina ya wafugaji na wakulima na makundi mengine usiwepo. Wote wana haki ya kuwepo na wanatakiwa kuishi kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imelisahau kabisa Ziwa Nyasa. Uvuvi ulioko huko ni wa enzi za Adamu na Hawa. Zaha zote ni za kizamani. Ni Ziwa pekee linalotumia mitumbwi badala ya maboti katika kuvua samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu ya Uvuvi hutolewa kwenye maeneo ambayo haina uhusiano na uvuvi mfano Iramba, Mpwapwa, Singida, Moshi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam wa uvuvi hasa Maofisa Uvuvi hawana utaalam wa uvuvi hata kuogelea hawajui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upandikizaji samaki ziwa nyasa ni muhimu kwa vile upande wa pili wa ziwa nchi ya Malawi samaki hupandikizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia hadi kufikia hapa leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuchangia suala la ufugaji. Ni vipi tatizo la wafugaji kuvamia mashamba litakwisha? Ni kwa nini Serikali inapohamisha wafugaji kutoka eneo fulani (Mkoa/Wilaya) hayaanzi maandalizi ya miundombinu itakayosaidia kuwawezesha wafugaji wawe kwenye eneo ambalo halitaleta migogoro na hasa ukizingatia kwamba nchi yetu ina eneo kubwa la Ardhi. Naomba Serikali ipatie majibu ya utatuaji wa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Pwani una eneo kubwa la bahari, na visiwa vidogo vidogo, vingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya juhudi za Serikali kwa wavuvi, ni vyema sasa ikaongeza mafunzo, vifaa na mbinu mbalimbali za kilimo cha mwani kwa wenye uzoefu wa kilimo hicho. Je, Serikali imejipanga vipi katika kuongeza bei ya mwani na kuwapatia soko wakulima hao na ukizingatia wakulima wengi ni wanawake? Naiomba Serikali inipatie majibu.

Mheshimiwa mwenyekiti, je, ni lini ujenzi wa machinjio unaoendelea Ruvu Mkoani Pwani utakamilika, ili kuwe na machinjio ya kisasa na kutoa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji na Madaktari wote wa mifugo wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Hanang ndiyo yenye mifugo mingi katika Mkoa wa Manyara, lakini haina miundombinu kama Mabwawa/Malambo, majosho, *crash* na Minada. Je Wizara inajua hivyo. Wilaya ipo kwa sehemu kubwa ndani ya Bonde la Ufa, hivyo, upatikanaji wa maji ni matatizo makubwa. Naiomba Wizara iweke katika mipango yake ujenzi wa malambo, jukumu ambalo haliko katika uwezo wa wananchi. Kulikuwa na malambo yaliyojengwa kabla ya uhuru lakini yote yamebomoka au kuharibika. Malambo hayo ni pamoja na Gidagamod, Woreta, Gidohababieg na kadhalika. Ninaiomba Wizara ione umuhimu wa kukarabati malambo hayo au/na kujenga mapya. Nitashukuru kama Wizara itatolea tatizo hili kauli na wananchi wa Hanang watashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na matatizo ya ufugaji, nilisahau kuongeza matatizo ya wavuvi Ziwa Basotu ambao wanakabiliwa na ukosefu wa zana bora za uvuvi. Ninaomba Wizara iwatume wataalam ambao tayari wana ushirika ili waweze kuwaelekeza suala zima la uvuvi bora. Wavuvi hawa wanataka kuelimishwa juu ya zana bora kwa uvuvi wao na nyakati bora za uvivu. Vile vile wanahitaji kushauriwa juu ya ujenzi wa soko la samaki na ikiwezekana wasaidiwe ujenzi wa soko bora la samaki. Wavuvi wasizalilishwe kwa kushindwa kiholela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na uvuvi haramu, wanaomba wasaidiwe usafiri ili walinde na kufanya doria kuzungukia ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hanang ni mbali na eneo la kupata zana bora. Wilaya inashauri njia rahisi ya kupata zana hizo. Matumizi ya makokoro yanaashiria samaki wasiotosheleza soko. Hivyo ni vyema tukaige Nigeria kwa wananchi kuanzisha mashamba ya samaki katika maeneo yao au *fish ponds*. Raslimali zinazotumika kukimbizana na wavuvi haramu zielekezwe katika kuwaelimisha wananchi kuanzisha *fish ponds*. Hatua hii itasaidia sana kwa sekta ya uvuvi kuondoa umaskini kati ya wananchi wetu.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo yote ni ya muhimu sana na hasa ng'ombe na mbuzi kwa ajili ya nyama na maziwa. Lakini wafugaji wanaelimishwa kuhusu ufugaji bora? Ng'ombe wanapigwa na ngozi yake kutobolewa hovyo na hivyo kuathiri thamani ya ngozi. Je, Serikali inajipanga vipi kuhusu kuongeza thamani ya bidhaa zinazotokana na mifugo yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa kuwa samaki wanapungua katika Ziwa Victoria na kusababisha bei ya samaki kupanda. Je, Serikali ina taarifa hii na inachukua hatua gani kukabiliana nalo?

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mungu kwa kuendelea kunijalia uhai na pia kutujalia raslimali hali ikiwemo samaki wa mito, maziwa na bahari wa aina kwa aina. Wanaolipa Taifa letu, pato kubwa japo kwa upande mwingine halijasimamiwa vyema ili kunufaisha vizuri sana Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kwa kuwa natoka katika Mkoa (Mara) ambao mbali na ufugaji, lakini pia ni Mkoa unajishughulisha sana na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa ninaotoka unajishughulisha sana na uvuvi wa samaki wa aina ya sangara ambao minofu yake imekuwa ikiuzwa nje ya nchi wakati maeneo ya samaki wanapotoka ni duni sana (kiuchumi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya wavuvi wa Mara na Kanda ya Ziwa siyo nzuri, wakati wawekezaji wa viwanda vya minofu ya samaki hao ndiyo pekee wanaofaidi raslimali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na juhudi za Serikali za kutengeneza Maabara za kisasa (Nyegezi) Mwanza na maeneo mengine, lakini bado samaki wanaoliwa na Watanzania, usalama wake ni wa mashaka, fedha nyingi zimetumika kuweka utaratibu na ujenzi. Sambamba na ukaguzi wa mazao ya samaki, lakini ni kwa ajili ya wanaoliwa nje huku Serikali ikiwa haijatilia mkazo wa samaki wanaoliwa ndani hasa maeneo ya vijijini hasa samaki wanaotokana na mito na mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado bidii ya Serikali katika kuweka ufugaji wa samaki kwa ajili ya matumizi ya ndani ni mdogo sana ukilinganisha na mahitaji wakati muafaka sasa kuhakikisha elimu ya ufugaji samaki na ulaji wa samaki upelekwe katika shule zenye maeneo ya kutosha na pia hamasa ifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni muhimu kuongeza viwanda vidogo vya usindikaji wa samaki kwa ajili ya matumizi ya ndani kwani bado uuzaji wa samaki ndani ya nchi unafanyika kienyeji na usiozingatia afya ya mlaji. Tuwekeze katika miundombinu ya kusafirishia mazao ya samaki hasa katika kujenga viwanja vikubwa vya ndege katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa kama vile Mara, huku njia za reli kutoka Mwanza na Kigoma ziimarishwe ili samaki kutoka maeneo hayo ziweze kufika katika bandari kuu ya Dar es Salaam na kiwanja cha ndege kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda katika mifugo kwa takwimu nilizonazo Tanzania ni nchi ya tatu kwa wingi wa mifugo (Afrika) lakini bado pia mifugo mingi haimpi faida mfugaji wa Tanzania pato kama inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Tanzania wapo ng'ombe, mbuzi, kondoo na mifugo mingine. Upo msemo kutoka katika makabila ya Mara kuwa, "katika ng'ombe hakuna cha kutupa", vyote ni mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni ukweli usiopingika, ukizingatia kila kilichopo katika ng'ombe ni cha kutumia ukianza na kinyesi – mbolea, ngozi – viatu, mikoba na kadhalika, mifupa-sahani na kadhalika, maziwa – kwa ajili ya afya na kwato – gundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado elimu kwa wafugaji ni ile ya asili na upatikanaji wa dawa za mifugo na za kuoshea wanyama ni ghali ambazo sio wakulima (wafugaji) wengi wanazimudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya Serikali ya kutengeneza maeneo ya hifadhi na kupunguza maeneo ya malisho bado ni tatizo kubwa linalopelekea wafugaji wengi kuhama na wakati mwingine kupelekea wafugaji kwenda kulisha katika maeneo ya kilimo na kusababisha uvunjifu wa amani na kuleta vita vya wenyewe kwa wenyewe, ni kosa kubwa sana na hatari kwa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuona bado tunawaita wawekezaji kuja na kuwapa ardhi kubwa ambayo ingetumika katika malisho na kuongeza migogoro isiyo ya lazima. Upo umuhimu wa Serikali kuangalia na kuepusha haya kwa kutochukuwa ardhi ya malisho na kuyafanya hifadhi sambamba na kutoa elimu ya uvunaji mifugo na pia kuwapa mafunzo ya kuongeza thamani ya ngozi na namna bora ya kuandaa ili kumpatia mkulima pato la kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana kuona sasa nchi yetu inatumia fedha za kigeni kuagiza samaki kutoka nje ya nchi na tayari kuna samaki wenye mashaka ambao yatari wapo nchini toka Japan ambao wameripotiwa kuwa na mionzi yenye athari: Je, kuna umuhimu gani wa kuwa na Maabara ya kukagua sumu na mionzi pale Nyegezi ilhali samaki wenye mashaka wanaingia nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado lipo tatizo la uingizaji wa zana haramu kutoka katika nchi za China na India. Zana hizi zinazoagizwa toka nje zinazopitia katika mipaka yetu yenye waangalizi wanalipiwa kutokana na kodi zetu. Ipo haja sasa ya kuwawajibisha watumishi na wasimamzi wa *entry point* ambao wamekuwa wakiacha zana hizi kuingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha Serikali kufukuzana na wavuvi wanaotumia nyavu zenye matundu madogo ni kuweweka wavuvi katika hali ya kuchukia Serikali. Si muda muafaka sasa wa kuzuia uingizaji huo haramu.

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima leo hii na kunipa uwezo wa kuchangia hotuba hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia kwa uchache sana na naomba nianzie na shughuli za mifugo. Sensa ya mifugo iliyofanyika katika vipindi tofauti inaonyesha kuwa kuna ongezeko kubwa la mifugo nchini. Ni vizuri, lakini hata hivyo kuna tatizo kubwa la udhibiti wa wanyama, na hivyo kusababisha matatizo na migogoro mingi na sekta nyingine za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na migogoro na uvamizi wa mifugo katika maeneo ya kilimo, eneo ya mabwawa ya maji, hivyo kuna umuhimu mkubwa wa kudhibiti mifugo hiyo kwa kuwatengea wafugaji maeneo maalum ya ufugaji ili kupunguza migogoro hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu sheria ya udhibiti au kupunguza mifugo. Sheria hii inaonekana haikuwashirikisha ipasavyo wafugaji, hivyo kutoeleweka na wafugaji hao, na hivyo upunguzaji wa mifugo, wafugaji wanahisi kuwa Serikali inawanyang'anya mifugo yao kupitia sheria. Bado naishauri Wizara iendelee kutoa taaluma ya dhumuni la sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ongezeko la uzalishaji wa nyama nchini, lakini bado ulaji wa nyama kwa Watanzania ni mdogo sana. Kwa mujibu wa *WHO*, kwa mtu anatakiwa ale nyama kilo 50 kwa mwaka, lakini wastani wa Tanzania ni kilo 11 kwa mwaka kwa mtu. Kama Waziri alivyosema katika hotuba yake, walaji wa nyama zaidi ni kwenye mahoteli na maeneo mengine yenye watu wenye kipato. Bado kuna tatizo kubwa la Watanzania kula nyama. Wengi wanashindwa kutokana na uwezo. Pamoja na uzalishaji mkubwa wa nyama, lakini bado bei ya nyama ni kubwa na Watanzania walio wengi hawamudu bei hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kwenye mifugo ni utumiaji wa dawa za binadamu na kupewa wanyama kwa ajili ya kuongeza uzito. Kuna tetesi kubwa kuwa sasa hivi hasa katika miji mikubwa kama vile Dar es salaam na Arusha mifugo, hasa kuku wa nyama wanapewa dawa za

kurefusha maisha kwa wagonjwa wa Ikimwi *(ARV)* ili wakue haraka na kuongeza uzito, lakini pia kunatumiwa dawa za *tetracycline* kwa maradhi ya mdondo. Nahisi jambo hili ni hatari na ninaomba katika majumuisho ya Waziri kwanza anithibitishie tetesi hizo na kama hiyo hali ipo: Je, Wizara inasemaji kuhusiana na matumizi ya dawa hizo kwa mifugo, na athari ambazo pia zinaweza kutoka kwa binadamu iwapo atatumia nyama hiyo? Lakini pia, Je, Wizara itachukua hatua gani dhidi ya wafugaji na wafanyabiashara wanaofanya hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nakushukuru sana, naomba kuchangia hoja.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua, katika Mkoa wa Shinyanga, ni kiasi gani kwa kila Wilaya idadi ya mifugo iliyonenepeshwa hadi mwaka huu?

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwasilisha kwako mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kuhusu Makadirio ya Matumizi ya fedha 2011/2012 kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Dr. Mathayo David (Waziri) kwa uwasilishaji wake mzuri na wenye weledi wa hali ya juu kabisa. Pili, nampongeza kwa imani, uvumilivu na moyo wa kujitolea sana katika kutusaidia sisi kama Wabunge, lakini pia katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku kiutendaji kwa Serikali na wananchi kwa ujumla bila kuchoka na bila uwoga. Nampongeza pia Naibu wake, Mheshimiwa Benedict Ole Nangoro na watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mazuri niliyoainisha, naomba nitoe mchango wangu katika maeneo machache kuwiana na hali halisi ya Jimbo la Kilwa Kaskazini na Wilaya ya Kilwa kwa ujumla. Hotuba ya bajeti imezungumzia mapinduzi ya ufugaji wa kuweka mioundombinu katika maeneo yote ya ufugaji. Wilaya ya Kilwa ni miongoni mwa maeneo ambayo wamepokea wafugaji wengi sana, pamoja na Serikali kujenga majosho, lakini eneo la Puyu, Kata ya Miteja halina lambo na mara zote wataalamu wamekuwa wanakuja kuchukua vipimo na tafiti bila utekelezaji kwa muda mrefu sana, tunataka utekelezaji sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya uvuvi yamepewa kipaumbele, ila napenda Serikali ichukue hatua zaidi kuimarisha ulinzi baharini kwa maana mpaka sasa hali ni mbaya na wananchi wanazuiwa kuvua katika baadhi ya maeneo huku wengine (wageni) wanavua na kuondoka na raslimali hizi bila kuzingatia malipo au athari zozote ambazo zitajitokeza baadaye. Ni heri wananchi wanaozuiwa kuvua basi wapewe mbinu mbadala ili kujiendesha katika maisha yao. Lakini pia zipo meli ambazo zinavua katika eneo la Somanga hadi Masoko na wana kawaida ya baada ya kuvua huchambua samaki na kuwatupa baadhi kufuatana na mahitaji yao kwa kuwafunga kwenye mifuko. Kwanini wasiwape wavuvi wadogo? Lakini hakuna mwenye hakika kama wamelipia leseni na mazao waliyovua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la mgawanyo wa ardhi baina ya wafugaji na wakulima katika nchi yetu ni kubwa sana na ipo haja sasa ya Serikali kuangalia upya namna ya kuboresha eneo hili kwa maana waathirika wakubwa ni wananchi ambao ni wa kipato cha chini. Naishauri Serikali iendelee kuboresha na kuainisha mipaka ili kusiwe na mwingiliano, lakini pia itolewe elimu ya kutosha, nini umuhimu wa kushirikiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni wakati muafaka wa kuangalia namna ambayo wananchi wanaoishi ukanda wa Pwani na maziwa kupata gawio kutokana na mauzo ya samaki na mazao mengineyo kama wale wa maeneo ya migodi wanavyopata *(royalty).* Hii itasaidia sana kuinua jamii husika pamoja na kusaidia wavuvi wadogo wadogo kupata dhana bora za kuvulia.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na mkakati wa kuimarisha soko la bidhaa za mifugo na samaki (maziwa, ngozi, nyama na kadhalika) lakini pia tuangalie namna ya kudhibiti bidhaa zinazotoka nje kwa maana zinatoa ufinyu wa soko kwa bidhaa zetu. Pamoja na mpango huu, tuhakikishe tunapata namna bora zaidi kwa kufufua viwanda vyetu bila kutegemea

wawekezaji wa nje ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa mzigo kwa wananchi na Taifa kwa ujumla na hii pia inapelekea kelele nyingi kwa wasiofahamu maana ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali ya ukame, ipo haja ya sasa Serikali kuelimisha na kuweka mkakati wa kutumia mabaki ya mazao kama mabua ya mahindi na magunzi yake, mtama, mashudu, majani ya maharage, majani ya migomba na kadhalika ili wanapovuna wahifadhi na kuwa akiba wakati wa ukame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali iliyopo sasa, suala la kilimo ni muhimu sana, na kama hotuba ilivyoainisha ni vyema tukatilia mkazo zaidi katika zana bora. Napendekeza tuyatumie vizuri majeshi yetu (JKT, Magereza, JKU) kwa kuyapa teknolojia na pia tuwaongezee mtaji ili wafanye ufugaji wa biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ichukue jitihada za makusudi kuelimisha jamii katika ufugaji wa kuku wa kienyeji ili kuinua kipato cha watu wa hali ya chini, lakini pia kuongeza mapato ya Serikali katika ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili yote haya yafanikiwe na kupata ufanisi wa kutosha, naishauri Serikali iharakishe mpango wa uanzishwaji wa Benki ya Kilimo ambayo itabeba pia wavuvi na wafugaji kama ulivyoanishwa katika hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba nikushukuru kwa kunipokelea maoni yangu kwa kuamini kuwa yatafanyiwa kazi stahiki. Nakutakia kila la kheri, namwomba Mungu atulinde sote.

Naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naunga mkono hoja bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hoja, naomba Serikali iangalie sana Mkoa wa Shinyanga kwa huruma, kwani Mkoa huu umekumbwa na ukame wa muda mrefu sana kiasi ambacho wananchi wamekuwa wakihangaika kwa muda mrefu kuhama Mkoa wao na kulazimika kuhamia Mikoa yenye malisho na maji ya kutosha. Siyo kwamba hawapendi kuishi katika Mkoa wao, lakini inawalazimu wafanye hivyo ili kunusuru mifugo yao, kwani ng'ombe, mbuzi na kondoo kwetu sisi ni kama almasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali na kwa sababu Serikali iliyopo madarakani ni sikivu, nina hakika haya yatafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihakikishe imetuchimbia malambo (mabwawa) kwa ajili ya mifugo yetu. Mifugo isife kwa kukosa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihakikishe kila Wilaya ijipange kutenga maeneo kwa ajili ya wafugaji, kwani tumechoka kuitwa vibarua wa Mikoa mingine tunayohamia, kwani wamesahau hata kama ng'ombe hawa ndiyo wanawasaidia kulima kutoka jembo la mkono kuingia katika kilimo cha jembe la kukokotwa na ng'ombe. Tunaupenda Mkoa wetu na tunaipenda mifugo yetu ndiyo maana tunahangaika nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iharakishe kufungua kiwanda cha nyama kilichofungwa kwa muda mrefu sasa. Kiwanda cha nyama Shinyanga hakifanyi kazi na kulazimu wafugaji kuhangaika na mifugo kuisafirisha kwenda Dar es Salaam, wakati wangeweza kufaidi mifugo yao kwa kuuza karibu na maeneo yao wanayoishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba maelezo ya kutosha wakati Waziri anajumuisha maelezo yake, awaeleze wananchi wa Mkoa wa Shinyanga ni lini kiwanda hiki kitafanya kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Mheshimiwa Benedict Ole Nangoro, Katibu Mkuu wa pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri yenye nia thabiti kuboresha Sekta ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge la Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa kazi kubwa iliyofanywa kushauri mambo mbalimbali kwenye bajeti hii kwa lengo la kuboresha bajeti hii kwa maslahi ya wafugaji na wavuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Singida kujenga kiwanda hiki ambacho kinafanya kazi ya kuwamba ngozi pamoja kutengeneza bidhaa mbalimbali kwa kutumia ngozi. Kwa kuwa Mkoa wa Singida ni wa nne kitaifa kwa ufugaji wa ng'ombe, hivyo ngozi ni nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali mambo yafuatayo:-

(1) Kiwanda kuongezewa vitendea kazi mbalimbali kwa kutengenezea bidhaa kama viatu, mishipi na kadhalika ili kiwanda kiweze kupata fedha za kujiendeleza;

(2) Wataalam waongezwe katika kiwanda hiki pamoja na kuwapeleka kozi wataalam waliopo ili kupata taaluma zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza juhudi za Halmashauri ya Wilaya ya Singida kwa kusogeza huduma kwa wananchi wafugaji kwa kujenga kiwanda kidogo cha kusindika maziwa. Ni ukweli usiopingika kuwa itawasaidia sana wafugaji kuondokana na adha ya kupeleka maziwa mjini Singida kila siku kwa baiskeli na kuyauza kwa bei ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wilaya zote za Mkoa wa Singida ni za wafugaji, ninaiomba Serikali kukipanua kiwanda hiki na kuongeza vitendea kazi ili maziwa toka Wilaya zote yaweze kupelekwa hapo kusindika ili yawasaidie wafugaji kukuza uchumi wao kupitia maziwa. Vile vile wataalam wapatiwe taaluma zaidi ili waweze kufanya kazi zao kitaalam zaidi kwa lengo la kuyafanya maziwa hayo yawe na soko la kitaifa, sio Singida tu kama ilivyo maziwa ya Tanga na Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kueleza kuwa Mkoa wa Singida una mifugo mingi sana, napenda kuishauri Serikali kuhakikisha kila Kijiji kujengewa josho lake ili kuwapunguzia adha wafugaji wa kupeleka mifugo mbali kwenda kuiogesha. Vipo vijiji ndani ya Mkoa wa Singida, havina majosho au kama yapo, basi yamechakaa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna tatizo la madawa ya mifugo kuchelewa kupeleka na kusababisha magonjwa ya mifugo kuathiri mifugo. Hivyo naiomba Serikali kupeleka madawa vijijini kwa utaratibu unaofaa. Hii itasaidia sana kuzuia kabisa magonjwa ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kujitahidi sana kuboresha Sekta ya Mifugo, bado kuna upungufu wa Maofisa Mifugo wa Kata ingawa pia Kata ni kubwa sana, kwani zina vijiji vingi na vyote vina wafugaji. Ni vyema Serikali iajiri Maafisa mifugo wa Vijiji. Hii itasaidia sana sekta hii kuwasaidia wafugaji kuwa na ufugaji wa kisasa wenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wengi bado wanapenda kuwa na mifugo mingi ambayo haina lishe bora. Vile vile hata soko lake linakuwa dogo sana wakati ule ule wafugaji hawana nyumba bora, malazi mazuri, lishe bora na watoto hawasomi. Ni hakika Maafisa Mifugo wakipelekwa vijijini watasaidia sana kuwapa ushauri wa kitaalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kuwapa Maafisa Mifugo usafiri kulingana na ukubwa wa kazi na maeneo ya kazi mfano Afisa Mifugo wa Kata, pikipiki na Afisa Mifugo wa Kijiji apewe baiskeli ili kuwezesha kufanyakazi zao ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuitaarifu Serikali kuwa wavuvi wa Ziwa Kitangiri wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, kwani wengi wao hawana vitendea kazi vyenye tija. Ninaishauri Serikali iwasaidie wavuvi mikopo yenye riba nafuu ili waweze kununua vifaa mfano nyavu na kadhalika kwa uvuvi wenye tija.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo raslimali nyingi katika Taifa letu ya kutuwezesha kuondoa umaskini na kukuza uchumi wa Taifa letu kama vile bahari, maziwa, mito na mabwawa ya asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ni ndogo ukilinganisha na umuhimu wa Wizara hii. Nashauri bajeti hii ili kutoa umuhimu wa mipaka ya bajeti, vifungu vya fedha vitenganishwe, mifugo bajeti yake na uvuvi bajeti yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wa Ziwa Rukwa hutumia zana duni kama vile mitumbwi ya kuchongwa kwa kutumia miti ya miembe, misufi na miti mingine ya asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Rukwa linatoa ajira kwa watu wengi sana kwa wavuvi wadogo wadogo ili kupata mahitaji yao ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kutumia zana duni, madhara yafuatayo hutokea: kuzama majini. Yapata wavuvi 5 – 8 hufa maji kila mwaka kwa matumizi duni ya zana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi haramu kwa kukosa zana za kisassa, kunasababisha wavuvi kuvua kandokando ya Ziwa Rukwa na kwenye mazalia ya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mamba wengi katika Ziwa Rukwa huleta madhara makubwa sana, wanakula samaki na kufanya uhaba wa samaki, wanakamata wavuvi na kuwala. Yapata wavuvi 3 – 4 huliwa na mamba kila mwaka. Akina mama na watoto wanaokwenda kuchota maji wapatao 1 – 2 hukamatwa na mamba kila mwaka. Hivyo, Serikali iwapunguze hao mamba. Majeruhi wapatao 6 – 7 hujeruhiwa kila mwaka. Serikali itoe fidia kwa ndugu wa Marehemu walioliwa na mamba, kwa ajili ya gharama za matibabu na kuwawezesha kupata riziki katika kipindi cha matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wito kwa Serikali:-

- mikopo ya zana za kisasa kwa wavuvi;
- *engine* za boti;
- ajira kwa mabwana samaki; na
- Elimu ya mazingira ya kuhifadhi maziwa, mito, na mabwawa na hasa ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea kuhusu unyanyasaji wa wavuvi. Wavuvi hunyang'anywa nyavu na kuchomwa moto, hunyang'anywa mitumbi na kuipasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutangulize elimu kwanza kwa wavuvi kabla ya kuchukua hatua kali kwani tutakuwa tunazalisha na kuongeza umasikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika eneo la kuhamishwa hamishwa wafugaji hasa walioko Mikoa ya Shinyanga, Mwanza na Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wamekuwa wakiishi kama wakimbizi ndani ya nchi yao. Hivi ni kwa nini Serikali inafikiri kuwa wafugaji wa Tanzania hawana haki ya kuwa na makazi ya kudumu na badala yake kuishi kama wakimbizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itafute njia mbadala itakayowawezesha wafugaji kulisha na kunywesha mifugo yao katika maeneo wanayoishi badala ya kuhamahama wakisaka malisho na maji kwa ajili ya mfugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kuhusu suala la kuingiza samaki nchini. Hivi kweli nchi yetu inajitaji kuagiza samaki kutoka nchi za nje wakati nchi yetu ina Bahari ya Hindi, ziwa Victoria, Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika, mito na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na taarifa zinazosema kuna samaki wenye mionzi kutokea Japan wameingizwa nchini, Serikali itoe maelezo, ni kwa nini inaruhusu Makampuni kuingiza nchini samaki jambo linalowashangaza Watanzania na dunia nzima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naitaka Serikali itoe maelezo ya kutosheleza kuhusu samaki waliongizwa nchini. Kwa wale waliotumia samaki hao, naitaka Serikali ipange utaratibu wa kuchunguza afya zao na endapo watakuwa wameathirika, basi Serikali itoe fidia kwa waathirika hawa mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono hoja endapo madai yote niliyoyatoa hapo juu yatatolewa maelezo ya kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. RUKIA K. AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina vyanzo vingi vya kupatia mapato ili wananchi wetu waondokane na umaskini uliokithiri kama vile uvuvi. Serikali yetu iwaandae watu wetu namna ya kuvua samaki kwa njia ya kisasa. Watu wetu wapewe taaluma ya uvuvi, wasiharibu matumbawe, kwani ndio mazalia ya samaki. Wasitumie nyavu za matundu madogo na kuvua samaki wadogo wadogo. Watanzania wameshindwa kufaidika na sekta hii ya uvuvi kwa kutokuwa na Elimu ya Kutosha. Zipigwe marufuku nyavu hizi kuingia nchini, wala kutengenezwa na wala kuuzwa. Pawekwe sheria atakayeuza au kutengeneza au kuingiza nyavu hizi katika nchi, pawekwe viwanda vya kusindika samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo ni mingi sana, lakini mapato yake ni madogo. Watu wetu wapewe taaluma namna ya kufuga kwa njia za kisasa. Serikali haijaweka utaratibu, elimu ili wafugaji wetu wanufaike na mifugo yao na Serikali iondokane na mzigo wa umaskini kwa wananchi wetu. Wafugaji wetu wapewe tiba ya mifugo yao ili nyama iwe bora kwa walaji. Pajengwe viwanda vya kusindika nyama ili tuweze kusafirisha nje na wafugaji wetu wanufaike. Hii itasaidia kunufaisha nchi yetu na wafugaji nao wataweza kupata fedha za kujiendeleza kiuchumi kwa kusomesha watoto wao na mambo mengine.

**MHE. SAIDI M. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja hii. Kuhusu bajeti, kuna mambo kadhaa ambayo naomba Waziri anieleze wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza wako wavuvi ambao walisalimisha nyavu zao haramu na kuahidiwa *fibre boat* na nyavu za kisasa, vikundi vya Kijiji cha Kijiweni, Maloo, Mvuleni, Ruvu, Mchinga I na Mchinga II. Ni lini vikundi hivyo vitanufaika na mradi wa *MACEMP II*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Jimbo la Mchinga hasa maeneo niliyoyataja hapo juu yanazalisha samaki wengi na hakuna soko na jokofu la kuhifadhia samaki, naiomba Serikali kutenga fedha kwa ajili ya soko la samaki katika Kijiji cha Mchinga II.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha kwa hatua, naunga tena mkono hoja.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, Waheshimiwa Makatibu Wakuu wa Wizara, wadau wote wa Wizara, pamoja na wananchi wote wafugaji na wavuvi. Hongereni sana kwa hotuba nzuri ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ni nzuri sana na imejikita katika maeneo mbalimbali. Lakini pamoja na hotuba nzuri, ziko changamoto mbalimbali ambazo zinawakabili wananchi katika utekelezaji wa majukumu yao katika Sekta ya Uvuvi na Ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Dar es Salaam, tumezungukwa na bahari ya Hindi. Hivyo basi, ni vyema Wizara ikasimamia uboreshaji wa Sekta ya Uvuvi katika Mkoa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa Makao Makuu ya Mkoa wa Dar es Salaam, hatujaona bidii binafsi inayofanywa katika Mkoa huu katika kuboresha uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wa Mkoa wa Dar es Salaam ni masikini sana ukilinganisha na hadhi ya Mkoa wenyewe. Uvuvi wao ni duni na hata hawajui fursa zao kama wadau wa sekta hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, samaki wanapatikana kwa wingi pale *Ferry,* lakini bado uvuvi sio mzuri. Hali kadhalika samaki hupatikana Kunduchi Wilaya ya Kinondoni na Gezaule, Kimbiji, Pemba na Mnazi Wilaya ya Temeke. Swali langu: Je, Serikali imewawezeshaje wavuvi hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi katika Mkoa wetu unazo changamoto nyingi sana ikiwemo ya kukosa masoko na kukosa vifaa vya kuhifadhia samaki. Samaki wanapatikana kwa msimu, kuna msimu samaki zinakuwa nyingi hapo. Kwa kumlinda mvuvi, lazima awe na hifadhi ya samaki ili wakati ambao siyo msimu wa samaki aweze kuuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nasikitika samaki wanapopatikana katika Mkoa Dar es Salaam hawauzwi katika *Supermakets* kubwa. Tatizo ni nini? Je, Wizara wameiona hiyo hali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika upande wa ufugaji, pia Mkoa wangu kuna ufugaji wa ng'ombe, mbuzi na ufugaji wa kuku wa kisasa na kuku wa kienyeji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa la wafugaji ni ukosefu wa masoko na gharama kubwa za madawa ya mifugo. Tatizo lingine kubwa ni kupanda kwa chakula cha mifugo mara kwa mara na bei ya kuku kubaki pale pale. Je, Serikali imeliangalia vipi suala hili na watawasaidiajie wafugaji kudhibiti hali hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo linguine, wafanyakazi wa sekta hizo walio wengi wanafanya kazi kinadharia tu. Wafanyakazi hao katika ngazi ya Halmashauri inawapanga katika Kata, lakini katika hizo kata wanakwenda katika vijiji. Wanapokwenda vijijini wanakutana na changamoto nyingi sana, kubwa ni kukosa vitendea kazi na posho ya kumwezesha afanye kazi hiyo kwa moyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ilione hilo. Naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa *DADPS* zimeegemea sana kwenye kilimo, siyo kilimo na mifugo. Serikali itenganishe *DADPS* ziwe pekee *(separate)* kati ya sekta hizi mbili. Jimbo la Igalula lina ng'ombe 115,000, mbuzi 45,000, kondoo 23,000, kuku 572,000. *DADPS* ya mifugo itasaidia mifugo hii kuboreshwa na Maafisa Ugani wa mifugo ngazi ya Vijiji na Vitongoji ili pato liongezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ng'ombe wa kienyeji waboreshwe ili kwa kuhamilishwa *(artificial inserminattion)* ili kuwa na nyumba bora, maziwa mengi, kutoka ng'ombe bora na wachache na kulinda mazingira na kuongeza pato la mfugaji. Elimu hii kupitia *NCA I* – Arusha itapeleka wafugaji

wengi Arusha na kupata mafunzo ya ufugaji bora wa kisasa. Hivyo, *DADPS* za mifugo zitajikita kupata wafugaji wa kisasa Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 30 Septemba, 2010 alihutubia wananchi Ilolansimba, Isikizya, Uyui, Tabora na kuahidi mpango wa kuboresha malisho ya mifugo. Wizara ituletee mradi wa *Range Land Improvement Projet* kwani malisho ni pungufu na yanaleta mvutano kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mvua zinaponyesha maji yanatiririka mpaka mito ya Ugala, Igombe, na Malagarasi. Kiangazi, ukame unaleta upungufu wa maji Jimboni. Tunahitaji mabwawa ya kufugia samaki, kunyweshea mifugo, na umwagiliaji mazao ya mpunga, mahindi mboga mbonga na matunda. Wizara itusaidie tuweze kuzitumia raslimali hizi vizuri zaidi kwa kupata mbegu bora za samaki na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuku wa kienyeji wakipata chanjo ya kideri, wana pato kubwa kwa wanajimbo wa Igalula. Wizara itusaidie kupitia *DADPS* ili kuku wa kienyeji waboreshwe kwa kukamilishwa na kuku na jogoo wakubwa na kuku wa wakisasa ili kupata kuku wengi, ubora na kuuza hasa treni ya kati – Tura na Malongire,Goweko na Igalula. Ufugaji bora ukiimarishwa kipato kitaongezeka.

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuweza kuchangia hoja hii kwa njia ya maandishi. Aidha, nazipongeza hotuba zote zilizosomwa na Waziri husika, Kamati husika pamoja na ya Kambi ya Upinzani. Naiomba Serikali chini ya Wizara hii izingatie hotuba iliyotolewa na Kambi ya Upinzani kwa kuchukua yale yenye manufaa kwa ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia juu ya mifugo na Sekta ya Uvuvi. Mifugo ina faida kwa maana kwamba ni raslimali muhimu sana kwa maendeleo ya familia na Taifa kwa ujumla. Mifugo inatupatia nyama, ngozi, mikoba, viatu, mapambo na hata gundi, fedha na vitu vingine vingi. Nasema hivyo kwa maana kwamba ili faida hizo ziweze kupatikana, kuhahitajika matunzo ya hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifugo yetu inahitaji malisho ya kutosha kwa maana ya maeneo mazuri ya kufugia. Wafugaji wamekuwa wakihamishwa katika maeneo yao mazuri ya malisho na kupelekwa sehemu ambayo hazina sifa ya malisho. Tunaitaka Serikali kuacha kuwasumbua wafugaji ili waweze kuishi maeneo ambayo wanaamini wao kwamba mifugo yao inaweza kupata malisho bora. Pia Serikali ihakikishe Maafisa wa Mifugo wanapatikana kwa urahisi hasa maeneo ya wafugaji ili mifugo iweze kukaguliwa mara kwa mara sambamba na kupata chanjo kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uvuvi nalo ni la kuangalia sana, kwani nalo linalipatia Taifa mapato makubwa pamoja na familia kwa ujumla. Tunaitaka Serikali iwapatie wavuvi vifaa bora vya kuvulia samaki sambamba na kupambana na uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kuagiza kitoweo aina ya samaki nje ya nchi ni aibu kubwa kwa kuwa tunayo bahari kubwa, maziwa na mito mingi yenye samaki wa kutosha. Hivyo hakuna sababu yoyote ya kuagiza samaki nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wapatiwe elimu ya uvuvi ni namna gani wanaweza kuwapata samaki, lakini pia wahakikishiwe soko la samaki la ndani na nje ya nchi, sambamba na usalama wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na tabia ya kutupa uchafu katika bahari hali ambayo ina hatarisha uhai wa viumbe walioko baharini hususan samaki ambao ni moja ya mategemeo ya mapato ya Taifa. Tunaitaka Serikali iimarishe ulinzi wa doria katika bahari na fukwe zetu ili kuzikamata meli hizi zinazomwaga uchafu katika bahari yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuchukua fursa hii kuchangia katika Sekta ya Uvuvi kuwa mazao ya Uvuvi yamekuwa yanafanyika mjini hasa katika Ziwa Tanganyika. Nchi za jirani wamekuwa wakifanya biashara ya ununuzi kwa wavuvi wetu, hivyo Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji kupoteza mapato na samaki wengi kuuzwa nchi za jirani pamoja na dagaa wazuri wa Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ziwa Tanganyika ni ziwa lenye kina kirefu, linahitaji zana za uvuvi za kutosha kwa kina hicho. Kwa kuwa zaidi ya asilimia 78 ya vyombo vya uvuvi havina usajili ambavyo ni takriban 3,795, kukosekana kwa usajili wa vyombo hivyo, kumesababisha ugumu kupata takwimu hasa za mazao ya uvuvi kutoka Ziwa Tanganyika, kusababisha athari za uharamia na utoroshaji wa mazao ya uvuvi: Je, Serikali imejipangaje ili kusajili vyombo hivi na kuzuia uharamia huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Tanganyika ni la pili kwa kina kirefu duniani likifuatiwa na ziwa lililoko Urusi, na la kwanza Barani Afrika. Pia kumekuwa na vifaa duni vinavyotumiwa na wavuvi katika ziwa hili. Lakini kuna samaki wengi na wakubwa ambao bado hawajavuliwa. Hivyo, wananchi wawezeshwe kuvua na pia Serikali ijenge viwanda vya samaki hasa Kigoma Mjini ambako kuna umeme.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote kwa kuandaa hotuba hii kwa kina na kuleta hapa Bungeni. Naipongeza Serikali kwa kufidia mifugo (ng'ombe watano) kwa wafugaji wa Loliondo na Lingido waliopotelewa na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imejaliwa kuwa na mifugo migi sana wakiwemo ng'ombe, mbuzi, kuku, nguruwe, bata na kadhalika. Hata hivyo, hatujaweza kuwa na mipango mikakati endelevu ya mifugo yetu kuweza kuchangia vizuri pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi kubwa ya ng'ombe na mbuzi tuliyonayo ni wa kienyeji wenye maumbo madogo na pia wanazalisha mazao ya maziwa kwa kiwango kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi za Serikali kuelimisha wafugaji na kuwawekea miundombinu ya kubadili mfumo wa ufugaji wa kienyeji kuwa wa kisasa, bado ni ndogo sana na havijaweza kuleta mabadiliko ya kuiahirisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikiwa kwa jambo hili, lazima kuwa na malengo na muda wa kiutekelezaji wa kusudio hilo. Wenzetu walioendeleza Sekta za Kilimo na Mifugo waliweka malengo na wakasimamia kwa umakini na utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ieleze Bunge, ni mipango gani ya uhakika ya kubadili mfumo wa ufugaji wetu wa kienyeji na kuwa wa kisasa zaidi? Wafugaji wafuge mifugo michache inayozalisha zaidi kwa wingi na kuniua uchumi wa Taifa pia kumudu maeneo ya ardhi tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ieleze Bunge, ni taratibu gani na sheria gani zinatumika kwa Wilaya kuendesha *operation* ya kukamata na kuhamisha mifugo kutoka kwenye vijiji vilivyosajiliwa kisheria na kuna huduma zote za jamii, Mfano, vijiji vya Shela, Maboha, Igagala – Urambo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la hamisha mifugo *(operation)* iliyoendeshwa na Serikali Wilaya na Kilosa, Urambo na Rukwa mwaka 2009 iliendeshwa kienyeji na kusababisha wafugaji kufilisiwa na kubaki maiskini huku Watendaji wakineemeka na kutajirika. Serikali iliunda Tume ya Kufuatilia *operation* ile na Waziri huku akikiri kuwa kwa utaratibu wa Maagizo na aliliambia Bunge, wale wote waliochukuliwa mifugo yao watafidiwa na Watendaji wote waliohusika watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Je, kwa nini taarifa ya Tume ile haijawekwa wazi? Je, Watendaji waliosababisha hasara kwa wafugaji mbona bado wanatanua Mitaani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo malalamiko mengi kutoka kwa Wabunge na wananchi wa maeneo ya Rufiji na Pwani, maeneo ambayo mifugo ilihamia katika Bonde la Ilhefu. Serikali kutofanya maandalizi ya kuhamisha mifugo kutoka eneo moja kwenda lingine limekuwa ni tabia ya kawaida. Badala ya kutatua tatizo, Serikali inahamishia tatizo kutoka eneo moja kwenda lingine. Je, ripoti iliyochunguza zoezi zima la *operation* ya Ihefu, kwa nini haiwekwi wazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kwamba kushindwa kuwajibika kikamilifu kwenye suala la mifugo, kuendesha *operation* za zima moto, kutotengeneza miundombinu ya huduma za mifugo na kusababisha idadi kubwa ya mifugo kufa ni kuchangia umaskini kwa Watanzania wafugaji na kupotezea Taifa mapato?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wajibu wa Serikali kulinda soko la ndani na nje kwa mazao ya mifugo hapa nchini ili kuinua pato la Taifa na wananchi pia. Je, ni kwa nini Serikali inaruhusu nyama za kuku kutoka nje kuuzwa kwenye *Supermarkets* za hapa ndani tena kwa bei kubwa wakati tuna kuku wa kienyeji na kisasa wanafugwa hapa ndani na hakuna masoko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri atueleze, ni namna gani Wizara hii inashirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii kuhakikisha hoteli za kitalii hapa nchini zinapata/zinanunua kitoweo na mayai kutoka ndani ya nchi kwa wafugaji wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoteli nyingi za kitalii zilizoko kwenye Hifadhi na hata hoteli kubwa kama *Kempisk, Kilimanjaro Hotel* na kadhalika wanaingiza nyama na mayai kutoka nje kwa matumizi ya hoteli zao. Ni kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngozi za mifugo yetu hapa ndani haina thamani kabisa. Ngozi zinaozea huko vijijini kwa sababu ya uelewa mdogo wa dhamani ya ngozi kwa wafugaji wetu na ukosefu wa masoko ya uhakika. Ni lazima Serikali ifufue viwanda vya ngozi hapa nchini na kujenga viwanda maeneo yote ya wafugaji wengi kwa ajili ya kuchakata ngozi, kwato, pembe na *product* nyingine za mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro inayoendelea hapa nchini dhidi ya wakulima na wafugaji imesababishwa na kutokuwepo mipango endelevu ya kutenga maeneo kwa ajili ya matumizi ya mfugo na kilimo. Kwa muda mrefu, Serikali imekuwa haiwangalii wafugaji kama wanastahili kutulia na kupewa ardhi kwa ajili ya kufuga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ieleze ni eneo kiasi gani limetengwa kwa wafugaji kwa Wilaya zenye mifugo hapa nchini?

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naunga mkono hoja. Nianze kuchangia hoja hii kwa kuzungumzia suala zima la mgogoro baina ya wafugaji na wakulima katika maeneo mengi nchini, lakini kwa upande wangu nizungumzie hasa migogoro iliyopo katika Wilaya ya Rufiji ambayo mimi natoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Jedwali Na. 6 linaonyesha maeneo yaliyopimwa na kutengwa kwa ajili ya ufugaji. Katika Wilaya ya Rufiji, jedwali linaonyesha vijiji 26 vyenye jumla ya hekta 77,179.91, zilitengwa kwa ajili ya kuwapokea wafugaji hasa waliotoka Ihefu Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiasi kikubwa, vijiji hivyo ambavyo wananchi walivitoa na kutenga maeneo hayo, wafugaji hao hawakwenda na badala yake waliamua kuingia katika Bonde la Rufiji ambalo halikutengwa kwa ajili ya kupeleka mifugo hiyo. Kutokana na wafugaji hao kuvamia eneo hilo ambalo wananchi wanalitumia kwa ajili ya kilimo, hivi sasa kumetoka tatizo kubwa la mauaji yanayoendelea kutokana na migogoro hiyo. Wakulima na wafugaji hawa siku zote huwa kwenye mapambano ambayo mara nyingi husababishwa na wafugaji kupeleka mifugo yao katika mashamba ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na migogoro hiyo, hivi sasa kuna kesi nyingi kwenye Mahakama za Mwanzo na Mahakama ya Wilaya zinazohusu makundi hayo mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na matatizo hayo, ni vizuri sasa wafugaji wakatumia nafasi waliyopewa ya kupeleke mifugo yao katika Vijiji ambavyo vimetengwa kwa ajili yao na waondolewe kabisa katika Bonde la Mto Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kuhusu mradi wa *MACEMP* unaoendeshwa katika Mikoa iliyo katika mwambao wa bahari ya Hindi. Mradi huu kwa kiasi kikubwa ulilenga kuwasaidia wananchi walio katika maeneo hayo ili watumie vyema raslimali zinazowazunguka. Wilaya ya Rufiji ni miongoni mwa Wilaya ambazo zimenufaika na mradi huu wa *MACEMP*. Karibu Shilingi milioni 800 zimetumika kwa kuwapatia wananchi wa maeneo hayo vifaa mbalimbali vya uvuvi na ufugaji wa nyuki. Suala hili ni jema sana ila ni vizuri kwa Serikali baada ya kutoa pesa kwa vikundi vikafuatilia utendaji wake wa kazi. Vikundi vingi vilivyopewa pesa za *MACEMP* havijatoa mwitikio chanya kwa kuwapunguzia umaskini wananchi hao. *MACEMP* itenge fedha za ufuatiliaji wa vikundi hivi ili lengo lililokusudiwa liweze kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miradi wa *MACEMP* kuna kitengo kinachohusiana na Benki za Jamii Vijijini *(VICOBA)* ambacho pia kipo kweme mradi wa RUMAKI. Katika vikundi hivi vya kuweka na kukopa kwa kiasi kikubwa kimesaidia kuwaendeleza wananchi wake. Baadhi ya vikundi kwa sasa vina hadi Sh. 15,000,000/= katika akiba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mafanikio hayo, ni vizuri sasa *MACEMP II* inayokuja iweze kwa kiasi kikubwa kuanzisha vikundi vingi vya Kuweka na Kukopa kwa kuwa vimeonyesha maendeleo makubwa kwa wananchi wengi walio katika vikundi hivyo.

Aidha, *MACEMP II* iweze pia kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo kuimarisha sekta hii ya uvuvi kwa kuwapatia zana bora zaidi zitakazowasaidia kwenda kuvua katika kina kirefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti naunga mkono hoja

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kukushukuru wewe kwanza kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya maisha na afya na nimshukuru kwa kunijalia kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu na kuchangia hoja hii ambayo ni ya muhimu sana kwetu. Mchango wangu nianze tu kwa kusema kwamba hoja iliyopo mbele yetu ninaiunga mkono asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia, naomba uniruhusu pia nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani kubwa ambayo Watanzania wameonesha kwake na kwa Chama cha Mapinduzi, wakamchagua kwa kura nyingi sana na kumpa kipindi kingine cha miaka mitano kuweza kutuongoza kama Taifa lakini pia kutupa huduma yake iliyotukuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie pia fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Bilal, kwa kuweza kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais. Nampongeza pia Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Katavi, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkuu lakini pia kuthibitishwa na Bunge lako Tukufu kwa upigaji wa kura zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie pia fursa hii kwa namna ya pekee nimpongeze Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Vilevile nawapongeza Mawaziri wote, Naibu Mawaziri kwa uteuzi walioteuliwa na Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwishoni mwa mwaka jana kila mmoja aliyepo hapa alitumia mchakato wa kuchaguliwa na naomba nitumie fursa hii kuwapongeza Wabunge wote waliopo hapa kutoka kwenye Vyama vyote na waliotoka kwenye mchakato wa Viti Maalum kwa kuweza kupewa imani kubwa na wapigakura ili waweze kuwa wawakilishi wao na kuwahudumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru kwa namna ya pekee Waziri wangu Dkt. David Mathayo David kwa ushirikiano anaonipa katika kuiongoza Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano ambao nimekuwa nikiupata ndani ya Bunge lakini pia nje ya Bunge kwa sababu ushirikiano wao umewezesha kuufanya mzigo huu kuwa mwepesi kuliko ambavyo ungekuwa bila kupata ushirikiano wao. Aidha, nawashukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Dkt.Charles Nyamrunda na Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Yohana Budeba, Wakuu wa Idara zote na Vitengo pamoja na taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakinipa katika shughuli za kuhudumia Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu kuwashukuru kwa namna ya kipekee wapigakura wangu waliopo katika vitongoji na vijiji vyote kwenye Jimbo la Kiteto kwa uchaguzi na kwa imani yao waliyonipa wakati wa Uchaguzi Mkuu uliopita. Nawashukuru sana pamoja na kwamba shughuli za Kitaifa zinachukua muda wangu, lakini bado nitaendelea kuwapatia huduma na utumishi uliotukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niishukuru familia yangu kwa namna ya pekee ikiwakilishwa na Mama Naomi kwa uvumilivu ambao wamekuwa nao kwa kipindi chote ambacho sikuwa nao nikitekeleza majukumu mengine ama ya Jimbo ama ya Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, sasa nianze kwa kujibu baadhi ya hoja zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge waliopata fursa ya kuchangia hoja hii ama kwa kuzungumza hapa Bungeni, ama wale waliochangia kwa njia ya maandishi. Nikiri tu kwamba wengi wamechangia na kwa muda tulionao hatutaweza kujibu kinagaubaga kila hoja iliyoibuliwa na Mbunge lakini nawaahidi kwamba tutawapa majibu ya hoja zote mlizotoa kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba mengi yameongelewa na katika hayo yote naomba nianze na hoja ya miundombinu. Miundombinu imeongelewa na Wabunge wengi, Kamati ya Bunge imeongelea, Kambi ya Upinzani pia wametaja, pamoja na ufinyu wa bajeti, Wizara imejipanga kushughulikia suala la miundombinu ikiwa ni majosho, malambo, vibanio pamoja na kukarabati mabwawa hasa yale yaliyoziba. Mheshimiwa Mary Nagu, Mheshimiwa Lekule Laizer na Mheshimiwa Rose Sukum wamechangia katika eneo hili, naomba kusema kwamba Serikali itajipanga na kuendelea kwa kupitia mipango ya *DADPS* kuhakikisha kwamba miundombinu ile iliyopo inakarabatiwa lakini pia na miundombinu mipya itaendelea kujengwa. Kwa hiyo, kwa Mheshimiwa Mary Nagu maeneo uliyoyataja maeneo ya Kigadabo, Wareki pamoja na vijiji vingine ulivyovitaja vitakuwa kwenye taratibu za Wizara kwa siku za usoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine iliyoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge wengi ni suala zima la ngozi kwa maana ya kuongeza thamani ya zao la ngozi lakini pia kuwezesha biashara ya ngozi ifanyike vizuri na kujaribu kuhakikisha kwamba usindikaji wa ngozi unafanyika vizuri ili thamani tunayoipata kutokana na zao hili iweze kuwa kubwa zaidi. Itoshe tu kusema kwamba kama Wizara tayari mwongozo umetolewa na sekta ndogo ya ngozi imewekwa katika mipango tuliyoitaja hapo awali hasa mpango wa kuendeleza sekta ya mifugo, kwamba zao la ngozi litapata mkazo na msukumo maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari viwanda ambavyo vipo kama vile *Lake Trading* iliyopo Mwanza, *Moshi Leather Industries* pamoja na kile Kiwanda cha Himo tayari vyote kwa pamoja vinazalisha ngozi ya thamani nzuri, Kiwanda cha Mwanza kinazalisha ngozi iliyosindikwa yenye futi za mraba 3,160,000, Kiwanda cha Moshi kinazalisha ngozi futi za mraba milioni kumi na Kiwanda cha Himo kinazalisha ngozi jumla ya futi za mraba milioni nne lakini tayari pia kwenye maeneo mengine mfano Mwanza pamoja na Arusha viwanda vingine vipya vinajengwa na Serikali itatoa msukumo wa pekee katika eneo hili la ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Wizara yangu ikishirikiana na wadau wengine wa maendeleo imefanya tafiti mbalimbali hasa zile zinazohusiana na *value chain analysis* kuhakikisha kwamba ngozi itaongezewa thamani na iuuzwe ikiwa si malighafi badala yake iuzwe ikiwa imeongezewa thamani. Tunatarajia kwamba mambo yaliyogundulika katika tafiti hizi zitatusaidia katika kujipanga vizuri na kuwawezesha wadau wanaozalisha, wanaofanya biashara pamoja na wale wanaotumia bidhaa za ngozi waweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo napenda kuiongelea ni hoja iliyoibuliwa na wengi ambayo ni hoja ya maziwa. Wabunge wengi wameongelea jambo hili akiwemo Mheshimiwa Pamba lakini Mheshimiwa Nkumba ameongelea, Kamati yetu ya Kilimo, Mifugo na Maji imeongelea, Mheshimiwa Profesa Kahigi pia amechangia lakini Mheshimiwa Jitu pia amechangia suala hili. Tayari tuna mkakati wa kuhamasisha Watanzania wote hasa katika ile Wiki ya Maziwa ili kuhakikisha kwamba unywaji wa maziwa tunauongeza kwa sababu ni zao, ukichukua maziwa kama lishe ni kitu chenye manufaa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na kuwa Programu ya Unywaji wa Maziwa Mashuleni, tayari Serikali imejipanga kwa njia nyingi, *VAT* imeondolewa katika vifungashio vyote vinavyohitajika katika suala zima la kufungasha maziwa. Viwanda kama Tanga Fresh, Viwanda vilivyopo Musoma, hivi ni ishara kwa kweli ya sera nzuri ya Serikali katika kuwawezesha wadau wa maziwa kuweza kuhakikisha kwamba wanachangia katika uzalishaji lakini pia biashara ya maziwa. Kutolewa kwa kodi katika zao hili tunatarajia kwamba uzalishaji utaongezeka lakini kubwa zaidi *processing* ya maziwa tunatarajia kwamba itaongezeka ili unywaji uweze kuongezeka si mashuleni tu, lakini pia hata majumbani na kiasi hicho tunachoambiwa kwamba tunakunywa maziwa kwa mwaka lita 44 kiweze kuongezeka na hatimaye kama si ndani ya miaka hii mitano angalau ndani ya miaka kumi tuweze kufikia kiwango kinachopendekezwa na *FAO* kwamba kila mtu aweze kunywa maziwa lita 200 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine iliyoibuliwa na Wabunge ni hoja ya kuboresha mifugo yetu, hili limetamkwa ndani ya sera lakini pia kanuni za Wizara tayari zimeshatoka na hata kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili ili wafugaji waweze kupata maarifa juu ya kuboresha mazao yao ya mifugo. Pia tayari tuna vituo kama kituo cha Tengeru cha *NAIC* ambacho kinafanya kazi ya uhamilishaji na vituo vingine vimefunguliwa katika Kanda, kwa hiyo tunatarajia ndani ya kipindi kifupi tutakuwa na uwezo wa kuzalisha mbegu bora na inayotakiwa kutegemeana na aina ya ekolojia ya kila mahali katika Kanda husika. Jambo hili ningewaomba Waheshimiwa Wabunge wahakikishe kwamba wanaendelea kutumia huduma hizi zinazopatikana ili isiwe lazima kwa wafugaji wetu wasio na uwezo kununua madume ambayo bei yake ni ghali. Uhamilishaji unarahisisha, unaweza kupata kila aina ya mbegu unayoipata, lakini pia utaipata kwa bei ambayo kila mfugaji anaweza akaimudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tayari pia kwa upande wa ufugaji wa kuku, mengi yamekuwa yakifanyika hasa katika maeneo kama ya Singida. Wizara imefanya kazi kubwa ikiwa ni upande wa chanjo hasa chanjo ya mdondo na kuku wameongezeka katika eneo hilo. Maafisa Wagani wamekuwa wakifanya kazi kubwa ya kuwaelimisha watu jinsi ya kufuga kuku wa kienyeji lakini wafuge kwa namna ambayo ni bora zaidi. Uchumi ulioboreka wa kufuga kuku umeonekana katika kuchangia hasa maendeleo ya elimu ya Sekondari za Kata katika maeneo ya Singida na kwingineko nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi wametaja suala zima la mikopo kwa wafugaji. Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Rose Kamili Sukum na wengine na huu ni mkakati ambao tunao Kitaifa. Wizara imekuwa na mkakati huu na tayari kumekuwepo na vikundi vya *SACCOS* kwenye Wilaya kama za Longido, Kiteto, Monduli, Singida Vijijini na vikundi hivyo vinaanza kupata mikopo ili mikopo hiyo iweze kuwasaidia ama katika kufuga vizuri ama katika kuboresha biashara ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine iliyoibuliwa na Wabunge wengi ni suala zima la kuhakikisha kwamba uendelezaji wa zao la ngozi kama tulivyosema tena unawekewa mkazo. Mheshimiwa Rita Mlaki pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine kama Mheshimiwa Betty Machangu wameongelea suala hili. Mheshimiwa Margaret Sitta, pia amechangia, Kamati pia

imechangia. Kama tulivyosema, wengi kati ya wale wadau wanaojihusisha hasa katika kuboresha zao hili la ngozi wanaweza na watapewa maelekezo pamoja na kuelekezwa kwamba mikopo inaweza ikapatikana wapi waweze kufanya kazi hiyo kwa ubora na kwa usahihi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ambayo napenda kuichangia iliyoibuliwa na Wabunge wengi ni kwamba mikakati ipo kwa sasa ya kuboresha ufugaji lakini pia kuboresha biashara ya mifugo. Wizara yangu imetoa nakala 2000 za kanuni ambazo zimetafsiriwa kwa Lugha ya Kiswahili zinazoelekeza kwa mujibu wa Sheria tulizopitisha hapa wenyewe kwamba ni kwa jinsi ipi wafugaji wanaweza wakaboresha biashara ya mifugo lakini niseme kwamba kumekuwepo na vikundi vinavyosaidia unenepeshaji na unenepeshaji huo umekuwa ukifanyika katika Mikoa kadhaa kama vile Mkoa wa Manyara, Shinyanga, Kagera, Tabora, Singida, Arusha, Manyara, Rukwa, Iringa, Morogoro pamoja na Mkoa wa Pwani. Kazi hii imeanza kuonyesha matunda katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni mashamba yaliyoko chini ya Wizara kwamba kuna mbegu nzuri inapatikana kwa wafugaji wale ambao watahitaji mbegu za kuboresha mifugo yao wanaweza bado wakapata katika mashamba hayo yaliyoko chini ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwishoni nitaomba pia niongelee suala la udhibiti wa magonjwa, Wabunge wengi wameongelea suala hili pamoja na Kamati ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi imegusia kwamba tunahitaji kuwa na *disease free zones* ili kuhakikisha kwamba biashara ya mifugo tunaisimamia vizuri zaidi. Haya yameanza kufanyika na Wizara imekuwa na *pilot areas* hasa Ruvu, eneo la Kongwa pamoja na Mizeli. Nikiongelea maeneo haya ni pamoja na *catchments areas* ambazo ziko kwenye maeneo haya. Kwa uhakika tunatarajia kwamba kwa juhudi tulizonazo Kiwizara maana mwakani tunatarajia kuanza kuzalisha chanjo ya mifugo kwa magonjwa mengi sisi wenyewe, kwa hiyo, tunatarajia kwa njia ya hamasa watu wachanje mifugo zaidi tutakuwa na maeneo mengi ambayo yatakuwa ni *disease free zones.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu unaniishia, lakini niwashukuru Waheshimiwa Wabunge, hoja zilizopo ni nyingi zote ni za msingi naahidi kwamba ushauri wote tulioupokea hapa kutoka Kamati, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, lakini pia wachangiaji waliozungumza na wale waliochangia kwa maandishi tutahakikisha kwamba tunaingiza katika taratibu zetu lakini pia tutawapa majibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuwashukuru wote kwa kunisikiliza, lakini pia naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani ule muda tuliompa Mheshimiwa Naibu Waziri umekwisha. Ninaomba tu nitoe taarifa moja hapa, wakati nikitoa maelekezo ya suala la samaki wenye kuhisiwa wana nyuklia ndani yake, Serikali imeshanipa taarifa ya suala hili. Sasa naomba kwa kweli kwa sababu suala hili kama nilivyosema ni suala nyeti, linagusa maisha ya Watanzania, nimruhusu Mheshimiwa Waziri, anapoanza kujibu hoja hii kwa kweli aanze kwanza kwa kutupa taarifa ya hali ilivyo. Baada ya hilo basi ofisi yetu itaona ni namna gani tutashirikiana na Serikali ili tatizo hili kwa kweli liweze kushughulikiwa kwa kadri itakavyokuwa inatakiwa.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, *Subhana Wataallah,* Mwingi wa Rehema, kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kumshukuru sana mke wangu Pamela David, Cleopatra David, Kelly David, Kenned David kwa kunivumilia na kunipa moyo wakati wote nikiwa kwenye majukumu ya Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kwa mara nyingine kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa imani yake alioonyesha kwangu na kwa kunipa jukumu la kuongoza Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumuahidi Mheshimiwa Rais, kwamba nitajitahidi kufanya kazi kwa kadri ya uwezo wangu na kwa kadri ambavyo Mwenyezi Mungu atanijalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa ushauri wake anaonipatia mara kwa mara katika kutekeleza majukumu yangu ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa salama za rambirambi kwa familia ya aliyekuwa Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali katika Wizara yangu, Ndugu John Patrice Yamo aliyefariki wiki iliyopita na kuzikwa jana kijijini kwao Kowaki, Wilaya ya Rolya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa namna ya pekee, napenda kuwapa pole wananchi wangu wa Jimbo la Same Magharibi, Kata ya Vudee, Kijiji cha Ndolwa, kwa ajili ya gari iliyotokea tarehe 6 Julai, Vudee Ndolwa na kuua watu saba (7). Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti, Katibu na Wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa mara nyingine kwa michango yao katika kutusaidia na kwa hoja ambazo wamezitoa. Niwaahidi kabisa kwamba hoja ambazo wamezitoa tutazijibu. Nawaahidi kabisa kwamba hoja zao zimetusaidia na tutaendelea kuzitumia katika kuboresha kazi za Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niwashukuru Wabunge wote waliochangia bajeti yangu kwa kuzungumza na kwa maandishi. Wachangiaji ni wengi sana kama alivyosema Naibu Waziri, hivyo si rahisi kujibu hoja zote katika muda mfupi huu nilionao lakini nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu kupitia baadhi ya hoja zilizotolewa na zitakazobakia zitajibiwa kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa shukrani hizi, napenda niwatambue Wabunge wote ambao wamechangia Hotuba ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Kwanza nimtambue Mheshimiwa Profesa David H. Mwakyusa, Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa Sylvester Mhoja Kasulumbayi, Waziri Kivuli wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, kwa michango yao mizuri ambayo ninaimani kabisa kuwa itatusaidia katika kuboresha utendaji wa kazi ya ofisi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia katika Hotuba ya Waziri Mkuu ni 39 na waliochangia kwa maandishi katika hotuba yangu ni 107 na waliochangia kwa kuzungumza ni 11.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia katika Hotuba ya Waziri Mkuu wa kwanza ni Mheshimiwa Dkt. Getrude Rwakatare, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Vick Kamata, Mheshimiwa Amos Makalla, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Modestus Kilufi, Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Christopher Ole- Sendeka, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kahigi, Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Hussein Amar, Mheshimiwa Dkt. Seif Rashidi, Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, Mheshimiwa Ally Mohamed, Mheshimiwa Zaynabu Vullu, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Ezekia Wenje, Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mheshimiwa Deo Filikunjombe, Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Desderius Mipata, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa John Shibuda, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mheshimiwa Nyambari Nyangwine, Mheshimiwa Goodluck Ole- Medeye, Mheshimiwa Abdallah Ameir, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa David Kafulila, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Haroub Shamis, Mheshimiwa Bahati Abeid na Mheshimiwa Subira Mgalu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia hotuba yangu kwa kuzungumza humu ndani Bungeni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Said Juma Nkumba, ambaye alitoa hotuba ya Kamati kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Sylvester Mhoja Kasulumbayi, ambaye ni Mbunge wa Maswa Mashariki lakini pia ni Waziri mwenzangu lakini yeye

ni Kivuli wa Upinzani wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Saleh Pamba, Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa Mohamed Rashid, Mheshimiwa Rose Sukum, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Charles Mwijage na Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mbunge wa Kiteto ambaye pia ni Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwatambue Wabunge 107 waliochangia hotuba yangu kwa maandishi, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mheshimiwa Betty Machangu, Mheshimiwa Zakia Meghji, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Khatib, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Amos Makalla, Mheshimiwa Amina Amour, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa AnnaMaryStella Mallac, Mheshimiwa Ali Hamis Seif, Mheshimiwa Gregory Teu, Mheshimiwa Omari Nundu, Mheshimiwa Pereira Silima, Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Ahmed Ngwali, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, Mheshimiwa Hamis, Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Riziki Juma, Mheshimiwa Lameck Airo, Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mheshimiwa Khatib, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa, Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Joseph Selasini, Mheshimiwa Mustapha Akunaay, Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse, Mheshimiwa Amina Mwidau, Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi, Mheshimiwa Eustace Katagira na Mheshimiwa Jitu Soni. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Zaynabu Vullu, Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Vincent Nyerere, Mheshimiwa Mbarouk Ali, Mheshimiwa Meshack Opulukwa, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Azza Hamad, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa Letecia Nyerere, Mheshimiwa Rukia Ahmed, Mheshimiwa Said Mtanga, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Eng. Athumani Mfutakamba, Mheshimiwa Philipa Mturano, Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Abdul Marombwa, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Kombo Hamis Kombo, Mheshimiwa Waride Jabu, Mheshimiwa Charles Mwijage, Mheshimiwa Joseph Genzabuke, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Mheshimiwa Charles Kitwanga, Mheshimiwa Zarina Madabida, Mheshimiwa Martha Mlata na Mheshimiwa Andrew Chenge. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Yussuf Khamis, Mheshimiwa Salim Khamis, Mheshimiwa Regia Mtema, Mheshimiwa Subira Mgalu, Mheshimiwa Rebecca Mngodo, Mheshimiwa Mwanamrisho Abama, Mheshimiwa Desderius Mipata, Mheshimiwa Augustino Masele, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Juma Ali, Mheshimiwa Amina Clement, Mheshimiwa Goodluck Ole – Medeye, Mheshimiwa Modestus Kilufi, Mheshimiwa Seif Rashidi, Mheshimiwa Nyangwari Nyangwine, Mheshimiwa Dkt. Augustino Mrema, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Rose Sukum, Mheshimiwa Maryam Msabaha, Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli, Mheshimiwa Hassan Nassor Omar, Mheshimiwa Salome Mwambu, Mheshimiwa Alphaxard Lugola, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Ezekia Wenje, Mheshimiwa Rashid Omar, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Haroub M. Shamis, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mheshimiwa Abia M. Nyabakari, Mheshimiwa Susan Kiwanga na Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutambua Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa heshima na taadhima naomba nitoe taarifa mahususi na taarifa ambayo ni muhimu sana kwa afya za Watanzania na mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa Kuhusu Kuingizwa Nchini kwa Samaki Wanaohisiwa Kuchafuliwa na Mionzi ya Nyuklia. Serikali ilipata taarifa siku ya Jumamosi tarehe 23 mwezi wa saba kwamba kuna samaki aina ya vibua yaani *Mackerel* zinazotoka Japan walioingizwa na Kampuni ya *Alfa Crust Limited* ya Dar es Salaam. Mzigo wa samaki hao uliwasili Dar es Salaam tarehe 8/07/2011 na kwamba samaki hao wanahisiwa kuchafuliwa na mionzi ya nyuklia iliyotokana na kuvuja kwa vinu vitatu vya nyuklia huku Japan mwezi Machi, mwaka 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu za uingizaji wa samaki hao. Watalaam wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, walifuatilia kuona kama utaratibu umefuatwa kulingana na kanuni na miongozo iliyopo. Ufuatiliaji huu uligundua yafuatayo:-

(a) Kibali cha Nguvu za Atomiki Tanzania kilitolewa tarehe 8/07/2011 baada ya kukagua *pre-shipment sample* ya samaki walioletwa kwa njia ya *DHL*.

(b) Kwamba Kibali cha Idara ya Uvuvi kilitolewa tarehe 8/7/2011 baada ya kukagua na kupima sampuli ya samaki wanaotegemea kuingizwa na kampuni husika.

(c) Mamlaka ya Chakula na Dawa yaani *TFDA* walitoa kibali namba TFDA 11/F/IER/0896 cha tarehe 11/07/2011 baada tu ya kuridhika na viambatanisho halali vilivyowasilishwa na muagizaji kutoka Kamisheni ya Nguvu za Atomiki Tanzania na Idara ya Uvuvi.

(d) Kwamba hao samaki wana kibali cha Japan *Frozen Food Inspection Corporation (JFFIC)* Shirika lililo chini ya Wizara ya Afya, Kazi na Ustawi wa Serikali ya Japan. Kibali hicho kinaonyesha samaki hao walisindikwa mwezi Desemba mwaka 2010 na muda wa mwisho wa matumizi ya samaki hao ni mwezi Juni, mwaka 2012.

(e) Kwamba kwa mujibu wa mamlaka ya mapato Tanzania *(TRA)* mzigo huo uliingia bandarini tarehe 18/07/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu hatua zilizochukuliwa na Wizara. Baada ya kuona vibali vya ukamilishwaji wa uingizwaji wa samaki hao, Serikali imeona ni vema kufuatilia na kuchunguza kwa makini ili kuhakiki zaidi usalama wa samaki hao kwa matumizi ya binadamu. Maamuzi hayo yametokana mazingira yaliyojitokeza ya uharaka wa uagizaji na uingizaji wa samaki hao pamoja na usambazaji wake. Pia taarifa za kuwepo wasiwasi wa kuchafuliwa na mionzo ya nyukilia kwa bidhaa za bandarini kutoka Japan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zifuatazo zimechukuliwa:-

(a) Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii iliagiza mamlaka ya Chakula na Dawa *(TFDA)* kuchukua hatua haraka za kuzuia usambazaji wa samaki hao hadi uchunguzi utakapokamilika. Hatua hizo zilianza mara moja tarehe 23, Julai, 2011 alasiri. Zoezi hili lilishirikisha wataalamu kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, *TFDA*, Idara za Afya za Halmashauri za Dar es Salaam, Morogoro, Jeshi la Polisi na Kampuni ya Alpha Crust ya Dar es Salaam.

(b) Baada ya shughuli za usambazaji na uuzaji kusitishwa, Mamlaka zifuatazo ziliagizwa kuchukua sampuli kwa ajili ya uchunguzi zaidi, Mamlaka ya Chakula na Dawa *(TFDA),* Idara ya Uvuvi, Kamesheni ya Nguvu za Atomic Tanzania. Sampuli zote zilichukuliwa chini ya uangalizi wa Idara ya Mganga Mkuu wa Serikali.

(c) Aidha, Serikali kupitia vyombo vya habari, iliwatahadharisha wananchi na kuomba kutoa ushirikiano ili samaki waliosambazwa warejeshwe sehemu husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya ufuatiliaji. Hadi kufikia asubuhi, tarehe 24, Julai, 2011 kiasi cha samaki wenye uzito wa tani 123,673 kati ya tani 124,992 walioingizwa nchini walipatikana na kuzuiliwa katika maghala ya Kampuni Alpha Crust. Aidha, samaki wenye uzito wa tani 1319 walikwishasambazwa. Kwa kutumia kumbukumbu kutoka kampuni hiyo zinazoonesha kwamba samaki hao walisambazwa kupitia soko la feri Dar es Salaam, Morogoro na Mji wa Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya ufuatiliaji huo ni kama ifuatavyo:-

(a) Tarehe 25, Julai, 2011 baada ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kutoa tahadhari kwa wananchi, samaki wenye uzito wa kilo 225 walirudishwa na mwananchi mmoja kutoka Dar es Salaam. Sasa hivi wamehifadhiwa kwenye Kampuni ya *Alpha Crust*.

(b) Tarehe 25, Juali, 2011 wananchi wa Kilombero walirejesha samaki kilo hamsini ambao wamehifadhiwa Morogoro Mjini wakisubiri kurudishwa Dar es Salaam.

(c) Kiasi cha samaki tani 1044 hawakupatikana, ufuatiliaji unaendelea katika maeneo ya Feri Dar es Salaam, Morogoro na Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilipopata taarifa ya kuwepo kwa samaki wenye utata kiafya, kazi ya ufuatiliaji na uchunguzi ilianza na inaendelea usiku na mchana hadi samaki hao watakapopatikana wote. Vilevile, Serikali itapeleka sampuli nyingine nje ya nchi (*reference laboratories*) kama vile Afrika Kusini na Kenya.

Aidha, taarifa ya kina kuhusu matokeo ya ufuatiliaji na uchunguzi itatolewa mara baada ya kazi kukamilika. Iwapo kama kutagundulika kuwepo kwa uzembe kwa mamlaka yoyote iliyopo chini ya Serikali au mtu binafsi, hatua za kinidhamu na kisheria zitachukuliwa dhidi yao. Pia Serikali inatumia Vyombo vya Dola na Usalama kufuatilia suala hili kwa karibu na taarifa zitakapopatikana, zitawasilishwa rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nilipo nina *copy* ya viambatanisho, *Certificate Of Origin* yaani Cheti cha Uwasilia wa Samaki hawa kilichoandikwa tarehe 2 Juni, 2011 na aliye-*sign* anaitwa Yoshiyo Suzuki na ninayo *Examination Certificate* ya tarehe 3, Juni, 2011 kutoka *Japan Frozen Food Inspection Cooperation Tokyo,* kilichosainiwa na Yoshimitsu Terui na nina *copy* ya kibali *(permit)* ya uingizaji wa samaki hao kutoka *TFDA* ya tarehe 11, Julai, 2011 na nina *copy* ya *permit* ya Tanzania *Atomic Energy Commission* au cheti chao cha tarehe 8 Julai, 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo na baada ya kutoa taarifa hizo muhimu sana kwa Taifa, naomba sasa ninywe maji halafu niendelee. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika kabisa kwamba muda niliopewa ni kwa vile tena nimeanza kusoma taarifa hii, muda hautatosha, lakini kama alivyosema Naibu Waziri tayari tumeshaandika majibu kwenye maandishi, kwa hiyo wale ambao hawatapata majibu yao tutawapatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba kujibu hoja za Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Waziri dakika moja, hapa Waheshimiwa Wabunge wengi wameshaniletea vijinoti wakiomba taarifa hizo wagawiwe. Waheshimiwa Wabunge, naomba kusema kwanza *Hansard* imeshanukuu hiki alichokisema, kwa hiyo kama kuna yeyote atataka kulijua hili, akishapata *Hansard* ya leo hiki cha utangulizi kipo kinapatikana kabisa, lakini suala la *copy,* tunaweza pia tukawasiliana na Serikali na tukaona jinsi bora ya kulifanyia kazi.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Hoja ambazo nitaendelea nazo ni zile ambazo Naibu Waziri hakuzigusia, lakini katika suala la ngozi ningependa kuongezea tu kwamba makusanyo ya jumla ya ngozi kwa maana ya vipande vya ng'ombe pamoja na vipande vya mbuzi na kondoo vimefikia milioni 5,100,000 lakini uwezo, *installed capacity* ya viwanda vile vyetu nane kusindika ni ngozi milioni 7,900,000 lakini sasa hivi uwezo wao wa kusindika, tuseme wanavyosindika sasa hivi ni vipande vya ngozi milioni 1, 400,000 kwa maana hiyo wanasindika ngozi chache sana kulinganisha na zile ambazo zinakusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka Mheshimiwa Rita Mlaki alikuwa anaomba kwamba tuongeze ushuru na wadau wengine wanasema tufute kabisa, tuseme kwamba tufute kabisa *export* ya ngozi nje, lakini mimi nasema kwamba kwa sababu hata *utilisation* ya viwanda vyetu bado haijafikia asilimia 100 ya uwezo wake, tunachoweza kufanya ni kuongeza ushuru kidogo ili tuwape nafasi wajenge uwezo wa kuchukua zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, machinjio na viwanda vya nyama, kwamba Serikali ijenge machinjio ya kutosha katika maeneo mbalimbali nchini na kuyakodisha. Serikali imejenga machinjio Dodoma na sasa hivi tuko kwenye asilimia 50 ya machinjio ya Ruvu ambayo yatakuwa yanachinja ng'ombe 800 kwa siku pamoja na kondoo na mbuzi 400 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifungue minada ya upili. Minada ya upili ni minada ambayo inauza ng'ombe ambao wanatoka kwenye minada ya awali, yaani minada ya awali ni ile ambayo iko kwenye Halmashauri na kwa sasa hivi Tanzania tuna minada 300 ya awali na minada ya upili 12 na minada mingine iko mipakani kwa sababu nchi jirani wanapenda kununua ng'ombe zetu, kwa hiyo, kule tuna minada 10. Kwa hiyo, tuna maeneo hayo muhimu sana katika masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuifanya minada ya awali kuwa ya upili inatokana na wadau wenyewe katika maeneo yale ya minada ya awali kama watakuwa wanahitaji kuwa na minada ya upili basi tunabadilisha mnada wa awali kuwa mnada wa upili. Mnada wa upili, ni *secondary market* kwamba wanakutana wafanyabiashara kwa wafanyabiashara, lakini mnada wa awali, wafugaji na wafanyabiashara ndiyo wanaokutana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vilivyobinafsishwa na havikuendelezwa virudishwe. Ni kweli vipo viwanda ambavyo vilibinafsishwa na havijaonesha matokeo yale ambayo walitoa kwenye *business plan* zao. Serikali inaendelea kufuatilia kusema kweli, viwanda vya ngozi, viwanda vya nyama kama mlivyosikia kuna Kiwanda cha Shinyanga kinaitwa *Triple S* na kile cha Mbeya tunakitangaza sasa hivi kusudi viwanda hivyo virudi tuweze kuwabinafsisha wawekezaji wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itenge maeneo yasiyo na maradhi kwa ajili ya unenepeshaji. Serikali imeshatenga maeneo hayo, tunaendelea kuyatenga maeneo ambayo ni *disease free zone* yani hayana magonjwa kwa maana ya unenepeshaji katika Ranchi za Taifa na za watu binafsi pamoja na maeneo yanayozunguka machinjio ya Ruvu na katika Wilaya ya Bagamoyo, Mvomero na kule Sumbawanga kuna kiwanda kinaitwa Safi, kuna maeneo ambayo tumeyatenga na ambayo yanadhibitiwa magonjwa kwa ajili ya kunenepesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wafugaji wa asili limeshazungumzwa na Naibu Waziri, lakini hadi sasa hekta milioni 2.6 za ardhi zimetengwa katika vijiji 440, Wilaya 38 na Mikoa 17 kwa ajili ya malisho na tunawaomba Halmashauri katika maeneo ambayo yametengwa kwa mfano maeneo ya Kilosa, Wilaya ya Kilombero pamoja na Kilindi, maeneo hayo, Halmashauri zitenge fedha kwa ajili ya kuweka miundombinu hususani majosho, malambo na masoko kwa ajili ya kuuza wale mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rita Mlaki ameuliza kuhusiana na uzuiaji wa uvuvi wa kambamiti, kambamiti kwa Kingereza wanaita *prawns*. Tulifunga mwaka 2008 uvuvi wa kambamiti kwa sababu ili uweze kuvua *prawns* au kambamiti wanatakiwa wawe wengi kiasi cha tani 1000 yaani zaidi ya tani 1000, lakini kipindi tunafunga walikuwa ni tani 200 tu na sasa hivi tumefanya utafiti, kiasi kilichoonekana ni tani 400. Kwa hiyo, tutaendelea kufunga mpaka watakapoongezeka, ikiwezekana hata wavuvi wadogo wa kambamiti nao tutafunga ili kambamiti wale waweze kuongezeka, tuweze kufungulia baadaye tufanye kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lekule Laizer amezungumzia kuhusu dawa, ruzuku katika ugonjwa wa Ndigana Kali, Ndigana Kali ni *East Coast Fever* inakuwa *transmitted* na kupe. Katika ugonjwa huu ambao ni hatari sana na kusema kweli, asilimia 70 ya vifo vya ng'ombe vinatokana na kupe. Serikali kuanzia mwaka 2006 mpaka leo imeshatoa bilioni 15 ambazo ziliwezesha kununua lita 999,000 za madawa ya kuogesha na kwa kweli kwa sababu *ECF*, (*East Coast Fever*) inayosababishwa na *Theileria parva* na ambayo inakuwa *transmitted* na *Rhipicephalus appendiculatus* basi tutahakikisha kwamba miaka ijayo tunatoa ruzuku kwa ajili ya ugonjwa huu kwa sababu chanjo na madawa yake yale ya *Butalex* inakuwa ni ghali sana kwa wafugaji na ni ugonjwa unaoua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ombi lake kwamba wale ng'ombe tunaotoa kwa ajili ya mbegu za kuwawezesha wafugaji ambao mifugo yao ilikufa yote tuchaganye na mbuzi, nadhani hilo ni wazo zuri kwa sababu mbuzi kwanza wanazaliana haraka. Kwa hiyo, kuna uwezekano mkubwa wa mfugaji yule kupata ukombozi kutokana na mbuzi kuliko ng'ombe watano ambao watachukua muda mrefu kuzaliana ukilinganisha na mbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ranchi za Taifa. Kuna Ranchi ambazo wamepewa wawekezaji na kushindwa kuziendeleza. Ni kweli kwamba zipo, tunazo Ranchi nne (4) katika zile 104 tulizobinafsisha wawekezaji ambazo wameshindwa kuziendeleza. Napenda kuzitaja kwamba ni Ranchi ya Mzeri Hill, Kitalu Na. 645/6 cha kampuni inaitwa Moja One na Mzeri Hill kitalu Na. 645/7 cha kampuni ya Shalon Farming. Kitalu kingine ni Mzeri Hill Na. 645/9 cha Mkuti Hotel na *camping site* pamoja na kile kitalu chenye Na. 33, kiko Uvinza ambacho kinamilikiwa na *Ndeko General Supplies Limited.* Nawajulisha kwamba kama hawataendeleza kwa muda ambao wameshawekewa kwa sababu sasa hivi tumeshaanza kuchukua hatua, tutazichukua Ranchi hizo kwa kutumia Sheria zilizopo na tutaweza kumilikisha kwa wafugaji wengine ambao wako makini na ndiyo maana nimeyataja haya majina bila aibu ili wajijue kwamba tuko *serious*, tutawanyang'anya, tutatoa kwa wafugaji ambao wako *serious*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maabara ya Mifugo. Kamati imependekeza kwamba maabara ijitegemee badala ya kuwa Idara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi. Mimi napenda kuihakikisha Kamati yangu na Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara yangu pamoja na Ofisi ya Rais, Menejimenti na Utumishi wa Umma inaanda utaratibu wa kuanzisha hii Maabara ya Taifa iwe Wakala ambayo itakuwa inajumuisha vituo vyote vya utafiti yaani *VIC*, Vituo vya Uchunguzi kwenye Mikoa na vya Kanda, Taasisi ya Utafiti Wwa Ndorobo na Ndigana na Kituo cha Utafiti kule Kigoma. Rasimu za nyaraka muhimu zinazohitajika yaani *business analysis na strategic plan and agency framework* tayari zimeshakamilika. Kwa hiyo, tunataka *National Laboratory* ya Temeke iwe Wakala kusudi waweze kuzalisha kama ni dawa ama chanjo waweze kuuza kibiashara na waweze kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya mifugo kwa maana ya malambo pamoja na majosho, Serikali tunaendelea kutoa fedha kupitia *DADPS*.

Mheshimiwa Mohamed Rashid ameuliza kuhusiana na mkataba ambao Serikali iliingia na Japan, napenda kumjulisha kwamba mkataba huu haukuendelea kwa sababu ya kutokea kwa maharamia katika eneo la *Horn of Africa* yaani Somalia kwenda mpaka Pwani ya Musumbiji. Kwa maana hiyo, Wajapani wale hawakuja kwa sababu ya wale maharamia, walikuwa wanaogopa usalama wao. Kwa hiyo, zile meli 52 na ushee hazikuja, meli zilizopo 72 zinatoka Ulaya hususani nchi ya *Spain*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leseni kwamba ni nyingi sana, kwamba kuna leseni ya mvuvi mwenyewe na leseni ya chombo cha uvuvi. Hii inatokana na Sheria Na. 22 ya Uvuvi ya mwaka 2003 na Kanuni za mwaka 2009, kifungu cha 5(1)(2) inazungumzia umuhimu wa vyombo kuwa na leseni na wavuvi kuwa na leseni. Kwanza vyombo vile vikiwa na leseni vitazuia mambo mengi sana. Uharamia ambao unaotokea sasa hivi Ziwa Victoria, wavuvi wananyang'anywa vyombo vyao ni kutokana na kwamba wavuvi wengine hawataki kusajili vyombo vyao, tukisajili vile vyombo, kwanza tutawezesha Serikali kupata mapato yake, lakini tutaweza ku-*monitor* kwamba ni chombo ambacho kinaweza kuwa kimefanya uharamia ama ujambazi, ama ujangili. Kwa hiyo, ni lazima vyombo visajiliwe katika Halmashauri, vyombo vile ambavyo vina urefu wa mita 11 kurudi chini vinasajiliwa katika Halmashauri zinazozunguka eneo lile la uvuvi lakini vyombo vyenye urefu wa mita 11 na kuendelea, vyombo vile vinasajiliwa na Mkurugenzi wa Uvuvi katika Wizara yangu na fedha hizi za leseni ni vyanzo vya mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mohamed Rashid anasema *MACEMP* haikumsaidia, mimi nadhani katika maeneo ambayo yamefaidika vizuri kwa mradi wa *MACEMP* ni Zanzibar, kwa sababu ya udogo wa eneo lake ukilinganisha na Bara kuanzia Tanga mpaka Mtwara, hizo fedha kwenye Halmashauri 16 zilikuwa zote zinatakiwa zihudumie *MACEMP*, lakini kiasi ambacho tumegawana cha fedha kutoka dola 61,000 wenzetu walipata asilimia 40 na sisi tulipata asilimia

60, lakini ukilinganisha mahitaji ya huku kwa kweli Zanzibar *MACEMP* imefanya kazi vizuri zaidi kuliko hata huku Bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumzia pia kwamba meli 200 za *FAO* zinavua samaki wetu, nasema kwamba mimi na Wizara yangu tutafanya uchunguzi, sisi taarifa tulizonazo ni meli 72, lakini kama zipo *data* zingine basi tutajaribu kuchunguza, lakini sisi kama Wizara, *Deep Sea Fishing Authority*. Mamlaka ambayo tumeianzisha kwa Sheria Na. 4 ya mwaka 2007 inafanya doria kila wakati, doria za kwenye maji, doria za nchi kavu na doria za angani. Vile vile tumeweka chombo kinachoitwa *Vessel Monitoring Devise* yaani *system* ambayo ina-*monitor* meli ambazo zinavua kwenye bahari kuu kwenye *exclusive economic zone.* Kwa hiyo tuna vyombo na vile vile tumeweka vyombo vinavyoitwa *FADs* yaani *Fish Aggregating Devise,* ukishakiweka hicho samaki wanakuja eneo lile. Kwa hiyo, ukiwa na chombo chako unakuja unavua samaki unavyotaka. Sasa hivi tuna *FADs* nne na tunatarajia kuongeza zingine 20, kusudi wavuvi waweze kupata kwenda moja kwa moja kwenye hizo *FADs* kuvua. Lakini vile vile tuna *weather monitoring system* ambazo tulizifunga Zanzibar pamoja na *TAFIRI* Dar es Salaam kwa ajili ya kubaini maeneo matabaka ya maji ya juu ambayo yana samaki wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nazungumzia uvuvi haramu. Mamlaka husika zisimamie Sheria zilipo ili ikibidi katika maeneo ya vijiji zitungwe sheria ndogo ndogo, tunakubaliana. Kwa sababu sisi kama Wizara pamoja na Halmashauri tumeunda *BMUs* yaani *Beach Management Units* ambazo zinaitwa Kamati za Ulinzi Rasilimali 703 zipo nchi mzima. Ziwa Victoria linaongoza kwa kuwa *BMU* nyingi ikifuatiwa na Ukanda wa Pwani. Zile *BMU* pamoja na kulinda zile rasilimali, lakini *BMU* zinasaidia katika kuelimisha kutoa elimu kwa sababu tunawapa elimu mara kwa mara na vitendea kazi ili waweze kuwaelimisha wavuvi na hata pale ambapo taratibu, sheria ama kanuni zinabadilika basi tunaongea na wale kwanza tunaweza kuwasaidia zaidi wale wavuvi wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya mradi wa ufugaji wa samaki kuhusu kuongeza uzalishaji wa vifaranga. Kule China pamoja na kwamba nchi yao ile imezungukwa na bahari lakini pale Beijing wanakula samaki wa kufugwa na sisi hatuna budi na sasa hivi tuna Idara kabisa, tuna Kitengo ambacho kinahusika na ukuzaji wa viumbe kwenye maji na imeendelea kuimarisha vituo vyake. Sasa hivi tuna kituo kule Kingorwila tunazalisha vifaranga wa samaki pale, Mbegani tunazalisha. Karanga, Mtama kule Lindi, Musoma, Bukoba, Mara. Kwa hiyo, lengo ni kuhakikisha kwamba watu wanafuga, wanafuga kambale wanafuga perege. Kifaranga kimoja cha perege ni shilingi 50 na kifaranga kimoja cha kambale ni shilingi 100. Kwa hiyo ni *affordable.* Watu wanunue, tutatoa ushauri, kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja wa Rukwa ameomba tumpelekee, tumsaidie ufugaji wa samaki, sisi tunasema tutampa ushauri, tutampa wataalam na tutamwonyesha wapi atapata mbegu. Lakini Halmashauri kupitia fedha za *DADPs* watenge fedha kwa maana ya wananchi wenyewe kama wana haja hiyo waibue miradi ile kusudi tuweze kuwapatia *technical know how* pamoja na vifaranga waweze kufuga na kwa kweli ndiyo njia pekee, kufuga samaki ndiyo njia pekee ya kupunguza nguvu ya uvuvi katika maziwa yetu. Nguvu ya uvuvi katika bahari zetu itasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hoja ya kwamba bajeti ya Wizara ni ndogo. Ni kweli ni ndogo. Lakini sasa bajeti maana yake una *resources* ambazo ni ndogo. Kwa hiyo unapanga kutokana na vipaumbele. Mwalimu Nyerere alisema kupanga ni kuchagua. Kwa hiyo, sasa kama Waziri wa Wizara hii zile pesa nilizopewa nimeridhika nazo kwa sababu naona pale kasungura ketu ni kadogo, nikisema kwamba nichukue zote maana yake ni kwamba kwenye barabara pia tutakosa hela, kwenye afya tutakosa, kwenye maji tutakosa. Kwa hiyo, kwa sasa nimeridhika kwamba hii kwa sasa tutaifanyia kazi lakini tunategemea kwamba miaka ijayo kwa sababu sasa hivi tuna mpango wa kuendeleza sekta ya uvuvi na mifugo, mipango hiyo ambayo programu ambazo zimekwishaingizwa kwenye Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ijayo kuna mambo mengi sana ambayo yatatendeka katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Kwa hiyo nawahakikishia wananchi kwamba wasiwe na wasiwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile huu ni mwaka wa kwanza katika kipindi hiki cha miaka mitano. Hii ni bajeti ya kwanza. Tuna zaidi ya miaka mitano ijayo na vile vile tuna miaka mingi mpaka tufikie 2020-2025. Lakini hata hivyo, sisi kama Wizara tunaongeza mapato yetu kutokana

na kuuza vifaranga wa samaki, kuuza chanjo za magonjwa mbalimbali pamoja na marobota ya hei, yaani majani yaliyokaushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa wataalam wa ugani. Mwenzangu nadhani atakuwa ameshaeleza kwamba mwaka huu Vyuo vyetu vya Mifugo vina *capacity* ya wanafunzi 1,500. Lakini bado kwa sasa hivi ambao wameshaajiriwa tayari ni 4,100 na bado tuna pengo la karibia 11,000 wataalam wa ugani wa mifugo na pengo la zaidi ya 15,000 wataalam wa ugani wa uvuvi. Sasa hivi tunao 703.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilisema kwamba, Taasisi za Utafiti ziongezewe bajeti. Serikali imeendelea kuongeza bajeti za taasisi za utafiti nchini ikiwa ni pamoja na kufanya ukarabati wa maabara, majengo, kununua vitendea kazi. Lakini pia tunasomesha wataalam ili waweze kupata utaalam mkubwa zaidi, pamoja na kuongeza vitendea kazi lakini bado tunasomesha wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, amezungumzia kwamba wafugaji wa asili hawaheshimiwi. Si kweli. Wafugaji wa asili kama tungesema kwamba hawathaminiwi hata zile bilioni 8.7 ambazo tunazitoa ili waweze kupata mbegu zisingetoka. Tukumbuke kwamba uzuri wa nchi yetu ni kwamba kuna *political will,* Rais wetu, Makamu wa Rais wetu, Waziri wetu Mkuu, tena Waziri wetu Mkuu ni mtoto wa mkulima na nimefika kule nyumbani kwake nimekuta ana shamba kubwa pamoja na mifugo na anafuga nyuki. Tumpongeze kidogo Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba kuna *political will* ya viongozi wetu, wanasukuma msukumo katika kuhakikisha kwamba, wafugaji wanapata ukombozi. Nadhani mmeshamsikia Rais wetu mara nyingi akisema kwamba anasikitika sana kuona ng'ombe amekonda pamoja na mfugaji mwenyewe amekonda. Ndiyo maana fedha hizi zote zinatolewa, fedha za ruzuku, fedha za *DADPs*, fedha za ruzuku za madawa zinatolewa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunamkomboa mfugaji. Sasa hivi Serikali imeshatoa mamilioni ya fedha kwa ajili ya kutenga maeneo ili wafugaji waweze kupata maeneo ya kufuga ili tuweze kupunguza migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, hatuwezi tukafuga kila mahali katika nchi hii na vile vile hatuwezi tukalima kila mahali katika nchi hii, ni kweli na pia hatuwezi tukalima kila mahali. Lazima maeneo ya kilimo yafahamike na yatumike kwa kilimo na maeneo ya wafugaji yafahamike kutokana na mipango mizuri ya ardhi katika Halmashauri na katika vijiji vyetu. Kwa hiyo, kusema ukweli matatizo yanaanzia huko huko chini kwa sababu utakuta Halmashauri zingine ama viongozi wengine na vijiji vingine wanatoa ardhi bila kuwashirikisha wananchi. Mifano iko mingi sana, wanatoa ardhi kwa wawekezaji bila kushirikisha wananchi. Wananchi wamekuja kwenye mikutano ya kawaida, wanaandikishwa majina ya mahudhurio na *signature* pale halafu baadaye wanakuja kusema kwamba, haya majina walikubali kuuza hii ardhi, wakati ilikuwa ni mahudhurio ya tarehe nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunataka Watendaji wa Vijiji wahakikishe kwamba wanahusisha wananchi kutokana na Sheria ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 ni lazima tuhakikishe kwamba tunawashirikisha wananchi. Tunawaheshimu sana wafugaji, kwanza nyama tunazokula kila siku tunakula nyama na tunakunywa maziwa, ni kwa sababu ya wafugaji na vile vile wanaongeza pato la Taifa. Nadhani Mheshimiwa Lekule Laizer alizungumza *point* moja ambayo nadhani huko baadaye itabidi tuifikirie kwamba Halmashauri ziweze kuheshimu wafugaji basi tutoze kodi kwenye mifugo ili na wao wawe wanachukua nafasi kuwatafutia maeneo ya kufuga ili waweze kutoza kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kwamba Msemaji wa Kambi ya Upinzani amesema kwamba maeneo ya wafugaji yamepungua. Si kweli kwamba yamepungua, tuna hekta milioni 50 ambazo zinafaa kwa kufuga. Lakini tumetumia hekta 26.1 milioni. Maana yake tuna zaidi ya asilimia 48 bado haijawa *utilized.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni soko la uhakika wa mifugo. Sasa hivi tunajenga machinjio makubwa kabisa pale Ruvu. Tuna machinjio ya Dodoma, kule Sumbawanga kuna machinjio safi. Halmashauri zina machinjio madogo madogo, Simanjiro wana machinjio na Monduli wana machinjio. Kwa hiyo, lengo letu kusema kweli ni kupeleka machinjio katika maeneo ya wafugaji kusudi machinjio yale yasaidie katika soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro Longido na Kampuni ya uwekezaji ya *Oritelo Business Co-operation.* Masuala haya tutaya-*forward,* nadhani watu wa Maliasili na Utalii wameshasikia, wajiandae kwa sababu bajeti yao bado. Basi wajiandae kujibu hili suala la mgogoro katika eneo hili ambalo ni *Game Controlled Area,* ni eneo la Hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kidogo kuhusiana na wawekezaji wa Kampuni inaitwa *Agrisol*. Maeneo haya ya Katumba na Mishamo ni maeneo ya kiuchumi ambayo Serikali iliamua kuyatangaza kwa lengo la kuvutia wawekezaji. Ndipo mwaka 2008 Kampuni ya *Agrisol* ya Marekani ilionesha nia ya kuwekeza katika maeneo hayo ya Katumba na Mishamo. Mwezi Februari mwaka 2010 yaani mwaka jana Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda ilipokea maombi ya Kampuni ya *Agrisol* kupitia kwa Mkuu wa Mkoa tarehe 5 Machi, 2010 maombi hayo yalijadiliwa na timu ya wataalam wa Halmashauri na kufikia muafaka, kwamba wale wataalam wakaafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarehe 14 mwezi wa tatu, mambo hayo yalifikishwa kwenye Kamati ya Fedha na Utawala na Mipango na Kamati ilishauri utafiti ufanyike ili kufahamu vya kutosha kuhusiana na uwekezaji huu. Tarehe 22 Machi, 2010 Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango ilijadili maombi hayo, baada ya kufanyiwa utafiti zaidi na timu ya wataalam. Kamati ilikubali na kuamua kuwa ombi hilo lifikishwe kwenye Baraza la Madiwani. Tarehe 26 Baraza la Madiwani lilipokea ombi hilo na liliomba Uongozi wa *Agrisol* uende lakini tarehe 22 Aprili *Agrisol* walituma mwakilishi wao wakakutana na Madiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 11 Agosti makubaliano kati ya Halmashauri na *Agrisol* kufanya utafiti yakinifu wa udongo katika maeneo Katumba na Mishamo yalitiwa saini. Sasa manufaa ya uwekezaji kwa kampuni hii ya *Agrisol*, Tanzania kwanza itapata fursa ya mafanikio katika sekta ya kilimo kwa sababu itakuwa ni *Private Public Partnership*. Niseme tu kwamba, jamani wale watu wanaozungumza kuhusu hii *Agrisol* hebu wasafiri kwa gari kutoka Sikonge kwenda mpaka Mpanda waone hilo pori lililopo kwenye Mkoa huo wa Katavi. Eneo halijatumika na wakati huo huo tunasema kwamba tunataka kuvutia wawekezaji, watu waweze kusafiri tu sio lazima uende Ulaya, twende South Africa. South Africa kutoka Free State, Free State kwenda Blue Fontein, I mean Blue Fontein ndiyo Free State kwenda Mafe King South Africa, unaweza ukasafiri hapa mpaka Gairo ni shamba la mtu mmoja. Anakagua shamba lake kwa helikopta mamilioni ya hekta shamba la mtu mmoja. Sasa leo hii tunapata wawekezaji, tunaanza kusema *aah* wanakuja kupora ardhi yetu, sasa tuitumie basi. Tunaosema kwamba hawa watu wanakuja kupora hebu twende Mpanda na Rukwa na Katavi tukaone walivyo na eneo kubwa ambalo haliko *utilized.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wanakuja wanawekeza, wanatuzalishia chakula, wanakuja wanazalisha mifugo, tunapata chakula na tunaweza kupata usalama wa chakula. Kwa hiyo, tusiwe tunapinga, tusiwe tunapinga tu uwekezaji, tunapinga uwekezaji, tunapinga uwekezaji. Sasa hiyo ardhi itakaa mpaka lini? Tunataka *modernization, modernization* siyo kuwa na *power tiller* peke yake. Lazima tuwe na wawekezaji wenye fedha, waje wawekeze ili wazalishe na nchi iweze kupata kwanza kodi, lakini wananchi wanaozunguka eneo lile watakuwa wanauza mazao yao pale. Kuna vijiji 27 ambavyo vitanufaika na mradi huu. Wataongeza thamani ya mazao yao. Kutakuwa na sayansi na teknolojia zitaenea kwa sababu hawa mabwana wasisaini mkataba, maana sasa hivi hawajasaini mkataba. Kutakuwa na programu za mafunzo na mambo yatakuwa ni mazuri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madiwani wanashirikisha wananchi pamoja na Wenyeviti wa Halmashauri pamoja na wataalam. Wananchi wameshirikishwa na wanaelewa na maeneo haya siyo kwamba yalikuwa yanamilikiwa na wananchi. Maeneo haya ni ya Serikali yalikuwa yanakaliwa na wakimbizi. Sasa mnataka wakimbizi wakae miaka 20 pale badala ya kumpa mwekezaji atuzalishie chakula? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani tuunge mkono, kama hivi *political will,* viongozi wetu wametuonesha. Lazima tuwaunge mkono. Tukikataa leo, akienda Rwanda pale amekwishapata eneo na ameshapata vibali.

Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge hoja imetolewa na imeungwa mkono.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MWENYEKITI:** Kanuni ya ngapi? Kwa ufupi sana Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali. Naomba mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 67(8) na mwongozo ninaouomba unahusu maamuzi

**MWENYEKITI:** Kanuni ya, kanuni namba?

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Kanuni ya 68(7) inayohusu mwongozo wa Spika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kikao cha leo asubuhi kulikuwa na mvutano juu ya hoja niliyotoa kwamba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu alikuwa ametoa kauli isiyokuwa ya ukweli na niliomba nithibitishe hiyo kauli yangu na baadaye Mheshimiwa Mwenyekiti alitoa uamuzi kwamba nitoe uthibitisho kufikia saa tano asubuhi na nilifanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uthibitisho niliuandika ushahidi wote wa nyaraka na nimeupeleka Ofisi ya Spika tangu saa tano asubuhi. Sasa naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 63(iv) natakiwa niwasilishe huu uthibitisho mbele ya Bunge hili Tukufu ili kuliridhisha Bunge kwamba nilichokisema kilikuwa sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge nimepokea hiyo taarifa ya mwongozo. Nitautolea maamuzi baadaye na kwa kuwa Katibu ameshanipa mwongozo wa hatua inayofuata. Naomba sasa tuingie kwenye Kamati ya Matumizi.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 99 – WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI**

Kif. 1001 - *Administration and General…………*Sh. 7,420,422,000/=

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge wengi walisimama ili kuchangia katika kifungu tajwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge hebu Katibu anzeni kunisaidia kuorodhesha majina.

*(Hapa, majina ya Waheshimiwa Wabunge, waliosimama kuhitaji ufafanuzi, yaliorodheshwa)*

**MWENYEKITI:** Jamani mmeona listi ilivyo! Kwa hiyo, hapo Waheshimiwa Wabunge, tuelewane tu lugha moja kwamba, itabidi tuende kwa utaratibu na kwa spidi itakayowezekana, litakalowezekana litafanyika. Vinginevyo hatutaweza kumaliza.

Haya, naomba nianze na Mheshimiwa Lekule Laizer.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningependa kukanusha kabla ya kusema jambo langu. Ningependa kukanusha usemi wa Waziri, alisema kwamba, nilisema kwenye mchango wangu kwamba ng'ombe walipiwe kodi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikusema hivyo kabisa! Nilisema Halmashauri nyingine wamekuja kuchukia ng'ombe baada ya kufutwa kodi, sikusema walipishwe kodi! Baada ya kufutwa kodi ndio wakaja kuchukia mifugo kuwepo katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kupata uthibitisho kuhusu ranchi ambazo Serikali inataka kubinafsisha na nilisema kwenye maelezo yangu, hizo ranchi wangepewa vijiji vinavyozunguka au wananchi ambao wamenyang'anywa maeneo hayo. Nilitaka kupata uthibitisho huo.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lekule Laizer, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme, alinikumbusha kwamba, kama tutakuwa tunachukua kodi maana yake ni kwamba Viongozi watakuwa wanaheshimu mifugo na kwa hiyo, watakuwa wanawatafutia maeneo ili waweze kutoza ushuru na waweze kupata mapato. Lakini kama hatutozi kodi maana yake ni Viongozi hawatakuwa wanaheshimu na Viongozi wale wa Halmashauri hawatakuwa wanatafuta maeneo ya kufuga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala lake la ranchi. Nadhani angeniambia ni ranchi ipi? Kwa sababu, tunazo ranchi nyingi! Nimesema tulikuwa na mashamba 104 na tumeyabinafsisha yote. Lakini mashamba manne ndio ambayo wawekezaji wake hawajawa *serious* na nimeyataja! Kwamba matatu ni kule Mzeri na moja ni kule Uvinza. Kwa hiyo, labda anieleze ni wapi kwa sababu, suala la *West Kilimanjaro,* bado tunalifanyia kazi. Tulishatangaza tenda na bado tunaendelea kuchambua watakaokuwa wameshinda katika vitalu vitatu.

**MHE. CHISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Pamoja na shukrani zangu kwa Mheshimiwa Rais, Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kifuta machozi cha bilioni 8.7 kwa ajili ya wafugaji na bila ya kuathiri Mamlaka ya Rais ya kuunda Wizara kwa jinsi anavyoona inafaa. Je, Waziri, atakubaliana na mimi kupeleka salamu za ushauri kwa Mheshimiwa Rais, kwamba muundo wa sasa wa Wizara ya Mifugo, ambao hauwezi kushughulikia maji kwa ajili ya mifugo wala majosho kwa ajili ya mifugo, wala chanjo nyingine kama ambazo zilikuwa zinahitajika! Najua chanjo nyingine mnahusika lakini hizi za msingi mmeachana nazo kama hizi za *ECF!* Je, Mheshimiwa Waziri, atakubali kupeleka salamu zangu za kuiomba Serikali itafakari upya muundo wa Wizara hii, ili iweze kushughulikia mifugo kwa ukamilifu wake kwa maana ya maji na dawa, badala ya kubaki na sensa na kazi nyingine chache kwa faida ya wafugaji? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ole-Sendeka, kaka yangu na jirani yangu anaelewa kabisa kuna *D By D (Decentralisation By Devolution),* kupeleka madaraka kwa wananchi. Kinachofanyika hata Wizara ya Kilimo au hata Wizara ya Elimu, inapeleka madaraka kule kwenye Wilaya! Sio kwamba sisi basi hatujui kuhusu majosho au hatujui kuhusu malambo wala dawa! Sisi ndio *regulators* wenyewe wa hivyo vitu na sisi ndio tunapima viwango vya hiyo miundombinu ambayo inawekwa. Kwa hiyo, sio kweli kwamba iko mbali! Iko kwetu na ndio maana ina Wizara. Sasa muundo wa Wizara unatokana na Rais mwenyewe, atakavyoona inafaa.

**MHE. ZAYNABU M. VULLU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wakati Mheshimiwa Waziri, anatoa ufafanuzi katika suala la mifugo, alisema kwamba, migogoro ipo baina ya wafugaji na wakulima na mifugo inaweza ikafugwa kokote na hatuwezi kulima kila mahali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka aniambie ni kwa vipi atawasaidia wananchi ambao tayari walikuwa wako katika maeneo yao wanalima, wanavuna na wanaendesha maisha yao kwa kutumia kilimo? Lakini wakatolewa ng'ombe maeneo mengine wakapelekwa kule, matokeo yake wale wakulima wa kule wanapata adhabu ya kuvuna! Wao wanaendelea na mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Wilaya ya Rufiji maeneo ya Kata ya Mtunda, Kata ya Ruaruke, Wilaya ya Kisarawe, Kata ya Mafizi! Huko kote inapotokea migogoro wanaoathirika sana ni wakulima. Je, Serikali inasema nini kwa wale ambao ni wafugaji waliokwenda kuvamia maeneo ya wakulima. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, kwanza, sikusema kwamba, tunaweza tukafuga kila mahali na sikusema kwamba tunaweza tukalima kila mahali! Nimesema haiwezekani kufuga kila mahali, wala haiwezekani kulima kila mahali! Hivyo ndivyo nilivyosema na ndio maana nikasema kuna umuhimu wa mipango mizuri ya matumizi bora ya ardhi. Lazima Vijiji viangalie pamoja na Halmashauri ziangalie na zifuate taratibu nzima za kuangalia Sheria ya 1999 ya Ardhi pamoja na Sheria ya 1999 ya Vijiji; kusudi wananchi wawe wanajua na wawe wanajulishwa kwamba ardhi hii anagawiwa mtu fulani, ardhi hii wanagawiwa wafugaji, ardhi hii wanagawiwa wakulima!

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wafugaji na wakulima. Ndugu zangu, wafugaji ni Watanzania! Wakulima ni Watanzania! Kinachotakiwa pale sio kuwatoa! Tuzungumze kwamba, wakae wapi? Wapelekwe wapi wakati na wao wana haki ya kuishi, wana haki ya kumiliki mali. Mali yao na wao ni mifugo, mali ya wakulima ni mazao. Kwa hiyo, ni lazima tuangalie na tuzungumze kwamba na wao wanakwenda wapi? Tuzungumze kwa pamoja, lakini sio kusema kwamba, waende!

Mheshimiwa mwenyekiti, kule Rufiji tulitoa wafugaji Ihefu, tukawapeleka Rufiji na Mtwara na tunapeleka miundombinu. Halmashauri, zihakikishe kwamba wananchi wale wanaibua miradi ya majosho pamoja na malambo kusudi miundombinu ile iweze kuwasaidia wafugaji katika maeneo yale.

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Nadhamiria kama ningepata nafasi wakati wa kuchangia, nilikuwa mtu wa pili baada ya Mheshimiwa Ritta. Lakini bahati mbaya, nafasi yangu imehujumiwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Waziri wa Uvuvi, katika majumuisho yake ametwambia kwamba, vyombo vya uvuvi vyenye urefu usiozidi mita 11, vinatozwa leseni katika Halmashauri husika na kwa kuwa, wavuvi wana asili ya kuhama kutoka kisiwa kimoja kwenda kisiwa kingine! Nikiwa na maana ya kutoka Wilaya moja, *let say* Kome kwa Mheshimiwa Tizeba, kuja Ukerewe kwa Jamhuri yangu, ndio! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakilipa kwenye Halmashauri ya Kome, leseni za uvuvi pamoja na mitumbwi, wakifika Ukerewe, Halmashauri ile inatumia vyombo vya dola, nikiwa na maana ya Polisi, kutoza leseni mara mbili! Ambalo ni kosa la jinai, *double taxation!* Serikali inasema nini kukuhusu hili? Tunaomba maelezo.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria Namba 22 ya mwaka 2003. Kifungu Kidogo cha 5(1) na (2), kinasema kwamba, ni lazima mvuvi ahakikishe kwamba analipa leseni pamoja na chombo chake kinalipa leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama unatoka sehemu moja, unatoka Chato unakwenda Musoma, lakini kwa sababu kule Musoma nako unavua rasilimali ya uvuvi! Ni lazima ulipe mapato kwenye Halmashauri ile kwa sababu, unavuna pale kwenye Halmashauri yao.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu yoyote ile hutolewa ili mtu aweze kuyakabili mazingira yanayomzunguka pale. Sasa katika Hotuba ya Waziri, amesema elimu ya uvuvi bora imetolewa Iramba, Mpwapwa, Singida, Moshi, Arusha! Wakati hakuna miundombinu ya kuweza kufanya kazi ya uvuvi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaona Ziwa Tanganyika, sijaona Ziwa Nyasa, sijaona Viktoria! Hebu nithibitishie, elimu hii iliyotolewa kwa watu ambao hawahusiki, itakuja lini maeneo hayo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu ndugu yangu, kaka yangu na mshauri wangu, Mheshimiwa *Captain* John Komba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza elimu haitolewi kwenye maziwa peke yake! Maji ya baridi ni pamoja na mabwawa na maziwa na mito iliyoko ndani ya nchi. Ukifika kule Singida utakuta kuna bwawa, ukienda Kilimanjaro utakuta kuna Nyumba ya Mungu, ukienda Babati utakuta kuna Ziwa Babati! Kwa hiyo, elimu inatolewa. Lakini, naomba nikueleze kitu kimoja kizuri ambacho ninakileta kule kwako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu maji kwa upande wa Tanzania, kina chake ni kirefu na zana za uvuvi kwa Watanzania ni duni ukilinganisha na Malawi, ambao wana kina ambacho ni *shallow!* Sisi sasa hivi, tunajipanga kuleta kiwanda cha kutengeneza maboti ya kuvulia samaki katika Ziwa la Nyasa, kusudi wananchi wako nao waweze kufaidika na maboti hayo, yataambatana pamoja na elimu kwa wavuvi wako.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni, naomba kuongeza muda wa nusu saa ili tuweze kuendelea na kazi hii. Hapo, naendelea kumwita Mheshimiwa Mwijage.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wakati nachangia kwa maandishi na nilipokuwa nazungumza, nilizungumzia suala la wafugaji haramu wanaotoka nchi jirani kuja kufuga katika eneo letu, wakiwasumbua wawekezaji wenye *block* na kulisha kwenye mashamba ya wananchi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, hakunijibu na nilikuwa nimesisitiza, ningetaka hata amri ya Serikali, kujua Serikali itatusaidiaje? Watu wa Kagera, wamenipigia simu, wanaomba msaada wa Jeshi la Wananchi! Wana mapenzi na Jeshi la Wananchi, ndio maana wanaomba likawasaidie!

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu Mheshimiwa Mwijage, kaka yangu Mwijage, tena ni *school mate* wangu, maana tulisoma wote Tosamaganga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio chake hiki ni *genuine!* Ni halali kabisa, kwamba sisi hatuwezi tukaenda Rwanda wala Burundi kufuga kule kwao na wala Uganda! Kwa hiyo, na sisi Serikali tulishatuma Makatibu kutoka Wizara saba, Makatibu Wakuu saba, kufuatilia suala hili! Hili suala liko Serikalini na Waziri wa Mambo ya Ndani, amekwenda juzi tu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachosema ni kwamba, Serikali inalichukulia hili suala *very serious.* Baada ya muda mfupi mtasikia tu, mambo yanavyoendelea. Lakini si halali watu wanatoka nje, wavamie eneo letu! Kwa sababu, hata sisi hatuendi kwao! Tungekuwa tumekwenda, Rwanda, wangekuwa wameshaturudisha. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naamini watu wengi hawaelewi kama Singida pia tunashughulika na uvuvi. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, leo Watanzania wajue kwamba Ziwa Kitangiri, liko Singida katika Wilaya ya Iramba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu Mheshimiwa Waziri, anisaidie kwamba, kulikuwa na matatizo ya mgogoro kati ya Wilaya ya Meatu na Wilaya ya Iramba, kuhusu mpaka wa Ziwa Kitangiri. Kwa hiyo, naomba ufafanuzi wako, Ziwa hilo liko wapi? Ahsante.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la dada yangu, Mheshimiwa Martha Mlata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli ninachoweza kusema ni kwamba, Kitangiri iko Singida na iko Tanzania. Lakini kusema kwamba iko eneo gani! Sasa hilo ni mpaka tutume

Wataalam wa Ardhi na Wataalam wengine, waweze kuthibitisha. Mimi hapa siwezi nikathibitisha. *(Makofi)*

**MHE. REV. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Napenda kumwuliza Waziri, kwa kuwa Serikali imekuwa ikipigia debe sana Sera za Uwekezaji na Mheshimiwa Waziri, ameongea kwa mbwembwe sana, akitolea mfano wa *South Africa,* nimebahatika kukaa Kwazulu Natal, takriban miaka mitano na wananchi wa *South Africa,* wanapata tabu sana na nasema ni bomu ambalo litakuja kulipuka kwa jinsi ambavyo waliporwa ardhi yao, wakatupwa upenuni! Ni watu ambao wanalalamika kwamba, wawekezaji waliwatoa maeneo yao wako kwenye makorongo kule. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa je! Hili ndio linaashiria kwamba, Tanzania inataka kuwafanyia hivyo wafugaji watupwe maporini, wawekezaji waje wakae katika maeneo mazuri? *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia ya Tanzania, hatukuwa na Sera za Ubaguzi wa Rangi. Wale wana historia ya ubaguzi wa rangi na mashamba yale yalikuwa yanaandikwa kwenye Katiba kwamba, ni ya weupe, sisi mashamba ni ya Watanzania. Lakini tunapozungumza kuendelea kiuchumi, ni lazima kuwe na uwekezaji. Hakuna nchi ambayo inaweza kuendelea bila uwekezaji ambao ni *serious! (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukienda Marekani kule, unaweza ukashangaa shamba la mahindi sio la Mmarekani! Kwa sababu, uwekezaji unatokana na wanaotoka dunia nzima na kwenda kuwekeza katika maeneo mbalimbali.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi, nilitaka kujua ni vigezo gani vinatumika kupima na kutenga maeneo ya ufugaji. Kwa mfano, Mkoa wa Shinyanga, ni katika Wilaya ya Bariadi tu, ndiko kuna eneo ambalo limetengwa kwa ajili ya wafugaji! Sasa Mkoa wa Shinyanga wote ni wa wafugaji! Wilaya ya Kahama, kuna wafugaji wengi na mifugo mingi, hakuna eneo kama hili!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kila jambo ni lazima pawepo mahali pa kuanzia. Hata tungeanza Maswa, wa Bariadi wangesema ni kwa nini mmeanzia Maswa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni uwezekano tu na uwepo wa fedha! Tuna Tume ile inafanya kazi, imeshazunguka Tanzania nzima, imeshapima hekta milioni 2.03 katika Vijiji 440! Wanaendelea na zoezi hilo. Tukipata fedha, tutaendelea kupima hata kule kwako ambako hawajapima kwa ajili ya matumizi bora ya ardhi.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Katika mchango wangu nilizungumzia kuhusu Serikali kuangalia jinsi gani inaweza kuwasaidia watu wa mwambao katika ufugaji wa samaki kwenye mabwawa. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 133 kama sikosei, ametaja mikoa, mikoa ya Pwani au mwambao yote karibu haipo kasoro Lindi. Naona iko mikoa ya Bara ambayo wengine si wafugaji wa samaki. Sasa naomba nimwulize Waziri je, Mkoa kama wa Dar es Salaam, Pwani, Tanga ambayo yote iko katika ukanda haimo katika mpango wake?

**MWENYEKITI:** Muda umekwisha, majibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu dada yangu Mheshimiwa Madabida kama ifuatavyo:-

Kwa kweli hata tusipotaja Dar es Salaam na Pwani ndiyo maeneo hasa ya ufugaji. Nadhani hili ni suala ambalo liko wazi tu, kwamba ndiyo maeneo yenyewe, sasa usipowasaidia watu wa Pwani, utasaidia wapi maana ndiyo kwenye ukanda wa bahari ya Hindi ambako ndiyo kuna ufugaji, kilimo cha mwani, kilimo cha lulu, kilimo cha kaa na ndiyo kwenye kilimo cha chaza.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi, nilikuwa nimesema kwamba katika kipindi cha mwaka 2010/2011, wafugaji wa nguruwe katika Mikoa ya Mbeya, Iringa na Dar es Salaam waliathirika sana kwa nguruwe wapatao 11,845 kufa, lakini Serikali imezungumzia kuwafidia wafugaji wa ng'ombe waliopotelewa au kufiwa na ng'ombe wao lakini hawazungumzii kuwafidia wale wafugaji ambao nguruwe wao wengi wamekufa na hawa wengine pia walikuwa wamekopa benki. Sasa Waziri anatueleza nini, nchi hii ina sera ya upendeleo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii haina sera ya upendeleo, lakini vigezo vya kufidia viko hivi, kama ugonjwa umetokea na Serikali imeamua kuwauwa kwa maana hiyo nazungumzia nguruwe, kama tumeamua kuuwa ili ule ugonjwa usienee, basi tuta-*compensate* tutazilipa fidia, au kama tumeamua kuchinja nguruwe basi tuta-*compensate*, lakini kama wamekufa wenyewe kwa ugonjwa hatuwezi tuka-*compensate*. Kwanza ugonjwa huu ni *endemic, endemic* maana yake ni ugonjwa ambao upo, ni sawa na kusema mtu akiugua mafua apate *compensation*, mafua yapo, yapo tu, sasa ugonjwa huu upo tu, ni *endemic*, kwa hiyo hakuna fidia kwa sababu nguruwe wale walikufa wenyewe na baadhi ya watu hawakufuata taratibu tuliweka karantini, wakawa bado wanasafirisha usiku maana wanawaita wajumbe wa mkutano mkuu eti wanawapeleka Dar es Salaam. Kwa hiyo tunachosema ni kwamba tunapoweka taratibu, tunapoweka sheria lazima tuzifuate. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, katika mchango wangu wa maandishi, nilipenda Serikali itoe ufafanuzi hapa Bungeni, nini hatima ya wafugaji wa Tanzania waliofilisiwa na kuachwa maskini mwaka 2009 baada ya mifugo yao yote kuchukuliwa kutokana na zoezi la *operation* hamisha mifugo, ambalo lilihujumiwa na watendaji. Wananchi wale wameshindwa kusomesha watoto wao, wameshindwa kujiendeshea maisha, wengine mpaka sasa hivi hawajui waende wapi, Serikali iliunda Tume mpaka leo Tume ile haijatoa taarifa popote wala hatujui nini kinachoendelea. Nini maelezo ya Serikali leo hapa Bungeni juu ya wananchi hao?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Sakaya, kwanza wafugaji wale walipewa *notes*, wakapewa na muda waamue wanakwenda wapi. Walipewa muda wa kutosha kabisa, waamue mahali pa kwenda, hawakwenda, wengine walikwenda walifuata taratibu wakaenda huko walikoona kwamba panafaa, wengine walikwenda Lindi, wengine walikwenda Mtwara. Lakini kuna waliorudi tena, sasa hawa unaozungumzia Mheshimiwa Sakaya, ni wale ambao walirudi wakiuka maagizo ya Serikali, walikamatwa, wapo waliokamatwa mia moja na ushee, ni mia kama na thelathini hivi halafu na wengine wanne kesi zao bado zinaendelea Mahakamani na walipigwa faini, maana waliingiza ng'ombe 4,100 walipigwa faini ya milioni 79 kwa ujumla kwa sababu ya kukiuka, nazungumzia suala la Ihefu kule Usangu, ndiyo eneo ambalo nalizungumzia.

**MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Vunjo eneo ni dogo, watu ni wengi, lakini wana ujuzi wa kufuga ng'ombe wa kisasa wa maziwa. Nimeongea na baadhi ya maafisa wa Benki ya Dunia na hili Shirika la Taifa *International*, wakasema kama utaandika *write up* kama Serikali yako itakuunga mkono, wako tayari kukopesha fedha za kununua ng'ombe wa kisasa ili tuweze kuwakopesha wananchi wa Vunjo lile eneo dogo wakope wazalishe halafu warejeshe ule mkopo.

La pili mpaka...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mrema ni moja tu.

**MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA:** Siyo swali la pili ni nyongeza ya hilo la kwanza.

**MWENYEKITI:** Umeshauliza swali sasa baada ya kuuliza swali huwezi kuweka nyongeza, Mheshimiwa Waziri majibu, swali limeshaulizwa, Mheshimiwa Lyatonga tafadhali.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVIVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la jirani yangu na kaka yangu Dokta Lyatonga Mrema kama ifuatavyo:-

Wazo lake hilo ni nzuri la kwamba waweze kupata mkopo ili wanunue ng'ombe, lakini kwa sasa hivi kabla hatujakaa chemba mimi na wewe tukaongea kwamba likoje hilo suala siwezi nikai-*commit* Serikali hapa, ni vema tukae tuongee. Lakini kabla hatujaongea, uongee na Halmashauri yako kuna fedha za *DADPs* mnunue mitamba, tunazalisha mitamba zaidi ya 10,000 ili uweze kupeleka kwa ajili ya kukopa ng'ombe lipa ng'ombe na kopa mbuzi lipa mbuzi. Tunayo hiyo programu kwenye Wizara yangu, tunaweza tukakuletea kwa bei nzuri.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, niliiuliza Serikali, inawasaidia vipi wavuvi wa Ziwa Tanganyika hasa katika Vijiji vya Kalema na Ikora, ambako Ziwa Tanganyika lina kina kirefu, uvuvi wake unahitaji kuwa na vifaa vya kisasa, je, Serikali imejipanga vipi kuwasaidia wavuvi hao?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Ziwa Tanganyika kuna programu ya kuendeleza Bonde la Ziwa Tanganyika, ambayo Makao Makuu yake yako Burundi na programu hii inahusisha nchi nne, Zambia, Tanzania, Burundi na *DRC*. Programu hii iko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Makamu wa Rais na inahusisha uvuvi, majitaka na majisafi pamoja na mazingira na programu hii imepanga kwamba watajenga mialo 47 lakini kwa sasa hivi Wizara yangu itajenga mialo miwili, Kigoma Uvinza na Kigoma yenyewe halafu na Sumbawanga pamoja na Wilaya jirani pale.

**MWENYEKITI:** Inatosha.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Kwamba waweze kupata mialo ya kukusanyia samaki. Kwa hiyo, ninachoweza kumwambia ni kwamba, kwa sasa hivi kusema kweli wanachama wale...

**MWENYEKITI:** Muda umekwisha Mheshimiwa Waziri nimwite Mheshimiwa Hilary.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona, kwa kuwa Serikali imeshawatengea sehemu maalum wafugaji na sasa kuna sehemu kubwa katika Jimbo langu ambalo limevamiwa na wafugaji, je, Serikali itawaondoa lini wafugaji hao ambao wamevamia katika Kata ya Mnyuzi, Kagunda, Mkaramo, Mswaha, pamoja na Mazinde, Serikali kwa sababu sasa wameshawatengea sehemu, naomba waniambie ni lini watawaondoa wafugaji hao*? (Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ngonyani kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema pale awali, wafugaji wale ni Watanzania na nadhani wenyeji ambao wapo pale ambao ni wakulima vile vile wanajihusisha na ufugaji. Kwa hiyo, suala la kufanya hapa uongee na Halmashauri yako, ili muweze kuwa na mipango mizuri kutokea kule kwenye vile vijiji kwa kutumia zile sheria nilizozitaja, kusudi muweze kutenga maeneo ya wafugaji lakini siyo kwa kuwafukuza maana ni Watanzania, hawana pa kwenda, ni Watanzania wanaoongea Kiswahili, Kisambaa au Kipare.

**MHE. RITA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nilipochangia kwa maandishi nilitaka kupata ufafanuzi kuhusu mradi wa machinjio ya kisasa uliopo katika Kata ya Mwambata, Manispaa ya Iringa Mjini, mradi ule umeshakuwa wa muda mrefu sana na tayari kuna milioni 113 zimeshatumika katika jengo lile na Halmashauri ilishaleta andiko katika Wizara yako yenye thamani ya sh. 630,000,000/= na nimeshamfuatilia Mheshimiwa Waziri mara nyingi sana na yeye mwenyewe

ni shahidi, sasa nataka niombe, je, ni lini tutapata mradi ili wananchi wa Iringa wakae mkao wa kula?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, machinjio haya ambayo anayazungumzia Mheshimiwa Kabati, ni machinjio ya Halmashauri ya Wilaya. Kwa hiyo, namwomba kwanza waweke mipango mizuri kuonyesha kwamba kwenye Halmashauri ya Wilaya wanahitaji hayo machinjio. Kama wanahitaji wayatengee fedha, halafu watakapokwama basi watatueleza, sisi Wizara tutajua cha kufanya.

**MHE. AMOS G. MAKALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Katika mchango wangu wa maandishi, nilitaka kujua hatma ya wafugaji wa asili wa Kijiji cha Wami Sokoine, kutokana na Waraka Namba (2) wa Baraza la Mawaziri wa mwaka 2002 ulielekeza kwamba *ranch* ya *NARCO* igawanywe kama ifuatavyo:-

Mtibwa *Sugar* hekta 10,000; walipewa wakulima wa miwa hekta 5000 wa Wami Luhindo, hekta 2000 walipewa wafugaji wa kisasa ambayo ni *ranch* ndogo walipewa hekta 5000. Lakini mpaka leo wafugaji wa asili hawajapewa hekta 5000 lakini Waziri alinijibu kwa barua kwamba hekta hizo 5000 walishapewa na anazifanananisha kwamba hizo hekta ni za watu aliowataja ni Elisa Mollel na Katenda *Group*....

**MWENYEKITI:** Muda umekwisha, majibu Mheshimiwa Waziri.

**MHE. AMOS G. MAKALA:** Sasa nilitaka kujua ni lini watapewa hizo ekari 5000?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu rafiki yangu na kijana mwenzangu Mheshimiwa Amos Makala kama ifuatavyo:-

Kwanza, niwajulishe wananchi wa Mvomero kwamba Mheshimiwa Amos Makala anawatetea sana katika kuwatafutia maeneo ya malisho ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Mawaziri Waraka wake Namba 2 wa tarehe 29 Agosti, 2002, ilitoa maelekezo yafuatayo: Kwamba hekta 50,000 za Dakawa, zigawanywe kwa wawekezaji wadogo, wafugaji, wawekezaji wadogo wa miwa pamoja na Mtibwa Sugar kwa hekta 30,000. Sasa wafugaji wa asili ambao anawazungumzia wa Wami Sokoine, walipewa hekta 5,000 na Mkurugenzi wa Halmashauri alithibitisha tarehe 10 Juni, 2009 kwamba wamepokea eneo hilo ambalo ni kitalu 299/2 na 299/4. Vile vitalu wanavyovizungumzia vya 299, *three* B na *three* A, vimechukuliwa na Mheshimiwa Mollel ambaye alipewa kama mwekezaji mfugaji mdogo pamoja na Katenda *group* ambayo ilipewa 299/3/ A. Kwa hiyo, eneo lile walishapewa na Mkurugenzi wao alisharidhika kwamba walishapewa.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona, katika mchango wangu wa maandishi nimejaribu kuonesha kwamba Jimbo langu la Manyovu, linalo wafugaji wa mifugo, ambao minada yao imefungwa kwa muda mrefu na ndani ya Wizara amejaribu kuonyesha kwamba wana *promote* minada ya mipakani na muda wa awali wa Kata ya Muyama, Kajana, Kilelema, Mgera imefungwa, kwa hiyo wafugaji hawana pa kuuzia mifugo yao. Nataka kujua Wizara inasemaje na tumejaribu kuwaambia Wilaya wanashughulikia lakini bado hawajatoa majibu na wananchi wanahangaika kweli kweli. Naomba majibu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Obama kama ifuatavyo:-

Kuna minada 300 Tanzania nzima, minada ya awali 300, na minada 12 ya upili na minada 10 ya mipakani. Sasa kwa sababu ametaja mnada huu ni wa awali, huu mnada upo chini ya Halmashauri. Kwa hiyo, naomba awasiliane na Halmashauri yake na ikibidi nitaiuliza Halmashauri kwa nini mnada huu ulifungwa, kwa sababu inawezekana kuna sababu za kufunga mnada huo ndio maana haufunguliwi.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri ametueleza kuhusu kampuni ya *Agresal* kutoka Marekani inayowekeza Tanzania chini ya mpango wa *PPP*. Naomba atoe ufafanuzi je, inawekeza na kampuni gani? Katika mkataba ambao unatarajiwa kusainiwa itashughulika vipi katika shughuli za maendeleo ya jamii hii *Agresal*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nyerere swali ni moja tu kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri utajibu moja, ndiyo utaratibu tuliojiwekea.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachosubiriwa sasa hivi ni *business plan*, ambayo wanaiandaa pamoja kama nilivyosema kwamba ile ni *private public partnership*. Mkataba bado haujasainiwa wakati wa kusainiwa ndiyo tutakuwa tuna *negotiate* kwamba wanatoa huduma gani kwa jamii.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu wa maandishi, nilisema kwamba, pamoja na kwamba tunaunga mkono jitihada za Serikali za kuzuia uvuvi haramu, lakini kuna tatizo kubwa la Maafisa Uvuvi wakishirikiana na Polisi kwenda kwenye maeneo ya masoko kunyang'anya akinamama samaki kwa kisingizio kwamba ni samaki wadogo ambao hairuhusiwi kuvuliwa na taarifa nilizonazo katika masoko ya Mkuyuni, Maina kati kule Nyamagana hata baada ya siku tano zilizopita akinamama walinyang'anywa samaki, naomba kauli ya Serikali kuhusu hili tatizo.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Samaki namba 22 ya mwaka 2002, kifungu cha 66 kwenye kanuni zake za mwaka 2009 kinazungumzia saizi ya nyavu, macho gani ya nyavu yanaruhusiwa kuvua samaki. Kwa mfano, Sangara, wanatakiwa wawe sangara ambao wa sentimeta 50 mpaka 85 ndiyo wanaruhusiwa kuvuliwa, kama amevua sangara ambaye ni mdogo kuliko hivyo viwango nilivyokupa lazima atakamatwa ili samaki wawe *destroyed*. Kama sato hajafikisha sentimita 25 haruhusiwi, kama dagaa amevuliwa lakini amevuliwa na nyavu ya milimita ambayo imepungua nane kwenye maji ya baridi pia ni kosa, kama anavua dagaa Dar es Salaam, Pwani, Mtwara lakini jicho la nyavu ni milimita chini ya kumi anachukuliwa hatua. Kwa hiyo, ni kweli hata mimi nimeshawahi kuchukua samaki kama hao tukawa-*destroy* kwa sababu hawaruhusiwi ambao ni *under size*.

**MHE. ABDULKARIM ESMAIL HASSAN SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa wakati wa kuchangia nilizungumzia suala dogo la mwananchi mmoja ambaye alirejesha nyavu zake yeye mwenyewe na kuzisalimisha pale Halmashauri. Namwomba Waziri anipe kauli ya kwamba, Serikali itamsaidiaje katika kumpa zana mbadala zinazohifadhi mazingira na uvuvi endelevu ili na yeye aweze kujikimu katika maisha? Naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie hilo.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuchukua nyavu ambazo hazina viwango na ku-*replace* na zile ambazo zina viwango tumeshazifanya kule Mnazi Bay, makutano ya mto Ruvuma kule Kusini. Kwa hiyo, hata mzee huyo nadhani tutakutana ili tuongee na wewe vizuri hili tujue tumsaidieje, kwa sababu huyo ambaye amejisalimisha alikuwa na nia nzuri.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Rukwa na hasa Vijiji vya Pito, Wipanga, Mmoro, Chana na sehemu zingine watu walichimba mabwawa na kuweza kufuga samaki. Lakini kwa bahati mbaya wale samaki waliweza kubanana kwa ujuzi mdogo na hata wale wananchi hawawezi kuuza. Sasa je, Serikali imepanga mikakati gani ya kuwakopesha hao wananchi wa hizo sehemu pamoja na kuwapa semina ni jinsi gani waweze kufuga na kuwatoa katika mabwawa yao ili ziwe kuwasaidia katika maisha yao.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Kwanza nawashauri wafugaji hawa wadogo wa samaki. Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane ili niweze kukupa wataalam ili waweze kupata utaalam mzuri na mahali ambapo watapata mbegu nzuri. Lakini pia kwa sasa nawaomba wajiunde vikundi vidogo vidogo au *SACCOS* ili waweze kupata nguvu ya kukopa na kupanga bei za mazao yao.

**MWENYEKITI:** Niingie *Central Corridor*, Mheshimiwa Lusinde!

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Katika mchango wangu wa maandishi nilimwomba Mheshimiwa Waziri aniambie Sheria gani inatumika kuzuia Tarafa nzima ya Mvumi Misheni yenye Kata saba kuzuia wananchi wa Tarafa hiyo wasifuge na hayo maziwa aliyokuwa anayasema kwamba wanatakiwa wanywe na hizo nyama watazipata wapi kama vijiji vyote zaidi ya 21 wanakatazwa kufuga tangu mwaka 1986. Naomba sasa tamko la Serikali juu ya Tarafa hiyo.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikiri kwamba, nimeshaongea na Mheshimiwa Kabajaji Livingstone J. Lusinde .....

**MWENYEKITI:** A.k.a Kibajaji! *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Lusinde maana yeye ni maarufu kwa jina la Kibajaji, kwa hiyo nimechanganya.

Mheshimiwa Lusinde alishalizungumzia suala hilo na kwa kweli ni suala muhimu sana kwa ajili ya wafugaji wake. Kwanza napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Dodoma kwa sababu wananchi wa Dodoma ni wafugaji lakini hawahamihami. Kwa hiyo, nitahakikisha kwamba tunalichunguza hilo tujue ni kipingamizi gani ambacho kiliwekwa, wasifuge tangu mwaka 1986 ili ikiwezekana tuweze kuwafungulia. Kama ni kigezo cha mazingira siyo ng'ombe peke ambaye anaharibu mazingira bali hata madini na kilimo nacho kinaharibu mazingira na wakata miti na wachoma mikaa nao wanaharibu mazingira. Kwa hiyo, ni lazima tuwaangalie wananchi hawa.

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kuhusu utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa mwezi wa Oktoba, 2009 alipotembelea shamba la ng'ombe wa maziwa Kitulo baada ya kuona hali yake kuwa siyo nzuri aligeuzwa na akaahidi kulifufua lile shamba ndani ya miaka mitatu na huu ni mwaka wa pili bado mwaka mmoja sijaona hatua zinazochukuliwa. Naomba maelezo kutoka kwa Waziri.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la kaka yangu Dokta Mahenge kama ifuatavyo:-

Kama alivyosema bado mwaka mmoja, napenda tu kumhakikishia kwamba ahadi yoyote ya Rais ni lazima tuitekeleze. Kwa hiyo, tukishamaliza bajeti hii tutakutana naye ili niweze kupata undani vizuri ili tuweze kuanza utekelezaji huo. Kwanza, hata hivyo, ilani hii ni ya miaka mitano na huu ni mwaka wa kwanza na tuna mpango wa maendeleo wa sekta ya mifugo kwa miaka mitano ijayo ambayo imeshaingizwa kwenye Mpango wa Kitaifa wa Miaka Mitano mpaka mwaka 2015/2016. Kwa hiyo, asiwe na wasiwasi kwani tutahakikisha kwamba suala hilo tunalishughulikia.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wakati nilipochangia kwa maandishi sikupata majibu na niliuliza je, Serikali ipo tayari kumkopesha mfugaji au vikundi vya wafugaji kwa riba nafuu kwa kupitia Taasisi za fedha na hasa *TIB* na dhamana ya huo mkopo uwe ni mifugo kwa sababu wafugaji wengi hawana ardhi ya kuweka dhamana na kama ni hivyo ni lini watafanya ili wafugaji waweze kujiendeleza kwa kufuga kwa kisasa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, jibu swali moja.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyotaja *TIB, TIB* sasa hivi unaweza ukaingia pale kwa dirisha maana tumetenga fedha kwenye dirisha kwa ajili ya mifugo pamoja na kilimo. Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Jitu Soni vikundi vyake viweze kuji-*organise* vizuri tena, yeye ni mfanyabiashara, kwa hiyo anaelewa masuala haya ya mikopo, awasaidie wapate mikopo kwenye benki ya *TIB* wakati tunasubiri mchakato wa Benki ya Kilimo ukikamilika tuweze kuwasaidia wafugaji lakini wawe na *SACCOS* na vyama vyao ambavyo vitawafanya wawe na nguvu ya kukopa.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Katika mchango wangu wa kimaandishi nilielezea wasiwasi wangu wa bajeti ndogo iliyotengwa kwenye sekta ya uvuvi kwa upande wa maendeleo ambao ni shilingi bilioni 4.2 ukilinganisha na mwaka uliopita ambao ulikuwa ni shilingi bilioni 8.2 lakini wasiwasi huo ulitokana na sekta hii ya uvuvi kuchangia kwa kiasi cha 74% ya mapato ya Wizara hiyo. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba sekta hii ya uvuvi haikutendewa haki?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama suala ni kwamba bajeti isipotosha haikutendewa haki, basi ni kwamba hakuna Wizara ambayo imetendewa haki kwa sababu suala ni kwamba tunagawana kasungura kadogo ambako kapo. Nasema kwamba, kama Waziri wa Wizara hii naridhika na kiasi nilichopewa kwa sababu najua kiasi ambacho kinakusanywa na Serikali.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Katika kuchangia kwangu kwa maandishi nilimwomba Mheshimiwa Waziri wafugaji waliorudishwa kutoka Mbarali kwenda Pwani, Rufiji na maeneo mengine ya Mtwara kwamba warudishiwe fedha zao ambazo walitozwa faini wakati hawakuwa wamekaidi amri yoyote halali ya Serikali na vilevile mifugo yao mingi ilikufa katika kipindi hicho cha faini kwa sababu ilikusanywa mahali pamoja bila kula. Sasa sioni sababu kwa nini Serikali isiwalipe fidia na kuwarudishia fedha zao ambazo walitozwa wakati hawakuwa wamekaidi amri yoyote halali ya Serikali.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili linahitaji mimi kama Waziri wa Wizara hii kuthibitisha kwamba, kweli walitozwa faini lakini hawakuwa na makosa ili tuweze kujua taratibu nyingine kwa sababu haya ni maelezo yake na ni lazima nijiridhishe kwa kutumia Wataalam wangu na vyombo vya Serikali vilivyopo kusudi tujue.

Lakini kama ninavyoelewa hakuna mfanyakazi wa Serikali ambaye atatoza ushuru kama kweli yule mfugaji hakufanya kosa lolote au atatoza faini kama hawakufanya kosa lolote. Lakini pia kama wanafanya makosa lazima watozwe na walipe fedha hizo.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika!

**MWENYEKITI:** Hakuna Mwongozo katika hatua hii, kwani tuna kazi nzito na nyeti hapa. Naomba sasa tupitishe mafungu haya kwa pamoja.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - Finance and Accounts …………Sh. 675,572,000/=
Kif. 1003 - Policy and Planning ……………Sh. 649,071,000/=
Kif. 1004 - Livestock Res. & Train. Instit....Sh. 6,680,706,000/=
Kif. 1005 - Inform., Commun. and Educ....…Sh. 90,518,000/=
Kif. 1006 - Nat. Livest. Instit. -Mpwapwa…Sh. 797,097,000/=
Kif. 1007 - Internal Audit Unit………………..Sh.119,289,000/=
Kif. 1008 - Procurement Man. UnitvSh.............. 110,000,000/=
Kif. 1009 - Legal Services Unit………………...Sh. 70,000,000/=
Kif. 7001 - Veterinary Services…………Sh. 10,622,661,000/=
Kif. 7002 - Livest.Identif. Registration & Traceable Unit.Sh...........................140,196,000/=
Kif. 7003 - Pastoral Sys. Develop.................Sh. 158,302,000/=
Kif. 7004 - Central Veterinary Lab...............Sh. 606,728,000/=
Kif. 7005 - Veterinary Counc.of Tanzania...Sh. 125,346,000/=
Kif. 8001 - Animal Production ……………Sh. 2,049,061,000/=
Kif. 9001 - Fisheries Develop. Division.....Sh. 5,667,626,000/=
Kif. 9002 - Aquaculture Develop. Div........Sh. 328,915,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati

ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU 99- WIZARA YA MAENDELO YA MIFUGO NA UVUVI**

Kif. 1001 - Administration and General ………….......Sh. 0/=
Kif. 1003 - Policy and Planning …………..Sh. 2,456,694,000/=
Kif. 1004 - Livestock Research and
Training Instititution...................Sh. 2,186,180,000/=
Kif. 1006 - National Livestock Institute -
Mpwapwa.................................Sh. 1,473,650,000/=
Kif. 7001 - Veterinary Services………….Sh. 6,044,093,000/=
Kif. 7002 - Livestock Identif. Regist and
Traceable Unit………..................... Sh. 909,962,000/=
Kif. 7003 - Pastoral System
Development……..........................Sh. 240,200,000/=
Kif. 7004 - Central Veterinary Lab. Sh.............. 875,149,000/=
Kif. 7005 - Veterinary Counc. of Tanzania..Sh. 118,000,000/=
Kif. 8001 - Animal Production ……………Sh. 1,580,176,000/=
Kif. 9001 - Fisheries Develop. Division.....Sh. 4,711,079,000/=
Kif. 9002 - Aquaculture Develop. Div.……Sh. 258,500,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya Bunge kumaliza hoja yake naomba nimwite mtoa hoja Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia makadirio ya matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ya mwaka wa fedha 2011/2012, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe makadirio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2011/2012 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono na idadi ya Wabunge inayotakiwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya walioafiki kushinda basi Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri niwapongeze kwa kazi ya leo lakini kwa mujibu wa michango mbalimbali na maoni ya Waheshimiwa Wabunge, basi naamini kabisa Wizara yako itachukua nafasi ya kutosha kusimamia shughuli hizi zinazohusu uvuvi na mifugo ili Taifa letu liweze kwenda mbele lakini hasa kuwapa nafasi Watanzania kuweza kunufaika na kujiongezea kipato kwa mujibu wa taratibu zitakazowekwa kupitia katika sekta hiyo ya uvuvi na mifugo.

Waheshimiwa Wabunge, niliombwa mwongozo na Mheshimiwa Tundu A.M. Lissu. Kwanza kabisa kwa mujibu wa Kanuni namba 21(2) Mheshimiwa Tundu Lissu ametimiza wajibu wake,

aliagizwa na Mheshimiwa Mwenyekiti aliyekuwa anaongoza kikao asubuhi ya leo hapa Bungeni awasilishe maelezo yake haraka sana tena akampa tu masaa nadhani matatu ili apeleke maelezo yake kwenye Ofisi ya Katibu wa Bunge. Kwa hiyo, Mheshimiwa Tundu A.M. Lissu ametekeleza. Baada ya Mheshimiwa Tundu A.M. Lissu kutekeleza kitakachofuata sasa ni Ofisi ya Spika kuona namna ya kuhitimisha suala hili ili shughuli za kikanuni na miongozo iliyotolewa na kutekelezwa iweze kufikia hatma yangu. Kwa hiyo, huo ndio mwongozo wangu, katika mwongozo aliouomba Mheshimiwa Tundu Lissu.

Baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge.

*(Saa 2.10 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi Tarehe 28 Julai, 2011 3.00 Asubuni)*